# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# KIKOSI KAZI CHA MHESHIMIWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KILICHOFANYIA KAZI MASUALA YANAYOHUSU DEMOKRASIA YA VYAMA VINGI VYA SIASA NCHINI

## RIPOTI YA KIKOSI KAZI

**OKTOBA 2022**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

Anwani ya simu: 'SIASA'
Simu: 026 2137232
Fax: 026 2136924

Unapojibu tafadhali taja:

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa
Viwanja Vya Nanenane Nzuguni
Jengo la Wizara ya Kazi,
Mtaa wa Nzuguni A
P.O. Box 2851
**DODOMA**

Kumb. Na. CHA. 269/322/01/6

21 Oktoba, 2022

Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
1 Barabara ya Julius Nyerere, Chamwino
S.L.P. 1102
40400- **DODOMA**

Yah: **KUWASILISHA RIPOTI YA KIKOSI KAZI**

***Mheshimiwa Rais,*** kwa heshima na taadhima tunaomba urejee suala tajwa hapo juu.

***Mheshimiwa Rais***, wajumbe wa Kikosi Kazi tunakushukuru na kukupongeza kwa juhudi unazofanya za kutuletea Watanzania maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii, hususani kuboresha mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa nchini.

***Mheshimiwa Rais***, tunamshukuru na kumpongeza pia, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa juhudi anazofanya Zanzibar za kuleta maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii, ikiwemo kuboresha mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa.

***Mheshimiwa Rais***, wajumbe wa Kikosi Kazi tuliteuliwa tarehe 23 Desemba 2021 na tukaanza kazi tarehe 11 Januari 2022. Wakati wa uzinduzi tulipewa hadidu rejea ambazo zimekuwa zikituongoza katika utendaji kazi wetu. Baada ya uzinduzi, tulichambua maoni ya wadau na kuainisha masuala tisa muhimu ya kufanyia kazi.

***Mheshimiwa Rais,*** baada ya kufanya kazi kwa muda wa miezi kumi (10), sasa tunayo heshima kuwasilisha kwako matokeo ya kazi uliyotupatia. Ripoti ya Kikosi Kazi tunayowasilisha ina sura kumi na moja ambapo kila sura imeeleza suala husika, maoni ya wadau, uzoefu wa nchi nyingine, uchambuzi na mapendekezo ya Kikosi Kazi.

***Mheshimiwa Rais***, masuala mahsusi yanayohusu Zanzibar, yamewasilishwa kwenye Kamati Maalum ya Zanzibar yenye jukumu kama la Kikosi Kazi hiki kwa ajili ya kufanyiwa kazi na ripoti ya Kamati hiyo itakuwa ni sehemu ya Ripoti hii.

***Mheshimiwa Rais,*** tunaomba kutumia fursa hii kukushukuru tena kwa kuanzisha Kikosi Kazi hiki, kutuamini kufanya kazi hii na kutuwezesha kwa hali na mali kutekeleza jukumu hili. Vilevile, tunamshukuru tena Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutupa fursa ya kuongea naye na wasaa mbalimbali katika kufanya kazi yetu.

***Mheshimiwa Rais,*** tunaomba kuwasilisha.

..............................................
Profesa Rwekaza Sympho Mukandala
**MWENYEKITI WA KIKOSI KAZI**

..............................................
Hamad Rashid Mohamed
**MAKAMU MWENYEKITI WA KIKOSI KAZI**

# WAJUMBE WA KIKOSI KAZI

| Na. | Jina | Wadhifa | Saini |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mizengo Kayanza Pinda | Mjumbe | |
| 2. | Prof. Bernadeta Kilian Mchapwaya | Mjumbe | |
| 3. | Prof. Alexander Boniface Makulilo | Mjumbe | |
| 4. | Mhe. Balozi Amina Salum Ali | Mjumbe | |
| 5. | Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe | |
| 6. | Mhe. Juma Ali Khatib | Mjumbe | |
| 7. | Bw. Zitto Zuberi Kabwe | Mjumbe | |
| 8. | Bw. Abdul Juma Mluya | Mjumbe | |
| 9. | Bw. Saum Hussein Rashid | Mjumbe | |
| 10. | Sheikh Dkt. Alhad Mussa Salum | Mjumbe | |
| 11. | Mchungaji George Paul Fupe | Mjumbe | |
| 12. | Bibi. Anna Meela Kulaya | Mjumbe | |
| 13. | Bibi. Jamila Mahmoud Juma | Mjumbe | |
| 14. | Bw. Deodatus Mutalemwa Balile | Mjumbe | |
| 15. | Dkt. Lucas Luhende Kija | Mjumbe | |
| 16. | Bw. Ali Omar Makame | Mjumbe | |

| Na. | Jina | Wadhifa | Saini |
|---|---|---|---|
| 17. | Bw. Martin Bernard Mung'ong'o | Mjumbe | |
| 18. | Kamishna wa Polisi, Benedict Michael Wakulyamba | Mjumbe | |
| 19. | Prof. Edward Gamaya Hoseah | Mjumbe | |
| 20. | Bw. Slim Said Abdallah | Mjumbe | |
| 21. | Dkt. Ave Maria Emilius Semakafu | Mjumbe | |
| 22. | Bibi. Fatma Abdulhabib Fereji | Mjumbe | |

.........................................................................

Bw. Sisty Leonard Nyahoza

**KATIBU WA KIKOSI KAZI**

## WARATIBU WA KIKOSI KAZI

| Na. | Jina | Jukumu |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Jaji Francis S.K. Mutungi | Msajili wa Vyama vya Siasa, Mratibu wa Kikosi Kazi |
| 2. | Mhe. Mohammed Ali Ahmed | Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Mratibu Msaidizi |

## SEKRETARIETI YA KIKOSI KAZI

| Na. | Jina | Jukumu |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Said Ally Nzori | Mwandishi wa Sheria |
| 2. | Bibi Hollo Steven Kazi | Mtafiti |
| 3. | Bw. Muhidin Salim Mapeyo | Mtafiti |
| 4. | Bibi Grace Dominick Mushi | Mtafiti |
| 5. | Bw. Abdulrazak Said Ali | Mtafiti |
| 6. | Bibi Fatma Haji Mohamed | Mtafiti |
| 7. | Bw. Ally Sabuni Hozza | Mtafiti |
| 8. | Bw. Buhari Mdiliko Seiph | Mtafiti |
| 9. | Bw. Eleuter Medard Mazome | Afisa Mipango na Bajeti |
| 10. | Bw. Alexander Mbogo Munubi | Mhasibu |
| 11. | Bw. Edmund Salvatory Mugasha | Mhasibu |
| 12. | Bibi Khadija Ramadhani Wanjara | Mhasibu |
| 13. | Bw. Eliuter Medard Mazome | Afisa Mipango |
| 14. | Bw. Abuu Muhiddin Kimario | Afisa Habari |
| 15. | Bibi Edna Stephen Assey | Afisa Manunuzi |
| 16. | Bw. Chaddy Anthony Zawuya | Afisa TEHAMA |
| 17. | Bw. Gerald Maregesi Kibanda | Msaidizi wa Mratibu |
| 18. | Bw. Mathias Elieza Mwenesi | Msaidizi wa Mratibu |
| 19. | Bibi Bahati Jumbe Lugome | Katibu Mahsusi |

| | | |
|---|---|---|
| 20. | Bi. Hamida Mohammed Ali | Katibu Mahsusi |
| 21. | Bibi Ummy Omar Gumbo | Mtunza kumbukumbu |
| 22. | Bibi Rose Posta Kayuni | Mtunza kumbukumbu |
| 23. | Bw. Gerald Raymond Mapembe | Mtunza kumbukumbu |
| 24. | Bibi Latifa Said Ahmed | Msaidizi wa Ofisi |
| 25. | Bw. Marco Paul Kazyoba | Msaidizi wa Ofisi |
| 26. | Bw. Mike Nelson Kanyika | Dereva |
| 27. | Bw. Gasper Calolian Mlambo | Dereva |
| 28. | Bw. Baraka Juma Mohammed | Dereva |
| 29. | Bw. Richard Emanuel Richard | Dereva |

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# KIKOSI KAZI CHA MHESHIMIWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KILICHOFANYIA KAZI MASUALA YANAYOHUSU DEMOKRASIA YA VYAMA VINGI VYA SIASA NCHINI

## RIPOTI YA KIKOSI KAZI

## 21 OKTOBA 2022

## YALIYOMO

SURA YA KWANZA ........................................................................................... 1

UTANGULIZI ........................................................................................... 1

1.1 Usuli ........................................................................................... 1

1.2 Dhamira ya Mheshimiwa Rais Kukuza Demokrasia na Maendeleo ............................ 6

SURA YA PILI ........................................................................................... 10

UUNDWAJI NA MAJUKUMU YA KIKOSI KAZI ............................................ 10

2.1 Chimbuko la Kikosi Kazi ........................................................................ 10

2.2 Uundwaji wa Kikosi Kazi ........................................................................ 10

2.3 Uzinduzi wa Kikosi Kazi ........................................................................ 11

2.4 Hadidu Rejea ........................................................................................... 12

2.5 Masuala Yaliyofanyiwa Kazi ................................................................... 13

2.6 Kazi Zilizofanywa na Kikosi Kazi ............................................................ 13

2.7 Ratiba ya Kazi ........................................................................................ 14

2.8 Kuchambua na Kuandaa Maoni na Mapendekezo Kuhusu Suala la Mikutano ya Hadhara na Mikutano ya Ndani ya Vyama Vya Siasa ........................................ 16

2.9 Kukaribisha Maoni ya Ziada ................................................................... 16

2.10 Kuzungumza na Wadau Mbalimbali wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa ... 16

2.11 Kuchambua Maoni ya Wadau na Kuandaa Ripoti ya Kikosi Kazi ............................ 17

SURA YA TATU ........................................................................................... 18

MAMBO YA MSINGI YA KITAIFA ............................................................... 18

3.1 Utangulizi ........................................................................................... 18

3.2 Uhuru wa Kujitawala, Amani, Utulivu na Umoja wa Kitaifa ........................................ 18

3.3 Uwepo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania .......................................................... 20

3.4 Uwepo wa Mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi .................................................... 20

3.5 Utawala wa Sheria ..... 22

3.6 Kazi na Maendeleo ..... 22

3.7 Uhuru na Usawa ..... 23

3.8 Uzalendo ..... 23

3.9 Uadilifu ..... 23

3.10 Hitimisho ..... 24

SURA YA NNE ..... 25

USHINDANI WA KISIASA ..... 25

4.1. Utangulizi ..... 25

4.2. Mikutano ya Hadhara na Mikutano ya Ndani ya Vyama Vya Siasa ..... 26

4.2.1. Maoni ya Wadau ..... 27
4.2.2. Uzoefu wa Nchi Nyingine ..... 28
4.2.3. Mapendekezo ya Kikosi Kazi ..... 28
4.3. Demokrasia Ndani ya Vyama Vya Siasa ..... 28

4.3.1 Maoni ya Wadau ..... 30
4.3.2 Uzoefu wa Nchi Nyingine ..... 31
4.3.3 Mapendekezo ya Kikosi Kazi ..... 31
4.4. Ruzuku Kwa Vyama Vya Siasa ..... 32

4.4.1 Hali Ilivyo Sasa ..... 32
4.4.2 Maoni ya Wadau ..... 34
4.4.3 Uzoefu wa Nchi Nyingine ..... 34
4.4.4 Uchambuzi ..... 36
4.4.5 Mapendekezo ya Kikosi Kazi ..... 37
SURA YA TANO ..... 39

UCHAGUZI ..... 39

5.1 Utangulizi ..... 39

5.2 Mfumo wa Uchaguzi ..... 39

5.2.1. Aina za Mifumo ya Uchaguzi ..... 40
5.2.2. Hali Ilivyo Sasa ..... 42
5.2.3. Mapendekezo ya Tume, Kamati Mbalimbali na Utafiti ..... 42
5.2.4. Maoni ya Wadau ..... 43
5.2.5. Uzoefu wa Nchi Nyingine ..... 44
5.2.6. Mapendekezo ya Kikosi Kazi ..... 44
5.3 Dhana ya Uhuru wa Tume za Uchaguzi ..... 45

5.3.1. Maana ya “Uhuru” wa Tume ya Uchaguzi ..... 45

5.3.2. Uhuru wa Tume ya Uchaguzi ya Tanzania....50
5.4 Uteuzi wa Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi ....53
5.4.1 Hali Ilivyo Sasa ....53
5.4.2 Mapendekezo ya Tume, Kamati Mbalimbali na Hukumu za Mahakama....53
5.4.3 Maoni ya Wadau ....56
5.4.4 Uzoefu wa Nchi Nyingine....57
5.4.5 Mapendekezo ya Kikosi Kazi....59
5.5 Matokeo ya Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kutohojiwa Mahakamani....60
5.5.1 Hali Ilivyo Sasa ....60
5.5.2 Mapendekezo ya Tume na Kamati Mbalimbali....61
5.5.3 Maoni ya Wadau ....61
5.5.4 Uzoefu wa Nchi Nyingine....62
5.5.5 Mapendekezo ya Kikosi Kazi....62
5.6 Watendaji wa Tume ya Uchaguzi ....62
5.6.1 Hali Ilivyo Sasa ....62
5.6.2 Mapendekezo ya Tume na Kamati Mbalimbali....63
5.6.3 Maoni ya Wadau ....64
5.6.4 Uzoefu wa Nchi Nyingine....66
5.6.5 Mapendekezo ya Kikosi Kazi....67
5.7 Bajeti ya Tume ya Uchaguzi....67
5.7.1 Hali Ilivyo Sasa ....67
5.7.2 Mapendekezo ya Tume, Kamati Mbalimbali na Utafiti....68
5.7.3 Maoni ya Wadau ....68
5.7.4 Uzoefu wa Nchi Nyingine....68
5.7.5 Mapendekezo ya Kikosi Kazi....69
5.8 Usimamizi wa Uchaguzi....69
5.8.1 Uwezekano wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa....70
5.8.2 Sheria Zinazosimamia Masuala ya Uchaguzi....76
5.9 Matumizi ya TEHAMA Katika Uchaguzi....77
5.9.1 Hali Ilivyo Sasa ....78
5.9.2 Maoni ya Wadau ....79
5.9.3 Uzoefu wa Nchi Nyingine....79
5.9.4 Mapendekezo ya Kikosi Kazi....80
SURA YA SITA....81
DEMOKRASIA NA UONGOZI ....81
6.1 Utangulizi....81
6.2 Ushiriki wa Wanawake katika Siasa, Demokrasia na Uongozi ....82
6.2.1 Mikataba, Itifaki na Matamko ya Kimataifa Kuhusu Ushiriki wa Wanawake katika Siasa, Demokrasia na Uongozi ....82
6.2.2 Historia ya Ushiriki wa Wanawake Katika Siasa, Demokrasia na Uongozi ....85

6.2.3 Mafanikio Yaliyopatikana katika Kupigania Haki za Wanawake Kushiriki katika Siasa, Demokrasia na Uongozi Nchini ........ 86
6.2.4 Maoni ya Wadau ........ 89
6.2.5 Mapendekezo ya Tume Mbalimbali ........ 92
6.2.6 Uzoefu wa Nchi Nyingine ........ 94
6.2.7 Uchambuzi ........ 94
6.2.8 Mapendekezo ya Kikosi Kazi ........ 97
6.3 Ushiriki wa Watu Wenye Ulemavu katika Siasa, Demokrasia na Uongozi ........ 99
6.3.1 Mikataba, Itifaki na Matamko kuhusu Ushiriki wa Watu Wenye Ulemavu katika Siasa, Demokrasia na Uongozi ........ 99
6.3.2 Historia ya Kupigania Haki za Watu Wenye Ulemavu Kushiriki katika Siasa, Demokrasia na Uongozi ........ 101
6.3.3 Maoni ya Wadau ........ 103
6.3.4 Mapendekezo ya Tume Mbalimbali ........ 105
6.3.5 Uzoefu wa Nchi Nyingine ........ 106
6.3.6 Uchambuzi ........ 107
6.3.7 Mapendekezo ya Kikosi Kazi ........ 108
6.4 Ushiriki wa Vijana katika Siasa, Demokrasia na Uongozi ........ 110
6.4.1. Mapendekezo ya Kikosi Kazi ........ 111
SURA YA SABA ........ 112
ELIMU YA URAIA ........ 112
7.1 Utangulizi ........ 112
7.2 Historia ya Utoaji wa Elimu ya Uraia Nchini ........ 112
7.3 Hali Ilivyo Sasa ........ 113
7.4 Maoni ya Wadau ........ 114
7.4.1 Maoni ya Wadau kuhusu Elimu ya Uraia kwa Ujumla ........ 114
7.4.2 Maoni ya Wadau Kuhusu Elimu ya Mpiga Kura ........ 116
7.5 Mapendekezo ya Tume na Kamati Mbalimbali ........ 117
7.6 Uzoefu Kutoka Nchi Nyingine ........ 117
7.7 Mapendekezo ya Kikosi Kazi ........ 119
SURA YA NANE ........ 120
RUSHWA NA MAADILI KATIKA SIASA NA UCHAGUZI ........ 120
8.1 Utangulizi ........ 120
8.2 Historia ya Mapambano Dhidi ya Rushwa Nchini ........ 121
8.3 Mafanikio Katika Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini ........ 124
8.4 Hali Ilivyo Sasa ........ 125

8.5 Maoni ya Wadau ........................................................................................................ 130

8.5.1 Maoni ya Wadau Kuhusu Kuzuia na Kupambana na Rushwa ........................ 130
8.5.2 Maoni ya Wadau Kuhusu Usimamizi wa Maadili Nchini .................................. 134
8.6 Mapendekezo ya Tume na Kamati Mbalimbali; ........................................................ 135

8.6.1 Mapendekezo ya Tume ya Rais ya Kuchunguza Masuala ya Rushwa (Tume ya Rushwa ya Warioba) ........................................................................................ 135
8.6.2 Kamati ya Kuratibu Maoni Kuhusu Katiba, iliyoongozwa na Mheshimiwa Jaji Robert Kisanga katika taarifa yake ya tarehe 20 Agosti 1999, ilipendekeza masuala yafuatayo katika kukabiliana na tatizo la rushwa nchini: ........................................ 136
8.6.3 Katiba Inayopendekezwa ................................................................................ 137
8.7 Uzoefu wa Nchi Nyingine ............................................................................................ 138

8.8 Mapendekezo ya Kikosi Kazi ........................................................................................ 138

SURA YA TISA ................................................................................................................ 142

MFUMO WA MARIDHIANO ILI KUDUMISHA HAKI, AMANI, UTULIVU NA UMOJA WA KITAIFA ................................................................................................................ 142

9.1 Utangulizi ...................................................................................................................... 142

9.2 Utaratibu wa Maridhiano .............................................................................................. 148

9.3 Mapendekezo ya Tume na Kamati Mbalimbali ............................................................ 149

9.4 Maoni ya Wadau ........................................................................................................... 149

9.5 Uzoefu wa Nchi Nyingine ............................................................................................. 152

9.6 Mapendekezo ya Kikosi Kazi ........................................................................................ 153

SURA YA KUMI ............................................................................................................... 155

MAWASILIANO KWA UMMA, VYOMBO VYA HABARI NA SIASA ............................ 155

10.1 Utangulizi .................................................................................................................... 155

10.2 Hali Ilivyo Sasa ........................................................................................................... 156

10.3 Mafanikio .................................................................................................................... 158

10.4 Maoni ya Wadau ......................................................................................................... 159

10.5 Mapendekezo ya Taasisi Mbalimbali .......................................................................... 163

10.6 Uzoefu Kutoka Nchi Nyingine ..................................................................................... 163

10.7 Mapendekezo ya Kikosi Kazi ...................................................................................... 165

SURA YA KUMI NA MOJA ............................................................................................. 167

KATIBA MPYA.......... 167

11.1 Utangulizi.......... 167

11.2 Michakato Mbalimbali ya Mabadiliko ya Katiba Tanzania (1961-2015).......... 168

11.3 Changamoto Zilizojitokeza katika Juhudi za Kupata Katiba Mpya.......... 171

11.4 Maoni ya Wadau kuhusu Katiba.......... 172

11.4.1. Hakuna Haja ya Katiba Mpya, Katiba ya Sasa Ifanyiwe Marekebisho.......... 173
11.4.2. Kuna Haja ya Kuwa na Katiba Mpya.......... 173
11.5 Uzoefu wa Nchi Nyingine.......... 175

11.5.1 Kenya.......... 175
11.5.2 Afrika ya Kusini.......... 178
11.6 Uchambuzi.......... 179

11.7 Ipo Haja ya Kujadili na Kukubaliana Misingi Mikuu ya Kitaifa Kabla ya Kuanza Mchakato wa Katiba Mpya.......... 181

11.8 Mapendekezo ya Kikosi Kazi.......... 182

SURA YA KUMI NA MBILI.......... 185

HITIMISHO.......... 185

ORODHA YA VIAMBATISHO.......... 187

**USHIRIKI WA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM KATIKA SIASA,**

## ORODHA YA MAJEDWALI

**Jedwali Na. 1:** Matokeo ya Uchaguzi Mkuu 1995 hadi 2020.......... 5

**Jedwali Na. 2:** Ratiba ya kazi zilizofanywa na Kikosi Kazi.......... 15

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli

Tanzania ilitimiza miaka sitini (60) ya Uhuru wa Tanzania Bara, miaka hamsini na saba (57) ya Mapinduzi ya Zanzibar na miaka hamsini na saba (57) ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar Mwaka 2021. Katika kipindi hiki, nchi yetu imepitia katika awamu za uongozi na mifumo mbalimbali iliyokusudia kuimarisha uhuru, umoja, amani, utulivu, demokrasia na utawala bora. Ripoti hii inahusu juhudi zinazoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Sita za kuimarisha na kuboresha mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa na Utawala Bora.

Kabla ya uhuru, chama cha siasa Tanganyika African National Union (TANU) kilichoanzishwa mwaka 1954 kikiongozwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kiliongoza jitihada za kutafuta uhuru wa Tanganyika. Pamoja na TANU kulikuwepo na vyama vya siasa vingine vikiwemo, United Tanganyika Party (UTP) kilichoanzishwa mwaka 1956, African National Congress (ANC) kilichoanzishwa mwaka 1958 na All Muslim National Union of Tanganyika (AMNUT) kilichoanzishwa mwaka 1959 kwa upande wa Tanganyika. Kwa upande wa Zanzibar, kulikuwa na vyama vya siasa vifuatavyo, Afro-Shiraz Party (ASP) kilianzishwa tarehe 5 Februari 1957, Zanzibar and Pemba People’s Party (ZPPP) kilianzishwa mwaka 1959, Zanzibar Nationalist Party (ZNP) kilianzishwa mwaka 1955 na Chama cha Umma kilianzishwa

mwaka 1962. Vyama hivi vinadhihirisha kuwepo kwa mfumo wa demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa hata kabla ya uhuru. Tarehe 9 Desemba 1961 Tanganyika ilifanikiwa kupata uhuru wake kutoka kwa utawala wa kikoloni wa Uingereza na hivyo kuendelea na mfumo wa demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa baada ya uhuru, ambapo mfumo huo ulitamkwa katika Katiba ya Uhuru (Independent Constitution of 1961). Tarehe 9 Desemba 1962 Tanganyika ilipata Katiba Mpya, ambayo iliitangaza Tanganyika kuwa Jamhuri.

Tarehe 12 Januari 1964, chama cha siasa Afro-Shiraz Party (ASP), kikiongozwa na Sheikh Abeid Amani Karume, kiliongoza wananchi wa Zanzibar kufanya Mapinduzi na kuunda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Baada ya Mapinduzi Vyama vya Siasa vingine pamoja na asasi za kiraia vilipigwa marufuku.

Tarehe 26 Aprili 1964 Tanganyika na Zanzibar ziliungana na kuwa nchi moja inayoitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muungano huo wa nchi mbili, umedumu kwa miaka zaidi ya hamsini, hivyo ni muungano pekee hai katika bara la Afrika. Hata hivyo, kuna changamoto kadhaa katika Muungano huo ambazo zimekuwa zikifanyiwa kazi na kupungua siku hadi siku.

Baada ya Muungano kulikuwa na Katiba ya Muda ya Muungano inayoitwa “The Interim Constitution of the United Republic of Tanganyika and Zanzibar of 1964”, na mwaka 1965 ikatungwa Katiba Mpya ya Mpito inayoitwa “The Interim Constitution of Tanzania of 1965)”, iliyodumu hadi mwaka 1977. Katiba ya mwaka 1965 ilifuta mfumo wa vyama vingi vya siasa na kuanzisha mfumo wa chama kimoja cha siasa mwaka huo huo. Aidha, mwaka1967

lilitangazwa Azimio la Arusha ambalo liliweka misingi ya maendeleo ya uchumi na ustawi wa jamii katika mrengo wa ujamaa na kujitegemea na kuimarisha mfumo wa chama kimoja.

Mwaka 1977 vyama viwili vya siasa ASP na TANU viliungana na kuunda Chama cha Mapinduzi (CCM). Sambamba na hilo, ilitungwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 iliyoanza kutumika tarehe 26 Aprili 1977. Mwaka 1992, Serikali ya Awamu ya Pili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliunda Tume ya Rais ya Kukusanya Maoni Kuhusu Chama Kimoja au Vyama Vingi vya Siasa na kufanyika kwa Mabadiliko ya Nane ya Katiba yaliyorejesha mfumo wa vyama vingi vya siasa Tanzania. Sababu za mfumo huo kurejea ni hizi zifuatazo:

a) vuguvugu la mabadiliko ya kisiasa duniani, ambapo kulikuwa na msukumo wa nchi mbalimbali kutoka katika mfumo wa uchumi hodhi na siasa za kijamaa na kuelekea katika mfumo wa uchumi huria na demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa; na
b) msukumo wa ndani ya nchi wa kudai mabadiliko ya kiuchumi na kisiasa, kutokana na hali ngumu ya kiuchumi iliyokuwepo katika miaka ya themanini.

Baada ya mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa kurejea mwaka 1992, Vyama vya Siasa vimekuwa vikifanya jitihada za kutafuta wanachama, kunadi sera zao kupitia mikutano ya hadhara, kujiimarisha kitaasisi kupitia mikutano ya ndani na kuweka mifumo mbalimbali ya kiutawala. Hatimaye, vyama hivi vilianza kushiriki Uchaguzi Mkuu na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kutafuta uongozi wa kisiasa. Tangu mwaka 1992 mpaka mwaka 2015 kulifanyika

uchaguzi mkuu mara tano. Matokeo ya uchaguzi katika kipindi hicho yalionesha kukua kwa hali ya ushindani.

**Jedwali Na. 1:** *Matokeo ya Uchaguzi Mkuu 1995 hadi 2020*

| **Na.** | **Mwaka** | **Chama** | **Idadi ya Viti vya Ubunge** | **Asilimia** | **Idadi ya Kura za Urais** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1995 | CCM | 186 | 80.17 | 4,026,422 | 61.8 |
| | | Vyama vya Upinzani | 46 | 19.83 | 2,486,323 | 38.0 |
| 2 | 2000 | CCM | 202 | 87.45 | 5,863,201 | 71.50 |
| | | Vyama vya Upinzani | 29 | 12.55 | 2,309,083 | 28.50 |
| 3 | 2005 | CCM | 206 | 70.0 | 9,123,952 | 80.30 |
| | | Vyama vya Upinzani | 26 | 30.0 | 2,241,525 | 19.70 |
| 4 | 2010 | CCM | 186 | 60.04 | 5,275,899 | 61.16 |
| | | Vyama vya Upinzani | 53 | 39.96 | 3,122,709 | 38.84 |
| 5 | 2015 | CCM | 195 | 73.86 | 8,882,935 | 58.46 |
| | | Vyama vya Upinzani | 69 | 26.14 | 6,310,927 | 41.54 |
| 6 | 2020 | CCM | 256 | 96.97 | 12,516,252 | 84.40 |
| | | Vyama vya Upinzani | 8 | 3.03 | 2,313,943 | 15.60 |

**Chanzo:** *Taarifa za Tume ya Taifa ya Uchaguzi za Mwaka 1995 - 2020*

Baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, kulikuwa na matukio kadhaa katika muktadha wa ushindani wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini. Kwanza, kulikuwa na mchakato wa kupata Katiba Mpya ambao haukukamilika. Pili, mwaka 2016 Vyama vya

Siasa vilizuiwa kufanya mikutano ya hadhara, isipokuwa Wabunge na Madiwani katika majimbo na kata zao.

Tatu, kulifanyika marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258, Sheria ya Makosa ya Kimtandao Sura ya 443, Sheria ya Takwimu Sura ya 351 na kutungwa kwa Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari Sura 229 na Sheria ya Asasi Zisizo za Kiserikali Sura ya 56. Kwa upande wa Zanzibar, ilitungwa Sheria ya Uchaguzi Namba 4 ya Mwaka 2018 na kufuta Sheria ya Uchaguzi Namba 11 ya Mwaka 1984. Marekebisho haya yalilalamikiwa na Vyama vya Upinzani na wadau wengine wa demokrasia.

Nne, kiuchumi, Tanzania ilifanikiwa kuingia katika kundi la nchi za uchumi wa kati wa chini. Licha ya mafanikio hayo, mwaka 2019 kasi ya ukuaji wa uchumi ilipungua kutokana na athari za UVIKO-19 ambazo ziliathiri ukuaji wa uchumi wa dunia nzima.

Tano, matokeo ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ulionesha kupungua kwa ushindani wa kisiasa. Aidha, kulikuwa na malalamiko kadhaa kutoka kwa Vyama vya Siasa na wadau wengine wa demokrasia nchini.

## 1.2 Dhamira ya Mheshimiwa Rais Kukuza Demokrasia na Maendeleo

Baada ya kushika hatamu za uongozi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, aliweka bayana dhamira yake ya kukuza demokrasia na kuongeza kasi ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Dhamira hii

aliiweka wazi tarehe 22 Aprili 2021 alipolihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jijini Dodoma. Rais aliahidi "*kudumisha Tunu za Taifa letu, yaani amani, umoja na mshikamano, uhuru wa nchi yetu, Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, pamoja na Muungano wetu*." Mheshimiwa Rais alisisitiza nia yake ya kulinda misingi ya demokrasia na uhuru wa watu na vyombo vya habari. Alieleza kuwa "*Uhuru na demokrasia ni msingi wa amani katika nchi na pia vinasaidia kuchochea maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii*…". Vilevile, alieleza nia yake ya kukutana na viongozi wa vyama vya siasa Tanzania, ili kwa pamoja kuweka mwelekeo wa kuendesha shughuli za kisiasa zenye tija na maslahi ya nchi.

Tarehe 15 Septemba 2022 wakati wa kusheherekea Siku ya Demokrasia Duniani, Mheshimiwa Rais alirejea kusisitiza umuhimu wa uhuru wa watu ikiwemo, uhuru wa kutoa maoni, uhuru wa kukusanyika au kujiunga kwenye vikundi. Kuhusu masuala ya jinsia, aliahidi kuwa Serikali itajitahidi kushughulikia masuala ya haki za Wanawake, usawa wa jinsia, ili kukuza demokrasia nchini. Kuhusu masuala ya uchaguzi, alieleza umuhimu wa kutoa elimu na kuwahamasisha Wanawake kujitokeza zaidi kugombea nafasi mbalimbali. Vilevile, alisisitiza umuhimu wa kusimamia utekelezaji wa sheria kwa weledi, ili sheria zisitumike kuwanyima watu haki kwa masuala ya kiufundi.

Tarehe 1 Julai 2022 Tanzania iliadhimisha miaka 30 tangu kurejea kwa Mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa. Wakati wa maadhimisho hayo, Mheshimiwa Rais alisisitiza tena dhamira yake ya kukuza demokrasia nchini kupitia makala maalum aliyoiandaa ambapo alieleza kuwa "*nimedhamiria kwamba kwenye kuenzi*

*miaka yetu ya demokrasia ya vyama vingi, Serikali yangu itajitahidi kufanya mabadiliko katika mifumo ya kisiasa, kiuchumi na katika sheria za uchaguzi*." Aidha, Mheshimiwa Rais alieleza falsafa yeke kuongoza nchi iliyojengwa katika misingi minne, aliyoipa jina "4Rs" ambayo ni "*Reconciliation, Resilience, Reforms and Rebuilding"* ikiwa na maana ya Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Ujenzi Mpya wa Taifa.

Mheshimiwa Rais ameanza kutekeleza kwa vitendo dhamira yake ya kuboresha hali ya demokrasia na utawala bora nchini kwa kufanya mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

a) kuanzisha mazungumzo baina ya Serikali, chama tawala CCM na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) yenye lengo la kufikia maridhiano kuhusu masuala ya kidemokrasia;
b) kukutana na kufanya mazungumzo na baadhi ya viongozi wa kitaifa wa Vyama vya Siasa, viongozi wa dini, viongozi wa Serikali wastaafu na machifu kwa lengo la kubadilishana mawazo kuhusu namna ya kuboresha na kudumisha Mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa;
c) kufungulia vyombo vya habari kadhaa vilivyokuwa vimefungiwa kufanya kazi zake;
d) kuliasa Jeshi la Polisi kufanya kazi kwa weledi ikiwemo kutenda haki; na
e) tarehe 15 Desemba 2021 alifungua Mkutano wa Wadau wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa, uliojadili hali ya demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini na kuunda Kikosi Kazi cha kuchambua maoni yaliyotolewa katika

mkutano huo na kuandaa mapendekezo ya kuwasilisha serikalini.

Mfumo wa utawala wa nchi yetu upo imara na umewezesha nchi kuendelea kuwa salama, yenye amani, utulivu na kudumisha mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa. Pia, nchi yetu imekuwa na awamu za uongozi na mifumo mbalimbali iliyokusudia kuimarisha masuala hayo. Juhudi zinazofanywa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Sita ni za muhimu, kwa sababu zinalenga kudumisha na kuboresha maslahi mapana ya Watanzania na Taifa letu.

Hivyo basi uamuzi wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuelekeza hatua mbalimbali zichukuliwe ni wa kupongezwa. Hii ni pamoja na kuundwa kwa Kikosi Kazi hiki ili pamoja na mambo mengine, malalamiko kutoka kwa baadhi ya wanasiasa juu ya utaratibu wa shughuli za kisiasa ufanyiwe kazi kwa lengo la kukuza demokrasia na kuongeza kasi ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa nchini.

# SURA YA PILI

# UUNDWAJI NA MAJUKUMU YA KIKOSI KAZI

## 2.1 Chimbuko la Kikosi Kazi

Tarehe 15 hadi 17 Desemba 2021 kulifanyika Mkutano wa Wadau wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa Jijini Dodoma ulioitwa "Mkutano wa Wadau wa Kujadili Hali ya Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa nchini Tanzania". Mkutano huo ulijadili mafanikio na changamoto zilizopo katika suala la demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini. Mkutano ulifunguliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufungwa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Katika mkutano huo, masuala mengi yanayohusu Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa yalijadiliwa na washiriki walitoa maoni na mapendekezo ambayo idadi yake ilifikia tisini na nane (98). Kutokana na wingi wa maoni na mapendekezo hayo na kiu ya washiriki wa mkutano huo kuona yanafanyiwa kazi, washiriki wa mkutano huo waliazimia kwamba kiundwe Kikosi Kazi cha kuchambua na kuandaa mapendekezo ya kuwasilishwa Serikalini.

## 2.2 Uundwaji wa Kikosi Kazi

Kikosi Kazi kiliundwa na Msajili wa Vyama vya Siasa tarehe 23 Desemba 2021, kikiwa na wajumbe ishirini na nne (24), kati ya hao, kumi na sita (16) wanatoka Tanzania Bara wanane (8) wanatoka Tanzania Zanzibar. Baada ya Kikosi Kazi kuanza kazi, mjumbe Bibi

Christine Solomon Mndeme, Naibu Katibu Mkuu wa CCM alibadilishwa na nafasi yake ilichukuliwa na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Uundwaji wa Kikosi Kazi ulizingatia uwakilishi wa wadau waliohudhuria Mkutano wa Wadau wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa uliofanyika tarehe 15 hadi 17 Desemba 2021 Dodoma. Hivyo, muundo wake unajumuisha aina za wadau wafuatao: Wasomi, Wanasiasa, Vyama vya Siasa, Asasi za Kiraia, Taasisi za Dini, Taasisi za Serikali na Vyama vya Kitaaluma.

**2.3 Uzinduzi wa Kikosi Kazi**

Kikosi Kazi kilizinduliwa tarehe 10 Januari 2022 Zanzibar na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hafla ya uzinduzi ilihudhuriwa na Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, pamoja na viongozi wengine wa Serikali, viongozi wa dini, viongozi wa taasisi za kiraia, wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Baraza la Vyama vya Siasa, viongozi wa Vyama vya Siasa Wanawake na wanahabari.

Katika hotuba ya uzinduzi wa Kikosi Kazi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alisisitiza kudumishwa kwa utamaduni wa kukaa pamoja kujadili masuala muhimu ya maendeleo. Aidha, alisisitiza kudumishwa kwa mafanikio ambayo nchi yetu imeyapata katika miaka 30 ya demokrasia ya vyama vingi vya siasa na kufanyia kazi

changamoto zilizopo. Aliwaasa wajumbe wa Kikosi Kazi kutumia hekima, busara, uzalendo na uzoefu wao katika utekelezaji wa majukumu yao. Vilevile, aliahidi kwamba, Serikali zote mbili zitatoa ushirikiano kwa Kikosi Kazi ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

### 2.4 Hadidu Rejea

Wakati wa uzinduzi, Kikosi Kazi kilipewa hadidu rejea zifuatazo:

1. Kupitia hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyoitoa wakati akifungua Mkutano wa Wadau wa Kujadili Hali ya Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa Nchini, uliofanyika tarehe 15 hadi 17 Desemba 2021 na hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wakati akifunga mkutano huo, na kuainisha masuala ya kufanyiwa kazi;
2. Kupitia na kuchambua maoni yaliyotolewa na washiriki wa mkutano na kuandaa mapendekezo ya kuwasilishwa Serikalini;
3. Kupendekeza namna bora ya kutekeleza haki ya vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara, bila kukiuka Sheria na maadili ya nchi yetu; na
4. Kupendekeza utaratibu wa kudumisha utamaduni wa wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa kukaa pamoja na kuzungumza, kwa lengo la kupata suluhisho la changamoto zinapojitokeza.

## 2.5 Masuala Yaliyofanyiwa Kazi

Baada ya uchambuzi wa kina wa hotuba ya kufungua na kufunga mkutano pamoja na maoni ya wadau yaliyotolewa katika Mkutano wa Wadau wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa wa tarehe 15 hadi 17 Desemba 2021, Kikosi Kazi kiliainisha masuala tisa (9) ya kufanyia kazi yafuatayo:

1. Mikutano ya hadhara na Mikutano ya ndani ya Vyama vya Siasa;
2. Masuala yanayohusu Uchaguzi;
3. Mfumo wa maridhiano ili kudumisha haki, amani, utulivu na Umoja wa kitaifa;
4. Ushiriki wa Wanawake na Makundi Maalum katika siasa na Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa;
5. Elimu ya Uraia;
6. Rushwa na Maadili katika Siasa na Uchaguzi;
7. Ruzuku ya Serikali kwa Vyama vya Siasa;
8. Uhusiano wa Siasa na Mawasiliano kwa Umma; na
9. Katiba Mpya.

## 2.6 Kazi Zilizofanywa na Kikosi Kazi

Baada ya uzinduzi, Kikosi Kazi kilianza kazi tarehe 11 Januari 2022. Mpaka kuwasilishwa kwa Ripoti hii, Kikosi Kazi kimefanya kazi zifuatazo:

a) kupitia hadidu rejea;

b) kuchambua hotuba ya kufungua, kufunga, maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika mkutano wa wadau na kuainisha masuala muhimu ya kufanyiwa kazi;

c) kuandaa Mpango Kazi wa kufanyia kazi masuala tisa (9) yaliyoanishwa;

d) kuchambua na kuandaa maoni na mapendekezo kuhusu suala la mikutano ya hadhara na mikutano ya ndani ya Vyama vya Siasa;

e) kuandaa taarifa ya awali ya Kikosi Kazi iliyowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 12 Machi 2022;

f) kukaribisha maoni ya wadau;

g) kutoa maoni kwa Serikali kuhusu utungaji wa Kanuni za kuratibu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa;

h) kuzungumza na wadau mbalimbali wa demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa kwa upande wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ili kupata maoni yao; na

i) kuchambua maoni ya wadau na kuandaa ripoti ya Kikosi Kazi.

### 2.7 Ratiba ya Kazi

Baada ya kuzinduliwa tarehe 10 Januari 2022, Kikosi Kazi kilianza kazi tarehe 11 Januari 2022 na kukamilisha kazi ya kuandaa Ripoti tarehe 20 Oktoba 2022.

**Jedwali Na. 2:** *Ratiba ya kazi zilizofanywa na Kikosi Kazi*

<table>
<tr><th>Na.</th><th>Muda</th><th>Suala</th><th>Mahali</th></tr>
<tr><td>1</td><td>11 Januari 2022</td><td>Kujadili Hadidu Rejea kupata uelewa wa pamoja</td><td>Zanzibar</td></tr>
<tr><td>2</td><td>16 hadi 26 Januari 2022</td><td>Kuchambua maoni ya Mkutano wa Wadau wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa uliofanyika Dodoma na kuandaa masuala tisa ya kufanyia kazi</td><td>Dar-es salaam</td></tr>
<tr><td>3</td><td>27 Aprili hadi 12 Agosti 2022</td><td rowspan="2">Kupokea maoni na mapendekezo zaidi kutoka kwa wadau mbalimbali kwa njia ya mazungumzo na maandishi na kuandaa taarifa za kamati.</td><td>Dar-es salaam</td></tr>
<tr><td>4</td><td>15 Agosti hadi 3 Septemba 2022</td><td>Zanzibar (Unguja na Pemba)</td></tr>
<tr><td>5</td><td>5 Septemba hadi 18 Oktoba 2022</td><td>Kufanya uchambuzi wa masuala yanayofanyiwa kazi na kuandaa Ripoti ya Kikosi Kazi</td><td>Dar-es salaam</td></tr>
<tr><td>6</td><td>21 Oktoba 2022</td><td>Kuwasilisha Ripoti kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania</td><td>Ikulu, Dar es Salaam</td></tr>
</table>

### 2.8 Kuchambua na Kuandaa Maoni na Mapendekezo Kuhusu Suala la Mikutano ya Hadhara na Mikutano ya Ndani ya Vyama Vya Siasa.

Kikosi Kazi kilifanyia kazi suala la mikutano ya hadhara na mikutano ya ndani ya vyama vya siasa na kuwasilisha maoni na mapendekezo yake kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 12 Machi, 2022.

### 2.9 Kukaribisha Maoni ya Ziada

Tarehe 14 Aprili, 2022 Kikosi Kazi kilitoa taarifa kwa umma kupitia vyombo vya habari, kualika watanzania wote kuwasilisha maoni na mapendekezo kuhusu masuala tisa (9) yanayofanyiwa kazi, kwa njia mbalimbali ikiwemo, “WhatsApp” kupitia namba ya simu ya Katibu, barua pepe taskforcemaoni@orpp.go.tz, anuani ya posta ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na kuzungumza na wajumbe wa Kikosi Kazi ana kwa ana. Lengo lilikuwa ni kukaribisha maoni ya ziada kutoka kwa wadau, ili kupata mtazamo mpana kuhusu masuala tisa yanayofanyiwa kazi.

### 2.10 Kuzungumza na Wadau Mbalimbali wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa

Kuanzia tarehe 27 Aprili, 2022 hadi tarehe 9 Septemba, 2022, Kikosi Kazi kilikutana na jumla ya wadau 107 ikiwa ni watu binafsi na viongozi wa taasisi mbalimbali, kwa ajili ya kupata maoni zaidi na ufafanuzi wa maoni yaliyokwisha wasilishwa.

## 2.11 Kuchambua Maoni ya Wadau na Kuandaa Ripoti ya Kikosi Kazi.

Baada ya kupata maoni ya wadau, Kikosi Kazi kilifanya kazi ya kuyachambua maoni. Uchambuzi ulifanywa kwa utaratibu ufuatao:

a.) kugawa maoni katika masuala tisa muhimu;

b.) kuunda kamati nne za kuchambua maoni hayo na kuandaa mapendekezo;

c.) kupitia nyaraka mbalimbali na kupata ushauri wa kitaalam;

d.) kufanya majadiliano ndani ya kamati za Kikosi Kazi, ili kubadilishana mawazo na kufikia makubaliano;

e.) kuandaa Kamati za Uandishi wa rasimu ya ripoti, ambazo kila moja ilipewa kazi ya kuandaa sura husika na kuwasilisha rasimu katika kikao cha Kikosi Kazi;

f.) kupitia rasimu za ripoti za kamati, kujadiliana na kukubaliana kuhusu masuala mapya yaliyojitokeza katika Kamati za Uandishi;

g.) Kamati ya Uandishi wa Ripoti nzima kuandaa rasimu ya ripoti kamili na kuiwasilisha kwa Kikosi Kazi kwa ajili ya kupitiwa na kujiridhisha kuhusu makubaliano yaliyofikiwa.

# SURA YA TATU

# MAMBO YA MSINGI YA KITAIFA

## 3.1 Utangulizi

Kihistoria taifa lolote lenye mafanikio endelevu hujengwa katika msingi wa kitaifa unaojumuisha uhuru wa kujitawala, umoja, uzalendo, uadilifu, uwajibikaji, utawala wa sheria, haki na utendaji kazi. Msingi huu huheshimika na kuenziwa na wananchi wa nchi husika. Hivyo, Sura hii inabainisha masuala ya msingi ambayo jamii ya Watanzania inapaswa kuyazingatia ili kufikia malengo yake.

## 3.2 Uhuru wa Kujitawala, Amani, Utulivu na Umoja wa Kitaifa

Uhuru uliopatikana Tanganyika mwaka 1961 na Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964, ni matokeo ya mapambano yaliyokuwa na lengo kuu la kutaka kujinasua kutoka katika tawala dhalimu na kandamizi za kikoloni, ili kujitawala na kuleta maendeleo na ustawi wa jamii. Katika kufanikisha malengo yao, hususani unyonyaji wa kiuchumi, wakoloni walilazimika kuanzisha dola ya kisiasa, ili kuwatawala Waafrika. Utawala wa dola ya kikoloni uliwagawa Waafrika kwa misingi ya ukabila, ukanda, dini, jinsia na kuwakandamiza katika nyanja za siasa, uchumi na kijamii. Hivyo, harakati za ukombozi za kudai uhuru zililenga kuanzisha utawala wa Wananchi wenyewe na kuwaletea maendeleo.

Ripoti ya TANU ya Mwaka 1965 ilieleza kuwa, mataifa mapya kama Tanganyika, yanapata uhuru wao baada ya mapambano dhidi ya ukoloni. Mapambano haya yanawaunganisha watu wote katika taifa

na kuondoa tofauti miongoni mwao. Wapigania uhuru baada ya kuondosha ukoloni huunda Serikali katika nchi zao. Jukumu kubwa la Serikali mpya ni kuwaletea wananchi maendeleo ya kiuchumi na kijamii, ikiwemo kuondoa umaskini, ujinga na maradhi.

Katika Hotuba yake, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati akifungua mkutano wa wadau uliojadili hali ya demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini tarehe 15 Desemba 2021, alisisitiza kuhusu uhuru wa kujitawala pamoja na umoja wa kitaifa, ambapo alisema kuwa:- "*Hata hivyo, nitumie fursa hii kuwakumbusha kwamba, duniani kuna nchi moja tu inayoitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo ni Taifa huru lililojengwa katika misingi ya amani, upendo, mshikamano na linaongozwa kwa misingi ya Katiba na Sheria zilizotungwa na Bunge na sio utashi wa mtu au utashi wa mataifa mengine. Na wenye hilo taifa ni sisi tulioko hapa. Uendeshaji wa hili Taifa utatokana na sisi tuliopo hapa*."

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inasisitiza kuwa, uhuru wa kujitawala, umoja wa kitaifa, mshikamano wa kijamii, amani na utulivu ni nguzo muhimu katika kuleta maendeleo. Kwa kuwa mambo haya yamejengwa kwa muda mrefu na ndio yanaweka mazingira ya uimara wa Taifa na hivyo kuwa nguzo ya maendeleo, ni muhimu sana yakaendelezwa na kulindwa. Hadi sasa, tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa, kwa kiasi kikubwa Tanzania imeendelea kuwa ni nchi ya amani duniani. Mfano, Global Peace Index (2021) inaonesha Tanzania ipo nafasi ya kwanza kwa kuwa na amani katika nchi za Afrika Mashariki, ya saba (7) Bara la Afrika na ya Hamsini na Nane (58) duniani, kati ya nchi 163. Mifarakano katika baadhi ya nchi za Afrika na duniani, imesababisha kupotea

kwa maisha ya watu, mali na hatimaye nchi hizo kushindwa kuendelea kiuchumi na kijamii. Hivyo basi, maendeleo na ustawi wa Taifa yanategemea uwepo wa uhuru wa kujitawala, amani, utulivu na umoja wa kitaifa.

### 3.3 Uwepo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianzishwa tarehe 26 Aprili, 1964, kutokana na Muungano wa nchi mbili za Tanganyika na Zanzibar. Ibara ya 1 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Mwaka 1977 inatamka uwepo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tafiti mbalimbali, taarifa za Tume na Kamati, machapisho ya kitaaluma na maoni ya wadau waliofika mbele ya Kikosi Kazi, yanasisitiza umuhimu wa kuuenzi na kuudumisha Muungano wa Tanzania. Baadhi ya faida za Muungano zinazotajwa na wadau hao ni kwamba, Muungano unasaidia kuimarisha umoja wa kitaifa, amani na utulivu; kuleta maendeleo ya kiuchumi; kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi; kuenzi waasisi wa Taifa letu; kudumisha udugu wa wananchi wa pande zote mbili za Muungano na kuboresha huduma za jamii.

### 3.4 Uwepo wa Mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi

Mwaka 1992, Tanzania ilirejesha mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa. Uamuzi huu ulizingatia mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Rais ya Mfumo wa Chama Kimoja au Vyama Vingi vya Siasa, chini ya Mwenyekiti wake Jaji Francis Nyalali. Pamoja na mapendekezo ya wananchi walio wengi (takribani asilimia 77.2) ya kutaka mfumo wa chama kimoja cha siasa uendelee na wananchi

wachache (takribani asilimia 21.5) kutaka mfumo wa vyama vingi urejeshwe, Tume hiyo kwa kuzingatia mazingira na hali ya kisiasa ilivyokuwa, ilipendekeza kurejeshwa kwa Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa. Mfumo huu unatoa fursa pana kwa wananchi kushiriki katika demokrasia na utawala wa nchi. Ibara ya 3 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 pamoja na mambo mengine inaeleza kuwa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa. Utafiti wa Afrobarometer wa mwaka 2019 unabainisha kuwa, asilimia 78 ya Watanzania walioshiriki katika utafiti huo, wanapendelea mfumo wa demokrasia kuliko mfumo mwingine wowote wa kiutawala na asilimia 69 hawakubali mfumo wa Serikali ya chama kimoja. Utafiti huu unaonesha bayana kuwa, mfumo wa demokrasia ndio unakubalika kuendesha siasa za nchi. Katika mfumo huu wananchi wana uhuru wa kujieleza, kukusanyika, kubadilishana mawazo na kushiriki katika utawala wa nchi.

Katika Hotuba yake, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati akifungua mkutano wa wadau uliojadili hali ya demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa nchini Tanzania tarehe 15 Desemba 2021, alisisitiza uwepo wa mfumo wa demokrasia ya vyama vingi na malengo yake ya msingi. Mheshimiwa Rais alieleza kuwa:- “*Mwaka 1992 tulirejesha mfumo wa demokrasia ya vyama vingi, kwa nia njema ya kupanua wigo wa demokrasia, lakini pia kwenda sambamba na mfumo wa ulimwengu kwa wakati huo. Aidha, tulifanya hivyo kwa kuruhusu kuwepo kwa ushindani wa fikra, itikadi na sera ili kuwapa wananchi chaguo pana zaidi na fursa pana ya kuchangia mawazo ya namna bora ya kuongoza nchi hii na kuwaletea wananchi maendeleo*...” Hivyo basi,

mfumo wa demokrasia ya vyama vingi ni kichocheo cha kuleta maendeleo katika Taifa, endapo wadau husika watatimiza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria za Nchi na wanaweka maslahi ya Taifa mbele.

### 3.5 Utawala wa Sheria

Utawala wa Sheria ni nguzo mojawapo ya utawala bora. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ina masharti ya jumla na mahsusi kuhusu masuala ya utawala bora. Utawala uliojengwa katika misingi ya demokrasia, unathamini Sheria kama nyenzo ya kuendesha shughuli za nchi. Katika hali hiyo, hakuna aliye juu ya Sheria. Mhimili wa Mahakama ndicho chombo kilichoundwa kutoa haki kwa kutoa tafsiri ya sheria. Utawala wa sheria husimamia haki na kuleta usawa kwa mujibu wa sheria.

### 3.6 Kazi na Maendeleo

Taifa lolote haliwezi kuendelea bila watu wake kufanya kazi. Kazi ndio msingi mkuu wa maendeleo katika jamii yoyote. Kazi ni moja ya nguzo muhimu inayozaa utajiri wa mali katika jamii. Kila mtu anao wajibu wa kufanya kazi halali ya uzalishaji mali au kutoa huduma, kwa kujituma na uaminifu. Hivyo, kila mtu ni lazima atambue na kuamini kuwa, maendeleo ya mtu, kikundi na Taifa, yataweza kufikiwa endapo kila mtu atafanya kazi kwa bidii na uaminifu.

### 3.7 Uhuru na Usawa

Binadamu wote huzaliwa huru na wote ni sawa. Hivyo basi, kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake. Watu wote ni sawa na wanayo haki ya kutobaguliwa na sheria. Watu wasibaguliwe kwa misingi ya utaifa wao, kabila, mahali wanapotoka, maoni yao ya kisiasa, rangi, dini, jinsi au hali yao ya Maisha.

### 3.8 Uzalendo

Uzalendo ni hali ya mtu kuipenda, kuithamini na kujitoa kwa ajili ya nchi yake. Mzalendo huweka maslahi ya taifa mbele kuliko maslahi yake binafsi. Hivyo, mzalendo huilinda nchi yake dhidi ya maadui kwa kujitoa mhanga na ikibidi kufa kwa ajili ya kuitetea nchi yake. Wazalendo wanaijua jamii yao, historia, mila, desturi na tamaduni zao. Hivyo, uzalendo ni utambulisho wa utaifa.

### 3.9 Uadilifu

Uadilifu ni nguzo muhimu kwa taifa lolote, kwani ni msingi wa kukataa vitendo visivyofaa katika jamii. Vitendo hivyo ni kama vile, rushwa, ubaguzi, unyanyasaji na kutokuwajibika. Uadilifu husaidia mtu kuwa muaminifu, kujizuia na tamaa, kujiheshimu, kujituma na kutekeleza majukumu kwa weledi. Uadilifu hurahisisha na kuharakisha upatikanaji wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii, kutokana na wananchi kufanya kazi kwa kujituma, uaminifu na weledi.

### 3.10 Hitimisho

Uhuru wa Kujitawala, Amani, Utulivu na Umoja wa Kitaifa, Uwepo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Uwepo wa Mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa, Utawala wa Sheria, Kazi na Maendeleo, Uhuru na Usawa, Uzalendo na Uadilifu ni mambo ya msingi yanayopaswa kuwekewa mkazo kwa wananchi wa kawaida na viongozi katika nchi yetu, kuyafahamu na kuyazingatia katika maisha yao na kazi zao za kila siku. Masuala haya yanasaidia, kudumisha mazingira ya kuwaweka Watanzania pamoja, kuienzi misingi ya demokrasia ya vyama vingi vya siasa na kuharakisha maendeleo ya Taifa.

Katika ujenzi wa msingi wa Taifa, matarajio ya wananchi wengi, ambayo katika nchi nyingine huitwa ndoto ya Taifa, ni muhimu sana kuzingatiwa. Watanzania kama ilivyo kwa baadhi ya nchi, wanapaswa kuifahamu na kujitahidi kuifikia ndoto ya Taifa letu, ili kurahisisha na kuharakisha maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Hivyo, mchakato wa kuandaa dira mpya ya maendeleo ya Taifa baada ya dira ya sasa (Vision 2025) kuisha na mchakato wa kupata Katiba Mpya, itumike kubainisha ndoto ya Taifa.

# SURA YA NNE

# USHINDANI WA KISIASA

## 4.1. Utangulizi

Sura hii inajumuisha sheria zinazosimamia na kuratibu shughuli za Vyama vya Siasa, mikutano ya hadhara na mikutano ya ndani ya Vyama vya Siasa, demokrasia ndani ya Vyama vya Siasa na ruzuku kwa Vyama vya Siasa. Usimamizi na uratibu wa ushindani wa kisiasa kwa Vyama vya Siasa hufanyika kabla ya uchaguzi, wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi. Masuala haya ni miongoni mwa maeneo ambayo idadi kubwa ya wadau waliokutana na Kikosi Kazi waliyatolea maoni na mapendekezo.

Katika mfumo wa demokrasia, mamlaka ya kuongoza nchi hutokana na wananchi, kwa kuchagua viongozi wa kuwaongoza. Katika nchi yetu, viongozi wa kisiasa hupatikana kupitia uchaguzi unaohusisha wagombea waliodhaminiwa na Vyama vya Siasa. Aidha, Vyama vya Siasa vinawajibu wa kunadi sera zao ili kupata uungwaji mkono kutoka kwa wananchi, ikiwemo kupata wanachama na kushinda uchaguzi. Hivyo, ili Vyama vya Siasa vifanye kazi zao kwa ufanisi, vinahitaji mazingira wezeshi ya kisheria. Vilevile, vinawajibu wa kutii sheria, kanuni na miiko iliyokubalika kwa wote, ili kuwa na uwanja sawa wa ushindani.

Mwaka 2022 Tanzania imetimiza miaka thelathini (30) tangu kurejea kwa Mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa. Katika kipindi hicho kumekuwa na mafanikio makubwa katika ujenzi wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa. Vile vile kumekuwa na

changamoto mbalimbali zinazoathiri ukuaji endelevu wa mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa.

## 4.2. Mikutano ya Hadhara na Mikutano ya Ndani ya Vyama Vya Siasa

Mikutano ya ndani na mikutano ya hadhara ya Vyama vya Siasa, ni nyenzo muhimu katika kuimarisha na kuendeleza ushindani miongoni mwa Vyama vya Siasa. Mikutano hii inasaidia vyama vya siasa kunadi sera zake, ili kupata uungwaji mkono na wananchi kwa lengo la kuongeza wanachama, kushawishi mabadiliko ya sera na sheria, na kushinda uchaguzi. Aidha, mikutano ya ndani ya vyama vya siasa ni mikutano ya kikatiba, inayoandaliwa na chama cha siasa husika kwa mujibu ya katiba yake, kwa lengo la kuimarisha masuala ya kiutawala na uongozi wa chama.

Mikutano ya hadhara na mikutano ya ndani ya Vyama vya Siasa huleta hamasa kubwa kwa wanachama, viongozi na mashabiki wa chama cha siasa husika. Wakati mwingine hamasa hizo zinasababisha ukiukwaji wa sheria. Hivyo, mikutano ya hadhara na mikutano ya ndani ya Vyama vya Siasa, inahitaji kusimamiwa na kuratibiwa kisheria kwa umakini mkubwa, kwa kuzingatia haki ya Vyama vya Siasa kufanya mikutano hiyo na wajibu wa vyama hivyo kufuata matakwa ya sheria. Katika nchi yetu, haki ya kujumuika inatolewa na Katiba na kuratibiwa na Sheria mbalimbali ambazo zinazingatia msingi huo, ikiwemo Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 na Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi Sura ya 322.

### 4.2.1. Maoni ya Wadau

Katika eneo hili wadau walitoa maoni yafuatayo:

a) Mikutano ya hadhara na mikutano ya ndani ya Vyama vya Siasa iruhusiwe kwa kuzingatia sheria, kwani ilizuiliwa kinyume cha Katiba na sheria;

b) Sheria ya Vyama vya Siasa ifanyiwe marekebisho ili itoe maana ya mikutano ya ndani na mikutano ya hadhara ya Vyama vya Siasa;

c) Vyama vya Siasa viendelee kutoa taarifa katika Jeshi la Polisi na kwa namna yoyote ile isitafsiriwe kuwa ni kuomba kibali cha kufanya mikutano, bali ni kwa ajili ya kutoa ulinzi wakati wa mikutano;

d) taarifa itolewe katika kituo cha polisi kilicho karibu na eneo ambalo mkutano utafanyika ili kurahisisha utoaji wa taarifa ndani ya muda unaohitajika kisheria;

e) kuwepo kwa kumbukumbu za video katika mikutano ya hadhara ya Vyama vya Siasa ili kupatikana kwa taarifa za uhakika kunapotokea matukio ya ukiukwaji wa sheria; na

f) kifungu cha 11(8) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 kinatoa ruhusa kwa Jeshi la Polisi kuzuia mkutano ya hadhara linapokuwa na sababu za msingi kufanya hivyo, lakini hakiainishi ukomo wa muda wa kuweka zuio na hivyo kusababisha usumbufu pale ambapo maandalizi yote yamekamilika.

### 4.2.2. Uzoefu wa Nchi Nyingine

Katika eneo hili, Kikosi Kazi kilifuatilia uzoefu wa nchi mbalimbali ndani ya Afrika, Asia, Ulaya na Marekani, ili kuona jinsi mikutano ya hadhara inavyoratibiwa kisheria. Kwenye nchi nyingi zenye mfumo wa demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa, licha ya haki ya mikutano ya hadhara ya Vyama vya Siasa na maandamano kulindwa na katiba na sheria, lakini mikutano na maandamano hayo ni machache na mara nyingi hayaandaliwi na kuratibiwa na Vyama vya Siasa, kwa sababu baada ya uchaguzi siasa hufanyika katika vyombo vya uwakilishi (Bungeni).

### 4.2.3. Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Baada ya kupitia maoni ya wadau, uzoefu wa nchi nyingine na nyaraka mbalimbali, Kikosi Kazi kinapendekeza yafuatayo:

a) mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa iruhusiwe kufanyika kwa mujibu wa Katiba na Sheria;
b) mikutano ya ndani ya vyama vya siasa iendelee kufanyika bila vikwazo vyovyote;na
c) yafanyike marekebisho ya Sheria, ili kuhakikisha mikutano ya hadhara inafanyika kwa ufanisi. Sheria hizo ni pamoja Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258, Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi Sura ya 322 na Kanuni za Maadili ya Vyama vya Siasa za Mwaka 2019.

### 4.3. Demokrasia Ndani ya Vyama Vya Siasa

Eneo jingine ambalo wadau wametoa maoni mengi ni kuhusu demokrasia ndani ya Vyama vya Siasa. Licha kwamba, Tanzania

ina uzoefu wa miaka thelathini tangu kurejeshwa kwa mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa, lakini bado idadi kubwa ya Vyama vya Siasa vyenye usajili kamili, haviendeshwi kama taasisi na kwa kuzingatia misingi ya demokrasia. Hali hii inathibitishwa na uwepo wa malalamiko mengi na migogoro ndani ya Vyama vya Siasa, inayotokana na ukiukwaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa, Katiba na Kanuni za vyama hivyo.

Demokrasia ya ndani ya Vyama vya Siasa ni kiungo muhimu cha kukuza na kudumisha demokrasia nchini. Tafiti zinaonyesha kuwa, katika idadi kubwa ya Vyama vya Siasa ambavyo haviendeshwi kama taasisi na kwa kuzingatia misingi ya demokrasia, hali hiyo inasababishwa na mambo kadhaa yakiwemo:

a) kasumba ya waasisi wa vyama kutaka mawazo yao ndio yafuatwe;

b) idadi kubwa ya Vyama vya Siasa kutokuwa na fedha za kutosha kujiendesha, hivyo baadhi ya viongozi wa vyama hivyo kutumia fedha zao binafsi kugharamia shughuli za chama na hivyo kuwa na maamuzi makubwa ndani ya chama;

c) idadi kubwa ya Vyama vya Siasa kutokuwa na mfumo ambao unawapa sauti wanachama na hivyo maamuzi mengi kufanywa na viongozi;

d) idadi kubwa ya Vyama vya Siasa kutokuwa na kanuni madhubuti za uendeshaji wa shughuli zake za ndani, ikiwemo kanuni za fedha na kanuni za uchaguzi;

e) idadi kubwa ya Vyama vya Siasa kutozingatia suala la usawa wa jinsia, makundi maalumu na kudhibiti vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia;

f) uwepo wa rushwa ndani ya Vyama vya Siasa hasa wakati wa uchaguzi;na

g) idadi kubwa ya Vyama vya Siasa kutokuwa na mfumo kabisa au mfumo mzuri wa kuzuia na kutatua migogoro ya ndani ya chama.

#### 4.3.1 Maoni ya Wadau

Katika eneo hili wadau walitoa maoni yafuatayo:

a) kuwe na angalau theluthi moja ya wanawake katika kila chombo cha maamuzi cha chama cha siasa;

b) katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuanzishwe chombo maalumu cha kutatua migogoro ya ndani ya vyama vya siasa;

c) Msajili wa Vyama vya Siasa apewe mamlaka ya kisheria ya kusimamia uchaguzi wa ndani wa vyama vya siasa na kuhakikisha kuwa, vyama vya siasa vinatimiza matakwa ya sheria ya uwiano wa kijinsia na makundi maalum;

d) Ofisi ya Msajili wa Vyama ipewe uhuru zaidi katika utekelezaji wa kazi zake za kusajili na kusimamia demokrasia ya ndani ya vyama;

e) uainishwe utaratibu wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kutunza kanzi data ya kielektroniki ya wanachama wa Vyama vya Siasa; na

f) Baraza la Vyama vya Siasa liimarishwe kifedha na kiutendaji.

### 4.3.2 Uzoefu wa Nchi Nyingine

Sheria ya Vyama vya Siasa ya Kenya ya mwaka 2007 imeanzisha chombo maalum cha kutatua migogoro ya ndani ya vyama vya siasa kinachoitwa "Political Parties Disputes Tribunal". Jukumu la chombo hicho ni kusikiliza rufaa za vyama vya siasa dhidi ya maamuzi ya Msajili wa Vyama vya Siasa. Chombo hiki pia kina mamlaka ya kusikiliza kesi za wanachama wa vyama, dhidi ya vyama vyao na migogoro ndani ya vyama vya siasa. Aidha, iwapo Msajili anataka kuchukua hatua ya kufuta usajili wa chama cha siasa, hupaswa kupata ridhaa ya chombo hiki. Kanuni za uendeshaji wa chombo hiki huandaliwa na Jaji Mkuu wa Kenya.

Nchini Kenya, Msajili wa Vyama vya Siasa anao wajibu wa kuthibitisha, kutunza na kuweka wazi orodha ya wanachama wa Vyama vya Siasa, ili kuhakikisha hakuna mtu anakuwa mwanachama wa chama zaidi ya kimoja cha siasa. Aidha, uchaguzi wa viongozi wa chama cha siasa na uteuzi wa wagombea ndani ya vyama husimamiwa na Tume ya Uchaguzi.

### 4.3.3 Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Baada ya kupitia maoni ya wadau, uzoefu wa nchi nyingine na nyaraka mbalimbali, Kikosi Kazi kinapendekeza Sheria ya Vyama vya Siasa ifanyiwe marekebisho ili:

a) kulipatia Baraza la Vyama vya Siasa mamlaka ya kushughulikia suala la uvunjifu wa maadili ya Vyama vya Siasa kupitia Kamati yake ya Maadili;
b) Msajili wa Vyama vya Siasa awe na mamlaka ya kuandaa mwongozo wa uchaguzi wa ndani ya Vyama vya Siasa;

c) kuweka masharti kwamba idadi ya jinsi moja katika vyombo vya maamuzi vya chama cha siasa isipungue asilimia 40; na

d) kukitaka kila chama cha siasa kuwa na sera ya ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu katika shughuli za chama husika.

### 4.4. Ruzuku Kwa Vyama Vya Siasa

Tanzania iliporejesha mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992, Bunge liliweka utaratibu wa kutoa ruzuku kwa vyama vya siasa kutumia fedha za umma. Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995 wagombea wote walipewa fedha za umma kuwawezesha kushiriki kwa ufanisi katika uchaguzi huo. Hata hivyo, mwaka 1996 Sheria ya Vyama vya Siasa ilifanyiwa marekebisho, kuweka mfumo wa fedha za ruzuku kutoka Serikalini kupewa vyama vya siasa vyenye Wabunge wa majimbo, na mwaka 2005 Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho mengine, kuwezesha Vyama vya Siasa vyenye madiwani wa kata kupata ruzuku. Hivyo basi, ruzuku ya Serikali kwa Vyama vya Siasa inatolewa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258. Masharti na utaratibu wa kugawa fedha hizo umeainishwa katika Sheria hiyo.

#### 4.4.1 Hali Ilivyo Sasa

Kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, Serikali inapaswa kutenga kiasi cha fedha kisichozidi asilimia mbili ya Bajeti ya Serikali ya matumizi ya kawaida, baada ya kuondoa malipo ya deni la Taifa, kwa ajili ya ruzuku kwa Vyama vya Siasa. Utaratibu huu wa sheria umekuwa ukitekelezwa kwa miaka yote, ingawa kiwango

cha asilimia mbili hakijawahi kufikiwa. Fedha za ruzuku hukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kila mwaka, ambapo taarifa ya ukaguzi huwekwa wazi kwa umma. Fedha hizi hugawiwa kwa Vyama vya Siasa kwa utaratibu ufuatao:

a) Ruzuku ya Serikali hutolewa kwa chama cha siasa chenye Mbunge au Diwani;
b) fedha za ruzuku zilizotengwa katika bajeti ya Serikali hutolewa kila mwezi kwa kuzigawanya kwa miezi 12;
c) kiasi cha Tshs. 250,000,000/= kilichoanishwa na Mheshimiwa Waziri Mwenye dhamana ya masuala ya vyama vya siasa, kwa mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, hutengwa kila mwezi kwa ajili ya kugawa ruzuku kwa vyama vya siasa vyenye madiwani, kwa mujibu wa uwiano wa idadi ya Madiwani wa kuchaguliwa katika kata, ambao kila chama kimepata katika Uchaguzi Mkuu wa mwisho;
d) baada ya kuondoa fedha za ruzuku zilizotengwa kwa ajili ya Madiwani katika mwezi husika, asilimia hamsini (50%) ya fedha zilizobaki katika mwezi husika, hugawiwa kwa Vyama vya Siasa vyenye Wabunge wa jimbo kwa uwiano wa kura za ubunge ambazo kila chama cha siasa kimepata katika Uchaguzi Mkuu wa mwisho. Hata hivyo, chama cha siasa ni lazima kipate zaidi ya asilimia tano (5%) ya kura hizo, ili kuwa na haki ya kupata mgawo huo; na
e) asilimia hamsini (50%) iliyobaki ya fedha hizo, hugawiwa kwa Vyama vya Siasa vyenye wabunge kwa mujibu wa

uwiano wa idadi ya wabunge wa majimbo ambao kila chama kimepata katika Uchaguzi Mkuu wa mwisho.

### 4.4.2 Maoni ya Wadau

Katika eneo hili wadau walitoa maoni yafuatayo:

a) Baadhi ya wadau walipendekeza kuwa, Vyama vyote vya Siasa vipewe ruzuku, kwani vigezo vya sasa vya kugawa ruzuku vinasababisha vyama vingine kutopata fedha hizo na hivyo kushindwa kujiendesha kitaasisi. Hivyo, Sheria ya Vyama vya Siasa irekebishwe, ili kuainisha vigezo vipya vitakavyoruhusu vyama vyote vya siasa kupata ruzuku kwa viwango tofauti kulingana na masharti ya sheria. Hatua hii itaimarisha demokrasia ya vyama vingi na ushindani wa kisiasa;

b) Baadhi ya wadau walipendekeza kwamba, Vyama vya Siasa viendelee kupata ruzuku kwa utaratibu uliopo sasa, ili kuepuka kuwa na utitiri wa vyama vya siasa, kwani kuna watu wanaweza kuomba kusajili vyama vya siasa kwa lengo la kupata ruzuku; na

c) Baadhi ya wadau walipendekeza kuwa, vyama vya siasa vyote visipewe ruzuku, vijiendeshe vyenyewe kwa kutumia ada, michango ya wanachama na vyanzo vingine vya mapato na siyo fedha za umma.

### 4.4.3 Uzoefu wa Nchi Nyingine

Kikosi Kazi kimefanya utafiti wa nchi nyingine, ili kujielimisha namna wanavyoshughulikia suala la ruzuku kwa Vyama vya Siasa. Katika

eneo la Jumuiya ya Afrika Mashariki nchi zote isipokuwa Sudani Kusini, zimeweka utaratibu wa kuvipa Vyama vya Siasa ruzuku kwa kutumia fedha za umma. Nchini Kenya, sehemu ya 23 ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 2011, imeweka masharti ya Vyama vya Siasa kupata ruzuku kutoka Hazina ya Taifa lao. Kwa mujibu wa sheria hiyo, madhumuni ya ruzuku, ni kuimarisha demokrasia ya ushindani wa Vyama vya Siasa, kuwezesha ushiriki wa Wanawake na watu wenye ulemavu katika siasa za nchi yao. Vilevile, kuwezesha vyama vya siasa kutoa elimu ya uraia kwa wananchi.

Sheria ya Vyama vya Siasa ya Kenya inaelekeza kuwa, kiasi kisichopungua asimilia 0.3 ya makusanyo yote ya mapato ya Serikali iwekwe katika Mfuko wa Vyama vya siasa (Political Parties Fund). Asilimia 80 ya fedha hizo, zigawiwe kwa Vyama vya Siasa kwa mujibu wa uwiano wa kura ambazo kila chama kimepata katika Uchaguzi Mkuu wa mwisho. Asilimia 15 igawiwe kwa vyama vyote vya siasa kwa mujibu wa uwiano wa wagombea ambao chama cha siasa kiliweka katika uchaguzi huo. Vilevile, asilimia tano(5%) itumike kusimamia fedha hizo.

Katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Taifa la Zimbabwe, Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Afrika Kusini na Namibia, yana utaratibu wa Serikali kutoa ruzuku kwa Vyama vya Siasa. Nchini Zimbabwe, vyama vya siasa hupewa ruzuku kwa mujibu idadi ya Wabunge ambao kila chama kimepata. Aidha, nchini Afrika Kusini, Vyama vya Siasa hupewa ruzuku kwa mujibu wa uwiano wa kura ambazo kila chama cha siasa kimepata katika Uchaguzi Mkuu, bila kuwepo kwa kiwango cha chini.

### 4.4.4 Uchambuzi

Ni vyema kuendelea kuvipa ruzuku vyama vya siasa, ili kuviimarisha kiutendaji na kiushindani, kuviwezesha kutekeleza wajibu wao ikiwemo kutoa elimu ya uraia kwa wanachama wao na wananchi kwa ujumla, kuimarisha usalama wa nchi kwa kuepuka Vyama vya Siasa ufadhili wenye nia ovu dhidi ya nchi yetu.

Vilevile, baada ya uzoefu tuliopata wa miaka thelathini (30) ya demokrasia ya vyama vingi vya siasa, ni dhahiri kuwa, masharti ya sasa ya ruzuku yanapaswa kupitiwa upya, ili yaendane na mazingira ya sasa. Mfano, mwaka 2010 Sheria ya Vyama vya Siasa ilirekebishwa kumpa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), jukumu la kukagua taarifa ya fedha za Vyama vya Siasa, hata vyama ambavyo havipati ruzuku ya Serikali. Marekebisho hayo yanaonesha umuhimu wa vyama vyote vya siasa kupewa ruzuku, ili viweze kutekeleza masharti ya ukaguzi wa CAG na matakwa mengine ya Sheria ya Vyama vya Siasa.

Kuhusu ushauri kwamba, vyama vya siasa vyote vipewe ruzuku ya Serikali, kuna hoja kwamba, ni vyema kuainisha ni wapi fedha za nyongeza zitapatikana, kwani fedha za umma zina majukumu mengi. Hoja hii inajibiwa na Sheria ya Vyama vya Siasa ambayo imeweka utaratibu wa fedha za ruzuku kwa Vyama vya Siasa kutoka katika bajeti ya Serikali. Hivyo, fedha za kuvipa ruzuku vyama vyote vya siasa kwa lengo la kuviwezesha kujiendesha kiutawala na kutekeleza matakwa ya Sheria ya Vyama vya Siasa, zinaweza kutokana na sehemu ya fedha za ruzuku zinazotolewa sasa kwa Vyama vya Siasa vyenye Wabunge na Madiwani.

### 4.4.5 Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Baada ya kupitia maoni ya wadau, uzoefu wa nchi nyingine na nyaraka mbalimbali, Kikosi Kazi kinapendekeza yafuatayo:

a) mfumo wa sasa wa kugawa ruzuku ya Serikali kwa Vyama vya Siasa uendelee, isipokuwa asilimia 10 ya fedha za ruzuku kwa Vyama vya Siasa zilizotengwa katika bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha husika, igawiwe sawa kwa vyama vyote vya siasa vyenye usajili kamili kwa mujibu wa vigezo na masharti yafuatayo:

   (i) chama kiwe na usajili kamili;
   (ii) chama kiwe kimefanyiwa uhakiki na Msajili wa Vyama vya Siasa na kuthibitishwa kwamba, kinakidhi vigezo vya usajili kamili;
   (iii) chama kiwe kimeshiriki Uchaguzi Mkuu angalau mara mbili tangu kupata usajili kamili;
   (iv) katika mwaka wa fedha uliopita, chama husika kisiwe kimepata Hati Chafu ya Mahesabu kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na
   (v) ruzuku itumike kwa shughuli za kuendesha Ofisi ya Makao Makuu, Ofisi Ndogo au Ofisi Kuu ya Makao Makuu ya chama cha siasa husika.

b) Sheria ya Vyama vya Siasa itamke kuwa, asilimia ishirini (20%) ya fedha za ruzuku kwa Vyama vya Siasa inayotolewa na Serikali katika mwaka wa fedha, igawiwe kwa Vyama vya Siasa vyenye Madiwani wa kuchaguliwa katika kata, kwa mujibu wa uwiano wa idadi ya Madiwani

hao ambao kila chama kinao, kwani kwa sasa sheria haijatamka kiwango chochote bali imempa mamlaka Waziri Mwenye dhamana kuamua;

c) fedha za ruzuku zigawiwe kwa Vyama vya Siasa kwa mujibu wa idadi ya kura za ubunge na idadi ya wabunge ambao chama cha siasa kinao kwa wakati husika; na

d) Serikali iongeze fedha za bajeti ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Baraza la Vyama vya Siasa, ili liweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, ikiwemo jukumu linalopendekezwa la kusimamia Maadili ya Vyama vya Siasa.

# SURA YA TANO

# UCHAGUZI

## 5.1 Utangulizi

Uchaguzi ni njia ya kidemokrasia inayotumika kupata viongozi wa kisiasa. Aidha, Tume ya Uchaguzi ndiyo chombo chenye mamlaka ya kusimamia na kuendesha shughuli za uchaguzi katika nchi. Sura hii inaangalia uhuru wa Tume ya Uchaguzi, mifumo ya uchaguzi, usimamizi wa uchaguzi na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika uchaguzi.

## 5.2 Mfumo wa Uchaguzi

Mfumo wa uchaguzi ni utaratibu wa kutafsiri kura zilizopigwa wakati wa uchaguzi ili kupata ushindi wa viti vya uwakilishi kwa chama na wagombea. Tafsiri hii ya kura kuwa viti vya uwakilishi, inategemea kanuni iliyotumika, endapo ni uwiano wa kura, ushindi kwa kura nyingi au mseto. Hivyo, mfumo wa uchaguzi huakisi sheria za uchaguzi, mipaka ya majimbo ya uchaguzi, uandikishaji wa wapiga kura, karatasi za kupigia kura na namna kura zinavyohesabiwa. Vilevile, unatoa mwelekeo wa aina ya Serikali itakayoundwa, idadi ya watu watakaojitokeza kupiga kura, nidhamu ya chama, kampeni za uchaguzi, kumtambua mgombea huru (binafsi), uwakilishi wa wanawake pamoja na namna ya utatuzi wa migogoro ya uchaguzi.

### 5.2.1. Aina za Mifumo ya Uchaguzi

Kuna aina kuu tatu za mifumo ya uchaguzi. Mifumo hii ni uchaguzi wa Mshindi kwa Kura Nyingi (First Past the Post), Mfumo wa Uwiano (Proportional Representation) na Mfumo wa Uchaguzi wa Mseto (Mixed Electoral System).

#### 5.2.1.1. Mshindi kwa Kura Nyingi (First Past the Post)

Katika Mfumo huu mgombea anashinda uchaguzi ikiwa amepata kura nyingi kuliko wagombea wengine. Mfumo huu una faida zifuatazo:

a) ni rahisi kutumika na kueleweka kwa wapiga kura;
b) wapiga kura wanafahamu wagombea wa maeneo ya uchaguzi;
c) unaleta uhusiano wa moja kwa moja kati ya wapiga kura na kiongozi wao hivyo kuongeza uwajibikaji kwa wananchi na si chama;
d) unawezesha kuchagua watu na siyo chama na unatoa mwanya kwa mgombea binafsi maarufu kuchaguliwa; na
e) unasaidia wagombea kupiga kampeni kwa bidii na ufanisi katika majimbo yao na baada ya uchaguzi kusimamia vyema utekelezaji wa ilani ya uchaguzi.

Hata hivyo, Mfumo huu una changamoto zifuatazo:

a) unachochea rushwa kwa sababu wagombea wanashindana kama watu binafsi na siyo chama;

b) unaweka mazingira magumu kwa wanawake kuingia katika vyombo vya uwakilishi vya kisiasa, mfano Bunge;
c) unasababisha kura nyingi kupotea wakati wa uchaguzi, pale ambapo baadhi ya wapiga kura wanaona kuna dalili za mgombea wao kushinda au kushindwa uchaguzi; na
d) unapunguza nidhamu na mapenzi ya wanachama kwa chama chao.

#### 5.2.1.2. Mfumo wa Uwiano (Proportional Representation)

Mfumo wa Uwiano wa Kura unatumika zaidi pale ambapo chama na si mtu hupigiwa kura. Mfumo huu una faida zifuatazo:

a) unarahisisha bunge kuwa na uwakilishi mzuri wa makundi mbalimbali ya watu, ikiwemo wanawake na Watu Wenye Ulemavu;
b) unasaidia kupata idadi kubwa ya uwakilishi wa Vyama vya Siasa bungeni;
c) unaimarisha nidhamu na mapenzi ya wanachama kwa chama chao; na
d) unapunguza vitendo vya rushwa katika uchaguzi kwa kuwa hakuna mtu anayegombea jimbo kama mtu binafsi.

Mfumo huu una changamoto zifuatazo:

a) unalazimisha vyama vikubwa kuunda serikali ya mseto na vyama vidogo;
b) unaweza kuleta serikali dhaifu inayotokana na kuwepo kwa serikali mseto;
c) unaweza kuleta vyama vyenye itikadi na siasa kali serikalini; na

d) haumpi mpiga kura uwezo wa kumwajibisha kiongozi wake kwani kiongozi huyo hapigiwi kura.

#### 5.2.1.3. Mfumo wa Uchaguzi Mseto (Mixed Electoral System)

Kutokana na faida na changamoto za Mfumo wa Mshindi kwa Kura Nyingi na Mfumo wa Uwiano na kwa kuzingatia historia na hali halisi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii ya nchi husika, nchi nyingi hupendelea kuwa na Mfumo wa Uchaguzi Mseto (Mixed Electoral System). Hali hii inasaidia nchi kunufaika na faida za mifumo yote miwili.

### 5.2.2. Hali Ilivyo Sasa

Tanzania inatumia mifumo miwili ya uchaguzi kwa pamoja, ambayo ni Mfumo wa Mshindi kwa Kura Nyingi na Mfumo wa Uwiano. Mfumo wa Mshindi kwa Kura Nyingi unatumika kwa uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani na uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Mfumo wa Uwiano unatumia kwa kupata wabunge na madiwani wa viti maalum vya wanawake.

### 5.2.3. Mapendekezo ya Tume, Kamati Mbalimbali na Utafiti

Tume na kamati mbalimbali zilizoteuliwa kabla ya Kikosi Kazi ziliwahi kufanyia kazi suala la mfumo wa uchaguzi na kutoa mapendekezo yafuatayo, Tume ya Jaji Nyalali ilipendekeza Tanzania kuwa na Mfumo wa Uchaguzi Mseto uliojengwa kwenye msingi wa mgombea anayepata kura nyingi zilizopigwa kushinda wote ndiye anakuwa mshindi kwa nafasi ya Rais, Wabunge na

Madiwani. Vilevile, kuwa na Mfumo wa Uwiano kwa vile vyama vilivyopata ushindi angalau wa asilimia 5 ya kura zote zilizopigwa katika Uchaguzi Mkuu, viwe na uwakilishi bungeni.

Kamati ya Jaji Kisanga ilipendekeza kuwa, katika uchaguzi wa Rais mshindi ni lazima apate kura zaidi ya asilimia hamsini (50%).
Kamati hiyo ilieleza sababu za kupendekeza mfumo huo kuwa ni kuepuka Rais kupata kura za sehemu moja ya nchi, dini au kabila na kujenga umoja na uimara wa taifa. Katika nafasi za Ubunge na Udiwani, Kamati ilipendekeza mgombea atakayepata kura nyingi zaidi ya wagombea wenzake ndiye anatangazwa mshindi (Simple Majority System).

Ibara ya 80(6) ya Rasimu ya Pili ya Katiba iliyoandaliwa na Tume ya Jaji Warioba na ibara ya 89(6) ya Katiba Inayopendekezwa, zilipendekeza kuwa, mgombea Urais atahesabika amechaguliwa na ameshinda uchaguzi endapo atapata kura zaidi ya asilimia hamsini (50%) ya kura zote zilizopigwa. Aidha, katika nafasi za Ubunge na Udiwani, Tume hiyo ilipendekeza mgombea atakayepata kura nyingi zaidi ya wagombea wenzake ndiye atatangazwa kuwa mshindi.

### 5.2.4. Maoni ya Wadau

Katika eneo hili wadau walitoa maoni na mapendekezo yafuatayo:

a) Tanzania itumie mfumo wa uwiano kwa chaguzi zote za Serikali, ili kurahisha kuongeza idadi ya wabunge na madiwani wanawake bungeni na katika mabaraza ya

madiwani, kukuza vyama vichanga na demokrasia nchini; na

b) mfumo wa sasa wa uchaguzi uendelee, ili kulinda umoja na mshikamano wa kitaifa, kwani mfumo wa uchaguzi wa uwiano wa kura unazaa serikali na bunge dhaifu.

### 5.2.5. Uzoefu wa Nchi Nyingine

Kikosi Kazi kilifanya mapitio ya nyaraka mbalimbali kuhusu mifumo ya uchaguzi katika nchi mbalimbali ili kupata uzoefu kutoka katika nchi hizo. Nchini Kenya, mgombea urais anakuwa ameshinda uchaguzi wa Rais endapo amepata kura zaidi ya asilimia hamsini. Aidha, endapo hakuna mgombea urais aliyepata kura zaidi ya asilimia hamsini, uchaguzi wa urais unarudiwa kwa kuwashindanisha wagombea wawili waliopata kura nyingi zaidi ya wenzao. Katika hatua hii, mgombea aliyepata kura nyingi zaidi ya mwenzake, atakuwa ndiye mshindi wa kiti cha urais.

Nchi zinazofuata Mfumo wa Mshindi kupata Kura Nyingi ni Zimbabwe, Zambia, Kenya, Uganda, Ethiopia, Sudan, Nigeria, Gambia, United Kingdom, India, Malaysia, Nepal, Canada na Marekani. Aidha, nchi zinazotumia Mfumo wa Uwiano ni pamoja na Rwanda, Msumbiji, Afrika Kusini, Peru na Sierra Leone.

### 5.2.6. Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Baada ya kupitia maoni ya wadau, uzoefu wa nchi nyingine, nyaraka mbalimbali na historia ya siasa na demokrasia nchini, Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa:

a) Mfumo Mseto wa Uchaguzi (Mixed Electoral System) uendelee kutumika kwa uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Aidha, katika uchaguzi wa Rais ili mgombea ashinde uchaguzi iwe ni lazima apate zaidi ya asilimia hamsini ya kura zote halali zilizopigwa;
b) uchaguzi wa wabunge, madiwani na uchaguzi wa Serikali za Mitaa uendelee kutumia Mfumo wa Mshindi kwa Kura Nyingi; na
c) Mfumo wa Uwiano wa kura uendelee kutumika kupata wabunge na madiwani wa viti maalum vya wanawake.

## 5.3 Dhana ya Uhuru wa Tume za Uchaguzi

### 5.3.1. Maana ya "Uhuru" wa Tume ya Uchaguzi

Uhuru wa Tume ya Uchaguzi una maana kuu mbili. Maana ya kwanza huitwa "Uhuru halisi" *(Actual Independence)*. Aina hii ya uhuru wa Tume ya Uchaguzi ina maana kuwa, ni uwezo wa Tume ya Uchaguzi kusimamia mchakato wa uchaguzi, bila kulazimika kufuata amri, agizo au maoni ya mtu, taasisi au mamlaka yoyote ya Serikali. Uhuru huu huainishwa bayana katika Katiba na Sheria za nchi husika. Aidha, uhuru huo hauondoi dhana ya Tume kuwajibika kwa uzembe na ukiukwaji wa sheria wenye athari katika uchaguzi.

Maana ya pili huitwa "Uhuru wa Kimtazamo" *(Perceived Independence)*. Aina hii ya uhuru wa Tume ya Uchaguzi inatokana na *"mtazamo"* wa wadau wa uchaguzi juu ya utendaji wa kazi wa Tume ya Uchaguzi. Katika hali hii, mtazamo wa wadau ndio hujenga imani yao kwa Tume ya Uchaguzi kuhusu utendaji kazi

wake. Hivyo, wadau wa uchaguzi huona kwamba, Tume ya Uchaguzi ipo huru pale ambapo katika kusimamia uchaguzi, haifuati amri, agizo au maoni ya mtu, taasisi au mamlaka yoyote ya Serikali, kutokuwa na upendeleo, uadilifu wa watendaji wake, uwazi, ufanisi, weledi, ushirikishwaji na uwajibikaji. Misingi hii ya uhuru wa Tume ya Uchaguzi inafafanuliwa ifuatavyo:

a) *kutofuata amri, agizo au maoni ya mtu, taasisi au mamlaka yoyote ya Serikali*. Katika kusimamia mchakato wa uchaguzi, Tume ya Uchaguzi haipaswi kufuata amri, agizo au maoni ya mtu, taasisi au mamlaka yoyote ya Serikali;

b) *Kutokuwa na Upendeleo:* Ni hali ambayo Tume ya Uchaguzi inawatendea haki washiriki wote wa uchaguzi kwa usawa kwa mujibu wa Sheria, bila upendeleo kwa mshiriki yeyote unaotokana na maslahi ya kisiasa, kifedha au binafsi;

c) *Uadilifu:* Ni hali ya watendaji wa Tume ya Uchaguzi kutenda haki bila kupendelea mshiriki yeyote katika uchaguzi, kwa kuheshimu na kutekeleza sheria na taratibu za uchaguzi ipasavyo;

d) *Uwazi:* Ni hali ya Tume ya Uchaguzi kuweka wazi masuala muhimu kuhusu mchakato wa uchaguzi ambayo washiriki wa uchaguzi wanapaswa kufahamu ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika uchaguzi na kuwa na imani na uchaguzi huo. Uwazi huo ni pamoja na kuwapa taarifa washiriki wa uchaguzi kwa wakati;

e) *Ufanisi:* Ni hali ya tume kuendesha shughuli zake kwa kuzingatia malengo ya uwepo wake, uwepo wa uchaguzi na mafanikio yanayotarajiwa;

f) *Weledi;* Ni hali ambayo Tume ya Uchaguzi inakuwa na watendaji wenye ujuzi wa kutosha na sahihi kusimamia shughuli za uchaguzi. Tume inapaswa kuhakikisha kuwa, maafisa wote wa uchaguzi wanapewa mafunzo ya kitaalam kuhusu uchaguzi na kusimamia shughuli za

Uchaguzi;

g) *Ushirikishwaji;* Ni hali ambayo Tume ya Uchaguzi inawahusisha kwa uwazi wadau wote wa uchaguzi katika hatua muhimu za kusimamia shughuli za uchaguzi. Kitendo hiki huwawezesha, wadau wa uchaguzi kushiriki kikamilifu katika uchaguzi na kuwa na imani na Tume na mchakato mzima wa uchaguzi husika; na

h) *Uwajibikaji:* Ni hali ambayo hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi ya watendaji wa Tume ya Uchaguzi na wadau wote wa uchaguzi, pale wanapokiuka Sheria za uchaguzi, ikiwemo Maadili ya Uchaguzi.

Ni muhimu kuzingatia kuwa, ili Tume ya Uchaguzi iweze kudhihirisha kuwa ipo huru, ni lazima ionekane kuwa na uhuru halisi na uhuru wa kimtazamo. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kuwa, kuna aina kuu tatu za mifumo ya Tume za Uchaguzi. Mifumo hii ni Tume Huru (Independent Model), Tume ya Serikali (Governmental Model) na Tume Mseto (Mixed Model). Uchaguzi wa mfumo wa Tume ya Uchaguzi hutegemea mazingira ya nchi husika, historia, mfumo wa kisiasa, kiutawala na uchaguzi, kiwango cha ukomavu wa demokrasia, kuaminika kwa watendaji na mamlaka za Serikali, utamaduni wa kisiasa na ushirikishwaji wa wadau wa demokrasia katika masuala ya siasa na uchaguzi. Mifumo hii inafafanuliwa

katika aya zinazofuata kwa kueleza faida na changamoto za kila mfumo.

#### 5.3.1.1 Tume Huru (Independent Model)

Katika mfumo huu, Tume ya Uchaguzi haifungamani na mfumo wa kawaida wa utendaji wa Serikali. Tume hupata mamlaka yake kutoka kwenye katiba, husimamia bajeti yake na haiwajibiki kwa Wizara, idara au taasisi yoyote ya Serikali. Mfano wa nchi zinazofuata mfumo huu ni pamoja na Afrika Kusini, Nigeria, Kenya, Ghana, Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Faida ya Mfumo huu ni pamoja na Tume ya Uchaguzi kusimamia mchakato wa uchaguzi, bila kulazimika kufuata amri, agizo au maoni ya mtu, taasisi au mamlaka yoyote ya Serikali, Tume kusimamia bajeti yake na wadau wa uchaguzi kuwa na imani na Tume na mchakato mzima wa uchaguzi husika. Aidha, changamoto za mfumo huu ni pamoja na kuwa na gharama kubwa za kusimamizi uchaguzi, ugumu wa kupata watendaji wa Tume waaminifu, wazoefu na kuwawajibisha kwani wanakuwa siyo watumishi wa Serikali na tume kutokuwa na fedha za kutosha kujiendesha.

#### 5.3.1.2 Mfumo wa Kiserikali (Government Model)

Katika mfumo huu Serikali inasimamia uchaguzi kwa kutumia afisa wa Serikali, idara au Wizara. Bajeti ya uchaguzi chini ya mfumo huu inaratibiwa na Wizara husika. Mifano ya nchi zinazotumia mfumo

huu ni pamoja na Denmark, Singapore, Uswisi, Tunisia, Uingereza na Marekani.

Faida ya mfumo huu ni pamoja na uchaguzi kusimamiwa kwa gharama ndogo, pia inakuwa rahisi kupata watendaji waaminifu kusimamia uchaguzi, wazoefu na kuwawajibisha kwani wanakuwa ni watumishi wa Serikali. Changamoto ya mfumo huu ni pamoja na wasimamizi wa uchaguzi kufuata amri, agizo au maelekezo ya mamlaka za Serikali. Vilevile, kunakuwa na uwezekano mkubwa kwa wadau wa uchaguzi kutokuwa na imani na mchakato mzima wa uchaguzi.

#### 5.3.1.3 Mfumo wa Tume Mseto (Mixed Model)

Katika mfumo huu, kunakuwa na Bodi Huru ya Uchaguzi yenye mamlaka ya kutengeneza sera na kufuatilia usimamizi wa uchaguzi. Sambamba na bodi hiyo, kunakuwa na idara ya serikali yenye mamlaka ya kutekeleza sera na kusimamia uchaguzi. Nchi zinazofuata mfumo huu ni pamoja na Ufaransa, Japan, Peru, Hispania, Mali, Cameroon na Senegal.

Faida ya mfumo huu ni pamoja na weledi na kuheshimika kwa wajumbe wa bodi huru ya uchaguzi huongeza kukubalika na imani ya wadau wa uchaguzi kwa uchaguzi. Uendeshaji wa masuala ya uchaguzi unaweza kutumia wataalamu na watendaji kutoka ndani na nje ya Serikali. Aidha, Uchaguzi husimamiwa kwa gharama ndogo. Vilevile, inakuwa rahisi kupata wasimamizi wa uchaguzi waaminifu, wazoefu na kuwawajibisha kwani wanakuwa ni watumishi wa Serikali. Mojawapo ya changamoto za mfumo huu ni

kuwepo kwa uwezekano mkubwa wa wadau wa uchaguzi, kutokuwa na imani na mchakato wa uchaguzi kwa kuwa unasimamiwa na watendaji wa Serikali. Kuchanganya watumishi kutoka nje ya Serikali na watumishi wa Serikali, kunaweza kusababisha migongano ya kiutendaji kutokana na tofauti za uzoefu, maadili na uwepo wa maslahi binafsi.

Ni muhimu kufahamu kwamba, nchi nyingi za Afrika zinatumia mfumo wa Tume Huru ya Uchaguzi *(Independent Model)*. Utafiti uliofanywa na *International Institute for Democracy and Electoral Assistance* (International IDEA) mwaka 2014 ulioangalia aina ya mifumo ya Tume za Uchaguzi na ufanisi wake duniani, ulibainisha kuwa nchi 42 kati ya nchi 53 za Afrika, ambayo ni asilimia 79, zinatumia Mfumo wa Tume Huru ya Uchaguzi kusimamia uchaguzi. Nchi nane (8) kati ya nchi 53, ambayo ni asilimia 15, zinatumia Mfumo wa Mseto wa kusimamia uchaguzi. Aidha, nchi 3 kati ya nchi hizo 53, ambayo ni asilimia 6, zinatumia Mfumo wa Serikali kusimamia uchaguzi.

### 5.3.2. Uhuru wa Tume ya Uchaguzi ya Tanzania

#### 5.3.2.1. Hali Ilivyo Sasa

Kuhusu uhuru wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Ibara ya 74(11) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inaeleza kuwa "Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, Tume ya Uchaguzi haitalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali au maoni ya chama chochote cha siasa." Aidha, Ibara ya 74(12) ya Katiba

inatoa kinga kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kwa kueleza kwamba, Mahakama haitakuwa na mamlaka ya kuchunguza jambo lolote lililotendwa na Tume hiyo.

#### 5.3.2.2. Mapendekezo ya Tume na Kamati Mbalimbali

Tume na kamati mbalimbali nchini, ziliwahi kuifanyia kazi hoja ya uhuru wa Tume ya Uchaguzi na kuwasilisha mapendekezo yao.

Kamati ya Kuratibu Maoni Kuhusu Katiba ya Mwaka 1999, maarufu kama Kamati ya Jaji Kisanga, ilipendekeza Tume ya Uchaguzi iimarishwe ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu. Tume ya Mabadiliko ya Katiba, maarufu kama Tume ya Jaji Warioba katika ibara ya 193(5) ya Rasimu ya Pili ya Katiba, vilevile, Katiba Inayopendekezwa katika ibara ya 220(5) zinaeleza kuwa, katika kutekeleza madaraka yake, Tume Huru ya Uchaguzi isilazimike kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote, idara yoyote ya Serikali, maoni ya chama chochote cha siasa, taasisi au asasi yoyote.

#### 5.3.2.3. Maoni ya Wadau

Wadau walipendekeza utendaji wa Tume ya Uchaguzi uhojiwe Mahakamani, ili kuimarisha dhana ya utawala bora na uwajibikaji wa watendaji wa Tume. Aidha, itasaidia kulinda haki za wadau wa uchaguzi na kuongeza imani ya wadau hao kwa Tume ya Uchaguzi na mchakato mzima wa uchaguzi.

#### 5.3.2.4. Uzoefu wa Nchi Nyingine

Kikosi Kazi kilifanya mapitio ya nyaraka mbalimbali kuhusu uhuru wa Tume za Uchaguzi na uwajibikaji wa tume hizo katika nchi mbalimbali, ili kupata uzoefu kutoka katika nchi hizo. Nchini Ghana, ibara ya 46 ya Katiba ya nchi hiyo inaeleza kuhusu uhuru wa Tume ya Uchaguzi kwamba, katika kutekeleza majukumu yake, Tume ya Uchaguzi haitolazimika kufuata au kusimamiwa na mtu au mamlaka yoyote, isipokuwa kama itaelezwa na katiba au sheria nyingine yoyote.

Nchini Afrika Kusini, kifungu cha 3 cha Sheria ya Tume ya Uchaguzi kinaeleza kuwa, Tume ya Uchaguzi itakuwa ni chombo huru kwa mujibu wa katiba na sheria na itatekeleza kazi zake bila woga, upendeleo, hofu na kwa kufuata katiba na sheria. Aidha, sheria imeanzisha Mahakama ya Uchaguzi ambayo pamoja na mambo mengine, imepewa uwezo wa kushughulikia malalamiko yote yanayotokana na uamuzi wa Tume ya Uchaguzi. Kifungu cha 20(1)(a) cha sheria hiyo, kinaeleza kwamba, Mahakama ya Uchaguzi inaweza kufanya mapitio ya uamuzi wowote uliotolewa na Tume ya Uchaguzi kuhusu masuala ya uchaguzi.

#### 5.3.2.5. Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Baada ya kupitia maoni ya wadau, uzoefu wa nchi nyingine na nyaraka mbalimbali, Kikosi Kazi kinapendekeza yafuatayo:

a) Tume ya Taifa ya Uchaguzi isilazimike kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote, idara yoyote ya Serikali, maoni ya chama chochote cha siasa, taasisi au asasi yoyote; na

b) utendaji wa Tume ya Uchaguzi uruhusiwe kuhojiwa kwenye Mahakama ya Juu pale itakapoanzishwa ili kuongeza uwajibikaji wa Tume.

## 5.4 Uteuzi wa Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi

### 5.4.1 Hali Ilivyo Sasa

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeanzishwa na Ibara ya 74 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Tume ina wajumbe saba (7) ambao ni Mwenyekiti wa Tume, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wengine watakaotajwa na sheria iliyotungwa na Bunge, ambapo wote wanateuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kifungu cha 4 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343 kinaeleza kuwa, wajumbe wanaotajwa katika ibara ya 74(1)(c) ni Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Makamu Mwenyekiti, mjumbe mmoja atakayeteuliwa kutoka miongoni mwa wanachama wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika na wajumbe wengine wasiozidi wanne. Aidha, Katiba imeainisha sifa mahsusi za Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Tume.

### 5.4.2 Mapendekezo ya Tume, Kamati Mbalimbali na Hukumu za Mahakama

Tume na kamati mbalimbali nchini ziliwahi kulifanyia kazi suala la Uteuzi wa Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi na kuwasilisha mapendekezo yao. Tume ya Jaji Nyalali (1991) ilipendekeza kuwepo na Tume tatu za Uchaguzi, kwa sababu ilipendekeza

mfumo wa serikali tatu. Tume hizo ni Tume ya Uchaguzi ya Shirikisho, Tume ya Uchaguzi ya Tanganyika na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Wenyeviti wa Tume hizo wateuliwe na Bunge au Baraza la Wawakilishi linalohusika, lakini wasitokane na Wabunge au Wawakilishi.

Aidha, Kamati ya Jaji Kisanga (1999) ilipendekeza kuwa, Rais ateue wajumbe wa Tume ya Uchaguzi kwa kushauriana na Bunge kwa utaratibu ufuatao:

a) Rais awasilishe Bungeni orodha ya majina ya watu anaotarajia kuwateua kuwa wajumbe wa Tume ya Uchaguzi;
b) orodha hiyo ijadiliwe na Bunge; na
c) baada ya kujadiliwa na Bunge, orodha hiyo irudishwe kwa Rais, kwa ajili ya uteuzi wa wajumbe.

Tume ya Jaji Warioba kupitia ibara ya 191(1) ya Rasimu ya Pili ya Katiba, ilipendekeza kuwepo na Kamati ya Uteuzi wa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi yenye wajumbe wafuatao:

a) Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye atakuwa ni Mwenyekiti;
b) Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti;
c) Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar;
d) Spika wa Bunge la Tanganyika;
e) Jaji Mkuu wa Tanganyika;
f) Jaji Mkuu wa Zanzibar; na
g) Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Uongozi na

Uwajibikaji.

Kamati hii itakuwa na jukumu la kuchambua na kupendekeza kwa Rais kwa ajili ya uteuzi, majina ya watu walioomba na waliopendekezwa na asasi za kiraia wanaoweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi. Baada ya uteuzi, Rais atawasilisha majina hayo Bungeni, kwa ajili ya kuthibitishwa na Bunge.

Aidha, ibara ya 218(1) ya Katiba Inayopendekezwa inabainisha kuwepo na Kamati ya Uteuzi wa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wengine saba wa Tume ya Uchaguzi. Vilevile, ibara ya 217(5) ya Katiba Inayopendekezwa, imeainisha sifa wanazopaswa kuwa nazo Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wa Tume hiyo. Jukumu la Kamati ya Uteuzi ni kupokea, kuchambua majina ya watu walioomba kuwa wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi na kupendekeza kwa Rais, majina ya watu wanaofaa kuteuliwa kuwa wajumbe wa Tume ya Uchaguzi. Katiba Inayopendekezwa imependekeza Kamati hiyo iwe na wajumbe wafuatao:

a) Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye atakuwa ni Mwenyekiti;
b) Jaji Mkuu wa Zanzibar ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti;
c) Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
d) Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar;
e) Jaji kiongozi; na
f) Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Katika shauri la madai ya Mabere Nyahucho Marando na Edwin Mtei dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali namba 168 la mwaka

1993, iliyosikilizwa na kutolewa uamuzi na Mahakama Kuu ya Tanzania Masjala Kuu Dar-es salaam, lililohusu suala la uhuru wa Tume ya Uchaguzi, wadai walitoa hoja kuwa, Rais kuwa Mwenyekiti wa chama hapaswi kuhodhi mamlaka ya kuteua wajumbe wa Tume ya Uchaguzi. Mahakama iliamua kuwa, kitendo cha wajumbe wa Tume kuteuliwa na Rais ambaye ni kiongozi wa chama cha siasa, hakiifanyi Tume kushindwa kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo.

### 5.4.3 Maoni ya Wadau

Baadhi ya wadau walipendekeza mfumo wa sasa uendelee, kwa sababu Katiba inalinda uhuru wa Tume ya Uchaguzi. Katika kutetea hoja hiyo wadau hao walieleza kuwa, hoja ya kwamba wajumbe wa Tume ya Uchaguzi wanateuliwa na Rais ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Siasa haina msingi, kwa kuwa hata Majaji wanateuliwa na Rais na wanatenda haki. Walisema, kabla Rais hajafanya uteuzi, kuna mchakato hufanywa na vyombo mbalimbali vya Serikali kuhakikisha kwamba, mjumbe wa Tume ya Uchaguzi anayeteuliwa anakuwa ni mtu muadilifu mwenye ujuzi, weledi na heshima katika jamii.

Wadau wengine walipendekeza mfumo wa sasa wa kupata wajumbe wa Tume ya Uchaguzi uboreshwe, ili kuongeza uwazi katika mchakato huo. Wadau hao walipendekeza kwamba, kuwe na Kamati ya Uteuzi wa Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi, nafasi zitangazwe na watu wanaopenda kuwa wajumbe wa Tume ya Uchaguzi waombe. Kamati ya Uteuzi ifanye usaili, ichuje majina na kupendekeza kwa Rais watu wanaofaa kuteuliwa kuwa wajumbe

wa Tume ya Uchaguzi, na Rais ateue wajumbe wa Tume ya Uchaguzi kutoka miongoni mwa majina yaliyowasilishwa kwake na Kamati ya Uteuzi. Aidha, baadhi ya wadau walipendekeza kuwa, Rais asihusike kabisa katika mchakato wa uteuzi wa wajumbe wa Tume ya Uchaguzi, lakini hawakueleza jinsi wajumbe hao watakavyopatikana.

### 5.4.4 Uzoefu wa Nchi Nyingine

Kikosi Kazi kilifanya mapitio ya nyaraka mbalimbali kuhusu mchakato wa uteuzi wa wajumbe wa Tume za Uchaguzi katika nchi mbalimbali ili kupata uzoefu kutoka katika nchi hizo. Nchini Afrika Kusini, kuna Kamati ya Uteuzi wa wajumbe wa Tume ya Uchaguzi yenye wajumbe wafuataο:

a) Rais wa Mahakama ya Katiba ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati;
b) mwakilishi kutoka Tume ya Haki za Binadamu;
c) mwakilishi kutoka Tume ya Usawa wa Jinsia; na
d) Mlinzi wa Umma (Public Protector).

Jukumu la Kamati hiyo ni kupokea majina ya watu wanaoomba kuwa wajumbe wa Tume ya Uchaguzi, kuyachambua na kuandaa orodha ya majina ya watu yasiyozidi wanane (8) na kuyawasilisha kwa Kamati ya Bunge yenye uwakilishi wa vyama vyote. Kamati huwasilisha mapendekezo yake Bungeni ili kuidhinishwa kwa njia ya kupigiwa kura. Kisha Bunge huwasilisha mapendekezo yake kwa Rais kwa ajili ya uteuzi. Pamoja wa uwepo wa mchakato huo, Tume ya Uchaguzi ya Afrika Kusini inakuwa na mjumbe mmoja

ambaye huteuliwa na Rais bila kufuatwa kwa mchakato huo, mjumbe huyo anapaswa kuwa ni Jaji.

Nchini Kenya, inapohitajika kuteua mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, inaundwa Kamati ya Uteuzi wa Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi ambayo ina wajumbe tisa wafuatao:

a) watu wanne kwa kuzingatia jinsia waliopendekezwa na Tume ya Huduma za Bunge; na
b) watu watano (5) waliopendekezwa na taasisi za dini, ikiwemo, Mkutano wa Maaskofu Wakatoliki; Baraza la Taifa la Makanisa; Baraza la Waislamu; Umoja wa Makanisa ya Kiinjilisti na Baraza la Wahindu.

Kamati ya Uteuzi hufanya kazi ya kusaili watu walioomba kuteuliwa kuwa wajumbe wa Tume ya Uchaguzi, kisha kuwasilisha mapendekezo yake katika Bunge la Kenya. Bunge linajadili majina yaliyowasilishwa, kuyaidhinisha na kuyawasilisha kwa Rais kwa ajili ya uteuzi.

Nchini Botswana, Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi wanateuliwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama. Mwenyekiti anapaswa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu na Makamu Mwenyekiti ni mwanasheria. Wajumbe wengine watano huteuliwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama kutoka kwenye orodha ya watu waliopendekezwa na mkutano wa vyama vyote vya siasa.

Nchini Uganda, Tume ya Uchaguzi ina wajumbe saba ambao wanateuliwa na Rais na kuthibitishwa na Bunge. Nchini Zambia, Tume ya Uchaguzi ya Zambia inaundwa na Wajumbe watano ambao huteuliwa na Rais na kuridhiwa na Bunge.

### 5.4.5 Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Baada ya kupitia maoni ya wadau, uzoefu wa nchi nyingine na nyaraka mbalimbali, Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa, utaratibu wa kumpata Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi uboreshwe, ili kuongeza uwazi katika upatikanaji wao, Utaratibu huo uwe ifuatavyo:

a) kuwe na Kamati ya Uteuzi ya Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi itakayokuwa na wajumbe wafuatao:
   i) Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye atakuwa ni Mwenyekiti;
   ii) Jaji Mkuu wa Zanzibar ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti; iii) Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Tanzania Bara; iv) Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Zanzibar;
   v) Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu; na vi) wajumbe wengine wawili watakaoteuliwa na Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya kupendekezwa na Chama cha Wanasheria Tanganyika na Chama cha Wanasheria Zanzibar.

b) angalau wajumbe wawili wa Kamati ya Uteuzi wawe wanawake;

c) sifa za mtu kuwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ziainishwe;

d) nafasi ya mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi itangazwe na Mtanzania yeyote mwenye sifa aruhusiwe

kuwasilisha maombi kwa Kamati ya Uteuzi ya kuwa mjumbe wa Tume;

e) Kamati ya Uteuzi ifanye usaili wa watu waliowasilisha maombi ya kuwa wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na kupendekeza kwa Rais majina ya watu wanaostahili kuteuliwa kuwa wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi;

f) Kamati ya Uteuzi itawasilisha kwa Rais majina manne (4) zaidi ya idadi ya nafasi zinazohitajika kujazwa;

g) Rais ateue wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi miongoni mwa majina yaliyowasilishwa kwake na Kamati ya Uteuzi; na

h) Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambaye anapaswa kuwa ni Jaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani aliye madarakani au mstaafu na Makamu Mwenyekiti ambaye anapaswa kuwa na sifa ya kuwa Jaji wa Mahakama Kuu au mstaafu, wateuliwe na Mheshimiwa Rais bila kufuata utaratibu wa kuomba na kusailiwa na Kamati ya Uteuzi.

## 5.5 Matokeo ya Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kutohojiwa Mahakamani

### 5.5.1 Hali Ilivyo Sasa

Ibara ya 41 (7) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 imeainisha kuwa, iwapo mgombea ametangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwamba amechaguliwa kuwa Rais, basi hakuna Mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza kuchaguliwa kwake.

### 5.5.2 Mapendekezo ya Tume na Kamati Mbalimbali

Tume na kamati mbalimbali nchini, ziliwahi kulifanyia kazi suala la matokeo ya Rais kutohojiwa Mahakamani na kuainisha mapendekezo yao. Tume ya Jaji Nyalali (1991) ilipendekeza kwamba, matokeo ya uchaguzi wa Rais yasihojiwe wala kuthibitishwa na Mahakama au chombo chochote isipokuwa Tume ya Uchaguzi. Vilevile, kupitia ibara ya 81(1) ya Rasimu ya Pili ya Katiba, Tume ya Jaji Warioba ilipendekeza matokeo ya uchaguzi wa Rais yahojiwe Mahakamani na mgombea wa Urais yeyote ambaye hajaridhika.

Ibara ya 90(1) ya Katiba Inayopendekezwa inaeleza kuwa, mgombea yeyote wa Urais ambaye hajaridhika na matokeo ya uchaguzi wa Rais, anaweza kuwasilisha malalamiko katika Mahakama ya Juu kupinga matokeo ya uchaguzi huo. Malalamiko ya kupinga matokeo ya uchaguzi wa Rais yatawasilishwa Mahakama ya Juu ndani ya muda wa siku saba tangu siku ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi wa Rais. Mahakama ya Juu itasikiliza na kutoa uamuzi wa shauri la kupinga matokeo ya uchaguzi huo, ndani ya siku kumi na nne tangu kupokea malalamiko yaliyowasilishwa na uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

### 5.5.3 Maoni ya Wadau

Katika eneo hili wadau walitoa maoni kwamba Katiba na Sheria za Uchaguzi ziboreshwe ili kuruhusu matokeo ya uchaguzi wa Rais kuhojiwa Mahakamani, kama ilivyo kwa matokeo ya madiwani na wabunge. Wadau walitoa sababu kuwa, kwa kuzingatia dhana ya utawala wa sheria ni vyema uamuzi unaofanywa na vyombo

mbalimbali vya Serikali kuhojiwa Mahakamani, ili kutenda haki, kuleta uwazi na uwajibikaji. Aidha, wadau walieleza zaidi kuwa, matokeo ya uchaguzi wa Rais kuhojiwa Mahakamani inaongeza imani ya wadau kwa uchaguzi husika.

#### 5.5.4 Uzoefu wa Nchi Nyingine

Nchi za Kenya, Ghana, Afrika Kusini na Zambia ni mfano wa nchi ambazo katiba zao zinaruhusu kuhoji matokeo ya uchaguzi wa Rais Mahakamani.

#### 5.5.5 Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Baada ya kupitia maoni ya wadau, uzoefu wa nchi nyingine na nyaraka mbalimbali, Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa, matokeo ya uchaguzi wa Rais yahojiwe kwenye Mahakama ya Juu mara itakapoanzishwa.

### 5.6 Watendaji wa Tume ya Uchaguzi

#### 5.6.1 Hali Ilivyo Sasa

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina Sekretarieti inayoongozwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi anayeteuliwa na Rais. Mkurugenzi wa uchaguzi ni msimamizi wa kazi za kila siku za Tume ya Uchaguzi, Katibu wa vikao na Afisa Masuhuli wa Tume. Tume ina watendaji waliopo ofisi za makao makuu pekee. Wakati wa uchaguzi Tume huteua baadhi ya watumishi wa Serikali kusimamia shughuli za uchaguzi. Kifungu cha 7 (1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi

kinatamka kuwa, kila Mkurugenzi wa Jiji, Manispaa, Mji na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ni msimamizi wa uchaguzi wa jimbo. Kifungu cha 7(2) cha Sheria kinatamka kuwa, Tume inaweza kumchagua mtumishi wa umma kwa nafasi yake au jina kuwa Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi wa Jimbo. Aidha, Kifungu 7(3) cha Sheria hiyo kinatamka kuwa, Tume ya Uchaguzi inaweza kumteua afisa yeyote kwa nafasi ya ofisi yake au jina lake, kutoka utumishi wa umma, kuwa msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi katika jimbo. Ikitokea akateuliwa mtumishi mwingine wa umma, Mkurugenzi wa Jiji, Manispaa, Mji na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya watakoma kushika nafasi zao kama Wakurugenzi wa Uchaguzi au Wakurugenzi Wasaidizi wa Uchaguzi.

### 5.6.2 Mapendekezo ya Tume na Kamati Mbalimbali

Tume na kamati mbalimbali nchini, ziliwahi kulifanyia kazi suala la watendaji wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na kuainisha mapendekezo yao.

Kupitia ibara ya 196(3) ya Rasimu ya Pili ya Katiba, Tume ya Jaji Warioba ilipendekeza kwamba, katika kutekeleza madaraka yake Mkurugenzi wa Uchaguzi atatekeleza majukumu yake kwa kusaidiwa na watendaji ambao ni watumishi wa umma kwa kadri idadi itakavyohitajika. Mapendekezo hayo yaliridhiwa na Bunge Maalum la Katiba na kuwekwa katika ibara ya 223(3) ya Katiba Inayopendekezwa.

Aidha, Ripoti za Uchaguzi za Mwaka 1995, 2000, 2005, 2010, 2015 na 2020, zimesisitiza haja ya Tume kuwa na ofisi pamoja na watendaji wake hadi ngazi za halmashauri. Hali hii itasaidia uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura muda wote pamoja na shughuli nyingine za uchaguzi kuendeshwa kwa ufanisi zaidi katika ngazi ya Taifa na halmashauri.

Ripoti za waangalizi mbalimbali wa uchaguzi kutoka Tanzania na nje ya nchi, zimekuwa zikipendekeza Tume ya Uchaguzi kuwa na watendaji wake katika ngazi ya halmashauri ili kuongeza uhuru na ufanisi wake. Mfano, Ripoti ya Waangalizi wa Uchaguzi wa Umoja wa Afrika inaeleza kuwa *"There is a lack of a decentralized structures of NEC at the local levels and the use of local government officials as election managers with implications for the independence of the NEC."* Tafsiri ya Kiswahili ya maelezo haya iliyofanywa na Kikosi Kazi ni kuwa; "NEC haina mfumo wa ugatuzi wa madaraka hadi ngazi za chini na pia inatumia maafisa wa serikali za mitaa kama wasimamizi wa uchaguzi, kitu ambacho huathiri uhuru wa Tume." Hivyo, ripoti hiyo ilipendekeza kuwepo kwa ugatuzi wa madaraka ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi nchi nzima ili kuongeza uhuru na ufanisi wa Tume hiyo.

### 5.6.3 Maoni ya Wadau

Katika eneo hili wadau walitoa maoni na mapendekezo yafuatayo:

a) katika kutekeleza majukumu yake ya kusimamia uchaguzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatumia watendaji wa Serikali, hali inayojenga hofu kwa baadhi ya wagombea kuwa watendaji hao watapendelea baadhi ya wagombea;

b) kwa kuwa Tume inatumia watumishi wa Serikali kusimamia uchaguzi katika ngazi ya halmshauri, kuna hisia kuwa baadhi yao wamekuwa wakipata maelekezo kutoka kwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa;

c) endapo Tume ya Taifa ya Uchaguzi itakuwa na watumishi wake hadi ngazi ya halmashauri, wadau wenye mtazamo kuwa, uhuru wa Tume unaathirika kwa kutumia watumishi wa Serikali kusimamia uchaguzi wataona uhuru wa Tume kusimamia uchaguzi umeongezeka;

d) mfumo wa sasa uendelee kutumika, kwa kuwa watumishi wa Serikali na hasa wa Serikali za Mitaa wana uzoefu wa kusimamia uchaguzi na unapunguza gharama za kusimamia uchaguzi;

e) watumishi wa umma watumiwe kusimamia uchaguzi kwani, wanaweza kupatikana kwa urahisi na kuwajibishwa pale wanapokiuka maadili ya kazi;

f) kutumia watumishi wa umma katika kusimamia uchaguzi kuna gharama nafuu, ikilinganishwa na kuwa na ajira za kudumu za watumishi wa Tume, ambako kutaleta gharama kubwa za kulipa mishahara, mafao, marupurupu, kuandaa miundombinu ya ofisi, magari, pamoja na kuwa na bajeti kubwa ya matumizi ya kawaida;

g) kutumia ofisi na miundombinu mingine inayotumiwa na watumishi wa umma nchi nzima, kunarahisisha uendeshaji wa uchaguzi;

h) uchaguzi ni shughuli inayofanyika kila baada ya miaka mitano na hivyo hakuna haja ya Tume kuwa na wafanyakazi wake nchi nzima;

i) kutumia wafanyakazi wa umma kunaisaidia Tume kuwa na uzoefu na kumbukumbu ya kitaasisi, ambayo ni muhimu katika kuboresha shughuli za uchaguzi;

j) baadhi ya nchi ambazo demokrasia yao imekua na pia zina uchumi mkubwa kama vile Marekani, Uingereza, Denmark, Ufaransa na Uswizi, zinatumia watumishi wa umma kusimamia uchaguzi, hakuna malalamiko kuhusu matumizi ya watumishi hao; na

k) Tanzania imefanya Uchaguzi Mkuu mara sita tangu Mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa urejee mwaka 1992, katika uchaguzi huo, mara tano wametumika watumishi wa umma kusimamia uchaguzi na hapakuwa na malalamiko ya msingi kuhusu matumizi yao, isipokuwa uchaguzi wa 2020.

### 5.6.4 Uzoefu wa Nchi Nyingine

Kikosi Kazi kilifanya mapitio ya nyaraka mbalimbali kuhusu watendaji wa Tume za Uchaguzi katika nchi mbalimbali ili kupata uzoefu kutoka katika nchi hizo. Nchini Uganda, Tume ya Uchaguzi, kupitia Sheria ya Uchaguzi ya Uganda ya mwaka 1997, imepewa mamlaka ya kuteua wasimamizi wa uchaguzi kutoka sehemu yoyote. Tume hiyo haijafungwa kutumia watumishi wa serikali au wakurugenzi wa halmashauri.

Nchini Kenya, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ina Katibu wa Tume ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Tume, Makatibu Wasaidizi wawili (2) wa Tume, Wakurugenzi tisa (9), Mameneja ishirini na nne (24), Mameneja wa Uchaguzi wa Serikali za Majimbo arobaini na

saba (47) na Waratibu wa Majimbo ya Uchaguzi mia mbili na tisini (290). Maafisa hawa wa Tume huajiriwa na Tume yenyewe. Vilevile, Tume huajiri wasimamizi wa uchaguzi kwenye Serikali za Majimbo na Majimbo ya Uchaguzi.

### 5.6.5 Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Baada ya kupitia maoni ya wadau, uzoefu wa nchi nyingine na nyaraka mbalimbali, Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa:

a) Tume iendelee kutumia watumishi wa umma kusimamia uchaguzi;
b) watumishi wa umma wawajibike moja kwa moja kwa Tume ya Uchaguzi kwa masuala yanayohusu shughuli za uchaguzi kwa mujibu wa sheria;
c) wasimamizi wa uchaguzi wazingatie sheria, weledi, maadili, uwazi na ushirikishwaji wa wadau wakati wa kufanya kazi zao; na
d) wasimamizi wa uchaguzi watakaokiuka sheria na utaratibu wawajibishwe kwa mujibu wa Sheria.

## 5.7 Bajeti ya Tume ya Uchaguzi

### 5.7.1 Hali Ilivyo Sasa

Kifungu cha 122 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 kinaeleza kuwa gharama za kuendesha uchaguzi zitatolewa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Bajeti ya matumizi ya kawaida ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi hupitishwa na Bunge kila mwaka. Vilevile, fedha za kusimamia uchaguzi hutengwa pale inapohitajika.

### 5.7.2 Mapendekezo ya Tume, Kamati Mbalimbali na Utafiti

Tume mbalimbali zilizoteuliwa kabla ya Kikosi Kazi ziliwahi kujadili suala la bajeti ya Tume ya Uchaguzi na kutoa mapendekezo. Ripoti ya Utafiti ya Tume ya Jaji Warioba inapendekeza kuwa, Tume ya Uchaguzi iwe na bajeti yake ambayo inaidhinishwa na Bunge kila mwaka ili kuongeza uhuru wa Tume na ufanisi katika kutimiza majukumu yake.

Ripoti za Tume za Uchaguzi za mwaka 1995, 2000, 2005, 2010, 2015 na 2020 hazijaonesha tatizo la upatikanaji wa fedha kutoka serikalini katika kuendesha shughuli za uchaguzi. Aidha, ripoti hizo zinaeleza kuwa, ni vyema Tume ya Uchaguzi ikapewa fedha za kutosha kwa ajili ya kutoa elimu ya mpiga kura hata baada ya uchaguzi.

### 5.7.3 Maoni ya Wadau

Katika eneo hili wadau walitoa maoni na mapendekezo yafuatayo:

a) Tume iwe inapata bajeti yake kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina; na
b) kuanzishwe mfuko wa uchaguzi ili kuhakikisha Tume ya Uchaguzi inapata fedha kwa wakati na za kutosha ili itimize majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

### 5.7.4 Uzoefu wa Nchi Nyingine

Kikosi Kazi kilifanya mapitio ya nyaraka mbalimbali kuhusu bajeti za Tume za Uchaguzi katika nchi mbalimbali ili kupata uzoefu kutoka

katika nchi hizo. Nchini Afrika Kusini, kifungu cha 13 na 14 cha Sheria ya Uchaguzi kinaeleza kuwa Tume itapata fedha kutoka bajeti ya kila mwaka ya Serikali kupitia Bunge. Aidha, nchini Kenya, ibara ya 249(3) ya Katiba ya Kenya inaeleza kuwa, Bunge litatenga fedha za kutosha kwa Tume ya Uchaguzi ili iweze kutekeleza majukumu yake. Vilevile, katika nchi ambazo uchaguzi unasimamiwa na watumishi wa Serikali kupitia idara au Wizara ya Serikali (Government Model), bajeti ya kusimamia uchaguzi huratibiwa na Wizara husika.

#### 5.7.5 Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Baada ya kupitia maoni ya wadau, uzoefu wa nchi nyingine na nyaraka mbalimbali, Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ipewe fedha zilizotengwa katika bajeti kwa wakati, hata baada ya uchaguzi, ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote.

### 5.8 Usimamizi wa Uchaguzi

Usimamizi wa uchaguzi hufanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa upande wa Uchaguzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwa upande wa Zanzibar. Vyombo hivi ndio vimepewa nguvu ya kisheria kusimamia uchaguzi na kutangaza matokeo. Aidha, katika kusimamia uchaguzi, vyombo hivi hushirikisha wadau mbalimbali ikiwemo asasi za kiraia, waangalizi wa uchaguzi, Vyama vya Siasa, wadau wa maendeleo, vyombo vya habari na vyombo vya ulinzi na usalama. Uchaguzi wa

Serikali za Mitaa husimamiwa na ofisi ya Rais yenye dhamana na Serikali za Mitaa.

### 5.8.1 Uwezekano wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

#### 5.8.1.1 Hali Ilivyo Sasa

Ibara ya 145 na 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, zimeanzisha Mamlaka ya Serikali za Mitaa nchini na kuainisha majukumu yake. Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 146 ya Katiba, madhumuni ya kuanzishwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, ni kuimarisha demokrasia na kuitumia demokrasia katika kuharakisha maendeleo, kupeleka madaraka kwa wananchi, kuwahudumia wananchi na kuwajengea uwezo wa kisiasa, kiuchumi, na kijamii.

Ibara ya 3(1) na 8(1) ya Katiba zinabainisha wazi kwamba, Tanzania ni nchi ya kidemokrasia na wananchi ndio msingi wa mamlaka yote. Kama ilivyo kwa uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, viongozi wa Serikali za Mitaa hupatikana kwa kupigiwa kura kwa njia ya kidemokrasia. Uchaguzi wa viongozi ngazi ya vijiji, vitongoji na mitaa hufanyika kila baada ya miaka mitano. Kwa mara ya mwisho, uchaguzi huo ulifanyika tarehe 24 Novemba 2019 ikiwa ni uchaguzi wa sita tangu kurejea kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini, mwaka 1992.

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unasimamiwa na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288. Kwa kutumia mamlaka

aliyopewa na sheria tajwa, Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa, huandaa Kanuni ambazo hutumika kusimamia uchaguzi huo. Hivyo, kwa mujibu wa Ibara ya 145 na 146 ya Katiba, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unasimamiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Kwa mujibu wa kifungu cha 56(1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 kikisomwa pamoja na Kanuni ya 6 ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji za Mwaka 2019, Serikali ya kijiji inaundwa na wajumbe wasiopungua 15 na wasiozidi 25, miongoni mwao ni Mwenyekiti wa Kijiji, Wenyeviti wa vitongoji vilivyomo katika eneo la kijiji na Wajumbe wa kuchaguliwa wakiwemo wanawake wasiopungua moja ya tatu (1/3) ya wajumbe wote wa halmashauri ya kijiji.

Kwa mujibu wa kanuni ya 6 ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika Mamlaka za Miji za Mwaka 2019, Kamati ya Mtaa ina wajumbe wasiozidi sita ambao ni Mwenyekiti wa Mtaa na wajumbe wengine watano ambao kati yao wajumbe wawili ni wanawake. Katika Taarifa ya Tume ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, wadau wa uchaguzi wamependekeza Uchaguzi Mkuu na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa usimamiwe na mamlaka moja.

#### 5.8.1.2 Maoni ya Wadau

Katika eneo hili wadau walitoa maoni na mapendekezo yafuatayo:

a) kuwepo na mamlaka moja inayosimamia Uchaguzi Mkuu,

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kura ya maoni nchini;

b) utaratibu wa sasa uendelee, ambapo Tume ya Taifa ya Uchaguzi inasimamia uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani na Ofisi ya Rais TAMISEMI inasimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kwani ni vigumu uchaguzi huu kusimamiwa na mamlaka moja kutokana na ukubwa wa jukumu la kuusimamia;

c) maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa yaboreshwe;

d) uwepo ushirikishwaji wa kutosha na uwazi wa uendeshaji wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa;

e) uchaguzi wa Serikali za Mitaa usisimamiwe na Waziri ili kuufanya uwe huru na wa haki;na

f) endapo itaamuliwa kuwa Tume isimamie na kuratibu uendeshaji wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kutakuwepo na manufaa yafuatayo:

   i) uchaguzi utasimamiwa na kuratibiwa na chombo kimoja chenye utaalam na mifumo ya kusimamia uchaguzi nchini;

   ii) zoezi la uandikishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura litafanywa na mamlaka moja. Daftari hilo litatumika kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu; iii) baadhi ya vifaa kama vile vifaa vya TEHAMA, masanduku ya kura, vituturi, mihuri na taa vitatumika katika chaguzi zote mbili;

   iv) mifumo ya uchaguzi iliyopo itatumiwa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili kuongeza tija na ufanisi.

Changamoto zifuatazo zinaweza kujitokeza endapo Tume itapewa jukumu la kusimamia na kuratibu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa:

a) muda wa maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani unaweza kuwa changamoto kwa kuwa uchaguzi wa Serikali za Mitaa unapishana na uchaguzi huo kwa kipindi kifupi. Shughuli za maandalizi zinazoweza kuathirika ni kama vile ununuzi wa vifaa vya uchaguzi, ugawaji wa majimbo, uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ambao hutakiwa kufanyika mara mbili kati ya uchaguzi mkuu mmoja na unaofuata kwa mujibu wa sheria, mafunzo ya watendaji na marekebisho ya sheria;

b) kuna uwezekano wa gharama za kuendesha uchaguzi kuongezeka kwa kuwa Tume itatakiwa kuzingatia viwango vya uchaguzi vya kikanda na kimataifa ambavyo imekuwa ikivitumia katika kuendesha Uchaguzi Mkuu. Gharama hizi zitatokana na ongezeko la vifaa, matumizi ya mifumo ya menejimenti ya uchaguzi, mikutano ya wadau, ongezeko la watendaji wa uchaguzi, mafunzo ya watendaji na gharama za kuendesha kesi za uchaguzi;

c) inaweza kusababisha mgongano wa uwajibikaji kwani Serikali za Mitaa zipo chini ya mamlaka nyingine na hivyo kuifanya Tume ya Uchaguzi kuwajibika kwa Waziri wa TAMISEMI;

d) kuufanya uchaguzi wa Serikali za Mitaa usimamiwe na Tume ya Uchaguzi ni kuiondolea TAMISEMI jukumu lake la msingi kwa mujibu wa ibara ya 146 ya Katiba, ambalo ni kuimarisha demokrasia na kuitumia demokrasia katika kuharakisha maendeleo, kupeleka madaraka kwa wananchi, kuwahudumia wananchi na kuwajengea uwezo wa kisiasa, kiuchumi, na kijamii.

e) changamoto zilizopo katika uendeshaji wa uchaguzi wa serikali za mitaa zinaweza kuathiri utendaji wa Tume na kuaathiri usimamizi wa uendeshaji wa uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani;

f) itasababisha viongozi wa Serikali za Mitaa kudai stahiki ambazo kwa sasa hawana;

g) mahitaji ya vifaa vya uchaguzi yataongezeka kwani Tume ya Uchaguzi inatumia utaratibu tofauti na ule wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa;

h) idadi ya watendaji wa uchaguzi watakaotumika katika zoezi husika itaongezeka; na

i) gharama za uratibu wa zoezi la upigaji kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo zitaongezeka.

#### 5.8.1.3 Uzoefu kutoka Nchi Nyingine

Uzoefu unaonesha kwamba, tafsiri ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa inatofautiana kati ya nchi moja na nyingine, kulingana na sheria na desturi za nchi husika. Katika baadhi ya nchi ikiwemo Zimbabwe, Botswana na Burundi uchaguzi wa Serikali za Mitaa, unamaanisha uchaguzi wa madiwani. Kwa Afrika Kusini, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unahusisha uchaguzi wa madiwani na

mameya na hufanyika miaka miwili baada ya Uchaguzi Mkuu na unasimamiwa na Tume ya Uchaguzi. Aidha, kwa nchi ya Uganda, uchaguzi wa Serikali za Mitaa unamaanisha uchaguzi wa viongozi kwa ngazi ya tarafa, kata, mitaa na vijiji na hufanyika mwezi mmoja baada ya Uchaguzi Mkuu wa Rais na Wabunge. Nchini Rwanda, uchaguzi wa Serikali za Mitaa unahusisha uchaguzi ngazi ya chini kabisa ya utawala, shina na kijiji na unasimamiwa na Tume ya Uchaguzi ya Rwanda.

Nchini Zambia, kuna mamlaka mbili zinazosimamia uchaguzi, yaani Tume ya Uchaguzi ya Zambia na Tume ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Tume ya Uchaguzi inasimamia Uchaguzi Mkuu na Tume ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa inasimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

#### 5.8.1.4 Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Baada ya kupitia maoni ya wadau, uzoefu wa nchi nyingine, nyaraka mbalimbali na historia ya siasa na demokrasia nchini, Kikosi Kazi kinapendekeza yafuatayo:

a) kasoro zilizojitokeza katika uchaguzi uliopita zifanyiwe kazi; na
b) Serikali ifanye utafiti wa kina kuhusu namna bora ya kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili kuufanya uwe wa kidemokrasia zaidi.

### 5.8.2 Sheria Zinazosimamia Masuala ya Uchaguzi

#### 5.8.2.1 Hali ilivyo Sasa

Tume ya Taifa ya Uchaguzi haina sheria yake. Aidha, kuna sheria mbili zinazoratibu uchaguzi, ambazo ni Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343 na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura 292.

#### 5.8.2.2 Mapendekezo ya Tume na Kamati Mbalimbali

Katika ripoti za uchaguzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekuwa ikitoa mapendekezo ya kutungwa kwa Sheria ya Tume ya Uchaguzi, ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Katika ripoti hizo, imeelezwa kuwa, ni muhimu Tume ya Taifa ya Uchaguzi iwe na sheria yake, tofauti na sheria inayosimamia masuala ya uchaguzi, ili kurahisisha na kuongeza ufanisi wa kusimamia masuala ya muundo, utawala, utumishi na utendaji wake. Aidha, Tume ya Uchaguzi imekuwa ikipendekeza kuunganishwa kwa Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343 na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura 292, ili kurahisisha utekelezaji wa sheria hizo.

#### 5.8.2.3 Uzoefu wa Nchi Nyingine

Nchini Uganda, Tume ya Uchaguzi ina sheria yake “Electoral Commission Act, 1997”. Sheria hii ndio inaipa Tume mamlaka ya

kusimamia uchaguzi wote pamoja na kura za maoni. Nchini Kenya, Tume ya Uchaguzi ina sheria yake; “Independent Electoral and Boundaries Commission Act 9 of 2011”, inayoipa mamlaka ya kuwa chombo kinachosimamia uchaguzi na kura za maoni nchini Kenya. Vilevile, nchini Afrika Kusini, Tume ya Uchaguzi ina sheria yake iitwayo “Electoral Commission Act 51 of 1996”. Sheria hii inaweka masharti ya kuunda Tume ya Uchaguzi ya kusimamia uchaguzi wa Taifa, Majimbo, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Kura ya Maoni.

#### 5.8.2.4 Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Baada ya kuzingatia maoni ya wadau, taarifa mbalimbali na uzoefu wa nchi nyingine, Kikosi Kazi kinapendekeza yafuatayo:

a) itungwe sheria ya kusimamia shughuli za Tume ya Taifa Uchaguzi;
b) kuwepo na sheria moja ya uchaguzi itakayotumika kusimamia uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani, badala ya kuwa na sheria mbili ambazo ni Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343 na Sheria ya Uchaguzi wa Madiwani, Sura 292; na
c) maafisa wa Tume ya Uchaguzi watakaowaengua wagombea kushiriki katika uchaguzi bila kuzingatia sheria na weledi wawajibishwe kwa mujibu wa sheria.

### 5.9 Matumizi ya TEHAMA Katika Uchaguzi

Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika uchaguzi ni maendeleo ya takribani miongo miwili. Kuna nchi

chache Afrika ambazo zimeanza kutumia teknolojia hii katika kuandikisha wapiga kura, kupiga kura, kuhesabu na kufanya ujumlishaji wa mwisho na kutangaza mshindi. Nchi ambazo zimeanza kutumia TEHAMA kwa viwango tofauti ni pamoja na Kenya, Ghana, Nigeria, Afrika Kusini na Tanzania. Matumizi ya TEHAMA yanaongeza ubora wa uchaguzi, usalama wa kura, uwazi na uwajibikaji, urahisi na ufanisi katika kuendesha zoezi la uchaguzi. Hata hivyo, TEHAMA imekuja na changamoto zake kama vile usalama wa kura, gharama kubwa za mifumo ya TEHAMA, kushindwa kutumika katika baadhi ya maeneo kutokana na kukosekana kwa miundombinu na pia ina mashaka katika kuaminika.

Katika kusimamia uchaguzi, TEHAMA inaweza kufanya kazi kwa ufanisi kutegemea na sababu mbalimbali, ikiwemo kiwango cha maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika nchi husika, utamaduni wa kisiasa, historia ya uchaguzi katika nchi husika, utayari wa wadau kutumia TEHAMA na uwepo wa miundombinu inayowezesha TEHAMA kutumika. Hivyo, kuhusu suala la matumizi ya TEHAMA katika kusimamia uchaguzi, ni muhimu nchi husika kuchagua mfumo wa TEHAMA unaofaa kwa mazingira yake.

### 5.9.1 Hali Ilivyo Sasa

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeanza kutumia mifumo ya TEHAMA iliyosanifiwa na kujengwa na wataalam wa ndani ya nchi katika usajili wa wagombea, usajili wa watazamaji, uhakiki wa taarifa za wapiga kura na vituo, kujumlisha na kutangaza matokeo. Wakati wa kutekeleza zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga

Kura, Tume ilitumia mifumo ya TEHAMA ikijumuisha Mfumo wa Uandikishaji Wapiga Kura (Voters Registration System - VRS), Mfumo wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura (Permanent National Voters Register Sytem - PNVRS), Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole - AFIS na Mfumo wa Uhakiki wa Taarifa za Wapiga Kura (Voters Interaction System -VIS).

### 5.9.2 Maoni ya Wadau

Katika eneo hili wadau walitoa maoni na mapendekezo yafuatayo:

a) kiwango cha matumizi ya TEHAMA katika mchakato wa uchaguzi nchini hakijawekwa;
b) hakuna Kanuni mahsusi za matumizi ya TEHAMA kwenye uchaguzi; na
c) uwekezaji wa kutosha kwenye miundombinu ya TEHAMA na usalama wake unahitajika.

### 5.9.3 Uzoefu wa Nchi Nyingine

Nchini Kenya, kifungu cha 44 cha Sheria ya Uchaguzi ya Mwaka 2011 kinaweka masharti ya matumizi ya TEHAMA katika uchaguzi. Aidha, kuna Kanuni zinazoratibu matumizi ya TEHAMA katika uchaguzi zilizotungwa mwaka 2017. Kwa ujumla, Kenya inatumia TEHAMA katika kuandikisha wapiga kura, kuwatambua wapiga kura na kusafirisha matokeo kwenda kwenye kituo cha majumuisho ya kura. Aidha, matumizi ya TEHAMA nchini Kenya yamekuwa yakikutana na changamoto mbalimbali, zikihusisha ununuzi wa mifumo ya TEHAMA na kuaminika kwa mifumo hiyo. Nchi nyingine zinazotumia TEHAMA kwenye uchaguzi kwa viwango tofauti ni Afrika Kusini, Ghana, Uganda, Nigeria na Botswana.

### 5.9.4 Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Baada ya kuzingatia maoni ya wadau, taarifa mbalimbali na uzoefu wa nchi nyingine, Kikosi Kazi kinapendekeza yafuatayo:

a) matumizi ya TEHAMA katika mchakato wa uchaguzi yahamasishwe na kiwango chake kiongezwe;

b) zitayarishwe Kanuni mahsusi za kuratibu matumizi ya TEHAMA kwenye mchakato wa uchaguzi; na

c) kuwepo na uwekezaji wa kutosha kwenye miundombinu ya TEHAMA na usalama wake wakati wa uchaguzi.

# SURA YA SITA

# USHIRIKI WA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM KATIKA SIASA, DEMOKRASIA NA UONGOZI

## 6.1 Utangulizi

Makundi maalum kwa muktadha wa kisiasa, demokrasia na uongozi nchini ni wanawake, wazee, vijana na watu wenye ulemavu. Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania imesaini na kuridhia mikataba, itifaki na matamko mbalimbali ya kikanda na kimataifa zinazoelekeza nchi wanachama kulinda haki za Wanawake. Haki hizo ni pamoja na haki ya kutobaguliwa, haki ya kushiriki katika siasa, demokrasia, uongozi na kushiriki katika shughuli za kiuchumi. Vilevile, kupinga unyanyasaji na udhalilishaji wa wanawake. Tanzania imeweka baadhi ya matakwa ya mikataba, itifaki na matamko hayo ya kimataifa katika Katiba ya nchi, sera na sheria zake. Vilevile, zimeundwa taasisi na kuweka mikakati kusimamia utekelezaji wa misingi hiyo ya Katiba na Sheria, ili kuhakikisha haki za wanawake zinahifadhiwa na kutumiwa ipasavyo.

Tangu kupatikana kwa uhuru na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, zimekuwa zikifanya juhudi mbalimbali zinazolenga kuhakikisha makundi yote ya jamii yanashiriki kikamilifu katika shughuli za kisiasa, demokrasia na uongozi. Lengo kuu likiwa ni kuhakikisha matakwa ya Katiba ya usawa katika jamii yanatekelezwa, kama inavyoelezwa katika Ibara ya 12(1) ya Katiba

ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ibara ya 12 ya Katiba ya Zanzibar.

Wakati akipokea taarifa ya awali ya Kikosi Kazi Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alivisisitiza vyama vya siasa kuzingatia suala la usawa wa kijinsia kwa kutoa nafasi kwa wanawake ili washiriki katika siasa ndani ya vyama vyao. Vilevile, aliwataka wanawake kujua wajibu wao katika vyama vyao na katika jamii kwa ujumla na kuhakikisha kuwa wanaelewa ipasavyo agenda zinazowasemea.

## 6.2 Ushiriki wa Wanawake katika Siasa, Demokrasia na Uongozi

### 6.2.1 Mikataba, Itifaki na Matamko ya Kimataifa Kuhusu Ushiriki wa Wanawake katika Siasa, Demokrasia na Uongozi

Mikataba, itifaki na matamko ya kimataifa kuhusu ushiriki wa wanawake katika siasa, demokrasia na uongozi ambayo Tanzania imesaini na kuridhia ni pamoja na ifuatayo:

a) Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la Mwaka 1948 (Universal Declaration for Human Rights, 1948) lililobainisha usawa wa binadamu wote na haki ya kutobaguliwa;

b) Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa Mwaka 1966 (International Covenant on Economic, Social and Cultural Rights of 1966);

c) Azimio la Kimataifa kuhusu Haki za Kiraia na Kisiasa (International Covenant on Civil and Political Rights of 1966), linatoa haki za kisiasa na kiraia kwa watu wote;

d) Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (Convention on the Elimination of Discrimination Against Women CEDAW, 1979). Mkataba huu unaelekeza nchi wanachama kuchukua hatua stahiki katika kutokomeza ubaguzi wa aina zote dhidi ya wanawake. Aidha, unazitaka nchi wanachama kuchukua hatua za makusudi za muda mfupi na muda mrefu kurekebisha tofauti ya jinsia katika uongozi;

e) Mkataba Kuhusu Haki za Kisiasa za Wanawake wa Mwaka 1952 (The Convention of Political Rights of Women of 1952);

f) Azimio la Beijing la mwaka 1995 na mpango kazi wake (*Beijing Platform For Action 1995*). Mpango kazi huo ulibainisha maeneo 12 mahsusi ya kufanyia kazi kwenye kupambana na ubaguzi wa wanawake. Katika maeneo hayo 12, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilibainisha maeneo ya awali manne ya kipaumbele, ambapo moja wapo wa maeneo hayo ni ushiriki wa wanawake katika uongozi wa kisiasa na ngazi za maamuzi;

g) Mkataba wa Nchi za Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu (African Charter on Human and Peoples Rights, 1984);

h) Mkataba wa Afrika kuhusu Demokrasia, Uchaguzi na Utawala (African Charter on Democracy, Elections and Governance, 2007);

i) Tamko la Umoja wa Afrika kuhusu misingi inayoongoza uchaguzi wa kidemokrasia ndani ya Afrika. (African Union Declaration of Principal Governing Democratic Elections in Africa of 2022);

j) Sera ya Jinsia ya Umoja wa Afrika ya Mwaka 2009 (African Union Gender Policy of 2009);

k) Itifaki ya Mkataba wa Afrika juu ya haki za wanawake (Protocol to the African Charter on Human and Peoples' Rights on The Rights of Women in Africa, 2003, (Maputo Protocol)).

l) Sera ya Jinsia ya SADC (SADC Gender Policy);

m) Tamko la Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Jinsia na Maendeleo la Mwaka 1997 (SADC Declaration on Gender and Development, 1997);

n) Misingi na Miongozo inayoongoza uchaguzi wa kidemokrasia katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika. (SADC Principles and Guidelines Governing Democratic Elections, 2004 revised 2015);

o) Tamko la Jumuiya ya Maendeleo la Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) la Mwaka 2005 na Itifaki ya SADC ya Jinsia na Maendeleo la Mwaka 2008 (SADC Protocol on Gender and Development of 2008) linazitaka nchi wanachama kutekeleza kiwango cha chini cha uwakilishi wa wanawake kuwa asilimia 30, na baadaye kukipandisha kiwango hicho kuwa asilimia 50 katika ngazi zote za uongozi na maamuzi katika siasa na vyombo vya umma. Nchi wanachama wanahitajika;

p) kuhakikisha kuna usawa wa jinsia katika ngazi zote za Maamuzi;

q) kuwezesha wanawake kufikia na kumiliki rasilimali za nchi sawa na wanaume;

r) kurekebisha sheria zote kandamizi na zenye ubaguzi;

s) kuhakikisha wanawake wanapata haki ya elimu sawa na wanaume;

t) Ufuatiliaji wa Masuala ya Jinsia na Maendeleo wa Mwaka 2022 (SADC Gender and Development Monitor, 2022);

u) Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 1999 (The East African Community Treaty of 1999 (Articles 6(d),
7(2) na 121,);

v) Sera ya Jinsia ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (East African Community Gender Policy of 2018); na

w) Misingi ya Jumuiya ya Africa Mashariki kuhusu Uangalizi na Tathmini ya Uchaguzi ya Mwaka 2012 (East Africa Community Principles for Elections Observation and Evaluation of 2012).

### 6.2.2 Historia ya Ushiriki wa Wanawake Katika Siasa, Demokrasia na Uongozi

Wakati wa ukoloni wanawake wa TANU wakiongozwa na Bibi Titi Mohamed, waliungana kuhamasisha Wanawake wa Tanganyika kuunga mkono chama cha TANU. Baada ya uhuru walihamasisha wanawake wenzao kushiriki katika vyombo vya maamuzi, hivyo waliunda Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) tarehe 2 Novemba 1962 ambao ulikuwa ni jumuiya ya TANU na Mwenyekiti wake wa Kwanza alikuwa Bibi Titi Mohamed. Tarehe 4 Oktoba 1978 Umoja huo ulibadilishwa kuwa Jumuiya ya Wanawake wa Tanzania.

### 6.2.3 Mafanikio Yaliyopatikana katika Kupigania Haki za Wanawake Kushiriki katika Siasa, Demokrasia na Uongozi Nchini

Juhudi zilizofanyika na zinazofanyika katika kujumuisha Wanawake katika siasa, demokrasia na uongozi, ni pamoja na kuwa na sera zinazotoa mwongozo kuhusu ushiriki wa makundi hayo katika shughuli za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni, pamoja na kuwa na sheria, kanuni na miongozo inayoratibu suala hilo. Aidha, kuna mikakati mbalimbali inayosaidia utekelezaji wa sera, sheria, kanuni na miongozo hiyo. Hali kadhalika, kuna taasisi na programu maalum za kutetea, kushughulikia na kuratibu masuala ya Wanawake katika jamii. Mathalan, katika nchi yetu kuna nafasi maalum za ubunge, uwakilishi na udiwani kwa wanawake, pia kuna mikopo maalum kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Hivyo, kutokana na mikakati na jitihada hizo kuna mafanikio yaliyopatikana katika kupigania haki za wanawake kushiriki katika siasa, demokrasia na uongozi nchini ambayo ni pamoja na:

a) uwepo wa utashi wa kisiasa kushughulikia suala la haki za wanawake nchini;
b) kuongezeka kwa ushiriki wa wanawake katika siasa, demokrasia na uongozi, ikiwemo kuongezeka kwa idadi ya viongozi wanawake nchini, kuwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwanamke, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwanamke, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi mwanamke, Waziri wa Ulinzi wa kwanza mwanamke, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji mwanamke, Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwanamke, Wenyeviti wawili

Wanawake wa Vyama vya Siasa, Makatibu Wakuu wawili Wanawake wa Vyama vya Siasa, Wajumbe wanne Wanawake katika Baraza la Vyama vya Siasa, n.k.;

c) Tanzania kusaini na kuridhia mikataba, itifaki na matamko ya kimataifa kuhusu ushiriki wa wanawake katika siasa, demokrasia na uongozi;

d) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulinda haki za raia wote, ikiwemo haki ya wanawake kushiriki katika siasa, demokrasia na ngazi za maamuzi. Aidha, Ibara ya 12 inaeleza kuwa binadamu wote ni sawa ilhali Ibara ya 21 inaainisha haki ya wananchi wote kushiriki katika utawala wa nchi na Ibara 66 imeweka viti maalum vya wanawake Bungeni;

e) kuwepo kwa Sera ya Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 1992 (Policy on Women Development in Tanzania of 1992);

f) kuwepo kwa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya Mwaka 2000

g) kuanzishwa kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum;

h) kuwepo kwa Mkakati wa Maendeleo ya Jinsia wa Mwaka 2005 (Tanzania National Strategy for Gender Development of 2005);

i) kuwepo kwa Mwongozo wa Kisera wa Sekta ya Afya wa Kuzuia na Kupambana na Ukatili wa Kijinsia wa Mwaka 2013;

j) kuwepo kwa Mpango Mkakati wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (NPA-VAWC, 2017/18 - 2021/2022);

k) kuwepo kwa vifungu vinavyotoa mwongozo kuhusu masuala ya haki za wanawake na jinsia katika sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Vyama vya Siasa, Sheria za Uchaguzi, n.k;

l) kuwepo kwa Sheria ya Makosa ya Kujamiiana, Sura ya 101 (Sexual Offences (Special Provisions) Act Cap 101);

m) kuwepo kwa madawati ya jinsia katika taasisi za Serikali na binafsi, ikiwemo katika vituo vya Polisi;

n) katiba za vyama vya siasa kutambua na kueleza kuhusu masuala ya haki za wanawake na jinsia;

o) kuwepo kwa Jumuiya za Wanawake katika Vyama vya Siasa;

p) kuwepo kwa Asasi za Kiraia zinazotoa elimu na kupigania haki za wanawake na usawa wa jinsia;

q) kuwepo kwa vyombo huru vya habari vinavyotoa elimu kuhusu haki za wanawake na usawa wa jinsia na kutoa taarifa kuhusu ukiukwaji wa haki za wanawake na vitendo vya ukatili wa kijinsia;

r) kuwepo kwa mikakati na programu za Serikali za kuwaendeleza Wanawake kiuchumi (mikopo kwa wanawake), ajira (upendeleo endapo mwanamke na mwanaume wana sifa sawa) na kitaaluma (shule maalum za wanawake) inayowezesha wanawake kuwa na uwezo wa kiuchumi na kimaarifa wa kushiriki katika siasa, demokrasia na uongozi;

s) kuboreshwa kwa huduma za jamii na miundombinu ikiwemo huduma za afya, upatikanaji wa maji safi na salama, ujenzi wa barabara za kudumu, kutoa elimu bure katika shule za Sekondari, kukabiliana na uharibifu wa

mazingira, kurudisha Watoto wa kike shuleni waliokatisha masomo kwa kupata ujauzito. Jitihada hizi zimewapa Wanawake wengi fursa na nafasi ya kushiriki katika shughuli za kisiasa, kidemokrasia na uongozi;

t) kuwepo kwa Umoja wa Wabunge na Wawakilishi wanawake ambao unasaidia kujengeana uwezo wa uongozi katika kutekeleza majukumu yao;

u) kuzingatiwa kwa jinsia katika nafasi za uwakilishi katika mabunge mengine. Mfano, Bunge la Jumuiya ya Madola, Bunge la Afrika na Bunge la Afrika Mashariki;

v) Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi, huzingatia suala la jinsia katika kupanga wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge na Baraza la Wawakilishi; na

w) kuwepo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ambayo pamoja na mambo mengine inashughulikia masuala ya wanawake na jinsia.

### 6.2.4 Maoni ya Wadau

Kuhusiana na suala la ushiriki wa wanawake katika siasa, demokrasia na uongozi wadau walitoa maoni yafuatayo:

a) utaratibu wa viti maalum kwa Wabunge, Wawakilishi na Madiwani Wanawake ufutwe kwa sababu kuu mbili, mosi unawanyima wanawake kuwa na haki ya kuwachagua wawakilishi wao, kwani haki ya kuchagua wawakilishi wa wanawake imehodhiwa na Vyama vya Siasa na hivyo kuwafanya wateuliwa wawe wawakilishi wa Vyama vya Siasa badala ya kuwa wawakilishi wa wanawake. Pili,

unaendeleza mfumo kandamizi ambao wanawake wabunge, wawakilishi na madiwani wa viti maalum kuwa na hadhi tofauti na wale wa majimbo, kwani hawawezi kuteuliwa kushika nafasi ya Waziri Mkuu na hawapati fedha za Mfuko wa Jimbo. Tatu, kukosekana mfumo maalum unaoongoza suala la uteuzi wa wawakilishi wa viti maalum na uongozi ndani ya Vyama vya Siasa; Hivyo, walipendekeza kuzifanya Halmashauri/Manispaa kuwa Jimbo la Uchaguzi na kuwa na wagombea wawili wa kupigiwa kura na wananchi, ambapo mmoja atakuwa ni mwanaume na mwingine ni mwanamke. Aidha, viti maalum vibakie kwa watu wenye ulemavu na wale 10 wa kuteuliwa na Rais. Vilevile, kuwe na viti maalum kwa vyama vya siasa ambavyo vimeshiriki uchaguzi mkuu na kufanikiwa kupata kiwango cha kura kitakachokubalika, ambavyo vitakua kwa wanawake na wanaume ambapo viongozi wakuu wa vyama husika wateuliwe kuwa

Wabunge;

b) awepo mgombea huru katika ngazi za ubunge na udiwani, kwani uwepo wake kutafungua fursa kwa wanawake ambao sio wanachama wa vyama vya siasa na ambao wanakubalika na jamii kushiriki na kuchaguliwa;

c) mazingira magumu yanayowakabili baadhi ya wanawake wanaotia nia ya kugombea uongozi ndani ya Vyama vya Siasa, au kuomba kuteuliwa kuwa wagombea. Kwanza ni unyanyapaa ndani ya chama ambapo huambiwa wasubiri viti maalum. Pili, udhalilishaji wa maneno yenye kutweza utu wa mwanamke. Tatu ni kufanyiwa vitendo vya ukatili

wa kijinsia. Hivyo, inapendekezwa kuwekwa kwa uwanda sawa wa ugombea kama njia ya kudumu ya kupunguza unyanyapaa kwa wanawake, ili kuboresha ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi;

d) ushiriki wa Wanawake katika siasa, demokrasia na uongozi haujafikia malengo ya kitaifa na kimataifa. Mfano, idadi ya wanawake katika uongozi wa vyama vya siasa na wagombea katika uchaguzi bado ni ndogo. Hivyo, ili kuwa na usawa wa kijinsia katika uchaguzi wa wabunge na madiwani ni vyema kukawa na nafasi za ubunge na udiwani katika jimbo na kata ambapo nafasi moja inakuwa kwa ajili wa wanawake na nyingine kwa ajili wanaume. Aidha, idadi ya majimbo ipunguzwe kwa kufanya Halmashauri kuwa jimbo la uchaguzi;

e) katiba za vyama vya siasa ziwe na ibara zinazoshughulikia masuala ya ukatili wa jinsia;

f) kuwe na programu shirikishi kwa ajili ya kuwajengea uwezo wanawake kugombea nafasi mbali mbali za uongozi;

g) Baraza la Vyama vya Siasa liongeze idadi ya wanawake ili kuweka uwiano ulio sawa;

h) Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa iwe na dawati la jinsia litakalofanyia kazi masuala ya jinsia ndani ya Vyama vya Siasa;

i) Sheria ya Vyama vya Siasa ifanyiwe marekebisho ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi ndani ya vyama vya siasa ambapo ianze na angalau 1/3 mpaka kufikia asilimia 50 ili kuwa na usawa wa jinsia

kuanzia ngazi ya tawi mpaka Taifa. Aidha, ivitake vyama vya siasa kuwa na sera ya jinsia na makundi maalum;

j) kila chama kiwe na mpango mkakati wa kufikia usawa wa kijinsia;

k) ili kupata kwa urahisi usawa wa jinsia ni vyema ukaanzishwa mfumo wa uchaguzi wa uwiano wa kura katika ubunge na udiwani (Proportional Representation);

l) kuwe na utaratibu wa kisheria utakaoeleza kuwa katika uongozi wa vyama vya siasa, kuwe na usawa wa kijinsia, mfano Mwenyekiti akiwa mwanaume Makamu Mwenyekiti awe mwanamke;

m) kuwe na sifa zitakazomuwezesha mtu kuteuliwa kuwa mbunge wa viti maalum;

n) ili kuhakikisha kuna uwazi ndani ya vyama vya siasa wakati wa uteuzi wa wagombea, ni muhimu sheria ya uchaguzi kujumuisha masuala ya jinsia katika miongozo inayoainisha mambo ya msingi yanayopaswa kuzingatiwa na kila chama kwa mujibu wa sheria;

o) ubunge wa viti maalum uwekewe ukomo wa miaka 10 ili iwe sehemu ya kupata uzoefu na kutoa nafasi kwa wanawake wengine wenye nia ya kupata ujuzi wa masuala ya siasa na uongozi.

### 6.2.5 Mapendekezo ya Tume Mbalimbali

Katika kushughulikia masuala ya wanawake, kumekuwepo na Tume na Kamati mbalimbali za kitaifa zilizofanyia kazi na kutoa mapendekezo kuhusu masuala ya ushiriki wa wanawake katika siasa na uongozi.

Miongoni mwa Tume hizo ni pamoja na Tume ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2013 iliyoongozwa na Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba, katika kuimarisha demokrasia ndani ya vyama vya siasa na vyombo vya maamuzi, ilipendekeza kupunguza majimbo ya uchaguzi na kutengeneza mfumo utakaowezesha kila chama cha siasa kupendekeza wagombea wawili ambao watapigiwa kura na wananchi wa jimbo husika ambapo mmoja atakuwa ni mgombea mwanamke na mwingine mgombea mwanaume.

Ibara ya 6(2)(g) ya Katiba Inayopendekezwa inaainisha misingi ya utawala bora katika Jamhuri ya Muungano inayojumuisha usawa wa jinsia. Aidha, Ibara ya 57 ya Katiba inaeleza kuwa kila mwanamke ana haki ya:

a) kuheshimiwa, kuthaminiwa na kutambuliwa utu wake;
b) kulindwa dhidi ya ubaguzi, udhalilishaji, dhuluma, unyanyasaji, ukatili wa kijinsia na mila potofu;
c) kushiriki bila ya ubaguzi katika uchaguzi na ngazi zote za maamuzi;
d) kupata fursa na ujira sawa na mwanamme katika kazi zenye sifa zinazofanana;
e) kulindwa ajira yake wakati wa ujauzito na pale anapojifungua;
f) kupata huduma bora ya afya ikiwemo afya ya uzazi salama na kumiliki mali. Vilevile, Ibara ya 208(1)(g) inaeleza kuwa,kuhakikisha kwamba uteuzi na ajira katika nafasi mbalimbali unazingatia uwezo wa kitaaluma, weledi, maarifa, ujuzi, usawa wa kijinsia na uzoefu katika eneo husika na fursa kwa Watu Wenye Ulemavu.

### 6.2.6 Uzoefu wa Nchi Nyingine

Kikosi Kazi kiliangalia uzoefu wa nchi za Kenya, Uganda, Morocco na Rwanda kufahamu kiwango kilichofikiwa cha ushiriki wa wanawake na wanaume katika uongozi na ngazi za maamuzi. Ibara ya 75 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Rwanda ya Mwaka 2003 inaainisha muundo wa manaibu wabunge kuwa uwakilishi wa makundi mbalimbali katika ofisi ya manaibu wabunge (chamber of Deputies), miongoni mwa manaibu 80 wanawake wanapaswa kuwa 24 (30%). Aidha, Ibara ya 139 (3)(a) ya Katiba ya Rwanda inaeleza uwepo wa Baraza la taifa la Wanawake.

Ibara ya 32 (1), 33 (4) ya Katiba ya Uganda ya mwaka 1995 zinaeleza kuwa wanawake watakuwa na haki sawa na wanaume katika kuwa na fursa sawa za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Aidha, ibara ya 98 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Kenya ya Mwaka 2010 imeainisha kuwa wanawake 16 watateuliwa na vyama vya siasa kulingana na uwiano wa idadi ya maseneta. Vilevile, ibara ya 19 ya Katiba ya Morocco inaainisha masharti yanayohusu usawa bila kujali jinsia katika haki za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kimazingira.

### 6.2.7 Uchambuzi

Baadhi ya wadau wamependekeza kuwa, ili kupata kwa urahisi usawa wa jinsia katika nafasi za ubunge, uwakilishi na udiwani, ni vyema kuwa na mfumo wa uchaguzi wa uwiano wa kura (Proportional Representation). Dhamira ya mapendekezo ya mfumo huu ni nzuri, lakini changamoto yake ni kuwa mbunge hachaguliwi na wananchi. Hivyo, hakuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya wananchi na mbunge wao. Hali hii inafanya

wananchi wakose mtu wa kuwasilisha malalamiko yao na hakuna mtu anayewajibika kwa maendeleo ya eneo husika. Vilevile, ni vigumu mfumo huu kutekelezeka katika nchi ambayo wananchi wamezoea mfumo wa kuchagua watu wa kuwawakilisha, kutokana na kuwafahamu uwezo na utayari wao wa kushughulikia changamoto za kijamii na kimaendeleo katika eneo husika. Mfano, katika uchaguzi wa Tanganyika wa mwaka 1961, TANU ilimteua Chifu Amri Dodo kuwa mgombea wa ubunge jimbo la Mbulu, ambapo Chifu Herman Sarwatt alieshindana naye na wananchi wengi wa Mbulu hawakuridhishwa na uteuzi huo, hali iliyofanya Chifu Herman Sarwatt kugombea kama mgombea huru na kumshinda Chifu Amri Dodo katika uchaguzi huo. Mfano mwingine ni Dkt. Willbrod Peter Slaa alishinda kura za maoni kugombea ubunge katika jimbo la Karatu kwa udhamini wa Chama cha Mapinduzi (CCM), lakini CCM ikamuengua na kumteua Bwana Patrick Qorro kuwa mgombea wake. Hali hii ilimfanya Dkt. Willbrod Slaa kuhama chama na kugombea katika jimbo hilo kwa udhamini wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na kushinda uchaguzi huo. Mifano hii ipo mingi katika nchi yetu, hali inayoonyesha kuwa suala la wananchi kumchagua mtu badala ya mvuto wa chama chake lina historia ndefu na ni utamaduni wa kisiasa uliojengeka nchini.

Kuhusu Viti Maalum vya Ubunge na Udiwani, Wadau wengi wamependekeza kufutwa kwa mfumo huo na kupendekeza kuwa na nafasi mbili katika jimbo na kata za uchaguzi ambapo moja itagombewa na wanawake pekee na nyingine itagombewa na wanaume. Changamoto ya mfumo huu ni kuwa utaondoa dhana ya wananchi kuwa na mwakilishi mmoja mwenye dhamana na

anayewajibika kwa wananchi wa jimbo husika. Aidha, kufanya hivyo kunaweza kuwa ni chanzo cha ugomvi, mivutano na misuguano baina ya wawakilishi hao wawili endapo wanatoka katika vyama viwili tofauti. Aidha, Kenya waliona ni vyema kuwa na wawakilishi wanawake wanaochaguliwa katika ngazi ya "County" badala ya jimbo, ili kuepuka kuwa na changamoto hizo ambazo zinaweza kurudisha nyuma jitihada za kusimamia shughuli za maendeleo badala ya kuziongeza. Vilevile, kufanya halmashauri kuwa jimbo kutapunguza ufanisi wa kusimamia shughuli za maendeleo na uchaguzi na hata kufanya kampeni za uchaguzi katika jimbo husika, kutokana na jimbo kuwa kubwa.

Kuhusu pendekezo la kuwa na mgombea huru katika ngazi za ubunge na udiwani, kwa hoja kuwa uwepo wake utafungua fursa kwa wanawake ambao sio wanachama wa vyama vya siasa na ambao watakubalika na jamii kushiriki uchaguzi na kuchaguliwa linachangamoto kwamba mgombea huru akishinda hakuna mfumo wa kitaasisi kama chama cha siasa wa kumwajibisha kutekeleza sera na ahadi zake. Pili, kunaweza kuchochea rushwa kwa watu wenye fedha nyingi kutumia fedha zao kutafuta nafasi za uongozi, bila ya kuwepo mfumo wa kichama wa kudhibiti suala hilo. Aidha, chama cha siasa kimojawapo kinaweza kutumia fedha kumfadhili mgombea na kumshawishi mbunge au diwani huru kuwa mshirika wake ili kuongeza idadi ya wawakilishi wa wananchi wanaounga mkono hoja ya chama husika. Vilevile, kunaweza kufifisha ukuaji na ufanisi wa vyama vidogo ambavyo havina fedha za kuwapata wagombea katika mchakato wa uchaguzi, kwani wagombea wataona ni vyema kuwa wagombea huru kuliko kugombea kwa tiketi ya chama ambacho hakina fedha. Hali kadhalika, kunaweza

kuwa na siasa za kifamilia, kidini, kikabila, kikanda na zenye sera na vitendo vinavyopelekea kuvunja Muungano wetu, kutokana na mgombea huru kutosajili kama chama cha siasa kwani usajili wa chama cha siasa una masharti yanayokataza ni, ukabila, ukanda, sera pamoja na vitendo vinavyoweza kusabisha Muungano kuvunjika na kuhatarisha usalama wa nchi kwa mgombea huru kupokea fedha na ahadi kutoka kwa watu, taasisi au nchi za nje kwa lengo la kutekeleza matakwa yao.

### 6.2.8 Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Kwa kuzingatia hoja zilizowasilishwa na wadau wa demokrasia pamoja na mapitio ya nyaraka mbalimbali, Kikosi Kazi kinapendekeza yafuatayo:

a) Sheria ya Vyama vya Siasa irekebishwe ili:
   i) kuweka sharti la kila chama cha siasa kuwa na sera ya jinsia na ujumuishi wa makundi maalum katika jamii;
   ii) kuweka sharti la kisheria kwamba idadi ya jinsi moja katika vyombo vya maamuzi ndani ya chama cha siasa isipungue asilimia 40;
   iii) Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa za Mwaka 2019 ziwe na vigezo vya ufuatiliaji ili kupima utekelezaji wa Sheria, katiba na kanuni za vyama vya siasa, kuhusu masuala ya jinsia na ujumuishaji wa makundi maalum ya jamii katika chama na uchaguzi; na

b) katiba za vyama ziwe na Ibara zinazoshughulikia masuala ya ukatili wa jinsia ikiwemo udhalilishaji wa wanawake;

c) kila chama cha siasa kiwe na programu maalumu kwa ajili ya kuwajengea uwezo wanawake kugombea ubunge, uwakilishi na udiwani, ikiwemo kuwa na mipango na mikakati ya kufikia usawa wa kijinsia;

d) Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na kila chama cha siasa kiwe na dawati la jinsia litakalofanyia kazi masuala ya jinsia ndani ya vyama vya siasa;

e) utaratibu wa kuwa na viti maalum vya Wabunge, Wawakilishi na Madiwani wanawake uendelee, isipokuwa sheria ziboreshwe kuweka ukomo wa miaka kumi kwa mtu kuwa Mbunge, Mwakilishi au Diwani wa viti maalum vya wanawake. Uwakilishi huu uwe ni njia ya kupata uzoefu na kisha kupisha wanawake wengine wenye nia ya kuongeza ujuzi wa masuala ya siasa na uongozi.

f) kuwepo na mwongozo wa kisheria wa uteuzi wa wagombea na uchaguzi wa viongozi ndani ya Vyama vya Siasa, ikiwemo wabunge wa viti maalum ili kusaidia uteuzi na uchaguzi huo kuwa wa haki, uwazi na huru;

g) kila chama cha Siasa kiweke mkakati wa kuongeza idadi ya wanawake wanaogombea katika majimbo na kata za uchaguzi; na

h) kwa kuwa idadi ya wanawake ni ndogo katika Baraza la Vyama vya Siasa aongezwe mjumbe mmoja mwanamke kutoka kila chama cha siasa kuwa mjumbe wa Baraza la Vyama vya Siasa;

i) Wabunge wa Viti Maalum vya Wanawake waitwe Wabunge wa Taifa na Madiwani, waitwe Madiwani wa Wilaya, kwa sababu wabunge hao wanatokana na kura za nchi nzima na Madiwani wanatokana na kura za Wilaya.

Aidha, Sheria ya Mfuko wa Jimbo ifanyiwe marekebisho ili itambue Wabunge wa Taifa kuwa miongoni mwa Wabunge wanaofaidika na fedha za Mfuko huo.

### 6.3 Ushiriki wa Watu Wenye Ulemavu katika Siasa, Demokrasia na Uongozi

Watu wenye Ulemavu ni miongoni mwa makundi maalum yanayoundwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na sheria mbalimbali za nchi. Aidha, Katiba ya Jamhuri ya Muungano na sheria hizo zinatoa haki sawa kwa watu wenye ulemavu na kuhakikisha kuwa Watu Wenye Ulemavu wanashiriki kikamilifu katika masuala yote muhimu katika jamii, zikiwemo siasa, demokrasia na uongozi.

Katika kuimarisha haki na kuendeleza haki hizo serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetayarisha Sera, Sheria, Programu na Mikakati mbalimbali pamoja na kuanzisha Wizara, taasisi na vitengo vinavyosimamia na kuratibu utekelezaji na uendelezaji wa shughuli zinazohusu ustawi na maendeleo kwa watu wenye ulemavu nchini ikiwemo ushiriki wao katika masuala ya siasa, demokrasia na uongozi.

#### 6.3.1 Mikataba, Itifaki na Matamko kuhusu Ushiriki wa Watu Wenye Ulemavu katika Siasa, Demokrasia na Uongozi.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesaini mikataba Itifaki na Matamko mbalimbali ya kimataifa inayoelekeza nchi washirika kulinda haki za Watu Wenye Ulemavu. Haki hizo ni pamoja na haki ya kutobaguliwa, haki ya kushiriki katika siasa,

maamuzi na uongozi. Aidha, Tanzania imeweka matakwa ya mikataba, itifaki na matamko hayo katika Katiba ya nchi, sera na sheria zake. Vilevile, zimeundwa taasisi za kusimamia utekelezaji wa misingi hiyo ya Katiba na Sheria, ili kuhakikisha haki za Watu wenye ulemavu zinalindwa na kutekelezwa ipasavyo. Baadhi ya Mikataba, Itifaki na Matamko hayo ni:

a) Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la mwaka 1948 (Universal Declaration for Human Rights, 1948) lililobainisha usawa wa binadamu wote na haki ya kutobaguliwa;
b) Mkataba wa kimataifa kuhusu haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni wa mwaka 1966 (International Covenant on Economic, Social and Cultural Rights of 1966);
c) Azimio la Kimataifa Kuhusu Haki za Kiraia na Kisiasa (International Covenant on Civil and Political Rights of 1966), linatoa hali za kisiasa na kiraia kwa watu wote;
d) Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu wa Mwaka 2006 (United Nations Convention on the Rights of Persons with Disabilities of 2006), Mkataba huo unawataka nchi wanachama kuhakikisha kuwa, kuna ushiriki kamili wa watu wenye ulemavu katika siasa na maisha ya kijamii;
e) Mpango wa Utekelezaji wa Muongo wa Afrika kwa Watu Wenye Ulemavu wa Mwaka 1999-2009 (Plan of Action for the African Decade of Persons with Disabilities 1999–2009);
f) Sera ya Jinsia ya SADC (SADC Gender Policy) Ibara ya 9;

g) Sera ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2012 (East Africa Community Policy on Persons with Disabilities of 2012).

### 6.3.2 Historia ya Kupigania Haki za Watu Wenye Ulemavu Kushiriki katika Siasa, Demokrasia na Uongozi

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya na inaendelea kufanya juhudi nyingi kuhakikisha haki za Watu Wenye Ulemavu zinalindwa, juhudi hizo ni Pamoja na zifuatazo:

a) Ibara ya (11(1)) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inatambua haki ya mtu kufanya kazi, kupata elimu na haki ya kupata msaada kwa watu wenye ulemavu;
b) utambuzi wa watu wenye ulemavu katika azimio la Arusha la mwaka 1967, kuwa miongoni mwa makundi machache yanayostahili usaidizi kutoka kwa jamii;
c) kuandaliwa na kutekeleza Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2004 (National Policy on Disability of 2004);
d) kuandaa na Kutekeleza Sera ya Watu Wenye Ulemavu Zanzibar (Disability Policy (2004);
e) kuwepo kwa Sera ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2012 ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inawajibisha nchi wanachama kuhakikisha watu wenye ulemavu wanashirikishwa katika kutunga na kutekeleza sera, sheria, ufuatiliaji na tathmini ya programu zinazolenga ustawi na ujumuishwaji wao katika jamii;

f) kutungwa kwa sheria mbalimbali zinazosimamia na kutetea haki za watu wenye ulemamu zikiwemo:

i) National Disability Mainstreaming Strategy (2010- 2015);

ii) Disabled Persons (Employment) Act, 1982; iii) Disabled Persons (Care and Maintenance) Act

1982 (No. 3); iv) National Employment Promotion Service Act

1999 (No. 9);

v) Employment and Labour Relations Act, 2004

(No. 6); vi) Zanzibar Labour Act 1997

(No. 3); vii) Labour Relations Act 2005 (No.

1) viii) Zanzibar Disabilities Act, 2006 ix)

The Persons with Disabilities Act, 2010;

g) Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania II (MKUKUTA II) 2010- 2015;

h) Mkakakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar II (MKUZA II) 2010- 2015;

i) Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi (Tanzania National Strategy on Inclusive Education) 2009-2017;

j) Mabadiliko ya Sera ya Elimu Zanzibar kuelekea Elimu Jumuishi (Zanzibar Education Policy: Transition Towards Inclusive Education of 2006;

k) Kuanzishwa kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watu wenye ulemavu;

l) kuanzishwa kwa Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar.

m) kuundwa kwa Shirikisho la Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu Zanzibar (SHIJUWAZA);

n) kuundwa kwa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA); na
o) uwepo wa viti maalum vya wabunge kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu ndani ya Chama cha Mapinduzi (CCM).

### 6.3.3 Maoni ya Wadau

Kuhusiana na ushiriki wa Watu Wenye Ulemavu katika siasa, demokrasia na uongozi, wadau wengi walikuwa na maoni yafuatayo:

a) kuwepo na asilimia 5 ya viti maalum vya Wabunge kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu kwa kufanya mabadiliko katika Ibara ya 66(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;
b) ziandaliwe programu za kuwajengea uwezo Watu Wenye Ulemavu kushiriki katika michakato ya kisiasa na demokrasia;
c) Katiba na Kanuni za vyama vya siasa zitamke wazi juu ya ushiriki wa Watu Wenye Ulemavu katika siasa pamoja na ushirikishwaji katika Baraza la Vyama vya Siasa;
d) Vyama vya Siasa vitakiwe kutenga asilimia 10 ya mapato ya mwaka kuwajengea uwezo Watu Wenye Ulemavu;
e) yaandaliwe mazingira wezeshi kwa Watu Wenye Ulemavu kushiriki kikamilifu katika siasa na uchaguzi mfano, kupunguza gharama za kuchukua fomu;
f) Sheria ya Vyama vya Siasa ifanyiwe marekebisho ili kuvitaka vyama vyote vya siasa viwe na jumuiya ya Watu

Wenye Ulemavu na takwa hilo liwe ni sharti kwa chama kinachoomba usajili;

g) kila chama cha siasa kiwe na mpango mkakati wa kuimarisha ushiriki wa Watu Wenye Ulemavu katika siasa, demokrasia na uongozi;

h) ushiriki mdogo wa watu wenye ulemavu katika siasa, demokrasia na uongozi;

i) mazingira ya kufanya shughuli za kisiasa yanachangamoto zinazozuia watu wenye ulemavu kushiriki katika shughuli za kisiasa mfano, uwepo wa mfumo kandamizi, udhalilishaji, unyanyapaa (dhana ya kwamba watu wenye ulemavu hawawezi kufanya shughuli za kisiasa, kijamii na kiuchumi.), rushwa, matumizi makubwa ya fedha katika siasa na uchaguzi, na uwepo wa demokrasia hafifu kwa baadhi ya vyama vya siasa;

j) Vyama vya Siasa havifanyi juhudi za kutosha kutekeleza haki za Watu Wenye Ulemavu, mfano kutowepo kwa Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu katika vyama vya siasa kama ilivyo kwa makundi maalum mengine mfano, wanawake, vijana na wazee. Vyama vya Siasa kutokuwa na sera, miongozo au mikakati ya kushughulikia suala la Watu Wenye Ulemavu;

k) kutokuwepo kwa viti maalum kwa Watu Wenye Ulemavu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Baraza la Wawakilishi na Madiwani;

l) uhaba wa miundombinu na nyenzo saidizi kwa Watu Wenye Ulemavu. Mfano, hakuna katiba au kanuni ya chama cha siasa iliyo katika maandishi ya breli. Pia, kutokuwepo kwa wakalimani wa lugha za alama katika

mikutano ya vyama vya siasa. Vilevile, majukwaa ya kampeni za uchaguzi na mikutano mingine ya vyama vya siasa kutokua rafiki kwa mazingira ya watu wenye ulemavu. Kutokuwepo kwa eneo lenye kivuli la kuketi watu wenye ulemavu wa Ngozi wakati wa mikutano ya hadhara; na

m) kifungu 6A(2) cha Sheria ya Vyama Vya Siasa kinachoelekeza chama cha siasa kuzingatia suala la ujumuishwaji wa makundi maalum ya jamii katika masuala ya Vyama vya Siasa na demokrasia, hakijawekewa kanuni za utekelezaji. Vilevile, katazo la ubaguzi kwa Watu Wenye Ulemavu katika vyama vya siasa, lililopo katika kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria hiyo liwahusu pia viongozi wa Vyama vya Siasa.

### 6.3.4 Mapendekezo ya Tume Mbalimbali

Katika kutimiza majukumu yake, Kikosi Kazi kilipitia maoni na mapendekezo ya Kamati na Tume mbalimbali za kitaifa zilizozungumzia masuala ya Watu Wenye Ulemavu, miongoni mwa Kamati hizo ni:

a) Kamati ya Kuratibu Maoni ya Katiba ya Mwaka 1999 iliyoongozwa na Jaji Robert H. Kisanga ilipendekeza kuwa vianzishwe viti vya ubunge kwa ajili ya makundi mbali mbali, ikiwemo Watu Wenye Ulemavu; na

b) ibara ya 129(2)(b) ya Katiba Inayopendekezwa inaainisha kuwa kutakuwa na wabunge watano Wenye Ulemavu watakaoteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye

sifa za kuchaguliwa kuwa wabunge na ibara ya 208 (1) (c) ya Katiba hiyo inaeleza kuwa uteuzi na ajira katika nafasi mbalimbali utazingatia uwezo wa kitaaluma, weledi, maarifa, ujuzi, usawa wa kijinsia na uzoefu katika eneo husika na fursa kwa Watu Wenye Ulemavu. Vilevile, ibara ya 215(2)(b) inaitaka mamlaka inayosimamia uchaguzi kuzingatia misingi kwamba Watu Wenye Ulemavu wanapewa fursa za uwakilishi. Hali kadhalika, ibara ya 224(2)(e) inatoa masharti kwamba, ili chama cha siasa kipate usajili ni lazima uongozi wake uchaguliwe kwa kuzingatia jinsi, Watu Wenye Ulemavu na uwakilishi wa pande zote mbili za Muungano kwa njia za demokrasia.

### 6.3.5 Uzoefu wa Nchi Nyingine

Uzoefu kutoka Jamhuri ya watu wa Kenya unaonesha kuwa katiba ya nchi yao Ibara ya 54 (2) imebainisha kuwa angalau asilimia 5 ya watu watakaochaguliwa/kuteuliwa katika vyombo vya maamuzi watapaswa kuwa Watu Wenye Ulemavu.

Katiba ya Jamhuri ya Uganda ya mwaka 1995 Ibara za 35 na 59(4) zinafafanua haki za Watu Wenye Ulemavu ikiwa ni pamoja na ushiriki wao katika masuala ya siasa. Vilevile, Ibara ya 78 (1) (c) inabainisha kuwa Watu Wenye Ulemavu watakuwa miongoni mwa wabunge watakaochaguliwa au kuteuliwa kulingana na sheria ya bunge. Kifungu cha 37 cha sheria ya Bunge ya mwaka 1996 kinatoa nafasi 5 za uwakilishi wa Watu Wenye Ulemavu katika Bunge.

Katiba ya Jamhuri ya Rwanda ya mwaka 2003 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2015 Ibara ya 51 inazingatia ustawi

wa Watu Wenye Ulemavu na makundi mengine. Aidha, Ibara ya 75 (4) inainisha uwakilishi wa makundi mbalimbali ikiwemo mwakilishi mmoja kutoka kundi la Watu Wenye Ulemavu aliyechaguliwa kutoka Baraza la Taifa kwa Watu Wenye Ulemavu katika Manaibu Wabunge (Chamber of Deputies). Vilevile, ibara ya 139 (3) (c) ya Katiba hiyo inazingatia uwepo wa baraza la taifa la Watu Wenye Ulemavu.

### 6.3.6 Uchambuzi

Kuna maoni ya wadau kwamba, Sheria ya vyama vya siasa sura 258 irekebishwe kuweka kifungu kinachowajibisha vyama vya siasa kujumuisha Watu Wenye Ulemavu kwenye shughuli za Baraza la Vyama vya Siasa. Changamoto ya utekelezaji wa suala hili ni kuwa, kila chama cha siasa kinapaswa kuwa na wajumbe wawili katika Baraza la Vyama vya Siasa, kati ya wajumbe hao mmoja anapaswa kutoka Tanzania Zanzibar na mwingine Tanzania Bara na wote wanapaswa kuwa ni viongozi wakuu wa kitaifa wa chama.

Aidha, kuna ushauri kwamba, kwa kuwa idadi ya wanawake ni ndogo katika Baraza hilo, basi aongezwe mjumbe mmoja mwanamke kutoka kila chama cha siasa. Hatua hii itaongeza idadi ya wajumbe wa Baraza la Vyama vya Siasa na kuongeza gharama za uendeshaji. Hivyo, endapo ataongezwa tena mjumbe mmoja ambaye ni mtu Mwenye Ulemavu kutoka kila chama cha siasa, idadi ya wajumbe wa Baraza la Vyama vya Siasa itakuwa kubwa na kufanya gharama za uendeshaji kuwa kubwa.

Vilevile, kuna maoni ya wadau kuwa, kuwe na ibara katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar,

inayoeleza kuhusu ushiriki wa Watu Wenye Ulemavu katika siasa, demokrasia na uongozi. Katiba hizo zinaeleza kuhusu usawa wa watu na zinalinda haki ya kila mtu, ikiwemo watu wa makundi maalumu kama Watu Wenye Ulemavu. Hivyo, kwa kuwa Katiba inaweka mwongozo na siyo kutoa maelekezo ya kina ya utekelezaji wa jambo husika, Ibara hii inaweza kukidhi haja ya maoni hayo.

### 6.3.7 Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Kwa kuzingatia hoja zilizowasilishwa na wadau wa demokrasia pamoja na mapitio ya nyaraka mbalimbali, Kikosi Kazi kinatoa mapendekezo yafuatayo:

a) sheria zisizozingatia ujumuishwaji wa Watu Wenye Ulemavu na zile zinazokwamisha ushiriki wao katika siasa, demokrasia na uongozi ndani ya vyama siasa zifanyiwe maboresho;

b) Vyama vya Siasa viweke mazingira rafiki yatakayowawezesha Watu Wenye Ulemavu kufanya shughuli za kisiasa bila vikwazo;

c) kila chama cha siasa kianzishe dawati la kushughulikia masuala ya Watu Wenye Ulemavu;

d) kuwepo na nafasi maalum kwa Watu Wenye Ulemavu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Madiwani. Viti vya uwakilishi wa Watu Wenye Ulemavu Bungeni viwe katika uwiano utakaozingatia jinsi. Suala hili lifanyiwe kazi katika mchakato wa kutungwa kwa Katiba Mpya ili lifanyike kwa ufanisi. Hata hivyo, kwa

kuanzia kila chama cha siasa kitumie utaratibu wa sasa wa viti maalum vya Wanawake kujumuisha Watu Wenye Ulemavu;

e) Sheria ya Vyama vya Siasa irekebishwe ili:

   i) iweke sharti kwamba chama cha siasa kiwe na nakala ya Katiba na Kanuni zilizo katika maandishi ya breli. Aidha, katika mkutano mkuu wa chama taifa, awepo mkalimani wa lugha za alama;

   ii) katazo la ubaguzi kwa Watu Wenye Ulemavu katika vyama vya siasa lililopo katika kifungu cha 9(1)(c) cha sheria ya vyama vya siasa liwahusu pia viongozi wa vyama vya siasa; na

   iii) katiba ya chama cha siasa iwe na ibara inayokitaka chama husika kiwe na programu za kuwajengea uwezo watu wenye ulemavu kushiriki kikamilifu katika michakato ya kisiasa, demokrasia na uongozi ndani na nje ya chama.

f) zitungwe Kanuni za utekelezaji wa Kifungu cha 6A (2) cha Sheria ya Vyama vya Siasa kinachoelekeza chama cha siasa kuzingatia suala la ujumuishwaji wa Watu Wenye Ulemavu katika masuala ya vyama vya siasa na demokrasia;

g) vyombo vya habari viandae vipindi maalum vya elimu ya uraia vinavyoeleza haki na mahitaji ya Watu Wenye Ulemavu;

h) Serikali iboreshe Makazi maalum ya Wazee na Watu Wenye Ulemavu;

i) suala la kuondoa ombaomba mitaani lifanyiwe kazi kwa ufanisi, kwani linaleta taswira kuwa Watu Wenye

Walemavu ni maskini; na

j) elimu kuhusu masuala yote yanayohusiana na ulemavu na madhara yake ikiwemo afya ya uzazi, kinga kwa ajali, maradhi na njia bora za utabibu iongezwe ili kupunguza idadi na madhara ya ulemavu.

### 6.4 Ushiriki wa Vijana katika Siasa, Demokrasia na Uongozi

Vijana ni moja ya kundi linalojumuishwa miongoni mwa makundi maalum. Hata hivyo, katika muktadha wa kutoa upendeleo kwa makundi maalum, Serikali imefanya juhudi mbalimbali katika kulitambua kwa namna ya kipekee kwa kulitumia katika nyanja na sekta mbalimbali za kiuchumi, kisiasa, na kijamii. Juhudi hizo zimeleta mafanikio yafuatayo:

a) idadi kubwa ya Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi wanatoka katika kundi la vijana;

b) idadi kubwa ya viongozi walioteuliwa na Serikali kushika nyadhifa mbalimbali serikalini ni vijana, mathalan Mawaziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, wakuu wa Wilaya, Wakurugezi Watendaji wa Halmashauri, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Watendaji Wakuu wa mashirika ya umma, na Taasisi mbalimbali, Wakurugenzi na Wakuu wa Idara na Vitengo ni vijana;

c) vijana ni kundi linaloongoza sekta ya uzalishaji mali, michezo na umiliki wa nyezo za uchumi na uzalishaji mali ikiwemo sekta binafsi;na

d) vijana ni wanufaika wakubwa kwenye ajira, mikopo, mitaji na na programu za kiuchumi nchini.

Kwa mantiki hiyo, Kikosi Kazi kinaamini kuwa kutokana na jitihada na mikakati iliyowekwa na Serikali inaridhisha kuwawezesha vijana na kuwafikisha katika hali bora zaidi.

### 6.4.1. Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Kwa kuzingatia hoja zilizowasilishwa na wadau wa demokrasia pamoja na mapitio ya nyaraka mbalimbali, Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa juhudi zinazofanywa na Serikali kuhusu ushiriki wa vijana katika siasa, demokrasia, uongozi, uchumi, ulinzi na usalama wa nchi yetu ziendelee na mikakati mipya ibuniwe ili kuongeza ufanisi na tija.

# SURA YA SABA

# ELIMU YA URAIA

## 7.1 Utangulizi

Elimu ya uraia ni moja ya nyenzo muhimu za kujenga uzalendo, utaifa na uwezo wa wananchi kushiriki katika masuala ya demokrasia. Kumekuwa na njia mbalimbali zinazotumika kutoa elimu ya uraia tangu nchi yetu ilipopata uhuru. Baadhi ya njia hizo ni pamoja na elimu inayotolewa kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kupitia mfumo rasmi wa elimu shuleni, elimu ya mpiga kura inayotolewa na kuratibiwa na Tume za Uchaguzi wakati wa uchaguzi, elimu ya uraia inayotolewa na taasisi za Serikali kuhusu masuala mahsusi wanayofanyia kazi. Aidha, asasi za kiraia, taasisi za dini, vyombo vya habari na watu binafsi wanasaidia kutoa elimu hiyo.

## 7.2 Historia ya Utoaji wa Elimu ya Uraia Nchini

Historia inaonesha kuwa, kabla ya kurejeshwa mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa mwaka 1992, elimu ya uraia ilikuwa inatolewa chini ya mfumo wa chama kimoja cha siasa. Msisitizo mkubwa uliwekwa katika falsafa ya itikadi ya Ujamaa na Kujitegemea, ili kusaidia wananchi kufahamu wajibu na haki zao ili waweze kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa. Elimu ya uraia ilikuwa ni sehemu ya mtaala wa shule na ilitolewa katika mfumo wa elimu ya siasa kwa vijana walio shuleni na vyuoni na ilikuwa sehemu ya mtihani wa Taifa. Kwa upande wa watu wazima, elimu ya uraia ilitolewa kwa njia mbalimbali kama vile kwenye kampeni

zinazohusu uchumi na maendeleo ya jamii mfano, kampeni ya “Ujamaa Vijijini”, “Mtu ni Afya” na kampeni ya “Siasa ni Kilimo”. Elimu hii ilitolewa kwa kupitia, mikutano ya ndani na mikutano ya hadhara ya Vyama vya Siasa au Serikali, redio na programu mbalimbali au kwa njia ya machapisho hasa kwenye vitabu vya Kiswahili na kwenye magazeti yaliyokuwa yanamilikiwa na Chama cha Mapinduzi au Serikali kama vile Uhuru, Mfanyakazi, Mzalendo, Sunday News na Daily News. Vilevile, hotuba za viongozi ambazo zilikuwa zinatolewa redioni kila siku na katika matukio maalum.

Baada ya kurejea mfumo wa vyama vingi vya siasa ikiwa ni matokeo ya mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Rais ya Mfumo wa Chama Kimoja au Vyama Vingi vya Siasa iliyoongozwa na Jaji Francis Nyalali. Tume hii ilishauri kuwa, pamoja na mambo mengine, ipo haja ya kuanzisha elimu ya uraia kwa umma inayokidhi mahitaji ya demokrasia ya mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Serikali iliamua kushirikisha wadau katika kutoa elimu ya uraia katika ngazi zote, ambao wengi wao walikuwa ni asasi za kiraia, vyama vya siasa na taasisi za kidini. Pamoja na elimu iliyokuwa ikitolewa kwa wakati huo, hapakuwa na dira ya taifa na chombo maalum cha kuratibu utoaji wa elimu ya uraia nchini.

### 7.3 Hali Ilivyo Sasa

Elimu ya uraia inayohusu siasa na demokrasia inatolewa kwa namna mbili. Namna ya kwanza ni elimu inayotolewa wakati wote, namna ya pili ni elimu inayotolewa wakati wa uchaguzi pekee. Elimu

inayotolewa wakati wote, ni ile inayotolewa kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kupitia mfumo rasmi wa elimu. Elimu ya uraia inayotolewa na taasisi za Serikali kuhusu masuala mahsusi wanayofanyia kazi, mfano Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, taasisi za kuzuia na kupambana na rushwa, Jeshi la Polisi, Wizara ya Afya na Tume ya Haki za Binadamuu na Utawala Bora.

Elimu inayotolewa wakati wa uchaguzi pekee ni elimu ya mpiga kura ambayo hutolewa kipindi cha uchaguzi kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi. Elimu hiyo hutolewa na wadau mbalimbali wa Uchaguzi na kuratibiwa na Tume za Uchaguzi. Tume za Uchaguzi hutoa mwongozo wa elimu ya mpiga kura na kutoa vibali kwa taasisi zilizoomba kutoa elimu hiyo katika kipindi husika.

Katika kuratibu elimu hiyo, Tume za Uchaguzi zina wajibu wa kisheria wa kukagua na kuthibitisha maudhui na nyenzo zinazotumiwa na mdau katika kutoa elimu ya mpiga kura. Aidha, mtu yeyote atakayekiuka utaratibu wa kisheria wa kutoa elimu ya mpiga kura hatoruhusiwa kuendelea kutoa elimu hiyo.

### 7.4 Maoni ya Wadau

#### 7.4.1 Maoni ya Wadau kuhusu Elimu ya Uraia kwa Ujumla

Katika eneo hili wadau walikuwa na maoni yafuatayo:

a) elimu ya mpiga kura itolewe wakati wote na itiliwe mkazo, ili kuainisha na kuzitambulisha kwa raia tunu zote za taifa na kujenga uwajibikaji na uzalendo kwa wananchi;

b) Serikali ifanye jitihada za makusudi kuanzisha mamlaka ya kukuza, kusimamia na kuratibu elimu ya uraia. Elimu ya mpiga kura iwe ni sehemu ya elimu ya uraia na isimamiwe na Baraza la ushauri la uchaguzi (National Electoral Advisory Council);

c) Serikali ipanue wigo kuruhusu taasisi zenye nia ya kutoa elimu ya uraia;

d) Vyama vya Siasa, taasisi za kidini na asasi za kiraia ziruhusiwe kutoa elimu ya uraia kwa kufuata miongozo itakayotolewa na Serikali;

e) Asasi za kiraia zipewe ruzuku kusaidia kutoa elimu ya uraia kwa umma kwenye masuala yatakayoainishwa;

f) Vyama vya siasa vitoe elimu ya uraia katika vyama vyao na wanachama wao katika mitaala inayotambuliwa na Serikali. Elimu ya uraia itolewe bila kujali itikadi za vyama vyao;

g) mbinu mbalimbali zitumike kufikisha elimu ya uraia ikiwa ni pamoja na kutumia vyombo vya habari, wasanii, filamu, simu za viganjani na mitandao ya kijamii;

h) suala la elimu ya uraia lifanyiwe utafiti wa kina kujua hali halisi na kuandaa moduli zitakazokidhi na zinazoendana na mahitaji ya sasa ya maendeleo ya sayansi na teknolojia;

i) Tume ya Taifa imekuwa haitoa vibali kwa baadhi ya taasisi za kiraia zinazoomba kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa uchaguzi;

j) uratibu baina ya Tume za uchaguzi (NEC/ZEC) na Serikali za Mitaa (LGAs) unahitaji kuimarishwa ili kuhakikisha ufanisi na uangalizi mzuri katika usimamizi wa Asasi za Kiraia zinazotoa elimu ya mpiga kura;

k) elimu ya uraia inayotolewa haijafikia malengo yanayokusudiwa, mfano, kutofikia watanzania wote wanaolengwa;

l) kutokuwepo chombo cha kitaifa kinachoratibu elimu ya uraia inayotolewa nchi nzima;

m) kutokuwepo kwa mwongozo wa kitaifa wa utoaji wa elimu ya uraia nchini, hali hii inaweza kusababisha wananchi kuwa na uelewa tofauti katika masuala yanayohusu elimu ya uraia;

n) ukosefu wa rasilimali fedha ili kuwezesha taasisi zinazotoa elimu ya uraia kufikia maeneo mengi nchini; na

o) Asasi za Kiraia zinazotoa elimu ya uraia kujihusisha na masuala ya kisiasa au kuwa na ushabiki wa kisiasa au kutoa elimu ya uraia yenye maudhui yanayoendana na matakwa ya mfadhili.

### 7.4.2 Maoni ya Wadau Kuhusu Elimu ya Mpiga Kura

a) upungufu wa rasilimali fedha, watu na vifaa vya kutoa elimu ya mpiga kura kuwezesha kuwafikia walengwa wote;
b) elimu ya mpiga kura kutoingizwa katika mtaala wa elimu ya uraia unaotolewa shuleni; na

c) elimu ya mpiga kura kutolewa kipindi cha uchaguzi peke yake kunafanya muda wa kuitoa kuwa mchache hivyo inaweza kuathiri kuwafikia walengwa wengi.

### 7.5 Mapendekezo ya Tume na Kamati Mbalimbali

Taarifa ya Tume ya Rais ya Mfumo wa Chama Kimoja au Vyama Vingi vya Siasa Tanzania (Tume ya Jaji Nyalali) ilipendekeza pamoja na mambo mengine, ipo haja ya kuanzisha mfumo wa elimu ya uraia kama sehemu ya kutambua mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa. Vilevile, ilipendekeza elimu hii ya uraia ifundishwe shuleni na vyuoni, watu waruhusiwe kujiunga na vyama vya siasa, watoe maoni kwa uhuru na pia wajumuike bila kikwazo.

Ripoti za Tume ya Uchaguzi kwa zaidi ya miongo Minne (4) zimependekeza kwa Serikali haja ya kuunda chombo kitakachotoa, kusimamia na kuratibu elimu ya uraia. Aidha, kwa upande wa elimu ya mpiga kura, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekuwa ikipendekeza kwa Serikali kuongeza fedha zitakazowezesha elimu ya mpiga kura kuwa endelevu, wakati wote bila kusubiri au kutegemea elimu hii kutolewa kipindi cha uchaguzi peke yake.Tume ya Taifa ya Uchaguzi imependekeza kuwa, Serikali iangalie uwezekano wa kuziwezesha kifedha asasi na taasisi zinazotoa elimu ya mpiga kura katika hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi.

### 7.6 Uzoefu Kutoka Nchi Nyingine

Kikosi Kazi kimefanya utafiti kwa kupitia nyaraka mbalimbali ili kujifunza na kupata uzoefu wa nchi nyingine zinavyotoa elimu ya

uraia ambao pia ukitumika nchini Tanzania unaweza kuongeza tija katika kuimarisha mifumo ya utoaji elimu ya uraia.

Nchini Ghana, suala la elimu ya uraia limewekwa katika Katiba na hivyo kupata nguvu ya kisheria. Mathalani, Ibara ya 231 ya Katiba ya Ghana ya Mwaka 1992 imeunda Tume ya Taifa ya Elimu ya Uraia. Kazi ya Tume hiyo, pamoja na mambo mengine, ni kuratibu shughuli za Elimu ya Uraia ili kuwajengea uelewa wananchi wa Ghana kufahamu demokrasia na kufanikisha maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii kupitia elimu hiyo. Tume ina wajibu wa kuhakikisha kuwa elimu ya uraia inatumika kama mkakati muhimu wa kuongeza uelewa kwa wananchi juu ya miiko ya utawala wa demokrasia, uzalendo na kuimarisha ushiriki wa wananchi katika masuala ya utawala:

Nchini Kenya, masuala ya elimu ya uraia yanasimamiwa na Sheria ya "County Government Act" ya mwaka 2012. Kifungu cha 100(2) cha sheria hii, kinaanzisha mfumo wa kitaifa wa elimu ya uraia, ili kuweka maudhui ya mtaala wa elimu ya uraia kama ilivyowekwa na Ibara ya 33 ya Katiba ya Kenya. Kwa mujibu wa kifungu cha 100, kila county inapaswa kuendesha programu ya elimu ya uraia na kuanzisha kitengo cha elimu ya uraia.

Nchini Uganda, mwaka 2019 Rais Yoweri Museveni alizindua mpango wa kitaifa wa elimu ya uraia "National Initiatives For Civic Education in Uganda-NICE-UG". Mpango huu ni shirikishi, ambao umeundwa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kama vile taasisi za umoja wa mataifa, asasi za kiraia, sekta binafsi, uongozi wa kimila na kidini. Lengo kuu la Mpango huu ni kukuza utoaji wa elimu ya uraia kwa kuzingatia ufanisi kama sehemu ya safari ya taifa kufikia maendeleo endelevu na mafanikio ya pamoja.

## 7.7 Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Kwa kuzingatia hoja zilizowasilishwa na wadau wa demokrasia pamoja na mapitio ya nyaraka mbalimbali, Kikosi Kazi kinatoa mapendekezo yafuatayo:

a) Serikali iandae mwongozo wa kitaifa, mpango kazi na mikakati ya utoaji elimu ya uraia, ili utoaji wa elimu hiyo uzingatie vipaumbele vya taifa na kuwa na uelewa wa pamoja wa walengwa;

b) elimu ya uraia ikiwemo elimu ya mpiga kura ifundishwe katika ngazi zote za mfumo wa elimu kuanzia shule za awali mpaka katika vyuo vya elimu ya juu. Aidha, mtaala wa elimu ujumuishe masuala ya elimu ya uraia;

c) Serikali na wadau wengine waongeze kiwango cha ufadhili katika kutoa elimu ya uraia ikiwemo elimu ya mpiga kura, ili kukabiliana na upungufu wa rasilimali, watu, fedha na vifaa katika kutoa elimu hiyo;

d) elimu ya mpiga kura itolewe kipindi chote siyo cha uchaguzi pekee, ili kuongeza muda wa kutoa elimu hiyo kuwezesha kuwafikia walengwa wengi zaidi; na

e) uratibu na ufuatiliaji wa elimu ya uraia unaofanywa na taasisi mbalimbali kwa mujibu wa sheria uendelee, isipokuwa ufanywe katika hali isiyokwamisha juhudi za kuwafikia watanzania wengi kupata elimu hiyo.

# SURA YA NANE

# RUSHWA NA MAADILI KATIKA SIASA NA UCHAGUZI

## 8.1 Utangulizi

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zinatambua rushwa kuwa ni tatizo linaloathiri maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii na zimedhamiria kuzuia na kupambana na rushwa katika nchi yetu. Hivyo, mapambano dhidi ya Rushwa ni jambo muhimu katika kufikia maendeleo endelevu ya Taifa lolote. Rushwa na Maadili ni dhana mbili zinazokinzana kwani hazikai pamoja. Tatizo la rushwa linakuwepo iwapo hukuna uadilifu katika jamii.

Mwelekeo wa Vita dhidi ya rushwa nchini unaongozwa na masharti yaliyoainishwa kwenye Ibara ya 8(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *ya* Mwaka 1977 inayoeleza kuwa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii. Vilevile, Ibara ya 10(b) na 69(4) ya Katiba ya Zanzibar zinatoa mwongozo wa mapambano dhidi ya rushwa.

Mwelekeo huu ulisisitizwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati akihutubia Bunge la 12 tarehe 22 Aprili 2021 kwa kusema, *"Hatutawaonea aibu viongozi na watumishi wazembe, wezi na wabadhirifu wa mali za umma. Tutaendeleza pia juhudi za kupambana na rushwa kwenye utumishi wa umma."*

### 8.2 Historia ya Mapambano Dhidi ya Rushwa Nchini

Tanzania ilirithi sheria ya kikoloni ya Kuzuia Rushwa ya mwaka 1958 (The Prevention of Corruption Ordinance, 1958). Baada ya Uhuru vitendo vya rushwa viliongezeka kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kuongezeka kwa mmomonyoko wa maadili katika jamii; Udhaifu katika utekelezaji wa Sheria na Kanuni; Usimamizi na uwajibikaji hafifu; Taratibu ndefu na ngumu za kupata huduma; kuadimika kwa bidhaa muhimu; Maslahi madogo ya wafanyakazi ikiwemo mishahara midogo; Kupanda kwa gharama za bidhaa na mafao duni ya wastaafu.

Mwaka 1967 Chama cha TANU kilitangaza Azimio la Arusha ambalo moja ya madhumuni yake ilikuwa ni kuondosha rushwa katika jamii ya Watanzania. Kutangazwa kwa Azimio la Arusha kulisababisha kutungwa kwa Sheria ya Utekelezaji wa Miiko ya Viongozi ya Mwaka 1973 (The Committee for the Enforcement of Leadership Code Act No. 3/1973) ambayo ililenga kusimamia miiko na maadili ya viongozi wa umma.

Hali hii ilisababisha Serikali kutunga Sheria ya Kuzuia Rushwa mwaka 1971 (The Prevention of Corruption Act, No. 16/1971) hatimaye kuunda Kikosi cha Kuzuia Rushwa mwaka 1975 (Anti-Corruption Squad). Kabla ya kuanzishwa kwa Kikosi hicho shughuli za kuzuia rushwa zilifanywa na Jeshi la Polisi. Kikosi kilikuwa na jukumu la kuzuia rushwa katika utumishi wa umma na siyo kwa sekta binafsi. Majukumu ya kikosi hiki yalikuwa ni kuzuia rushwa, kufanya upelelezi na kuendesha mashtaka dhidi ya watuhumiwa wa rushwa nchini. Pamoja na jitihada za Serikali za kupambana na rushwa, kazi ya kuzuia rushwa ilikuwa ngumu kutokana na kuwepo

kwa uhaba wa bidhaa, huduma muhimu na kuongezeka kwa magendo.

Mwaka 1983 Serikali iliendesha msako wa wahujumu uchumi nchi nzima, ili kupambana na wanaotoa na kupokea rushwa. Pamoja na watuhumiwa na mali nyingi kukamatwa, hatua hii haikuweza kupata ufumbuzi wa tatizo la kuadimika kwa bidhaa nchini. Kwa hiyo Serikali ilichukua hatua ya kulegeza masharti ya biashara na kuruhusu watu waliokuwa na fedha zao nchi za nje kuingiza bidhaa. Hali hii ilipunguza kwa kiasi kikubwa rushwa iliyokuwa imeshamiri katika Mashirika ya Umma ya biashara.

Tarehe 25 Februari 1991 Halmashauri Kuu ya CCM ilitangaza Azimio la Zanzibar ambalo madhumuni yake ilikuwa ni kutoa tafsiri sahihi ya siasa ya Ujamaa na Kujitegemea kulingana na wakati uliokuwepo wa soko huria. Azimio hilo lilisababisha kufutwa kwa Sheria ya Utekelezaji wa Miiko ya Viongozi ya Mwaka 1973 hali ambayo iliongeza mmomonyoko wa maadili ya viongozi wa umma na kuongezeka vitendo vya rushwa.

Mwaka 1995 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanyiwa mabadiliko kwa kuweka Ibara ya 132 iliyoanzisha Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambayo ilianza kazi mwezi Julai mwaka 1996. Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilianzishwa ili kutekeleza Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya mwaka 1995 iliyotungwa kwa madhumuni ya kuanisha misingi ya Maadili ya Viongozi wa Umma nchini. Sheria hiyo imeweka masharti kwa viongozi wa umma kutangaza mali zao kila mwaka.

Mwaka 1996 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliunda Tume Maalum ya kukusanya maoni juu ya hali halisi ya rushwa, kufanya tathmini na kutoa mapendekezo Serikalini juu ya hatua za kutatua tatizo la rushwa nchini ambayo iliitwa “Tume ya Kero ya Rushwa Nchini” iliyoongozwa na Jaji Joseph Sinde Warioba. Kutokana na mapendekezo ya Tume hiyo, Serikali ilitengeneza Mkakati maalum wa kitaifa wa kuzuia na kupamba na rushwa nchini (The National Anti-Corruption Strategy and Action Plans (1999, 2006, 2017, 2021-NACSAP).

Mara baada ya uchumi huria kuanza na sekta binafsi kukua, iliundwa Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU) mwaka 1991. Mwaka 2007 Serikali ililazimika kutunga Sheria mpya ya Rushwa na kuanzisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa sababu zifuatazo:

a) kuiongezea majukumu Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU) kwa kuipa jukumu la kupambana na rushwa na kutoa elimu kwa umma;
b) kupanua wigo wa kupambana na rushwa kwa kujumuisha sekta binafsi; na
c) kuongeza makosa ya rushwa yakiwemo makosa ya rushwa katika siasa, ngono, ajira,biashara na matumizi mabaya ya madaraka;

Hivyo, TAKUKURU ilianzishwa kwa malengo makuu mawili, mosi kuhakikisha Nchi inaongozwa kwa kuzingatia Misingi ya Utawala Bora, Pili kuhakikisha kuwa rushwa inatokomezwa nchini. Katika kuhakikisha malengo hayo yanatimia, kwa mujibu wa kifungu cha 4

kikisomwa pamoja na kifungu cha 7 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, majukumu ya TAKUKURU ni:

a) kuelimisha umma juu ya rushwa, njia za kuikabili na kuhamasisha ushiriki wa umma katika mapambano hayo;
b) kufanya utafiti ili kubaini mianya ya rushwa na kushauri namna ya kuondoa mianya hiyo;
c) kushirikiana na taasisi mbalimbali za ndani na nje katika vita dhidi ya rushwa;
d) kufuatilia mapato na matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo kwa lengo la kuzuia ubadhirifu wa fedha za umma;
e) kuchunguza tuhuma za rushwa na makosa yanayofanana nayo; na
f) Kuendesha kesi mahakamani dhidi ya watuhumiwa wa rushwa kwa mujibu wa Sheria.

### 8.3 Mafanikio Katika Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini

Kwa kuzingatia mwelekeo huo na jitihada za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumekuwa tukishuhudia mafanikio katika vita dhidi ya rushwa. Baadhi ya mafanikio hayo ni:

a) imani ya Wananchi kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeongezeka
b) nidhamu ya Watumishi kwenye utumishi wa umma imeongezeka na kuimarika;
c) udhibiti wa fedha za umma umeongezeka;
d) usimamizi wa Sheria umeongezeka;

e) uwajibikaji katika kutekeleza miradi ya maendeleo umeongezeka;

f) kuimarika kwa utoaji wa huduma kama vile afya, elimu; na

g) kupungua kwa migogoro katika jamii na hususan eneo la ardhi.

### 8.4 Hali Ilivyo Sasa

Pamoja na kwamba nchi yetu inakabiliwa na tatizo la rushwa ambalo linaonekana katika sekta na maeneo mbalimbali, Serikali imeendelea kuchukua hatua kadhaa za kukabiliana na tatizo hilo, Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na:

a) kuwepo kwa utashi wa kisiasa wa kuzuia na kupamba na rushwa;

b) kuridhiwa na kuingizwa katika sheria za nchi masharti ya mikataba na itifaki za kikanda na kimataifa ya kuzuia na kupambana na rushwa, ikiwemo *United Nation Convention Against Corruption* (UNCAC), *African Union Convention Against Corruption* (AUCAC), SADC *Protocol Against Corruption* (SPAC), *East Africa Protocol Against Corruption* (EAPAC);

c) kuwepo kwa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wa III, ambao unatoa mwongozo wa kuzuia na kupambana na rushwa nchini;

d) kutungwa kwa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Mwaka 2007;

e) kutungwa kwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma

Sura ya 398;

f) uwepo wa Kifungu cha 114(1)(2) katika Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura 343 na Kifungu cha 106(1)(2) katika Sheria ya Uchaguzi wa Madiwani Sura 292 vinavyodhibiti rushwa katika uchaguzi;
g) uwepo wa Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200;
h) kutungwa kwa Sheria ya Ununuzi ya Umma Sura ya 410;
i) kutungwa kwa Sheria ya Utakasishaji Fedha Haramu, Sura ya 256.
j) kutungwa kwa Sheria ya Ukaguzi Sura ya 418 na Kuanzishwa kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inayoongozwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye kazi yake ni kukagua mapato na matumizi ya fedha za umma;
k) Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298;.
l) Sheria ya Uhalifu wa Makosa ya Kimtandao, Sura ya 914;
m) Sheria ya Miamala ya Kieletroniki, Sura ya 443;
n) kutungwa kwa Kanuni za Maadili ya Vyama vya Vyama vya Siasa za Mwaka 2019;
o) uwepo wa Maadili ya Uchaguzi Mkuu wakati wa Uchaguzi Mkuu (Ibara ya 2.2(k) ya Maadili ya Uchaguzi ya Mwaka 2020);
p) uwepo wa Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma Tanzania za Mwaka 1998;
q) kuundwa kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ambayo ina ofisi hadi ngazi za Wilaya;
r) kuanzishwa kwa taasisi za kusimamia masuala ya utawala bora ambazo miongoni mwa majukumu yake ni kupambana na rushwa. Taasisi hizo ni Tume ya Haki za

Binadamu na Utawala Bora na Kitengo cha Utawala Bora-Ikulu;

s) kuanzishwa kwa mamlaka ya manunuzi ya umma na mamlaka ya rufaa ya manunuzi ya umma chini ya Sheria ya Manunuzi ya Umma, Sura ya 410;

t) kuongeza uwazi na uwajibikaji katika utoaji huduma za umma;

u) uelimishaji wa umma kuhusu rushwa na madhara yake;

v) uwepo vyuo vinavyotoa elimu ya uongozi na maadili ya uongozi katika utumishi wa umma na mfumo wa vyama vingi vya siasa, mfano Chuo cha Utumishi Umma, Uongozi Institute, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Chuo cha Uongozi wa Mahakama na National Defence College;

w) ushirikishaji wananchi katika kuzuia na kupambana na rushwa. Mfano, kuanzisha kamati za uadilifu katika wizara na idara za Serikali, kuanzisha vilabu vya kuzuia na kupambana na rushwa mashuleni na vyuoni, kuishirikisha sekta binafsi katika kuzuia na kupambana na rushwa, kushirikisha wataalamu na taasisi mbalimbali kufanya utafiti, kuwashirikisha viongozi wa dini kukemea rushwa, kushirikisha Asasi za Kiraia kutoa elimu ya kuzuia na kupambana na Rushwa, n.k.

x) kufanya utafiti uliobainisha maeneo yenye ushawishi wa rushwa;

y) kutungwa kwa Sheria ya Gharama za Uchaguzi Sura ya 278 ambayo moja ya malengo yake ni kudhibiti rushwa katika mchakato wa uchaguzi;

z) kuanzishwa kwa Divisheni ya Rushwa na Uhujumu

Uchumi katika Mahakama Kuu ya Tanzania; aa) kuimarishwa kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye jukumu lake ni kukagua mapato na matumizi ya fedha za umma;

bb) kuimarika kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kusimamia mapato na matumizi ya Serikali na kudhibiti vitendo vya rushwa katika jamii, ikiwemo kutumia Kamati za Kudumu;

cc) kwa mujibu wa kifungu cha 14(1) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, kabla au tarehe 31 Machi ya kila mwaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa inapaswa kuwasilisha Taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, katika kujadili hali ya utawala bora nchini, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hujadili pia Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya TAKUKURU. Hali kadhalika, kwa mujibu wa kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma (The Public Audit Act, CAP 418) taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali huwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bungeni. Aidha, nyaraka hiyo huwa ni wazi kwa matumizi ya umma; na

dd) uwepo wa somo la uraia na maadili linalofundishwa shule za msingi na sekondari.

Kutokana na juhudi zilizofanywa na Serikali kudhibiti rushwa nchini, hali ya rushwa imepungua. Hali hiyo imethibitishwa na taarifa za tafiti mbalimbali kama ifuatavyo:

a) Taarifa ya *Transparency International* (TI) iliyotolewa Januari, 2022 inaonesha kuwa Mwaka 2021 Tanzania ilipata alama 39/100 na kushika nafasi ya 87 kati ya nchi 180 zilizofanyiwa utafiti. Kwa matokeo hayo Tanzania imepanda kwa nafasi 7 ndani ya mwaka mmoja ukilinganisha na takwimu za mwaka 2020 ambapo Tanzania ilishika nafasi ya 94 kati ya nchi 128 duniani kwa kupata alama 38/100. Kwa mujibu wa taarifa hiyo Tanzania imeshika nafasi ya 2 katika nchi za Afrika Mashariki ikitanguliwa na Rwanda,

b) kutokana na utafiti wa *World Justice Project* (WJP) inayotumia kiashiria cha "Rule of Law Index" unaonesha kuwa kwa mwaka 2020 Tanzania iliendelea kufanya vizuri kwa mwaka wa pili mfululizo katika kukabiliana na vitendo vya rushwa, hususan katika kudhibiti matumizi mabaya ya madaraka katika mihimili ya Utawala, Mahakama na Bunge kwa kupata alama 0.47 na kushika nafasi ya 93 kati ya nchi 128 duniani, ikiwa ni nchi ya kwanza Afrika Mashariki na nchi ya 13 kwa nchi zilizopo chini ya Jangwa la Sahara. Kulingana na kiashiria hiki, nchi inayopata alama 0 ina maana kwamba vitendo vya rushwa vipo chini na usimamizi wa sheria ni madhubuti na nchi inayopata alama 1 inaelezwa kuwa na udhaifu sana kwenye usimamizi wa sheria na imekithiri kwa rushwa; na

c) Taarifa ya utafiti binafsi ya Research on Poverty Alleviation (REPOA) iliyotelewa Machi 2022 inaonesha kuwa Tanzania inafanya vizuri katika kulikabili tatizo la rushwa ambapo zaidi ya theluthi tatu (77%) ya Watanzania waliohojiwa wamesema rushwa imepungua nchini.

## 8.5 Maoni ya Wadau

### 8.5.1 Maoni ya Wadau Kuhusu Kuzuia na Kupambana na Rushwa

a) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa inapaswa kutoa elimu kwa umma, ili wananchi wapate uelewa wa kutosha juu ya aina za rushwa na madhara yanayosababishwa na rushwa;

b) zitungwe sheria kali ili kudhibiti rushwa ya ngono katika siasa;

c) uanzishwe mfumo maalum wa kimahakama wa kusikiliza na kutoa hukumu za adhabu kali kwa kesi zinazohusiana na rushwa katika uchaguzi ili liwe funzo katika jamii;

d) mchakato wa kura za maoni ndani ya vyama uwekewe utaratibu wa wazi kwa kusimamiwa au kushuhudiwa na Tume huru ya Uchaguzi na Msajili wa Vyama vya Siasa, badala ya kusimamiwa na vyama vya siasa vyenyewe;

e) TAKUKURU iundwe upya kama chombo huru chenye mamlaka ya kuchunguza na kuendesha mashtaka dhidi ya makosa yanayohusiana na rushwa bila kulazimika kupata idhini au kibali cha Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali. Taasisi hii isiwe chini ya Ofisi ya Rais bali iwe huru ya kikatiba, kama *Serious Fraud Office ya UK*, IGG ya Uganda na ACA ya Siera Leone inavyofanya kazi;

f) zitolewe adhabu kali kwa mtu aliyethibitika kutenda kosa la rushwa ikiwemo adhabu ya mtu kupigwa risasi hadharani;

g) Sheria ya Gharama za Uchaguzi ifanyiwe marekebisho ili kuongeza adhabu kwa wanaokiuka taratibu. Aidha, ukaguzi wa fedha za vyama vya siasa na taarifa ya ukaguzi zitolewe kwa umma kwa uwazi na bila kupendelea chama chochote;

h) rushwa zinazohusu matumizi mabaya ya rasilimali na madaraka zidhibitiwe kwa uzito wake;

i) kuwe na uwajibikaji katika suala la rushwa na maadili katika siasa, mfano mtu ukipatikana na hatia kwa kosa la kimaadili asiruhusiwe kushiriki katika uchaguzi;

j) matendo ya rushwa yaelezwe vizuri kwa wananchi na elimu ya rushwa ianze kutolewa kuanzia shule za msingi;

k) kuna haja ya kutolewa elimu kwa wananchi juu ya aina za rushwa, ubaya na madhara ya rushwa;

l) TAKUKURU, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi wanatakiwa kufanya kazi zao, ili kukabili rushwa wakati wa uchaguzi. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ambayo ni msimamizi wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi ishirikiane na TAKUKURU katika kufuatilia utekelezwaji wa sheria hiyo.

m) katiba za vyama ziwekewe vipengele vikali vya kudhibiti vitendo vya rushwa ndani ya vyama vya siasa na zitoe adhabu kali itakapobainika mtu ameteuliwa katika nafasi fulani au kuwa mgombea kwa kutumia rushwa, uteuzi wake utenguliwe na asiruhusiwe kugombea tena kwa kipindi cha miaka 5;

n) kuwe na uwazi katika mambo mengi ya umma, ili kuziba mianya ya rushwa;

o) kuwe na sheria mahususi ya kuratibu mgongano wa maslahi;

p) ziundwe klabu za rushwa kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu;

q) mmomonyoko wa maadili katika jamii. Mfano, tamaa ya mali (Greedy) na mwili inayosababishwa na kutokuwa na malezi mazuri, tabia ya ubinafsi na kutoridhika. Aidha, utamaduni uliojengeka katika jamii, ambapo kuna watu wanashiriki katika vitendo rushwa kwa sababu wanaona wenzao wanafanya hivyo. Vilevile, jamii kumthamini mtu mwenye mali nyingi bila kujali amezipataje;

r) rushwa bado ipo katika jamii na hasa katika siasa na uchaguzi;

s) wananchi wengi hasa wa vijijini hawajafahamu haki zao za kikatiba;

t) kipato kidogo kisicho kidhi mahitaji ya maisha huchochea rushwa (survival corruption);

u) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini haitekelezi majukumu yake ipasavyo;

v) elimu inayotolewa kuhusu kuzuia na kupambana na rushwa hailingani na hali ya tatizo;

w) kujengeka kwa utamaduni kwa baadhi ya wananchi wa kutoa na kupokea rushwa, hasa katika kipindi cha uchaguzi;

x) baadhi ya wananchi hawaelewi matendo gani ambayo ni rushwa na matendo ambayo siyo rushwa katika uchaguzi. Wakati wa uchaguzi watu wamekuwa wakipewa pesa taslimu, khanga, fulana, kofia na ahadi mbali mbali na hata

kupokea zawadi ambazo zilikuwa hazitolewi nyakati za kawaida;

y) baadhi wa wananchi hawaelewi madhara ya rushwa katika uchaguzi;

z) muhali; Mtu kushindwa kuchukua hatua za kisheria kwa sababu ya upendeleo au kuogopa lawama kwa ndugu, rafiki na jirani;

aa) sheria zinazodhibiti rushwa hazitekelezwi ipasavyo, mfano Sheria ya Gharama za Uchaguzi Sura 278; bb) baadhi ya vyama vya siasa havina mikakati thabiti ya kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa. Mikakati iliyopo haitekelezwi ipasavyo;

cc) kuwa na mifumo ya kiuchumi isiyotabirika au kumwezesha mtu kuishi maisha ya heshima;

dd) ugumu wa kuzuia na kupambana na rushwa kutokana na vitendo hivyo kutendwa kwa kificho;

ee) kutokuwepo kwa uwazi wa kutosha na uwajibikaji katika masuala ya kifedha na utoaji huduma katika jamii;

ff) upungufu katika Sheria zinazodhibiti rushwa unafanya kazi ya kuzuia na kupambana na rushwa isifanyike kwa ufanisi. Mfano Sheria ya Gharama za Uchaguzi. Sheria hii inakiadhibu chama cha siasa badala ya mgombea anayeshindwa kufanya marejesho ya gharama za uchaguzi ndani ya wakati. Vitendo vinavyokatazwa havina sifa ya kuwa kosa la jinai. Nyaraka za uthibitisho wa matumizi ya gharama za uchaguzi kutakiwa kuwasilisha kwa msajili wa vyama vya siasa badala ya kubaki katika chama cha siasa husika ili kwa ajili ya ukaguzi; na

gg) Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ambayo kifungu cha 25 cha Sheria hiyo hakimwajibishi mtu anayetoa rushwa ya ngono. Kifungu hicho kinapunguza adhabu ya makosa ya ngono inayotolewa chini ya Sheria ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA), ambayo adhabu ya kosa hilo ni kifungo cha miaka 30 jela. Vilevile, Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6 haitambui dhana ya Ushahidi wa mazingira (Circumstantial Evidence), hali inayosababisha kushindwa kuthibitishwa kwa makosa mengi ya rushwa.

### 8.5.2 Maoni ya Wadau Kuhusu Usimamizi wa Maadili Nchini

Katika eneo hili wadau wametoa maoni kwamba maadili yameporomoka kwa sababu zifuatazo:

a) utandawazi, kuiga mambo ya nchi nyingine ambayo hayaendani na utamaduni na mazingira ya nchi yetu;
b) kuacha kufuata mila na desturi za asili zinazofaa;
c) baadhi ya viongozi wa dini kutotekeleza wajibu wao ipasavyo;
d) kushindwa kulea watoto kimaadili tangu wakiwa wadogo katika familia na shuleni;
e) kutokuwepo mpango na mkakati mahususi wa kitaifa wa kukuza uadilifu;
f) maisha ya kifamilia kutopewa kipaumbele na msisitizo wakutosha;
g) maadhi ya watu kutoa tafsiri mbaya ya haki za binadamu katika jamii. Mfano, haki ya mtu binafsi kuamua juu ya maisha yake, hutafsiriwa na baadhi ya watu kuwa, mtu ana haki ya kuamua kufanya jambo lolote juu ya maisha na

mwili wake. Haki ya mtoto kutafsiriwa na baadhi ya watu kuwa, mtoto hastahili kukemewa au kuadhibiwa anapofanya kosa;

h) shinikizo kutoka kwa baadhi ya wadau wa maendeleo wanaofadhili miradi na shughuli mbalimbali za kijamii nchini, kutaka taasisi zinazotekeleza miradi au shughuli hizo kukubali agenda zao; na

i) mkakati mahususi wa nchi za nje kupandikiza utamadumi wao katika nchi nyingine ikiwemo nchi yetu, kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo filamu, katuni, tamthilia, muziki, ufadhili wa masomo, vipindi vya televisheni.

## 8.6 Mapendekezo ya Tume na Kamati Mbalimbali;

Katika kushughulikia suala la rushwa Kikosi Kazi kilipata fursa ya kupitia maoni na mapendekezo ya Tume na Kamati mbalimbali. Maoni na mapendekezo ya Tume na Kamati hizo ni:

### 8.6.1 Mapendekezo ya Tume ya Rais ya Kuchunguza Masuala ya Rushwa (Tume ya Rushwa ya Warioba)

Tume ya Kero ya Rushwa Nchini iliyoongozwa na Jaji Mstaafu Mheshimiwa Joseph Sinde Warioba katika taarifa yake ya Novemba 1996, ilipendeza masuala yafuatayo katika kukabiliana na tatizo la rushwa nchini:

a) Tume inaamini ili kupambana na rushwa hatua za mwanzo ni lazima zihusu viongozi, viongozi wasio waadilifu wachukuliwe hatua mapema;

b) hatua zitakazochukuliwa zilenge kuwafanya viongozi wafuate maadili;
c) kazi ya kupambana na rushwa asiachiwe Rais peke yake;
d) wananchi wanatakiwa kuelimishwa kuhusu haki zao ili waweze kuzidai pale ambapo wataona kuwa wanadhulumiwa au kucheleweshwa;
e) vyombo vya habari vitumike ipasavyo kuzuia na kupambana na rushwa kwa kuwafichua wale wote wanaokiuka maadili kwa kudai na kupokea rushwa;
f) viongozi na watumishi wa umma wakipokea zawadi kutoka kwa mtu yeyote waziwasilishe kwa uongozi wa juu wa mahali pa kazi;
g) maadili yote yaorodheshwe katika sheria na adhabu za ukiukwaji wa maadili ziwekwe bayana; na
h) viongozi wa umma watangaze mali zao.

**8.6.2 Kamati ya Kuratibu Maoni Kuhusu Katiba, iliyoongozwa na Mheshimiwa Jaji Robert Kisanga katika taarifa yake ya tarehe 20 Agosti 1999, ilipendekeza masuala yafuatayo katika kukabiliana na tatizo la rushwa nchini:**

a) kurudiwa kwa uchaguzi kunaweza kusababisha kukua kwa vitendo vya rushwa, ulaghai na udanganyifu;
b) uanzishwe mfumo wa uwakilishi wa uwiano ili kuondoa rushwa inayoambatana na uchaguzi wa majimbo. Mfumo wa uchaguzi wa majimbo hutoa mwanya wa rushwa katika hatua mbili, hatua ya uteuzi na hatua ya kampeni ambapo mgombea hukutana moja kwa moja na wananchi. Katika Mfumo wa Uchaguzi wa Uwiano, mhusika ana hatua moja

tu ya mwanya wa rushwa, yaani, hatua ya kuteuliwa. Ni katika maana hii, uwiano hupunguza rushwa; na

c) kianzishwe Chuo cha Uongozi ambacho pamoja na mambo mengine kitafundisha Maadili ya Utumishi wa umma katika mfumo wa vyama vingi vya siasa.

### 8.6.3 Katiba Inayopendekezwa

Katika kuzuia na kupamba na rushwa, Katiba Inayopendekezwa inaeleza ifuatavyo:

a) Serikali na vyombo vyake vinawajibika kuelekeza sera, sheria na shughuli zake zote kwa lengo la kuhakikisha aina zote za dhuluma, vitisho, ubaguzi, ukatili, udhalilishaji, unyanyasaji, rushwa, uonevu au upendeleo zinaondolewa nchini (Ibara ya 8(2)(h));

b) katika eneo la malengo ya kisiasa, Katiba hiyo inaeleza kuwa, katika kuhakikisha utekelezaji wa lengo hilo, Serikali itachukua hatua zinazofaa ili kuhakikisha kuwa inazuia na kuondoa dhuluma, vitisho, ubaguzi, unyanyasaji, rushwa, uonevu na upendeleo miongoni mwa wananchi…(Ibara ya 12(2)(a);

c) Katika eneo la dhamana ya uongozi wa umma, Katiba hiyo inaeleza kuwa, mtu mwenye dhamana ya uongozi wa umma atazingatia mambo yafuatayo, anakapokuwa anafanya uamuzi wowote katika jambo lolote la umma atahakikisha uamuzi wake hautokani na udugu, ukabila, udini, rushwa au ubaguzi wa aina yoyote (Ibara ya 28(2)(b); na

d) Katika eneo la uchaguzi na kura ya maoni, Katiba hiyo inaeleza kuwa, … mamlaka ya kusimamia uchaguzi itazingatia misingi kwamba uchaguzi unakuwa huru na wa haki ambao, hauna matumizi ya nguvu, vitisho, vishawishi wala rushwa.

## 8.7 Uzoefu wa Nchi Nyingine

Singapore na Hong Kong zimepiga hatua kubwa katika kutokomeza rushwa na kujenga uadilifu. Serikali zimeonesha mfano wa kutoivumilia rushwa na vyombo vinavyopambana na rushwa vimeaminiwa kwa kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria. Wananchi wameviamini vyombo vyao kwa sababu wanapotoa taarifa kuhusu watu wanaojihusisha na vitendo vya rushwa wanaona hatua madhubuti zinachukuliwa.

Kwa upande wa maadili ya viongozi wa utumishi wa umma na wanasiasa, Serikali ilianzisha Sekretarieti ya Maadili inayoongozwa na Kamishna kushughulikia maadili kwa kuweka mfumo wa kuwataka viongozi wa umma kutoa matamko yao ya mali na madeni.

## 8.8 Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Baada ya kupitia maoni ya wadau na nyaraka mbalimbali, Kikosi Kazi kinapendekeza yafuatayo:

a) suala la rushwa litamkwe katika Katiba, ili wananchi watambue kuwa vitendo vya rushwa havitavumiliwa wala

kuonewa muhali. Pendekezo hili lifanyiwe kazi katika mchakato wa kutungwa kwa Katiba Mpya ili litekelezwe kwa ufanisi;

b) Sheria ya vyama vya Siasa Sura 258 irekebishwe ili:

   i) kuweka sharti kwamba, katiba ya chama cha siasa iwe na adhabu ya kumwondoa katika mchakato wa uchaguzi, mtia nia au mgombea aliyedhaminiwa na chama, endapo atathibitika kujihusisha na vitendo vya rushwa;
   ii) Msajili wa Vyama vya Siasa apewe mamlaka ya kuandaa mwongozo wa kufuatilia mchakato wa uteuzi wa wagombea na uchaguzi wa viongozi, ndani ya Vyama vya Siasa; na iii) kukitaka kila chama cha siasa kuwa na Kanuni za Maadili, zitakazodhibiti ukiukwaji wa maadili ndani ya chama, ikiwemo mwanachama kujihusisha na vitendo vya rushwa. Kanuni hizo ziweke utaratibu wa kushughulikia ukiukwaji wa maadili na adhabu, ikiwemo onyo, karipio, faini, kuvuliwa ujumbe wa kikao husika, kutoruhusiwa kugombea uongozi ndani ya miaka kumi tangu alipopatikana na hatia, kusimamishwa au kufukuzwa uanachama.

c) Sheria ya Gharama za Uchaguzi irekebishwe ili:

   i) kutoa adhabu kwa mgombea atakayeshindwa kufanya marejesho ya gharama za uchaguzi badala ya kukiadhibu chama cha siasa;
   ii) vitendo vinavyokatazwa katika sheria hiyo kuwa na sifa ya kuwa kosa la jinai;

iii) nyaraka za uthibitisho wa matumizi ya gharama za uchaguzi zibaki katika chama cha siasa husika badala ya kuwasilishwa kwa Msajili wa vyama vya siasa; na

iv) kuondoa upungufu mwingine wowote ambao ni kikwazo katika kuzuia na kupambana na rushwa katika mchakato wa uchaguzi;

d) Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6 irekebishwe kutambua Ushahidi wa mazingira (Circumstantial Evidence), ili uweze kutumika Mahakamani kuthibitisha makosa ya rushwa;

e) Sheria za Uchaguzi zirekebishwe kuweka masharti kwamba, mgombea atakayethibitika kujihusisha na vitendo vya rushwa aondolewe sifa ya kugombea katika uchaguzi wowote kwa miaka 10 mfululizo;

f) Sheria ya Watoa Taarifa na Ulinzi wa Mashahidi Sura ya 446 ifanyiwe marekebisho ili kuongeza kinga kwa mtoa taarifa wa siri;

g) Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa irekebishwe, ili kumwajibisha pia mtu anayetoa rushwa ya ngono. Aidha, adhabu zinazotolewa katika sheria hiyo kuhusu kosa la rushwa ya ngono ziendane na zile zilizopo katika Sheria ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA);

h) mitaala katika shule za msingi na sekondari iwe na moduli ya rushwa, badala ya kutajwa kama mengineyo kwenye somo la uraia;

i) matumizi ya teknolojia katika kuzuia na kupambana na rushwa yaongezwe, ili kuibua ushahidi uliojificha kwa

kutumia utaalam wa utambuzi (exhumation of hidden evidence through forensic expertise);

j) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa isiingiliwe kisiasa wala kiutawala kinapotimiza majukumu yake ilhali kinafuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa kisheria;

k) kujenga silka na hulka ya uadilifu kwenye kaya (familia) hadi ngazi ya Taifa kwa njia zifuatazo:

    i) kuwa na mpango na mkakati mahususi wa kitaifa wa kukuza uadilifu;
    ii) kudhibiti utandawazi ili kuepusha wananchi kuiga mambo ya nchi nyingine ambayo hayaendani na utamaduni na mazingira ya nchi yetu;
    iii) kuheshimu na kufuata mila na desturi za asili zinazofaa;
    iv) viongozi wa dini waendelee kutekeleza majukumu yao ipasavyo;
    v) familia na shule ziweke mkazo katika malezi ya watoto kimaadili.
    vi) shule za msingi na sekondari za umma na binafsi ambazo siyo seminari zitakiwe kuwa na vipindi vya dini, ili kuruhusu watoto kupata elimu ya dini ambayo kimsingi ni njia ya kujenga uadilifu; na
    vii) maisha ya kifamilia yapewe kipaumbele na msisitizo wakutosha;

l) Somo la uraia na maadili linalofundishwa shule za msingi na sekondari liwekewe mkazo wa kutosha na lifundishwe katika ngazi zote za elimu.

# SURA YA TISA

# MFUMO WA MARIDHIANO ILI KUDUMISHA HAKI, AMANI, UTULIVU NA UMOJA WA KITAIFA

## 9.1 Utangulizi

Maridhiano ni matokeo ya mazungumzo yanayofanyika kati ya pande mbili au zaidi zinazotofautiana, zilizo kwenye mgogoro au uhasama wa kisiasa ili kupata suluhu. Kwa tafsiri nyingine maridhiano ni makubaliano ya hiyari kati ya mtu na mtu, kikundi na kikundi au jamii nzima yanayofikiwa ili kupata lengo linalokusudiwa na lenye faida na maslahi mapana zaidi kwa pande zote husika.

Ili maridhiano yaweze kufikiwa inahitajika wahusika kuaminiana, kuwa tayari kusamehe na kupoteza sehemu ya madai yao, kujali zaidi maslahi ya nchi kuliko maslahi yao binafsi na kutimiza wajibu wao wa kisiasa na kijamii. Watanzania wana utamaduni wa kuzungumza inapotokea kutofautiana, hali inayofanya utatuzi wa migogoro ya kisiasa kuwa rahisi. Mfano ni mgogoro wa kisiasa uliotokea Zanzibar na kutatuliwa kwa njia ya mazungumzo na hatimaye kuundwa kwa Baraza la Vyama vya Siasa linalowezesha Vyama vya Siasa kukutana mara kwa mara ili kujadiliana.

Baraza la Vyama vya Siasa lipo kisheria, moja ya jukumu lake ni kujadili masuala yanayohusu demokrasia ya vyama vingi vya siasa na kuishauri Serikali. Vilevile, zipo fursa nyingine za Vyama vya Siasa kukutana na kuzungumza kupitia warsha, makongamano na mikutano inayoandaliwa na asasi za kiraia (AZAKI), vyuo vikuu, Tume ya Uchaguzi na taasisi nyingine.

Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, muktadha wa Maridhiano umeota mizizi kutokana na historia ya muda mrefu ya mivutano ya kisiasa. Kilio cha Maridhiano upande wa Zanzibar kimekuwa kikijitokeza nyakati za Uchaguzi tangu mwaka 1995 chini ya mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa na kusababisha mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar mwaka 2010 ambapo, Wazanzibari waliondokana na mfumo wa mshindi kuchukua kila kitu na badala yake Vyama vya Siasa kugawana madaraka kulingana na nguvu zao za kisiasa.

Kwa upande wa Tanzania Bara miaka ya hivi karibuni kumekuwa na wito kutoka kwa viongozi wa Serikali, viongozi wa dini, wanasiasa na wadau mbalimbali wa kisiasa kutaka maridhiano katika Taifa letu. Wito huu wa maridhiano umeanza kusikika baada ya mwaka 2018 kufuatia hisia kwamba vyama vya upinzani havipati haki sawa za kisiasa na kiuchumi kama ilivyo kwa chama kinachotawala.

Baada ya Serikali ya Awamu ya Sita kuingia madarakani Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameonesha utayari wa kuimarisha mshikamano na maridhiano kama alivyobainisha kupitia hotuba yake alipokuwa akilihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 1 Julai, 2022 kwa kueleza kuwa: *"…Ninaamini maridhiano hayawezi kupatikana penye ubaguzi na pale ambapo kuna wanaokosa fursa na haki zao za kiuchumi na kiraia…"* Vile vile, alipokuwa akizindua Mkutano wa Wadau wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa uliofanyika Dodoma tarehe 15 hadi 17 Desemba 2021 aliwasihi wanasiasa kutatua matatizo, changamoto na kuondoa tofauti baina yao kwa njia ya mazungumzo.

Mheshimiwa Rais ameendeleza utamaduni wa kukutana na kufanya mazungumzo na wadau mbalimbali wa siasa na demokrasia nchini kwa lengo la kutatua changamoto mbalimbali katika masuala ya kisiasa na demokrasia. Kwa muktadha huo, ni dhahiri kuwa yeye ni kiongozi anayetaka kuongoza Taifa lenye umoja na mshikamano.

Vilevile, Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025 inatambua uzalendo, utaifa na kuimarisha mshikamano wa kitaifa wa watu wote katika jamii kwa kuzingatia mazingira ya sasa ya kiuchumi, kisiasa na mambo mengine husika.

Miaka 30 imepita tangu Tanzania ilipoamua kurudisha Mfumo wa demokrasia ya Vyama Vingi Vya Siasa mwezi Julai, 1992. Harakati za ujenzi wa demokrasia katika sehemu mbalimbali duniani hata mataifa yanayoaminika kuwa na demokrasia ya kweli, hazitokei kwa njia rahisi bali huwa ni kwa njia ya mapambano.

Historia ya Tanzania nayo inatuonesha kwamba mfumo huo wa Siasa za Ushindani wa Vyama Vingi haukuwa rahisi katika utekelezaji wake, bali ulitawaliwa na mtiririko wa mapambano ya kidemokrasia.

Tanzania, kwa pande zote mbili, yaani Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara zilipitia misukosuko na changamoto mbalimbali katika ushindani wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa (mapambano ya kidemokrasia) na kuacha majeraha na makovu mengi.

Hadi mwaka 2015 hali ilikuwa nzuri kiasi kwa upande wa Tanzania Bara, Mwaka 2016 Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kikishirikiana na Vyama vingine vya Siasa kilizindua

operesheni iliyojulikana kama Umoja wa Kupinga Udikteta Tanzania (UKUTA) iliyokuwa na lengo la kupinga kile walichokiita ni ukandamizaji wa demokrasia nchini. Hatua hii ililenga kuhoji hatua mbalimbali zilizokuwa zikichukuliwa na Serikali, ikiwemo kupiga marufuku mikutano ya hadhara. Operesheni hii iliwataka baadhi ya wafuasi wa vyama vya siasa kufanya maandamano nchi nzima kwa lengo la kushinikiza Serikali kukubali yale waliyokuwa wanaamini ni haki yao kwa mujibu wa Sheria. Tishio hili lilipokuwa kubwa viongozi wa dini walilazimika kukaa na viongozi wa vyama vya siasa vilivyokusudia kufanya maandamano ili kufanya mazungumzo na kuwasihi wasitishe zoezi hilo. Viongozi hao walikubali kukaa katika meza ya mazungumzo na hatimaye kusitisha maandamano hayo.

Hata hivyo, kabla na baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 hali ya kisiasa ilichafuka zaidi huku wanasiasa wakiwa hawawezi kutekeleza majukumu yao ya kisiasa kwa mujibu wa sheria. Hali hii ilisababisha kuongeza uhasama kati ya Vyama na Vyama, na kwa upande mwingine Vyama vya Siasa na Serikali.

Mgogoro huu ulisababisha kuanzishwa kwa mazungumzo na wadau mbalimbali wa masuala ya demokrasia ili kutafuta suluhu juu ya yaliyotokea (na hatimaye kuanzishwa kwa Kikosi Kazi cha Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).

Kwa upande wa Zanzibar, ushindani huu wa kisiasa tangu ulipoanza mwaka 1992 na kuongezeka baada ya Uchaguzi wa 1995 uligubikwa na kutawaliwa na siasa za chuki, uhasama, ubaguzi wa kiitikadi na kiuzawa. Hali hii ilichangia kuzuka kwa migogoro kila baada ya Uchaguzi Mkuu kutokana na kuwa na ushindani wa kisiasa uliokaribiana kati ya vyama vikuu viwili vya

siasa ambavyo ni Chama Cha Mapinduzi (CCM) na The Civic United Front (CUF-Chama cha Wananchi) kwa wakati huo. Hali hiyo ya mitafaruku ya kisiasa Zanzibar ililazimisha kuanzishwa kwa mazungumzo baina ya vyama hivyo ambayo yalileta Muafaka wa Kwanza wa kisiasa wa mwaka 1999 baadhi ya mambo yalioafikiwa ni pamoja na:

a) Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kufanyiwa marekebisho ili kuifanya iwe Tume huru na ya haki kufuatana na mfumo unaokubalika katika nchi za Jumuiya ya Madola.
b) kuanzishwa kwa Daftari la Kudumu la Wapiga kura.
c) kufanyiwa mapitio Katiba ya Zanzibar na Sheria za Uchaguzi ili ziafikiane na matakwa ya demokrasia ya vyama vingi.
d) vyombo vya habari vya Serikali viepukane na upendeleo katika kutangaza shughuli za vyama vya siasa.
e) kuhakikisha kuwepo kwa uhuru wa vyama vya siasa kuendesha shughuli zake bila ya bughudha au vitisho.
f) Mahakama za Zanzibar kufanyiwa marekebisho ili kukuza uhuru wake, utalaamu na heshima yake mbele ya jamii.

Kutokutekelezwa kwa makubaliano hayo kulisababisha machafuko ya tarehe 26 na 27 Januari 2001, baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2000 Zanzibar, ambapo baadhi ya watu walipoteza maisha na kwa mara ya kwanza Tanzania ikazalisha wakimbizi kwenda shimoni Mombasa nchini Kenya. Viongozi wa vyama hivyo viwili walilazimika tena kuanzisha mazungumzo ya kujaribu kuleta suluhu ya kisiasa. Mazungumzo hayo yalizaa Muafaka wa Pili wa mwaka 2001. Kwa kutambua matatizo ya utekelezaji wa makubaliano yaliyopita ya mwaka 1999, Muafaka huu ulianzishwa kisheria chini

ya Tume ya Rais ya Pamoja ya Usimamizi (The Joint Presidential Supervisory Commission).

Baada ya kuendelea kwa migogoro kila unapoisha uchaguzi Mkuu Zanzibar, yalifikiwa maridhiano kati ya Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Makamu Mwenyekiti wa CCM (Zanzibar) na Maalim Seif Sharif Hamad, Katibu Mkuu wa CUF (Zanzibar) tarehe 5 Novemba 2009, ili kuondoa uhasama wa kisiasa uliokuwa umejengeka baina ya Wazanzibari. Kufuatia maridhiano hayo, iliamuliwa kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

Tarehe 31 Julai 2010 wananchi wa Zanzibar walipiga Kura ya Maoni ili kupata ridhaa kuhusu Muundo Mpya wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambapo wananchi waliridhia na kusababisha kufanywa kwa mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar 2010.

Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar wa Mwaka 2015 ulifutwa kabla ya kutangazwa kwa matokeo, kutokana na tukio hilo ilisababisha uchaguzi huo kurudiwa. Hata hivyo, Chama cha Wananchi (CUF) ambacho kilikuwa ni chama kikuu cha upinzani kilisusia kushiriki katika uchaguzi huo na kutotambua matokeo ya uchaguzi yaliokipa ushindi Chama Cha Mapinduzi (CCM). Hali hiyo iliendeleza migogoro ya kisiasa iliyodumu kabla na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Kutokana na mgogoro wa ndani ya chama cha siasa The Civic United Front (CUF-Chama cha Wananchi) Katibu Mkuu wa chama hicho ambaye alikuwa akikiwakilisha chama hicho katika mazungumzo hayo, alihama na kujiunga na chama cha Alliance for Change and Transparency (ACT-Wazalendo) na kuendeleza mazungumzo hayo akiwa Makamu Mwenyekiti wa chama hicho.

Matokeo ya mazungumzo hayo yalisababisha makubaliano baina ya Vyama hivyo viwili na hatimaye chama cha Alliance for Change and Transparency (ACT-Wazalendo) kilikubali kushiriki katika kuendesha Serikali ya Umoja wa Kitaifa kama ilivyo kwenye Katiba ya Zanzibar.

Kwa ujumla jitihada za makusudi zinahitajika kutibu majeraha na kuleta maelewano kwa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili nchi yetu iweze kupiga hatua za maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

### 9.2 Utaratibu wa Maridhiano

Kwa uzoefu wa Zanzibar, Maridhiano yalifanyika kwa kuanza na mazungumzo ya pande zinazohitilafiana na kuweka mezani maeneo muhimu ambayo yalikuwa yanalalamikiwa kwa pande zote mbili.

Baada ya kufikia makubaliano au maridhiano mwaka 2001 kulifuatiwa na kuundwa kwa chombo cha kusimamia makubaliano hayo kisheria.

Makubaliano ya Mwaka 2009 kati ya viongozi wakuu wa vyama vya siasa vya CCM na CUF yalisababisha kufanyika mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 2010 na uwepo wa kura ya maoni na hatimaye kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Kwa Upande wa Tanzania Bara, Kiongozi Mkuu wa nchi Mhe.Rais Samia Suluhu Hassan ameona umuhimu wa kuonana na kufanya mazungumzo na wadau wa siasa, kwa kundi moja moja au kwa pamoja na kuzungumza masuala yenye changamoto kisiasa.

## 9.3 Mapendekezo ya Tume na Kamati Mbalimbali

Mwaka 2001 Tume ya Rais ya Pamoja ya Usimamizi ilipendekeza kuwepo na kamati ya kudumu ya pamoja ya Mashauriano ya Vyama vya Siasa nchini itakayowajumuisha viongozi wa kitaifa wa vyama vyote vya siasa vilivyopo nchini. Kamati hiyo ilitakiwa kuwa jukwaa la kubadilishana mawazo na kujenga maelewano juu ya masuala mazito yanayohusu nchi yetu. Tume hiyo pia ilipendekeza kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Ibara ya 15(2)(d) ya Katiba Inayopendekezwa inazungumzia kujenga utamaduni wa kuwepo ushirikiano, maelewano, maridhiano, uvumilivu na kuheshimu mila, desturi na imani ya dini ya kila mtu.

Ripoti ya Kamati ya Kuratibu Maoni Kuhusu Katiba ya 1999 (Ripoti ya Jaji Robert H. Kisanga) ikizungumzia maridhiano ilisema, Muundo wa Muungano tunaoshauri ufikiriwe siyo lazima uwe suluhisho la kudumu la matatizo ya Muungano, kwani Muungano unategemea zaidi maridhiano na utashi wa kisiasa kwa pande zote mbili.

## 9.4 Maoni ya Wadau

Wadau mbalimbali waliwasilisha maoni yao mbele ya Kikosi Kazi kama ifuatavyo:

a) liwepo Jukwaa la Kudumu la Majadiliano litakalohusisha Vyama vya Siasa na wadau wengine muhimu, ikiwemo Serikali na viongozi wa dini;

b) kukifanya Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) kuwa jukwaa la kudumu la majadiliano litakalohusisha Vyama vya Siasa na wadau wengine ikiwemo Serikali kwa kukianzisha rasmi kwa mujibu wa Sheria ya Bunge na kuangalia namna bora ya kuimarisha muundo wake;

c) kuliboresha Baraza la Vyama vya Siasa kwa kuliongezea uwezo kifedha na kuongeza idadi ya wajumbe wake kutoka wajumbe wawili hadi wanne kwa kila chama cha siasa;

d) iundwe Tume ya Maridhiano ya Kitaifa yenye mchanganyiko wa wanasiasa, viongozi wa dini na watu wanaoaminika na kuheshimika ndani ya jamii. Mfano wa kuigwa ni Afrika ya Kusini;

e) uanzishwe mfumo rasmi wa kisheria wa kuvikutanisha vyama vya siasa pale tofauti zinapotokea hasa kila baada ya Uchaguzi Mkuu;

f) kuondokana na mfumo wa uchaguzi wa mshindi kubeba kila kitu na kumwacha aliyeshindwa bila chochote;

g) kuangalia uwezekano wa kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kila chama kinachotimiza masharti kiweze kushiriki katika juhudi za maendeleo ya Taifa;

h) Serikali ipitie changamoto zinazojitokeza wakati wa uchaguzi na kuzipatia ufumbuzi;

i) Katiba ifanyiwe mabadiliko na kutaja tunu za maridhiano ili kuimarisha haki amani na utulivu wa nchi;

j) kuna umuhimu wa Vyama vya Siasa kuaminiana katika masuala ya uchaguzi na uendeshwaji wa Serikali;

k) liwepo jukwaa la kudumu la majadiliano litakalohusisha Vyama vya Siasa na Serikali;

l) kuwe na Mkutano wa kila Mwaka kujadili changamoto za kisiasa nchini utakaowahusisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar, wadau wa siasa, viongozi wa dini na watu mashuhuri ndani ya jamii;

m) utumike uzoefu wa Zanzibar wa mwaka 2002-2005 ambapo walitumia Tume ya Rais ya Pamoja ya Usimamizi (Joint Presidential Supervisory Commission (JPSC) katika suala zima la kuleta maridhiano;

n) iundwe Tume ya ukweli na maridhiano kama ilivyo Afrika Kusini;

o) liundwe Baraza la usuluhishi la Taifa litakalo husika katika kutatua migogoro yote ya kisiasa pindi inapotokea;

p) itolewe Elimu ya Uraia kwa wananchi ili kuwajengea uwezo wa kufahamu haki zao za msingi, kujenga uzalendo, na kuwaelimisha kuhusu tunu za Taifa;

q) Sheria ya Vyama vya Siasa iweke utaratibu wa usuluhishi wa migogoro miongoni mwa Vyama vya Siasa kwa kuweka mfumo wa mpatanishi kama ilivyo kwa migogoro ya kibiashara;

r) kutokuwa na utaratibu rasmi au chombo cha kuwezesha mazungumzo baina ya vyama vya siasa pindi inapotokea migogoro;

s) tabia ya baadhi ya wanasiasa kutoaminiana inasababisha suala la mazungumzo kufikia Maridhiano kuwa gumu katika nyakati fulani;

t) Vyama vya Siasa na taasisi nyingine zinazohusiana na masuala ya siasa na demokrasia kutokuwa na tabia ya kuelekezana, kuelimishana na kujadiliana; na

u) ubinafsi wa baadhi ya viongozi na wanachama wa vyama vya siasa kujali zaidi maslahi binafsi na ya vyama vyao kuliko maslahi ya Taifa.

**9.5 Uzoefu wa Nchi Nyingine**

Kikosi Kazi kimepitia nyaraka mbalimbali kutoka nchi tofauti na kuona namna nchi hizo zilivyofanikiwa katika eneo la maridhiano.

Mwezi Desemba 1995, Afrika Kusini ilianzisha Tume ya Ukweli na Maridhiano (The South African Truth and Reconcilliation Commission (TRC)). Kusudi kuu likiwa ni kukuza upatanisho na msamaha kati ya wahalifu na waathiriwa wa ubaguzi wa rangi. Tume ilipewa kazi tatu maalum, kugundua sababu na asili ya ukiukwaji wa haki za binadamu nchini Afrika Kusini kati ya 1960 na 1994, kutambua waathiriwa kwa nia ya kulipa fidia; na kuruhusu msamaha kwa wale ambao walifichua kikamilifu kuhusika kwao katika ukiukaji wa haki za binadamu uliochochewa na ubaguzi wa rangi.

Katika nchi ya Ghana, mwaka 2002 Bunge la nchi hiyo liliteua Tume ya Kitaifa ya Maridhiano (National Reconciliation Commission (NRC)), ili kuendeleza maridhiano ya kitaifa miongoni mwa Waghana kwa kuweka kumbukumbu sahihi ya kihistoria ya ukiukwaji wa haki za binadamu na unyanyasaji uliofanywa na watu

na taasisi za umma na maafisa wa umma kati ya mwaka 1957 na mwaka 1993.

Nchini Kenya, kuna chombo maalum cha kitaifa kiitwacho National Cohesion Commission (NCC) ambacho kazi yake kubwa ni kuhakikisha kuwa wanashughulikia dalili zote za kuvunjwa kwa umoja wa Taifa lao. Chombo hiki ni cha kudumu.

Nchini Sierra Leone, kuliundwa Tume ya Ukweli na Upatanisho ikiwa kama sehemu ya Mkataba wa Amani wa Lomé, ambao ulimaliza mzozo wa miaka 11 wa vita vya wenyewe kwa wenyewe.

## 9.6 Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Baada ya kupitia, kuchambua na kufanya tathmini ya maoni ya wadau, Kikosi Kazi kinatoa mapendekezo yafuatayo:

a) kuanzishwe utaratibu wa mijadala kila mwaka (Annual State of Politics Conference) itakayohusisha viongozi wakubwa wa kitaifa wa dola na Vyama vya Siasa ambapo mjadala utalenga kutazama hali ya ushindani wa kisiasa na kuimarisha mshikamano miongoni mwa wanasiasa na Vyama vya Siasa. Mkutano huo ufanyike katika Siku ya Demokrasia nchini;

b) mahakama iwe na mamlaka ya mwisho ya kuamua pale maridhiano yatakapokuwa yamekwama kwa pande husika; na

c) kwa kuwa nchi yetu ina amini katika Utawala wa Sheria na utoaji wa haki, hivyo, vyombo vinavyosimamia utatuzi wa migogoro kama Mahakama, Tume ya Haki za Binadamu,

Tume ya Maadili na Kamati ya Amani ya Kitaifa ya Viongozi wa Dini na viongozi wa dini mbalimbali, ni lazima vifanye kazi kwa uadilifu na uaminifu wakati wote na hasa wakati wa migogoro inapotokea kupitia utaratibu huu wananchi watajenga imani kwa vyombo hivyo kama watoaji wa haki katika migogoro.

# SURA YA KUMI

# MAWASILIANO KWA UMMA, VYOMBO VYA HABARI NA SIASA

## 10.1 Utangulizi

Mawasiliano kwa Umma ni namna ya kufikisha ujumbe kwa umma kwa kutumia njia mbalimbali. Dhana hii imedumu kwa miaka zaidi ya 2,300 duniani tangu ilipoasisiwa na Mwanafalsafa Mgiriki, Aristotle.

Kukua kwa teknolojia ikiwemo ugunduzi wa mashine ya uchapaji, redio, televisheni na mtandao umerahisisha njia za mawasiliano kwa umma. Njia hizi zilianza kutumika kupashana habari badala ya njia za asili kama ngoma, baragumu, kuwasha moto usiku, kupiga ukunga, mikutano ya wazee au kutembea nyumba kwa nyumba kupashana habari.

Kwa muda mrefu, vyombo vya habari vimethibitika kuwa nyenzo muhimu inayotumika duniani kurahisisha watu kupata haki ya kupata taarifa. Vyombo vya habari vinatoa taarifa, vinaelimisha jamii, vinatengeneza ajenda, vinaunganisha watu, vinaburudisha watu na vinawezesha haki za kisiasa, kiuchumi na kijamii zilizo hatarini kupotea, kupatikana. Kutokana na nguvu viliyonayo ya kufikisha ujumbe kwa watu wengi kwa wakati mmoja, wanasiasa duniani waliamini na wanaendelea kuamini kuwa mtu yeyote mwenye uwezo wa kutumia vyema vyombo vya habari, anaweza kukubalika kwa wananchi na hivyo kushinda uchaguzi.

Wanasiasa wa Tanzania, sawa na wanasiasa wa nchi nyingine duniani, wanaamini kuwa mtu au chama cha siasa kinachopewa

nafasi kubwa katika vyombo vya habari, mwisho wake kinakuwa karibu na wananchi na hivyo kuwa na nafasi kubwa ya kushinda uchaguzi. Mtazamo huu umekuwa chimbuko la mgogoro miongoni mwa wanasiasa na vyombo vya habari, ambapo baadhi ya wanasiasa wanatuhumu vyombo vya habari kuwa vinatangaza habari kwa upendeleo na zinazokuza baadhi ya wanasiasa na vyama vyao mbele ya jamii.

Aidha, vyombo vya habari na waandishi wa habari nchini, wanatuhumiwa kutofanya kazi kwa weledi, kuendekeza rushwa, upendeleo, kujipendekeza na kuishi kwa matumaini ya kuteuliwa katika nyadhifa za kisiasa hali inayowafanya kuweka taaluma kando katika utendaji wao.

Kwa upande mwingine, waandishi wa habari wanadai kuwa wanasiasa hawafahamu matumizi sahihi ya vyombo vya habari, kwani huvitumia wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi huvikimbia.

### 10.2 Hali Ilivyo Sasa

Mfumo wa mawasiliano kwa umma duniani unatumia njia kuu nne zinazofahamika kama vyombo vya habari ambazo ni magazeti, redio, televisheni na mtandao (internet). Vyombo hivi husimamiwa na sheria mbalimbali katika kutimiza majukumu yake ya msingi ambayo ni pamoja na kutoa habari, kuelimisha na kuburudisha. Aidha, nchini Tanzania vyombo vya habari vinasimamiwa na Sheria mbalimbali ikiwemo, Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229 inayosimamia magazeti na Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki

na Posta, Sura ya 306 ambayo inasimamia redio, televisheni na mitandao. Vilevile, vyombo vya habari vinaongozwa na Kanuni za Maadili kwa Wanataaluma wa Habari.

Katika nyanja ya siasa inapofika wakati wa uchaguzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushauriana na vyombo vya habari vya umma, wagombea na Vyama vya Siasa huandaa Mwongozo kwa Vyombo vya Habari vya Umma kwa mujibu wa kifungu cha 53 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343. Mwongozo huo, hulenga kutoa fursa sawa kwa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais wa vyama vyote vya siasa kueleza ilani, sera za vyama vyao na kutangaza habari za mikutano ya kampeni kwa kutumia vyombo vya habari vya umma.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Kamati ya Uangalizi wa Uchaguzi Tanzania (TEMCO) ya Mwaka 2015, masuala ya habari yanasimamiwa na sheria mbalimbali nchini, lakini hakuna chombo kimoja kinachosimamia vyombo vya habari kwa ujumla wake na vyombo vya habari binafsi haviwajibiki kisheria kufuata Mwongozo huo.

Kutokana na hali hiyo, kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa wanasiasa, vyama vya siasa (hasa vya upinzani), watazamaji na waangalizi wa uchaguzi, kuwa baadhi ya nyakati vyombo vya habari vinakuwa na upendeleo wa wazi kwa kuchapisha au kufifisha habari za baadhi ya wagombea na vyama. Hali hii inahusishwa na ukiukwaji wa maadili unaotokana na mapenzi binafsi ya waandishi, rushwa au vitisho na maelekezo kutoka kwa baadhi ya wanasiasa. Kwa muktadha huo, uhusiano kati ya vyombo vya habari na baadhi ya wanasiasa nchini kwa muda mrefu umekuwa wa mashaka.

Kukua kwa teknolojia ya mawasiliano kumesaidia wanasiasa kuanzisha akaunti za mawasiliano ya kijamii kama vile facebook, twitter, Instagram, telegram na mingine ambayo wanaitumia kuwafikia wafuasi wao moja kwa moja na kwa urahisi bila kupitia kwa waandishi wa habari waliokuwa wanawalalamikia.

Hata hivyo, ukuaji huo wa teknolojia umekuja na changamoto zake mathalani baadhi ya wanasiasa na wadau mbalimbali wamekuwa wakiitumia mitandao kwa kusambaza habari za kughushi, kutoa lugha za kuudhi, kejeli, matusi na upotoshaji kwa baadhi ya wagombea na Vyama vya Siasa kupitia kwenye mitandao. Matukio haya, yamesababisha kutungwa kwa Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015 na Kanuni za Maudhui ya Mtandao za mwaka 2018.

### 10.3 Mafanikio

Katika eneo hili jamii imeshuhudia mafanikio yafuatayo:

a) uwepo kwa utashi wa kisiasa, mfano, tamko la Mheshimiwa Rais kwamba Sheria za Habari ziboreshwe kwa majadiliano;

b) kuundwa kwa Wizara inayoshughulikia masuala ya habari na masuala yanayohusiana na habari pekee;

c) kuongezeka kwa idadi ya vyombo vya Habari

   i) idadi ya Magazeti na Majarida = 257 ii) idadi ya Vituo vya Redio = 210

   iii) idadi ya Vituo vya Televisheni = 56

   iv) Simulcasting Radio = 26 v) Online

Radio = 24 vi) Simulcasting Television =
6 vii) Online Television = 663 viii)
Online Blogs = 63 ix) Web Blogs =
144
x) Online Forum = 10

(Chanzo, *tuvuti ya Idara ya Habari Maelezo, imepakuliwa tarehe 15 Septemba 2022 saa 10:50*)

d) kukua kwa uhuru wa vyombo vya habari;
e) uwepo wa Vitengo vya Habari na Mawasiliano kwa Umma na kuendelea kuviimarisha kwa kuongeza bajeti, mafunzo, kuimarisha muundo wake, kuwa na vikao vya kitaaluma kila mwaka;
f) Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa (Access to information Act, 2016) ambayo madhumuni yake ni wananchi kupata haki ya habari kwa mujibu wa Katiba; na
g) kukua kwa teknolojia ya habari, blogu na majukwaa ya mtandaoni (online fora).

**10.4 Maoni ya Wadau**

Wadau wengi waliofika mbele ya Kikosi Kazi katika hoja ya Mawasiliano kwa Umma, Vyombo vya Habari na Siasa walikuwa na hoja zifuatazo:

a) wanasiasa hawafanyi mawasiliano kwa umma kupitia vyombo vya habari kueleza mafanikio na changamoto za utendaji wao kama inavyotakiwa, badala yake wanatumia vyombo vya habari nyakati za uchaguzi pekee;

b) Vyama vya Siasa vinavyopata ruzuku havitumii sehemu ya fedha hizo kufanya siasa kupitia vyombo vya habari kama inavyotakiwa kuwa njia kuu ya kuwasiliana na umma baada ya uchaguzi kukamilika kama inavyofanyika kwa nchi nyingine duniani;

c) Vyama vya Siasa vya upinzani vinakandamizwa na kunyimwa uhuru wa kutumia vyombo vya habari vya umma na binafsi kutokana na vitisho kutoka serikalini;

d) wanasiasa wengi hawazingatii maadili ya upashaji habari wanapopata fursa ya kuwasiliana na umma kupitia vyombo vya habari kwani mara nyingi badala ya kujadili hoja hutumia vyombo vya habari kutoa matusi na kejeli kwa wanasiasa wenzao;

e) vyombo vya habari haviko huru kwani vinakuwa na upendeleo wa wazi kwa chama tawala wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi;

f) Tanzania haina Mwongozo au Kanuni za Maadili ya kisheria kwa vyombo vya habari vya umma na binafsi juu ya upashanaji wa habari kabla, wakati na baada ya uchaguzi;

g) hakuna chombo kilichoanzishwa kisheria kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari kabla, wakati na baada ya uchaguzi;

h) vyombo vya habari vya umma havitoi habari kwa usawa kwa vyama vyote vya siasa nchini;

i) baadhi ya wanasiasa wana tabia ya kuchochea wafuasi wao kuchukia au kushambulia waandishi wa habari na

vyombo vyao vya habari wakati wa kampeni pale wanapoona wanaelekea kushindwa;

j) waandishi wa habari wanatuhumiwa kula rushwa au kujipendekeza wakitarajia kuteuliwa wanapoandika au kutangaza habari katika kipindi cha uchaguzi;

k) vyombo vya habari vimesahau wajibu wake wa kutumikia jamii kwa njia ya kuibua na kuandika uovu unaotendeka serikalini na vyama vya siasa;

l) uhuru wa Vyama vya Siasa kutumia vyombo vya habari unapaswa kuongezeka kwa uwepo wa mijadala na makongamano kupitia vyombo vya habari hali itakayopunguza uhitaji wa mikutano mingi ya hadhara;

m) Mitandao ya Kijamii inapaswa iwekewe Kanuni za Maadili zitakazotumika kuratibu ubora na kudhibiti habari za kughushi bila kuathiri uhuru wa wananchi kupashana habari kupitia mitandao hiyo;

n) Vyama vya Siasa na Vyombo vya Habari vinapaswa kuwa na Kanuni za Maadili zitakazosaidia kuimarisha uhusiano na kuongeza ubora na kiwango cha mawasiliano kati ya pande hizi mbili;

o) uwekwe mfumo wa kuratibu uchapishaji wa taarifa za maendeleo kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Vyama vya Siasa upande wa Zanzibar kwani vyombo vya habari havitoi uzito unaostahili kwa taarifa za upande wa pili wa Muungano;

p) Sheria iainishe lugha inayopaswa kutumiwa na wanasiasa kupitia vyombo vya habari kama zilivyoainishwa Sheria 17 za FIFA katika mchezo wa mpira wa miguu kwa nia ya kuweka uelewa sawa kwa wananchi wanaowasikiliza

viongozi wa kisiasa ili nao washiriki kubaini iwapo mzungumzaji anatoa lugha iliyo kinyume cha sheria atachukuliwa hatua ipi;

q) Kanuni za Mawasiliano ya Umma ziweke mazingira yatakayowezesha watu wenye mahitaji maalum kama kutoona na kutosikia nao waendelee kupata haki ya kupata habari bila kubaguliwa au kuachwa nyuma;

r) kutoaminiana kwa baadhi ya wanasiasa, Vyama vya Siasa na vyombo vya habari;

s) baadhi ya vyombo vya habari kutotangaza kampeni za wagombea wote kwa usawa;

t) uhusiano kati ya vyombo vya habari, Vyama vya Siasa na wanasiasa kuimarika wakati wa uchaguzi na kufifia baada ya uchaguzi;

u) utoaji wa taarifa kufanywa na watu wasiokuwa na taaluma ya uandishi wa habari kupitia mitandao ya kijamii kunasababisha upotoshaji wa habari na ukiukaji wa maadili ya taaluma ya habari;

v) kuna madai kuwa baadhi ya viongozi wa Vyama vya Siasa huwaelekeza wafuasi wao kushambulia waandishi wa habari au kutotoa ushirikiano kwa baadhi ya vyombo vya habari wakati wa kampeni;

w) baadhi ya waandishi wa habari kujinasibisha na Vyama vya Siasa au kushiriki siasa, huku wakiendelea kufanya kazi ya uandishi wa habari hali inayoondoa imani ya wananchi kwa vyombo vya habari;na

x) kuna madai kwamba baadhi ya waandishi wa habari hujihusisha na vitendo vya rushwa hali inayosababisha

kuandika habari kwa upendeleo na kukandamiza upande mwengine.

## 10.5 Mapendekezo ya Taasisi Mbalimbali

Kamati ya Uangalizi wa Uchaguzi Tanzania (TEMCO) imependekeza kuundwa kwa chombo cha kitaifa kitakachosimamia maadili ya vyombo vya habari na utangazaji wakati wa uchaguzi. Aidha, Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229 inaanzisha Baraza Huru la Vyombo vya Habari. Hata hivyo, Baraza hilo halijaundwa hadi sasa, hivyo baadhi ya wadau wanapendekeza Sheria hiyo ifanyiwe marekebisho ili kuongeza jukumu la kuratibu vyombo vya habari wakati wote.Vilevile, Baraza Huru la Habari Tanzania, lisimamie  maadili ya wanahabari wakati wa uchaguzi.

Kwa upande mwingine, Asasi za Kiraia (AZAKI) zinapendekeza kuwa vyombo vya habari na waandishi wa habari wafuate na kuzingatia maadili ya taaluma yao kwa kuhakikisha kuwa taarifa wanazozitoa kwa umma hazipendelei chama au mgombea yeyote bali zilenge kuchambua sera za vyama na tija yake kwa wananchi. Aidha, vyombo vya habari vya umma vinavyoendeshwa kwa kodi za wananchi vihakikishe kuwa vinatoa fursa sawa ya kutangaza sera za wagombea na vyama vyote vya siasa.

## 10.6 Uzoefu Kutoka Nchi Nyingine

Kikosi Kazi kimefanya utafiti kwa njia ya nyaraka kuangalia utendaji katika Mawasiliano kwa Umma, Vyombo vya Habari na Siasa katika nchi mbalimbali duniani, ambapo kimebaini kuwa nchi nyingi zilizoendelea zinatumia vyombo vya habari kufanya siasa kwa

muda mwingi zaidi kuliko mikutano ya hadhara. Vyombo vya habari vinaandaa mijadala ya kitaifa kila linapotokea tukio kubwa. Aidha, wakati wa kampeni za uchaguzi wagombea wanashiriki mijadala na wananchi wanafaidika kwa kupata elimu ya uraia kutokana na mijadala hiyo inayorushwa na vyombo vya habari.

Kwa mfano, nchini Marekani, Ibara ya 1 ya Ibara za Nyongeza ya Mabadiliko ya Kwanza ya Katiba ya Marekani ya Mwaka 1776 inazuia Bunge la nchi hiyo kutunga Sheria itakayofifisha uhuru wa kutoa mawazo, uhuru wa habari na uhuru wa watu kukusanyika.

Pamoja na sheria nyingine, Ibara hii ya katiba inawapa wananchi wa Marekani haki ya kupata taarifa bila vikwazo na vyombo vya habari nchini humo vinaitumia haki hiyo kutangaza karibu kila jambo kwa uwazi isipokuwa, mambo yanayogusa ulinzi, usalama wa taifa na afya ya jamii kwa mujibu wa sheria.

Katiba ya Kenya inatoa uhuru kwa vyombo vya habari kutangaza na kushiriki kikamilifu katika mchakato wa siasa kwa kutoa elimu ya uraia na kutangaza matukio yote ya kisiasa ikiwemo, matokeo ya uchaguzi kila yanavyopatikana.

Katiba ya Ghana, imetoa uhuru mkubwa kwa vyombo vya habari katika kutoa elimu ya uraia. Aidha, nchini Ghana mtu yeyote anayetaka kuanzisha gazeti hapaswi kusajili gazeti Serikalini. Vilevile, chombo chochote hakiruhisiwi kuingilia Uhuru wa Vyombo vya Habari. Katika kusimamia na kuendeleza uhuru wa vyombo vya habari, Katiba ya nchi hiyo imeanzisha Tume ya Taifa ya Habari ambayo inashiriki kikamilifu katika kuendeleza uhuru wa vyombo vya habari.

Utafiti uliofanywa katika nchi nyingi duniani umeonesha kuwa nchi zilizoruhusu uhuru wa vyombo vya habari kwa kiasi kikubwa zimepata maendeleo haraka kutokana na ukweli kwamba vyombo vya habari vinafanya kazi ya kuhakikisha kila mtumishi wa umma anafanya kazi kwa mujibu wa sheria hali inayoimarisha utawala wa sheria, uongozi bora, matumizi sahihi ya rasilimali na kuzuia vitendo vya rushwa.

Vilevile utafiti umebaini kwamba katika nchi za Ghana na Kenya serikali za nchi hizo zimekuwa zikitoa ruzuku kwa vyombo vya habari kuviwezesha kutekeleza majukumu yao ya kila siku. Pamoja na juhudi hizo, upo mkakati maalum wa kutoa elimu na mafunzo kwa wanahabari.

### 10.7 Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Baada ya kupitia nyaraka mbalimbali, kuchambua na kufanya tathmini ya maoni ya wadau, Kikosi Kazi kinatoa mapendekezo yafuatayo:

a) wanahabari wenyewe waunde chombo cha kusimamia maadili ya wanahabari na vyombo vya Habari;
b) uwekwe utaratibu wa kusimamia utekelezaji wa Sheria husika, ili vyombo vya habari vya umma vitoe fursa sawa ya kutangaza habari za wagombea na Vyama vya Siasa wakati wa uchaguzi bila upendeleo;
c) ziandaliwe Kanuni zitakazoelekeza vyombo vya habari kuheshimu maadili ya taaluma ya uandishi wa habari, ikiwemo mwanahabari kuhakikisha anahakiki habari

aliyoipata kutoka pande zinazohusika, kabla ya kutangaza au kuchapisha habari husika;

d) wagombea, viongozi na wanachama wa Vyama vya Siasa waepuke kutumia lugha za kuudhi, kejeli, uchochezi na matusi kupitia vyombo vya habari au mikutano ya hadhara;

e) sheria husika irekebishwe, ili kuondoa mamlaka ya Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo kufungia vyombo vya habari bila kuwepo mchakato wa wazi wa kuviwajibisha;

f) ili kuruhusu wananchi kushiriki ipasavyo katika shughuli za maendeleo na kuwafikia wananchi wengi zaidi wakati na baada ya uchaguzi, ni vyema wanasiasa wakafanya siasa kupitia vyombo vya habari kwa kufanya mahojiano, vipindi maalum, kushiriki mijadala na mazungumzo kama ilivyokuwa katika nchi nyingi duniani; na

g) sheria zinazoratibu uhuru wa habari ziboreshwe ili kukuza uhuru wa Habari na demokrasia nchini.

# SURA YA KUMI NA MOJA

# KATIBA MPYA

## 11.1 Utangulizi

Tanzania inaongozwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inayozingatia misingi ya demokrasia, haki za binadamu na utawala wa sheria, ambapo mamlaka yote ya kuendesha nchi hutokana na wananchi kwa njia ya uchaguzi. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, ndizo Sheria Kuu katika nchi yetu ambazo zimeweka muundo wa utawala, kugawa na kudhibiti mamlaka ya utawala na kulinda haki na kubainisha wajibu wa kila mwananchi.

Hata hivyo, kumekuwepo na madai ya Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka kwa baadhi ya wananchi na baadhi ya vyama vya siasa na asasi za kiraia. Sababu kadhaa zimetolewa ikiwemo, kwamba Katiba ya sasa ilitungwa wakati wa mfumo wa chama kimoja cha siasa, hivyo haina misingi thabiti ya kukidhi mfumo wa vyama vingi vya siasa. Aidha, hoja nyingine inadai Katiba iliyopo imekosa uhalali wa kisiasa na kisheria kwa sababu wananchi hawakushirikishwa kikamilifu katika utungwaji wake. Kutokana na madai hayo ulianza mchakato wa kutengeneza Katiba Mpya mwaka 2011. Juhudi hizi zilisimama mwaka 2014 kupisha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2015 baadhi ya wananchi waliendelea kueleza umuhimu wa Tanzania kuwa na Katiba Mpya.

## 11.2 Michakato Mbalimbali ya Mabadiliko ya Katiba Tanzania (1961-2015)

Katika historia ya nchi yetu, juhudi za kupata Katiba Mpya zimekuwa zikifanyika tangu uhuru, kutokana na mabadiliko na changamoto mbalimbali katika jamii. Tangu kupata uhuru, kumekuwepo na katiba tano zifuatazo:

a) Katiba ya Uhuru ya mwaka 1961(Independence Constitution of 1961);
b) Katiba ya Jamhuri ya Tanganyika ya mwaka 1962 (The Republican Constitution of 1962);
c) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya mwaka 1964 (The Interim Constitution of Tanganyika and Zanzibar of 1994);
d) Katiba ya Muda ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1965 (The Interim Constitution of Tanzania of 1965); na
e) Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya Mwaka 1977.

Kwa upande wa Zanzibar, baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964, kumekuwa na katiba mbili zifuatazo:

a) Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Mwaka 1979; na
b) Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 imebadilishwa mara kumi na nne (14), ili kuendana na mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kwa mujibu wa ibara ya 98 ya Katiba

hiyo, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limepewa mamlaka ya kufanya mabadiliko ya Katiba. Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 imefanyiwa mabadiliko mara kumi (10), yakiwemo ya mwaka 2010 ambayo pamoja na mambo mengine, yalianzisha mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar.

Mabadiliko makubwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 yalifanyika mwaka 1992, wakati Tanzania ilipofanya uamuzi wa kutoka katika mfumo wa chama kimoja cha siasa kwenda katika mfumo wa vyama vingi vya siasa. Katika kufanikisha uamuzi huo, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Pili, mwaka 1991 aliunda Tume iliyoongozwa na Jaji Francis Nyalali ambayo ilikusanya maoni kutoka kwa wananchi 36,299 na kutoka kwa Watanzania 341 waliokuwa nje ya nchi. Tume hiyo ilikusanya maoni kutoka katika mikoa yote 25 ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar iliyokuwepo kwa wakati huo na ilipendekeza pamoja na mambo mengine, kuanzishwa kwa Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa, na hivyo kusababisha kufanyika kwa mabadiliko ya Katiba ya nane ya mwaka 1992. Aidha, Tume hiyo ilipendekeza kutungwa kwa Katiba Mpya, hoja ambayo haikutekelezwa.

Pamoja na mabadiliko mbalimbali yaliyofanywa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, madai ya Katiba Mpya yaliendelea kutolewa na makundi mbalimbali. Kutokana na madai hayo, mwaka 1998, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Tatu aliunda Kamati Maalum ya kukusanya maoni ya wananchi kuhusu mabadiliko ya Katiba. Kamati hiyo iliyojulikana kama “Kamati ya Jaji Kisanga”, ambayo ilikusanya maoni kutoka kwa wananchi takribani

600,000 na jumla ya maoni milioni sita yalitolewa, kutoka mikoa yote 25 ya Tanzania Bara na Zanzibar. Hata hivyo, Ripoti hii haikufanikisha kupatikana kwa Katiba Mpya.

Jitihada nyingine za kupata Katiba Mpya zilifanyika mwaka 2011, ambapo Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Nne, aliunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliyoongozwa na Jaji Joseph Sinde Warioba. Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Sura ya 83, ilielekeza Tume ya Mabadiliko ya Katiba ya kuratibu, kukusanya maoni ya wananchi nchi nzima na kuandaa rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tume hiyo iliandaa mikutano 1,763 iliyohudhuriwa na jumla ya wananchi 1,365,337 (wanawake 531,480 na wanaume 833,857) ambao walitoa maoni yao. Aidha, maoni mengine yalikusanywa kutoka kwa viongozi wa kitaifa waliokuwa madarakani na wastaafu na makundi mbalimbali ya kijamii. Katika kutimiza matakwa ya Sheria, Tume iliwasilisha Rasimu ya Kwanza ya Katiba kwa Mabaraza ya Katiba yaliyoundwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 177 za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wadau wengine kwa ajili ya kupata maoni. Mchakato huo ulisaidia kupatikana kwa Rasimu ya Pili ya Katiba.

Katika ukusanyaji wa maoni, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ilielekeza Tume ya Mabadiliko ya Katiba kuzingatia uhifadhi wa maadili ya jamii na mambo ya msingi ya kitaifa yafuatayo:

a) kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano;
b) kuwepo kwa Serikali, Bunge na Mahakama; mfumo wa kiutawala wa kijamhuri;

c) kuwepo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; umoja wa kitaifa, amani na utulivu;

d) uchaguzi wa kidemokrasia wa mara kwa mara katika vipindi maalum kwa kuzingatia haki ya watu wote wenye sifa ya kupiga kura; ukuzaji na uhifadhi wa haki za binadamu; utu, usawa mbele ya sheria na mwenendo wa sheria; na

e) kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano isiyofungamana na dini yoyote.

Mwaka 2013, Sheria ya Kura ya Maoni, Sura 440. ilitungwa ili kuwezesha Rasimu ya Pili ya Katiba Inayopendekezwa kupigiwa kura ya maoni na wananchi. Hivyo, Rasimu ya Pili ya Katiba iliwasilishwa na kujadiliwa na Bunge Maalum la Katiba, ambalo liliandaa Katiba Pendekezwa ambayo tarehe 4 Oktoba 2014 iliidhinishwa kwa kupigiwa kura. Hata hivyo, mchakato huo haukukamilika na Katiba Mpya haikupatikana.

### 11.3 Changamoto Zilizojitokeza katika Juhudi za Kupata Katiba Mpya

Pamoja na juhudi kubwa zilizofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupata Katiba Mpya, lakini kumekuwa na changamoto zifuatazo:

a) baadhi ya wabunge wa Bunge Maalum la Katiba kujitoa katika mchakato rasmi wa kupata Katiba Mpya. Wabunge hao ni wale waliokuwa katika kundi la umoja wa vyama vya siasa, lililojulikana kama “Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA). Kitendo hicho kilisababisha baadhi

ya wananchi kuhoji uhalali wa Katiba Inayopendekezwa, ambayo iliridhiwa na wabunge wa Bunge Maalum la Katiba waliobakia bungeni;

b) kumekuwa na tafsiri mbalimbali kuhusu sababu za kutokamilika kwa mchakato wa kupata Katiba Mpya, kwa kumalizia hatua ya wananchi kupiga kura ya maoni. Kwa upande mmoja imeelezwa kuwa, muingiliano wa ratiba ya kupata Katiba Mpya na uchaguzi mkuu, ulisababisha mchakato wa kupata Katiba Mpya ulioanza mwaka 2011 kutokamilika. Kutokana na Katiba Inayopendekezwa kupatikana karibu na Uchaguzi Mkuu wa 2015, kulikuwa na muda mfupi kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kufanya zoezi la kura ya maoni na kuandaa Uchaguzi Mkuu, hivyo kusababisha kuahirishwa kwa zoezi hilo; na

c) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Awamu ya Tano kutoendeleza mchakato wa kupata Katiba Mpya;

Changamoto hizo zilisababisha baadhi ya watu kudhani kwamba kuna mkwamo wa kisiasa kuhusu suala zima la kupatikana kwa Katiba Mpya ya Tanzania, kwani miaka nane (8) imepita tangu Katiba Inayopendekezwa ipitishwe na Bunge Maalum la Katiba. Ni katika muktadha huo, madai ya Katiba Mpya bado yanaendelea kutoka kwa baadhi ya wadau, hasa wanasiasa na asasi za kiraia. Hata hivyo, kuna mitazamo tofauti ya namna ya kurejea katika mchakato wa kupata Katiba Mpya.

### 11.4 Maoni ya Wadau kuhusu Katiba

Kwa ujumla, Watanzania wanaonekana kugawanyika katika makundi makuu mawili (2), kuhusu masuala ya katiba.

### 11.4.1. Hakuna Haja ya Katiba Mpya, Katiba ya Sasa Ifanyiwe Marekebisho

Baadhi ya wadau wana maoni kwamba, suala sio Tanzania kuwa na Katiba Mpya, bali kuwa na Katiba bora na inayokidhi matakwa ya wananchi. Hivyo basi, Katiba iliyopo inaweza kufanyiwa mabadiliko ili kuingiza matakwa ya wakati uliopo.

### 11.4.2. Kuna Haja ya Kuwa na Katiba Mpya

Wapo wananchi wanaoamini kuwa kuna haja ya kuwa na Katiba Mpya. Kwa ujumla, Watanzania wanaonekana kugawanyika katika makundi makuu tano (5), kuhusu njia muafaka ya kupata Katiba Mpya. Makundi hayo ni  yafuatayo.

#### 11.4.2.1. Kuanza Mchakato Upya

Baadhi ya Watanzania wana maoni kwamba mchakato wa kupata Katiba Mpya ulitekwa na wanasiasa, na hivyo kugubikwa na mivutano na malumbano miongoni mwa Vyama vya Siasa. Kwa sababu hii, ipo haja ya kuanza mchakato upya kwa kupanua wigo wa ushiriki wa wananchi walio wengi.

#### 11.4.2.2. Kupigia Kura ya Maoni Katiba Inayopendekezwa

Baadhi ya wadau wanadai kwamba mchakato wa Katiba Mpya ulifanyika na ulikuwa shirikishi na ulifuata sheria. Hivyo, zoezi hilo likamilishwe kwa kupigiwa kura ya maoni Katiba Inayopendekezwa.

#### 11.4.2.3. Kupigia Kura ya Maoni Rasimu ya Pili ya Katiba (Rasimu ya Jaji Warioba)

Baadhi ya wananchi wana maoni kuwa, mchakato wa kutengeneza Rasimu ya Pili ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba ulishirikisha wananchi, hivyo rasimu hiyo inabeba muafaka wa kitaifa na ndiyo ipigiwe kura ya maoni ili kupata Katiba Mpya.

#### 11.4.2.4. Kuunda Jopo la Wataalam Kuoanisha Katiba Inayopendekezwa na Rasimu ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba

Baadhi ya wadau wametoa maoni kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aunde Jopo la Wataalam waliobobea (team of experts), ili waweze kuchambua na kuoanisha rasimu hizi mbili za Katiba na kutengeneza rasimu moja. Zoezi hili lifuatiwe na utoaji wa elimu kuhusu rasimu hiyo, ili kuwaelimisha wananchi kabla ya kupiga kura ya maoni.

#### 11.4.2.5. Ipo Haja ya Kujadili na Kukubaliana Misingi Mikuu kabla ya Kuanza Mchakato wa Katiba Mpya

Baadhi ya wananchi wana maoni kwamba, ipo haja ya kuwepo kwa mjadala wa kitaifa, ili kupata muafaka katika masuala ya msingi, kabla ya kumalizia mchakato wa kuandika Katiba mpya. Katika hili, wengine wanashauri kwamba, ni muhimu viongozi wa Kitaifa wa pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakutane na kujadili mustakabali wa masuala muhimu ya kitaifa ikiwemo Muundo wa Muungano.

Hoja nyingine inayoshabihiana na hii inashauri kwamba, ili kufanikisha kupatikana kwa Katiba Mpya, ni muhimu kujifunza

kutoka katika mchakato wa kuandaa Katiba Mpya wa mwaka 2011 hadi 2014. Hivyo, iko haja ya kutafuta ufumbuzi wa masuala muhimu ya kitaifa, yaliyopo kwenye Katiba ya sasa, kabla ya kuanza mchakato wa kupata Katiba Mpya. Baadhi ya mambo hayo ni yafuatayo:

a) uteuzi wa Tume ya Pamoja ya Fedha na Akaunti ya Pamoja ya Fedha kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
b) suala la Benki Kuu na mgawanyo wa hisa kati ya Serikali mbili katika Muungano;
c) suala la Mipaka ya Baharini kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar;
d) utata wa kisheria kuhusu suala la mafuta na gesi;
e) madaraka ya Rais;
f) muundo wa Muungano; na
g) nafasi ya Rais wa Zanzibar katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

## 11.5 Uzoefu wa Nchi Nyingine

### 11.5.1 Kenya

Kenya imekuwa na Katiba tatu (3) tangu uhuru, ambazo ni katiba ya uhuru ya mwaka 1963), katiba ya Kenya ya mwaka 1964 na katiba ya Kenya ya mwaka 2010. Kazi ya mchakato wa kudai Katiba mpya iliongezeka wakati wa vuguvugu la kubadilisha mfumo kutoka chama kimoja cha siasa, kuelekea mfumo wa vyama vingi vya siasa, mwanzoni mwa miaka 1990. Kufuatia madai hayo, kumekuwa na sheria kadhaa za mabadiliko ya katiba katika nyakati

tofauti. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 1997; Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 1998, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2002, na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2009. Upatikanaji wa sheria hizi uligubikwa na malumbano na mivutano ya hoja kutoka kwa makundi mbalimbali, ikiwemo Vyama vya Siasa, viongozi wa dini na asasi za kiraia.

Wakati mwingine Serikali ya Kenya ilijikuta ikitofautiana na wananchi kuhusu mchakato na maudhui ya rasimu ya katiba mpya. Kwa mfano, baada ya kazi kubwa iliyofanywa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliyoongozwa na Profesa Yash Ghai na kuridhiwa na Mkutano Mkuu wa Kitaifa (Bomas), Serikali ilifanya marekebisho makubwa na kuja na rasimu ya Katiba nyingine iliyojulikana kama "Rasimu ya Wako" (jina la Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliyeongoza mchakato huo). Hali hii ilichangia wananchi kuipigia kura ya 'Hapana' Katiba Pendekezwa mwaka 2005 na kufanya Wakenya kuingia katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2007 bila katiba mpya. Uchaguzi huo ulitawaliwa na vurugu na kusababisha mauaji ya wananchi.

Mchakato wa kupata Katiba mpya ulianza tena kwa kupitisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2008, ambayo pamoja na mambo mengine, ilielekeza kuundwa kwa Jopo la Wataalam ili kuoanisha rasimu za awali za katiba na kuandika rasimu mpya. Aidha, Sheria hii iliunda Kamati ya Bunge yenye wabunge 27 kutoka vyama mbalimbali waliokuwa na jukumu la kutafuta ufumbuzi wa masuala yenye utata na kulishauri Jopo la Wataalam. Sheria hii iliipatia Bunge la Kenya jukumu la kupitia na kuridhia

Rasimu ya Katiba kabla ya kupelekwa kwa Wananchi kwa ajili ya Kura ya Maoni.

Hadidu rejea za Jopo la Wataalam zilikuwa zifuatazo;

a) kuainisha masuala ambayo wakenya wanakubaliana katika rasimu za nyuma za katiba;
b) kuainisha masuala yenye utata na ambayo Wakenya hawajakubaliana katika rasimu za katiba;
c) kukusanya maoni ya kimaandishi na mawasilisho kuhusu masuala yenye utata;
d) kukusanya maoni kutoka makundi na wataalam mbalimbali;
e) kufanya utafiti na tathmini kuhusu katiba na mifumo mbalimbali ya katiba;
f) kuchambua faida na hasara za mbinu pendekezwa za ufumbuzi wa masuala yenye utata;
g) kuwasilisha mapendekezo kwa Kamati ya Bunge kuhusu masuala yenye utata kwa mustakabali wa taifa la Kenya;
h) kutayarisha Rasimu ya Katiba itakayowasilishwa kwenye Bunge la Kenya; na
i) kushirikiana na Tume ya Uchaguzi ya Kenya kuandaa Kura ya Maoni ya Katiba Pendekezwa.

Kwa ujumla, iliwachukua Wakenya miongo miwili ya harakati na michakato ya mabadiliko ya katiba mpya, hadi walipofanikiwa kupiga kura ya maoni tarehe 4 Agosti 2010 na kuridhia Katiba Pendekezwa ya Mwaka 2010 kwa asilimia 67. Msingi mkubwa ulioongoza kupatikana kwa Katiba ya Kenya ya Mwaka 2010, ni uelewa wa pamoja miongoni mwa Wakenya kuwa, wanahitaji katiba

mpya ambayo itakuwa ni nyenzo ya kutatua migogoro ya kisiasa nchini mwao na kuleta maridhiano katika masuala muhimu.

### 11.5.2 Afrika ya Kusini

Mchakato wa kutengeneza katiba mpya huko Afrika Kusini, ni mfano unaotumika na baadhi ya watu kuonesha ni kwa jinsi gani nchi ambayo imekuwa katika mgawanyiko mkubwa, uliojikita katika ubaguzi na ukatili uliokithiri dhidi ya waafrika walio wengi, imeweza kufikia muafaka wa kitaifa na kuunda katiba inayokubalika na wananchi wengi. Msingi mkubwa wa mchakato wa mabadiliko ya Katiba nchini Afrika ya Kusini, umekuwa ni majadiliano na maridhiano, kufuatia miongo mingi ya mapigano ya umwagaji wa damu na harakati za kudai uhuru na haki. Majadiliano hayo yalianza miaka ya 80 na yaliendelea hadi miaka ya 90. Hali hii ilisababisha chama tawala cha siasa chenye mrengo wa ubaguzi wa rangi, kuruhusu vyama vingi vya siasa na kuachia wafungwa wa kisiasa kutoka gerezani akiwemo Hayati Nelson Mandela.

Mchakato wa mabadiliko ya katiba ulifanyika katika awamu mbili mwaka 1991 na mwaka 1994. Katika awamu ya kwanza iliyoanza mwaka 1991, Vyama vya Siasa na serikali vilifanya majadiliano kupitia jukwaa la kitaifa la majadiliano lililoitwa, Convention for a Democratic South Africa (CODESA). Majadiliano katika CODESA yalijumuisha uwakilishi wa Serikali, Vyama vya Siasa, viongozi wa dini na taasisi nyingine na yalijikita katika kuondoa mifumo ya kibaguzi, kufanya mabadiliko ya sheria, kujadili serikali ya mpito na maandalizi ya kupata katiba mpya ya Afrika Kusini huru. Kutokana na kuwepo kwa mikwamo kadhaa, vyama vya siasa vikaamua

kutengeneza jukwaa jingine la majadiliano lililoitwa “the Multi-party Negotiating Process- MPNP”, lililojumuisha vyama vya siasa, serikali na wadau wengine. Majadiliano hayo yalifanikisha kutengenezwa kwa Katiba ya Muda ya mwaka 1993, ambayo iliunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa iliyoongoza katika kipindi cha mpito. Aidha, iliainisha misingi 34 ya kuliongoza Bunge la Katiba katika utungaji wa Katiba ya kudumu, ambayo haiwezi kurekebishwa na chombo chochote. Mahakama ya Katiba ilipewa mamlaka ya kuhakikisha kuwa, misingi hiyo inafuatwa na Bunge la Katiba katika kutengeneza katiba ya Kudumu.

Awamu ya Pili ya kutengeneza katiba ya Afrika Kusini ilianza baada ya uchaguzi wa vyama vingi vya siasa wa tarehe 27 Aprili 1994. Baada ya uchaguzi huo, Bunge jipya liligeuka kuwa Bunge la Katiba na kuanza mchakato wa kuandika katiba, kwa kukusanya maoni kutoka asasi za kiraia na wananchi kwa ujumla. Katiba pendekezwa ilipelekwa katika Mahakama ya Katiba, ambayo ilikataa kuidhinisha kwa kukiuka baadhi ya misingi 34 iliyoanishwa katika katiba ya mpito. Hali hii ililazimisha Bunge la Katiba kufanya marekebisho katika rasimu ya katiba na hatimaye Mahakama ya Katiba iliridhia.

### 11.6 Uchambuzi

Kuhusu maoni ya baadhi ya wadau kwamba, Tanzania ianze upya mchakato wa kupata Katiba Mpya, utekelezaji wa mtazamo huu unahitaji gharama kubwa ya kifedha na muda mrefu ili kukamilika. Aidha, haina mantiki kurudia kufanya mchakato wa kukusanya maoni na kuandaa rasimu ya Katiba wakati ni muda mfupi umepita tangu maoni ya wananchi yakusanywe, pia mahitaji ya wananchi ya

sasa na ya wakati mchakato huo unafanyika yanaonekana kutotofautiana.

Kuhusu maoni ya baadhi ya wadau kwamba, mchakato wa kupata Katiba Mpya uendelee pale uliposimama, kwa Katiba Inayopendekezwa kupigiwa kura ya maoni. Mtazamo huu ungeweza kupunguza gharama, lakini una changamoto kwamba, sasa ni takribani miaka nane tangu Katiba Inayopendekezwa ipitishwe na Bunge Maalum la Katiba, hivyo utaratibu wa kupata Katiba Mpya uliowekwa na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba umepitwa na wakati na kuna hoja zimeibuka za kuboresha zaidi Katiba Inayopendekezwa ili iendane na wakati uliopo. Aidha, tangu Katiba Inayopendekezwa ipatikane, kumefanyika Uchaguzi Mkuu mara mbili, mwaka 2015 na 2020, ambazo zimetoa uzoefu wa aina mbalimbali unaoweza kuboresha Katiba Inayopendekezwa.

Vilevile, mabadiliko katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa nchini na duniani kwa ujumla yanahitaji kutazamwa, ili kupata muafaka mpya wa kitaifa.

Kuhusu maoni ya baadhi ya wadau kwamba, Rasimu ya Pili ya Katiba iliyoandaliwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba ndiyo ipigiwe kura ya maoni ili kupata Katiba Mpya. Mtazamo huu hautekelezeki, kwa sababu unakiuka utaratibu ulioainishwa katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, ambayo inaelekeza Rasimu ya Pili ya Katiba iwasilishwe katika Bunge Maalum la Katiba, ambalo ndilo lenye mamlaka ya kutunga Katiba Inayopendekezwa ya kupigiwa kura ya maoni na wananchi.

Kuhusu maoni ya baadhi ya wadau kwamba, liundwe Jopo la Wataalam kuoanisha Katiba Inayopendekezwa, Rasimu ya Pili ya Katiba iliyoandaliwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Mtazamo

huu unaonekana kuwa na tija kwani utapunguza gharama za kupata Katiba Mpya. Vilevile, wataalam wataandaa rasimu mpya ya Katiba inayotokana na masuala muhimu kwa Taifa yaliyopo katika rasimu hizo mbili za Katiba.

Kuhusu maoni ya baadhi ya wadau kwamba, hakuna haja ya Tanzania kuwa na Katiba Mpya, hivyo Katiba ya Sasa ifanyiwe mabadiliko. Maoni haya yanaweza kupelekea kupunguza gharama ya mchakato wa kupata Katiba Mpya, lakini yanaweza yasiwe suluhisho kwani kuna baadhi ya Watanzania wanapendelea kuwa na Katiba Mpya. Aidha, azma ya kuwa na Katiba Mpya imejidhihirisha kwa mchakato wa kupata Katiba Mpya kuanza mwaka 2011. Hata hivyo, suala hili halizuii kufanyika kwa mabadiliko ya Katiba ya sasa, ili kujuimuisha masuala ya msingi yanayohitajika katika wakati uliopo.

### 11.7 Ipo Haja ya Kujadili na Kukubaliana Misingi Mikuu ya Kitaifa Kabla ya Kuanza Mchakato wa Katiba Mpya

Kuhusu maoni ya baadhi ya wadau kwamba, kuna haja ya kujadili na kukubaliana misingi mikuu ya kitaifa kabla ya kuanza kwa mchakato wa kupata Katiba Mpya. Mtazamo huu unaweza kuwa na tija kwani utawezesha kupatikana kwa Katiba Mpya yenye muafaka wa kitaifa. Endapo ufumbuzi utapatikana kuhusu masuala ya msingi ya kitaifa, kuna uwezekano kuwa majadiliano ya kupata Katiba Mpya yakafikia tamati bila ya kuwepo kwa mkwamo . Kwa upande mwingine, mtazamo huu unaweza kuufanya mchakato wa kupata Katiba Mpya kuwa umeshirikisha makundi yote katika jamii.

### 11.8 Mapendekezo ya Kikosi Kazi

Kutokana na uchambuzi wa maoni ya wadau uliofanywa hapo juu, mapitio ya taarifa mbalimbali, uzoefu wa nchi nyingine na kwa kuzingatia hali halisi ya mazingira ya kisiasa, kiuchumi na kijamii nchini, Kikosi Kazi kinapendekeza kukamilishwa kwa mchakato wa kupata Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia hatua sita zifuatazo:

**Hatua ya Kwanza: Mjadala wa Kitaifa ili kupata Muafaka katika Masuala ya Msingi**

Kuanzishwa kwa mjadala wa kitaifa katika masuala ya msingi, ili kupata muafaka wa kitaifa kabla ya kuanza mchakato wa kuandika Katiba mpya. Mjadala huu ufanyike kwa ushiriki mpana wa wananchi. Masuala ya msingi yanajumuisha muundo wa Muungano, madaraka ya Rais, mfumo wa uchaguzi, madaraka ya Serikali za Mitaa, rushwa na maadili na mengineyo yatakayojitokeza.

**Hatua ya Pili: Kuhuisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na Sheria ya Kura ya Maoni**

Kuhuisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na Sheria ya Kura ya Maoni ili kuweka mahitaji ya sasa, yakiwemo kuainisha muda wa mchakato mzima, kutambua kuanzishwa kwa Jopo la Wataalam na kuainisha misingi ya kuzingatiwa katika mchakato wa mabadiliko ya Katiba. Aidha, kuwepo na ushirikishwaji mpana wa wananchi katika mchakato wa kuhuisha Sheria hiyo, kwa kufuata taratibu za utungaji wa sheria nchini.

**Hatua ya Tatu: Kuundwa kwa Jopo la Wataalam**

Baada ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kuhuishwa, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushauriana na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aunde Jopo la Wataalam, litakalopitia na kuoanisha Katiba Inayopendekezwa na Rasimu ya Pili ya Katiba iliyoandaliwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011 na kuandaa Rasimu ya Katiba Mpya itakayowasilishwa Bungeni.

Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa, katika utekelezaji wa majukumu yake, Jopo la Wataalam lizingatie masuala yafuatayo:

a) kufanya mapitio ya Katiba Inayopendekezwa ya Mwaka 2014, kwa kuzingatia hali ya sasa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii;
b) kurejea nyaraka zifuatazo, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984, Rasimu ya Pili ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011 na Ripoti ya Serikali kuhusu masuala muhimu ya kitaifa yaliyojadiliwa katika mjadala wa kitaifa wa Katiba; na
c) masuala muhimu ya kitaifa ambayo ni:
    i) mfumo wa kiutawala wa kijamhuri; ii) uwepo wa Jamhuri ya Muungano; iii) uwepo wa Serikali, Bunge na Mahakama; iv) uwepo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
    v) uwepo wa umoja wa kitaifa, amani na utulivu; vi) uwepo wa uchaguzi wa kidemokrasia katika vipindi maalum na kuzingatiwa kwa haki ya kila mtu mwenye sifa ya kupiga na kupigiwa kura;

vii) uhifadhi wa Haki za Binadamu na utawala wa sheria;na
viii) uwepo wa Serikali isiyofungamana na dini.

**Hatua ya Nne: Rasimu ya Katiba Mpya Kupitishwa na Bunge**

Baada ya Jopo la Wataalam kukamilisha kazi ya kuandaa Rasimu ya Katiba, itawasilishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kujadiliwa na kuipitisha kuwa Katiba Inayopendekezwa. Majukumu ya Bunge yatabainishwa katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba.

**Hatua ya Tano: Elimu ya Uraia kuhusu Katiba Mpya**

Kutoa elimu ya uraia kuhusu Katiba Inayopendekezwa kabla ya kupigiwa kura, ili wananchi waifahamu Katiba husika na kuwaandaa kupiga kura ya maoni kwa amani na utulivu.

**Hatua ya Sita: Kura ya Maoni**

Wananchi kupigia kura ya maoni Katiba Inayopendekezwa.

## SURA YA KUMI NA MBILI

## HITIMISHO

Wajumbe wa Kikosi Kazi tunarejea kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake, maono na juhudi zake kubwa za kuleta maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa nchini. Aidha, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa heshima aliyotupatia ya kuchangia mawazo katika kudumisha na kuboresha mifumo ya demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini.

Tunarudia kumshukuru pia, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa juhudi anazofanya Zanzibar za kuleta maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii, ikiwemo kuboresha mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa kwa kuunda Kamati Maalum, inayofanyia kazi masuala mahsusi ya Zanzibar yanayohusu demokrasia ya vyama vingi vya saisa.

Tunawashukuru viongozi na watumishi wa Serikali waliokuwa wakimsaidia Mheshimiwa Rais kuhakikisha Kikosi Kazi kinatekeleza majukumu yake ipasavyo, hususani Mratibu wa Kikosi Kazi, Mheshimiwa Jaji Francis S.K. Mutungi, Msajili wa Vyama vya Siasa. Vilevile, tunawashukuru wadau wote wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini kwa ushirikiano waliotupatia, hasa wadau walioshiriki mkutano wa wadau wa tarehe 15 hadi 17 Desemba Dodoma, wadau waliowasilisha maoni kwa maandishi na wadau waliokuja kuzungumza na Kikosi Kazi.

Ripoti hii imechambua maoni ya wadau na kutoa mapendekezo kwenye maeneo makuu tisa ambayo yamebeba jina la sura ya nne

hadi ya kumi na moja. Ni matumaini yetu kuwa mapendekezo haya yatayafanyiwa kazi ipasavyo, ili kudumisha na kuboresha mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini.

Aidha, masuala mahsusi yanayohusu Zanzibar, yanafanyiwa kazi na Kamati Maalum ya Zanzibar yenye jukumu kama la Kikosi Kazi hiki. Ripoti ya Kamati hiyo itakuwa ni sehemu ya Ripoti hii.

## Orodha ya Viambatisho

1. Mapendekezo ya Kikosi Kazi;
2. Hotuba ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati akifungua Mkutano wa Wadau wa Kujadili Hali ya Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa Nchini tarehe 15 Disemba 2021;
3. Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wakati wa kufunga Mkutano wa Wadau wa Kujadili Hali ya Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa Nchini tarehe 17 Desemba 2021;
4. Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wakati akizindua Kikosi Kazi tarehe 10 Januari 2022;
5. Mada zilizowasilishwa katika Mkutano wa Wadau wa wa Kujadili Hali ya Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa Nchini, uliofanyika tarehe 15 hadi17 Desemba 2021 Dodoma;
6. Maoni na Mapendekezo ya wadau yaliyotolewa katika Mkutano wa Wadau wa Kujadili Hali ya Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa Nchini, uliofanyika tarehe 15 hadi17 Desemba 2021 Dodoma;
7. Orodha ya Vyama vya Siasa vyenye Usajili Kamili;
8. Vyama vya Siasa vinavyopata ruzuku kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

9. Orodha ya wadau waliowasilisha maoni kwenye Kikosi Kazi; na
10. Maoni ya wadau yaliyowasilishwa katika Kikosi Kazi.

**Kiambatisho cha 1**

## MAPENDEKEZO YA KIKOSI KAZI

### 1. Kuhusu Mikutano ya Hadhara na Mikutano ya Ndani ya Vyama Vya Siasa,

Kikosi Kazi kinapendekeza Sheria ya Vyama vya Siasa ifanyiwe marekebisho ili**:**

a) kulipatia Baraza la Vyama vya Siasa mamlaka ya kushughulikia suala la uvunjifu wa maadili ya Vyama vya Siasa kupitia Kamati yake ya Maadili;

b) Msajili wa Vyama vya Siasa awe na mamlaka ya kuandaa mwongozo wa uchaguzi wa ndani ya Vyama vya Siasa;

c) kuweka masharti kwamba idadi ya jinsi moja katika vyombo vya maamuzi vya chama cha siasa isipungue asilimia 40; na

d) kukitaka kila chama cha siasa kuwa na sera ya ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu katika shughuli za chama husika.

**2. Kuhusu Ruzuku Kwa Vyama Vya Siasa** Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa:

a) mfumo wa sasa wa kugawa ruzuku ya Serikali kwa Vyama vya Siasa uendelee, isipokuwa asilimia 10 ya fedha za ruzuku kwa Vyama vya Siasa zilizotengwa katika bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha husika, igawiwe sawa kwa vyama vyote vya siasa vyenye usajili kamili kwa mujibu wa vigezo na masharti yafuatayo:

(i) chama kiwe na usajili kamili;

(ii) chama kiwe kimefanyiwa uhakiki na Msajili wa Vyama vya Siasa na kuthibitishwa kwamba, kinakidhi vigezo vya usajili kamili;

(iii) chama kiwe kimeshiriki Uchaguzi Mkuu angalau mara mbili tangu kupata usajili kamili;

(iv) katika mwaka wa fedha uliopita, chama husika kisiwe kimepata Hati Chafu ya Mahesabu kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na

(v) ruzuku itumike kwa shughuli za kuendesha Ofisi ya Makao Makuu, Ofisi Ndogo au Ofisi Kuu ya Makao Makuu ya chama cha siasa husika.

b) Sheria ya Vyama vya Siasa itamke kuwa, asilimia ishirini (20%) ya fedha za ruzuku kwa Vyama vya Siasa inayotolewa na Serikali katika mwaka wa fedha, igawiwe kwa Vyama vya Siasa vyenye Madiwani wa kuchaguliwa katika kata, kwa mujibu wa uwiano wa idadi ya Madiwani hao ambao kila chama kinao, kwani kwa sasa sheria haijatamka kiwango chochote bali imempa mamlaka Waziri Mwenye dhamana kuamua;

c) fedha za ruzuku zigawiwe kwa Vyama vya Siasa kwa mujibu wa idadi ya kura za ubunge na idadi ya wabunge ambao chama cha siasa kinao kwa wakati husika; na

d) Serikali iongeze fedha za bajeti ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Baraza la Vyama vya Siasa, ili liweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, ikiwemo jukumu linalopendekezwa la kusimamia Maadili ya Vyama vya Siasa.

**3. Kuhusu Mfumo wa Uchaguzi**

Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa:

a) Mfumo Mseto wa Uchaguzi (Mixed Electoral System) uendelee kutumika kwa uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Aidha, katika uchaguzi wa Rais ili mgombea ashinde uchaguzi iwe ni lazima apate zaidi ya asilimia hamsini ya kura zote halali zilizopigwa;

b) uchaguzi wa wabunge, madiwani na uchaguzi wa Serikali za Mitaa uendelee kutumia Mfumo wa Mshindi kwa Kura Nyingi; na

c) Mfumo wa Uwiano wa kura uendelee kutumika kupata wabunge na madiwani wa viti maalum vya wanawake.

**4. Kuhusu Uhuru wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

Kikosi Kazi kinapendekeza yafuatayo:

a) Tume ya Taifa ya Uchaguzi isilazimike kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote, idara yoyote ya Serikali, maoni ya chama chochote cha siasa, taasisi au asasi yoyote; na

b) utendaji wa Tume ya Uchaguzi uruhusiwe kuhojiwa kwenye Mahakama ya Juu pale itakapoanzishwa ili kuongeza uwajibikaji wa Tume.

**5. Kuhusu Uteuzi wa Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi**

Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa, utaratibu wa kumpata Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi uboreshwe, ili kuongeza uwazi katika upatikanaji wao, Utaratibu huo uwe ifuatavyo:

a) kuwe na Kamati ya Uteuzi ya Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi itakayokuwa na wajumbe wafuatao:

i) Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye atakuwa ni Mwenyekiti;

ii) Jaji Mkuu wa Zanzibar ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti; iii) Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Tanzania Bara;

iv)Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Zanzibar;

v) Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu; na vi) wajumbe wengine wawili watakaoteuliwa na Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya kupendekezwa na Chama cha Wanasheria Tanganyika na Chama cha Wanasheria Zanzibar.

b) angalau wajumbe wawili wa Kamati ya Uteuzi wawe wanawake;

c) sifa za mtu kuwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ziainishwe;

d) nafasi ya mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi itangazwe na Mtanzania yeyote mwenye sifa aruhusiwe kuwasilisha maombi kwa Kamati ya Uteuzi ya kuwa mjumbe wa Tume;

e) Kamati ya Uteuzi ifanye usaili wa watu waliowasilisha maombi ya kuwa wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na kupendekeza kwa Rais majina ya watu wanaostahili kuteuliwa kuwa wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi;

f) Kamati ya Uteuzi itawasilisha kwa Rais majina manne (4) zaidi ya idadi ya nafasi zinazohitajika kujazwa;

g) Rais ateue wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi miongoni mwa majina yaliyowasilishwa kwake na Kamati ya Uteuzi; na

h) Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambaye anapaswa kuwa ni Jaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani aliye madarakani au mstaafu na Makamu Mwenyekiti ambaye anapaswa kuwa na sifa ya kuwa Jaji wa Mahakama Kuu au mstaafu, wateuliwe na Mheshimiwa Rais bila kufuata utaratibu wa kuomba na kusailiwa na Kamati ya Uteuzi.

## 6. Kuhusu Matokeo ya Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kutohojiwa Mahakamani

Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa, matokeo ya uchaguzi wa Rais yahojiwe kwenye Mahakama ya Juu mara itakapoanzishwa.

## 7. Kuhusu Watendaji wa Tume ya Uchaguzi

Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa:

a) Tume iendelee kutumia watumishi wa umma kusimamia uchaguzi;

b) watumishi wa umma wawajibike moja kwa moja kwa Tume ya Uchaguzi kwa masuala yanayohusu shughuli za uchaguzi kwa mujibu wa sheria;

c) wasimamizi wa uchaguzi wazingatie sheria, weledi, maadili, uwazi na ushirikishwaji wa wadau wakati wa kufanya kazi zao; na

d) wasimamizi wa uchaguzi watakaokiuka sheria na utaratibu wawajibishwe kwa mujibu wa Sheria.

## 8. Kuhusu Bajeti ya Tume ya Uchaguzi

Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ipewe fedha zilizotengwa katika bajeti kwa wakati, hata baada ya uchaguzi, ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote.

## 9. Kuhusu Usimamizi wa Uchaguzi

Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa:

a) kasoro zilizojitokeza katika uchaguzi uliopita zifanyiwe kazi; na

b) Serikali ifanye utafiti wa kina kuhusu namna bora ya kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili kuufanya uwe wa kidemokrasia zaidi.

## 10. Kuhusu Sheria Zinazosimamia Masuala ya Uchaguzi

Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa:

a) itungwe sheria ya kusimamia shughuli za Tume ya Taifa Uchaguzi;

b) kuwepo na sheria moja ya uchaguzi itakayotumika kusimamia uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani, badala ya kuwa na sheria mbili ambazo ni Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343 na Sheria ya Uchaguzi wa Madiwani, Sura 292; na

c) maafisa wa Tume ya Uchaguzi watakaowaengua wagombea kushiriki katika uchaguzi bila kuzingatia sheria na weledi wawajibishwe kwa mujibu wa sheria.

## 11. Kuhusu Matumizi ya TEHAMA Katika Uchaguzi

Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa:

a) matumizi ya TEHAMA katika mchakato wa uchaguzi yahamasishwe na kiwango chake kiongezwe;

b) zitayarishwe Kanuni mahsusi za kuratibu matumizi ya TEHAMA kwenye mchakato wa uchaguzi; na

c) kuwepo na uwekezaji wa kutosha kwenye miundombinu ya TEHAMA na usalama wake wakati wa uchaguzi.

## 12. Kuhusu Ushiriki wa Wanawake katika Siasa, Demokrasia na Uongozi

Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa:

a) Sheria ya Vyama vya Siasa irekebishwe ili:

   i) kuweka sharti la kila chama cha siasa kuwa na sera ya jinsia na ujumuishi wa makundi maalum katika jamii;

   ii) kuweka sharti la kisheria kwamba idadi ya jinsi moja katika vyombo vya maamuzi ndani ya chama cha siasa isipungue asilimia 40;

   iii) Kanuni za Usajili na Ufuatiliaji wa Vyama vya Siasa za Mwaka 2019 ziwe na vigezo vya ufuatiliaji ili kupima utekelezaji wa Sheria, katiba na kanuni za vyama vya siasa, kuhusu masuala ya jinsia na ujumuishaji wa makundi maalum ya jamii katika chama na uchaguzi; na

b) katiba za vyama ziwe na Ibara zinazoshughulikia masuala ya ukatili wa jinsia ikiwemo udhalilishaji wa wanawake;

c) kila chama cha siasa kiwe na programu maalumu kwa ajili ya kuwajengea uwezo wanawake kugombea ubunge, uwakilishi na

udiwani, ikiwemo kuwa na mipango na mikakati ya kufikia usawa wa kijinsia;

d) Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na kila chama cha siasa kiwe na dawati la jinsia litakalofanyia kazi masuala ya jinsia ndani ya vyama vya siasa;

e) utaratibu wa kuwa na viti maalum vya Wabunge, Wawakilishi na Madiwani wanawake uendelee, isipokuwa sheria ziboreshwe kuweka ukomo wa miaka kumi kwa mtu kuwa Mbunge, Mwakilishi au Diwani wa viti maalum vya wanawake. Uwakilishi huu uwe ni njia ya kupata uzoefu na kisha kupisha wanawake wengine wenye nia ya kuongeza ujuzi wa masuala ya siasa na uongozi.

f) kuwepo na mwongozo wa kisheria wa uteuzi wa wagombea na uchaguzi wa viongozi ndani ya Vyama vya Siasa, ikiwemo wabunge wa viti maalum ili kusaidia uteuzi na uchaguzi huo kuwa wa haki, uwazi na huru;

g) kila chama cha Siasa kiweke mkakati wa kuongeza idadi ya wanawake wanaogombea katika majimbo na kata za uchaguzi; na

h) kwa kuwa idadi ya wanawake ni ndogo katika Baraza la Vyama vya Siasa aongezwe mjumbe mmoja mwanamke kutoka kila chama cha siasa kuwa mjumbe wa Baraza la Vyama vya Siasa;

i) Wabunge wa Viti Maalum vya Wanawake waitwe Wabunge wa Taifa na Madiwani, waitwe Madiwani wa Wilaya, kwa sababu wabunge hao wanatokana na kura za nchi nzima na Madiwani wanatokana na kura za Wilaya. Aidha, Sheria ya Mfuko wa Jimbo ifanyiwe marekebisho ili itambue Wabunge wa Taifa kuwa miongoni mwa Wabunge wanaofaidika na fedha za Mfuko huo.

## 13. Kuhusu Ushiriki wa Watu Wenye Ulemavu katika Siasa, Demokrasia na Uongozi

Kikosi Kazi kinatoa mapendekezo kuwa:

a) sheria zisizozingatia ujumuishwaji wa Watu Wenye Ulemavu na zile zinazokwamisha ushiriki wao katika siasa, demokrasia na uongozi ndani ya vyama siasa zifanyiwe maboresho;

b) Vyama vya Siasa viweke mazingira rafiki yatakayowawezesha Watu Wenye Ulemavu kufanya shughuli za kisiasa bila vikwazo;

c) kila chama cha siasa kianzishe dawati la kushughulikia masuala ya Watu Wenye Ulemavu;

d) kuwepo na nafasi maalum kwa Watu Wenye Ulemavu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Madiwani. Viti vya uwakilishi wa Watu Wenye Ulemavu Bungeni viwe katika uwiano utakaozingatia jinsi. Suala hili lifanyiwe kazi katika mchakato wa kutungwa kwa Katiba Mpya ili lifanyike kwa ufanisi. Hata hivyo, kwa kuanzia kila chama cha siasa kitumie utaratibu wa sasa wa viti maalum vya Wanawake kujumuisha Watu Wenye Ulemavu;

e) Sheria ya Vyama vya Siasa irekebishwe ili:

  i) iweke sharti kwamba chama cha siasa kiwe na nakala ya Katiba na Kanuni zilizo katika maandishi ya breli. Aidha, katika mkutano mkuu wa chama taifa, awepo mkalimani wa lugha za alama;

  ii) katazo la ubaguzi kwa Watu Wenye Ulemavu katika vyama vya siasa lililopo katika kifungu cha 9(1)(c) cha sheria ya vyama vya siasa liwahusu pia viongozi wa vyama vya siasa; na

  iii) katiba ya chama cha siasa iwe na ibara inayokitaka chama husika kiwe na programu za kuwajengea uwezo watu

wenye ulemavu kushiriki kikamilifu katika michakato ya kisiasa, demokrasia na uongozi ndani na nje ya chama.

f) zitungwe Kanuni za utekelezaji wa Kifungu cha 6A (2) cha Sheria ya Vyama vya Siasa kinachoelekeza chama cha siasa kuzingatia suala la ujumuishwaji wa Watu Wenye Ulemavu katika masuala ya vyama vya siasa na demokrasia;

g) vyombo vya habari viandae vipindi maalum vya elimu ya uraia vinavyoeleza haki na mahitaji ya Watu Wenye Ulemavu;

h) Serikali iboreshe Makazi maalum ya Wazee na Watu Wenye Ulemavu;

i) suala la kuondoa ombaomba mitaani lifanyiwe kazi kwa ufanisi, kwani linaleta taswira kuwa Watu Wenye Walemavu ni maskini; na

j) elimu kuhusu masuala yote yanayohusiana na ulemavu na madhara yake ikiwemo afya ya uzazi, kinga kwa ajali, maradhi na njia bora za utabibu iongezwe ili kupunguza idadi na madhara ya ulemavu.

## 14. Kuhusu Ushiriki wa Vijana katika Siasa, Demokrasia na Uongozi

Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa juhudi zinazofanywa na Serikali kuhusu ushiriki wa vijana katika siasa, demokrasia, uongozi, uchumi, ulinzi na usalama wa nchi yetu ziendelee na mikakati mipya ibuniwe ili kuongeza ufanisi na tija.

## 15. Kuhusu utoaji wa Elimu ya Uraia ikiwemo elimu ya mpiga kura nchini

Kikosi Kazi kinatoa mapendekezo yafuatayo:

a) Serikali iandae mwongozo wa kitaifa, mpango kazi na mikakati ya utoaji elimu ya uraia, ili utoaji wa elimu hiyo uzingatie vipaumbele vya taifa na kuwa na uelewa wa pamoja wa walengwa;

b) elimu ya uraia ikiwemo elimu ya mpiga kura ifundishwe katika ngazi zote za mfumo wa elimu kuanzia shule za awali mpaka katika vyuo vya elimu ya juu. Aidha, mtaala wa elimu ujumuishe masuala ya elimu ya uraia;

c) Serikali na wadau wengine waongeze kiwango cha ufadhili katika kutoa elimu ya uraia ikiwemo elimu ya mpiga kura, ili kukabiliana na upungufu wa rasilimali, watu, fedha na vifaa katika kutoa elimu hiyo;

d) elimu ya mpiga kura itolewe kipindi chote siyo cha uchaguzi pekee, ili kuongeza muda wa kutoa elimu hiyo kuwezesha kuwafikia walengwa wengi zaidi; na

e) uratibu na ufuatiliaji wa elimu ya uraia unaofanywa na taasisi mbalimbali kwa mujibu wa sheria uendelee, isipokuwa ufanywe katika hali isiyokwamisha juhudi za kuwafikia watanzania wengi kupata elimu hiyo.

**16. Kuhusu suala la Rushwa na Maadili katika siasa na uchaguzi**

Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa:

a) suala la rushwa litamkwe katika Katiba, ili wananchi watambue kuwa vitendo vya rushwa havitavumiliwa wala kuonewa muhali. Pendekezo hili lifanyiwe kazi katika mchakato wa kutungwa kwa Katiba Mpya ili litekelezwe kwa ufanisi;

b) Sheria ya vyama vya Siasa Sura 258 irekebishwe ili:

   i) kuweka sharti kwamba, katiba ya chama cha siasa iwe na adhabu ya kumwondoa katika mchakato wa uchaguzi, mtia nia au mgombea aliyedhaminiwa na chama, endapo atathibitika kujihusisha na vitendo vya rushwa;

   ii) Msajili wa Vyama vya Siasa apewe mamlaka ya kuandaa mwongozo wa kufuatilia mchakato wa uteuzi wa wagombea na uchaguzi wa viongozi, ndani ya Vyama vya Siasa; na

   iii) kukitaka kila chama cha siasa kuwa na Kanuni za Maadili, zitakazodhibiti ukiukwaji wa maadili ndani ya chama, ikiwemo mwanachama kujihusisha na vitendo vya rushwa. Kanuni hizo ziweke utaratibu wa kushughulikia ukiukwaji wa maadili na adhabu, ikiwemo onyo, karipio, faini, kuvuliwa ujumbe wa kikao husika, kutoruhusiwa kugombea uongozi ndani ya miaka kumi tangu alipopatikana na hatia, kusimamishwa au kufukuzwa uanachama.

c) Sheria ya Gharama za Uchaguzi irekebishwe ili:

   i) kutoa adhabu kwa mgombea atakayeshindwa kufanya marejesho ya gharama za uchaguzi badala ya kukiadhibu chama cha siasa;

   ii) vitendo vinavyokatazwa katika sheria hiyo kuwa na sifa ya kuwa kosa la jinai;

iii) nyaraka za uthibitisho wa matumizi ya gharama za uchaguzi zibaki katika chama cha siasa husika badala ya kuwasilishwa kwa Msajili wa vyama vya siasa; na

iv) kuondoa upungufu mwingine wowote ambao ni kikwazo katika kuzuia na kupambana na rushwa katika mchakato wa uchaguzi;

d) Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6 irekebishwe kutambua Ushahidi wa mazingira (Circumstantial Evidence), ili uweze kutumika Mahakamani kuthibitisha makosa ya rushwa;

e) Sheria za Uchaguzi zirekebishwe kuweka masharti kwamba, mgombea atakayethibitika kujihusisha na vitendo vya rushwa aondolewe sifa ya kugombea katika uchaguzi wowote kwa miaka 10 mfululizo;

f) Sheria ya Watoa Taarifa na Ulinzi wa Mashahidi Sura ya 446 ifanyiwe marekebisho ili kuongeza kinga kwa mtoa taarifa wa siri;

g) Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa irekebishwe, ili kumwajibisha pia mtu anayetoa rushwa ya ngono. Aidha, adhabu zinazotolewa katika sheria hiyo kuhusu kosa la rushwa ya ngono ziendane na zile zilizopo katika Sheria ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA);

h) mitaala katika shule za msingi na sekondari iwe na moduli ya rushwa, badala ya kutajwa kama mengineyo kwenye somo la uraia;

i) matumizi ya teknolojia katika kuzuia na kupambana na rushwa yaongezwe, ili kuibua ushahidi uliojificha kwa kutumia utaalam wa utambuzi (exhumation of hidden evidence through forensic expertise);

j) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa isiingiliwe kisiasa wala kiutawala kinapotimiza majukumu yake ilhali kinafuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa kisheria;

k) kujenga silka na hulka ya uadilifu kwenye kaya (familia) hadi ngazi ya Taifa kwa njia zifuatazo:

   i) kuwa na mpango na mkakati mahususi wa kitaifa wa kukuza uadilifu;

   ii) kudhibiti utandawazi ili kuepusha wananchi kuiga mambo ya nchi nyingine ambayo hayaendani na utamaduni na mazingira ya nchi yetu;

   iii) kuheshimu na kufuata mila na desturi za asili zinazofaa; iv) viongozi wa dini waendelee kutekeleza majukumu yao ipasavyo;

   v) familia na shule ziweke mkazo katika malezi ya watoto kimaadili.

   vi) shule za msingi na sekondari za umma na binafsi ambazo siyo seminari zitakiwe kuwa na vipindi vya dini, ili kuruhusu watoto kupata elimu ya dini ambayo kimsingi ni njia ya kujenga uadilifu; na

   vii) maisha ya kifamilia yapewe kipaumbele na msisitizo wakutosha;

l) Somo la uraia na maadili linalofundishwa shule za msingi na sekondari liwekewe mkazo wa kutosha na lifundishwe katika ngazi zote za elimu.

**17. Kuhusu mfumo wa maridhiano ili kudumisha haki, amani, utulivu na umoja wa kitaifa nchini**

Kikosi Kazi kinatoa mapendekezo kuwa:

a) kuanzishwe utaratibu wa mijadala kila mwaka (Annual State of Politics Conference) itakayohusisha viongozi wakubwa wa kitaifa wa dola na Vyama vya Siasa ambapo mjadala utalenga kutazama hali ya ushindani wa kisiasa na kuimarisha mshikamano miongoni mwa wanasiasa na Vyama vya Siasa. Mkutano huo ufanyike katika Siku ya Demokrasia nchini;

b) mahakama iwe na mamlaka ya mwisho ya kuamua pale maridhiano yatakapokuwa yamekwama kwa pande husika; na

c) kwa kuwa nchi yetu ina amini katika Utawala wa Sheria na utoaji wa haki, hivyo, vyombo vinavyosimamia utatuzi wa migogoro kama Mahakama, Tume ya Haki za Binadamu, Tume ya Maadili na Kamati ya Amani ya Kitaifa ya Viongozi wa Dini na viongozi wa dini mbalimbali, ni lazima vifanye kazi kwa uadilifu na uaminifu wakati wote na hasa wakati wa migogoro inapotokea kupitia utaratibu huu wananchi watajenga imani kwa vyombo hivyo kama watoaji wa haki katika migogoro.

**18. Kuhusu mawasiliano kwa umma, vyombo vya habari na siasa**

Kikosi Kazi kinatoa mapendekezo kuwa:

a) wanahabari wenyewe waunde chombo cha kusimamia maadili ya wanahabari na vyombo vya Habari;

b) uwekwe utaratibu wa kusimamia utekelezaji wa Sheria husika, ili vyombo vya habari vya umma vitoe fursa sawa ya kutangaza habari za wagombea na Vyama vya Siasa wakati wa uchaguzi bila upendeleo;

c) ziandaliwe Kanuni zitakazoelekeza vyombo vya habari kuheshimu maadili ya taaluma ya uandishi wa habari, ikiwemo mwanahabari kuhakikisha anahakiki habari aliyoipata kutoka pande zinazohusika, kabla ya kutangaza au kuchapisha habari husika;

d) wagombea, viongozi na wanachama wa Vyama vya Siasa waepuke kutumia lugha za kuudhi, kejeli, uchochezi na matusi kupitia vyombo vya habari au mikutano ya hadhara;

e) sheria husika irekebishwe, ili kuondoa mamlaka ya Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo kufungia vyombo vya habari bila kuwepo mchakato wa wazi wa kuviwajibisha;

f) ili kuruhusu wananchi kushiriki ipasavyo katika shughuli za maendeleo na kuwafikia wananchi wengi zaidi wakati na baada ya uchaguzi, ni vyema wanasiasa wakafanya siasa kupitia vyombo vya habari kwa kufanya mahojiano, vipindi maalum, kushiriki mijadala na mazungumzo kama ilivyokuwa katika nchi nyingi duniani; na

g) sheria zinazoratibu uhuru wa habari ziboreshwe ili kukuza uhuru wa Habari na demokrasia nchini.

## 19. Kuhusu Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Kikosi Kazi kinapendekeza kukamilishwa kwa mchakato wa kupata Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia hatua sita zifuatazo:

**Hatua ya Kwanza: Mjadala wa Kitaifa ili kupata Muafaka katika Masuala ya Msingi**

Kuanzishwa kwa mjadala wa kitaifa katika masuala ya msingi, ili kupata muafaka wa kitaifa kabla ya kuanza mchakato wa kuandika Katiba mpya. Mjadala huu ufanyike kwa ushiriki mpana wa wananchi. Masuala ya msingi yanajumuisha muundo wa Muungano, madaraka ya Rais, mfumo wa uchaguzi, madaraka ya Serikali za Mitaa, rushwa na maadili na mengineyo yatakayojitokeza.

**Hatua ya Pili: Kuhuisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na Sheria ya Kura ya Maoni**

Kuhuisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na Sheria ya Kura ya Maoni ili kuweka mahitaji ya sasa, yakiwemo kuainisha muda wa mchakato mzima, kutambua kuanzishwa kwa Jopo la Wataalam na kuainisha misingi ya kuzingatiwa katika mchakato wa mabadiliko ya Katiba. Aidha, kuwepo na ushirikishwaji mpana wa wananchi katika mchakato wa kuhuisha Sheria hiyo, kwa kufuata taratibu za utungaji wa sheria nchini.

**Hatua ya Tatu: Kuundwa kwa Jopo la Wataalam**

Baada ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kuhuishwa, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushauriana na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aunde Jopo la Wataalam, litakalopitia na kuoanisha Katiba Inayopendekezwa na Rasimu ya Pili ya Katiba iliyoandaliwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011 na kuandaa Rasimu ya Katiba Mpya itakayowasilishwa Bungeni.

Kikosi Kazi kinapendekeza kuwa, katika utekelezaji wa majukumu yake, Jopo la Wataalam lizingatie masuala yafuatayo:

a) kufanya mapitio ya Katiba Inayopendekezwa ya Mwaka 2014, kwa kuzingatia hali ya sasa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii;

b) kurejea nyaraka zifuatazo, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984, Rasimu ya Pili ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011 na Ripoti ya Serikali kuhusu masuala muhimu ya kitaifa yaliyojadiliwa katika mjadala wa kitaifa wa Katiba; na

c) masuala muhimu ya kitaifa ambayo ni:

i) mfumo wa kiutawala wa kijamhuri; ii) uwepo wa Jamhuri ya Muungano; iii) uwepo wa Serikali, Bunge na Mahakama; iv) uwepo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

v) uwepo wa umoja wa kitaifa, amani na utulivu; vi) uwepo wa uchaguzi wa kidemokrasia katika vipindi maalum na kuzingatiwa kwa haki ya kila mtu mwenye sifa ya kupiga na kupigiwa kura;

vii) uhifadhi wa Haki za Binadamu na utawala wa sheria;na viii) uwepo wa Serikali isiyofungamana na dini.

**Hatua ya Nne: Rasimu ya Katiba Mpya Kupitishwa na Bunge**

Baada ya Jopo la Wataalam kukamilisha kazi ya kuandaa Rasimu ya Katiba, itawasilishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kujadiliwa na kuipitisha kuwa Katiba Inayopendekezwa. Majukumu ya Bunge yatabainishwa katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba.

**Hatua ya Tano: Elimu ya Uraia kuhusu Katiba Mpya**

Kutoa elimu ya uraia kuhusu Katiba Inayopendekezwa kabla ya kupigiwa kura, ili wananchi waifahamu Katiba husika na kuwaandaa kupiga kura ya maoni kwa amani na utulivu.

## Hatua ya Sita: Kura ya Maoni

Wananchi kupigia kura ya maoni Katiba Inayopendekezwa.

**Kiambatisho Na. 2**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, WAKATI AKIFUNGUA MKUTANO WA WADAU UNAOJADILI HALI YA DEMOKRASIA YA VYAMA VINGI VYA SIASA NCHINI TANZANIA TAREHE 15 DISEMBA 2021

*Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*

*Waheshimiwa Wazee Wetu Wastaafu; Mzee Joseph Warioba, Waziri Mkuu Mstaafu;*

*Mzee Pandu Ameir Kificho, Spika Mstaafu;*

*Dada Anna Makinda, Spika Mstaafunwa Bunge la jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*

*Mzee Butiku, Mzee wetu maarufu Mstaafu wa mambo mengi ndani ya nchi hii (nilikuwa najiuliza ndie sie lakini hiyo kofia nadhani kniambia ndiye).*

*Lakini nitambue uwepo wa Mhe. Jesnista Mhagama, Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu;*

*Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri mliopo hapa;*
*Mhe. Mwenyekiti wa kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria, Ngugu yetu Najma;*

*Mheshimiwa Jaji wa Rufaa (Mst.) Semistocles Kaijage ambae ni Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*

*Lakini pia Mheshimiwa Jaji (Mst.) Hamid Mahmoud, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar;*

*Mheshimiwa Jaji Francis Mutungi, Msajili wa Vyama vya Siasa pamoja na Naibu Msajili;*

*Mheshimiwa Juma Ali Khatib, Mwenyekiti wa Baraza ka Vyama vya Siasa pamoja na Makamu Mwenyekiti;*

*Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Vyama vya Siasa na Viongozi wengine wa Vyama vya Siasa mliopo;*
*Kamati ya Uongozi ya Baraza;*

***Waheshimiwa Watoa Mada (tuliambiwa Mkutano utakuwa na Watoa Mada);***

***Mheshimiwa Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma; Mwenyekiti wa TCD, Mhe. Zitto Kabwe (sasa hivi utanipata kwenye Mkutano wako, nilikuwa nasubiri nifanye huu kwanza. Alishaniomba sijui mara tatu nabana kimya nilikuwa nasubiri huu. Sasa utanipata kwenye wako.***

***Waheshimiwa viongozi wengine wa Serikali mliopo;***
***Viongozi wa Dini;***
***Waandishi wa Habari;***
***Waalikwa wenzangu katika mkutano huu:***
***Mabibi na Mabwana;***

***NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA!!!***

Waheshimiwa mniruhusu nami niongoze sauti yangu katika kumshukuru Mungu kwa kutujalia uhai, uzima afya njema na kuwezesha kukutana hapa. Nimefurahi nilivyomuona Mzee Mrem

ana yeye yuko hapa. Aidha, naupongeza Uongozi wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, chini ya Mheshimiwa Jaji Francis Mutungi na Baraza la Vyama vya Siasa chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Juma Ally Khatib Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa kwa kunialika kuja kufungua mkutano huu mkubwa wa wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa. Ninaelewa kuwa mkutano huu siyo wa kisheria kama ilivyo kwa vikao vya Bunge na Baraza la Vyama vya Siasa, bali ni tukio ambalo linatokana na utamaduni tulionao hapa nchini kwetu wa kukaa meza moja na kuzungumza mambo yanayohusu maslahi ya Taifa letu. Utamaduni huu hutekelezwa katika nchi yetu kwa namna na ngazi mbalimbali. Kwa mfano katika ngazi ya mkoa kuna vikao vya Baraza la Ushauri la Mkoa na katika ngazi ya wilaya kuna vikao vya Ba raza la Ushauri la Wilaya. Kwa hiyo hizo ni ngazi za vikao hivyo vya mashauriano. Katika vikao hivyo vyama vya siasa na wadau wengine hualikwa kushiriki na kutoa maoni yao.

Lengo kubwa la utaratibu huu ni kuwashirikisha watanzania kupitia viongozi wao wa taasisi zilizosajiliwa kuchangia mawazo katika uendeshaji wa nchi yetu, huku tukitambua kwamba wananchi ni wadau muhimu na wana nafasi ya kutoa maoni yao katika uendeshaji wa shughuli za Serikali. Hivyo, naipongeza Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na Baraza la Vyama vya Siasa kwa kuendeleza utamaduni huu wa kidemokrasia. Kwa namna ya pekee nawapongeza viongozi wa vyama vya siasa mliopo hapa. Shughuli hii ni yenu, na michango yenu ni muhimu katika kuimarisha Demokrasia yetu. Aidha, nawashukuru viongozi wa Serikali mliopo au mliolipa umuhimu suala hili na kuhudhuria mkutano huu pamoja nami, mkiongozwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kitendo cha Vyama vya Siasa kukaa pamoja kuwashirikisha wadau na kujadili mambo yanayowahusu, ni ushahidi tosha wa kuwepo kwa umoja na mshikamano, kuwepo kwa ukomavu wa kisiasa na siasa za kistaarabu ndani ya taifa letu. Nakushukuruni pia viongozi wa dini, na asasi za kiraia kwa kutambua umuhimu wa mkutano huu na kujumuika hapa leo kwa maslahi mapana ya Taifa.

***Ndugu Viongozi,***
***Wageni Waalikwa,***
***Mabibi na Mabwana;***

Takriban miongo mitatu ya uhuru nchi yetu ilikuwa chini ya mfumo wa demokrasia ya chama kimoja cha siasa. Chama ambacho kwa kiasi kikubwa kilifanikiwa kujenga misingi ya umoja, upendo na mshikamano miongoni mwa Watanzania. Chini

ya mfumo wa chama kimoja, tuliweza kulinda uhuru wetu na kujenga umoja wa kitaifa. Mwaka 1992 tulirejesha mfumo wa demokrasia ya vyama vingi, kwa nia njema ya kupanua wigo wa demokrasia, lakini pia kwenda sambamba na mfumo wa ulimwengu kwa wakati huo. Aidha, tulifanya hivyo kwa kuruhusu kuwepo kwa ushindani wa fikra, itikadi na sera ili kuwapa wananchi chaguo pana zaidi, na fursa pana ya kuchangia mawazo ya namna bora ya kuongoza nchi hii na kuwaletea wananchi maendeleo.

Kwa kuwa malengo makuu ya kuwapo kwa mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa ni kuongeza kasi ya kuleta maendeleo kwa watu, basi ni vyema vyama vya siasa mnapofanya shughuli zenu mzingatie hayo, na kwamba, kuwa na mfumo wa vyama vingi na mawazo mbadala haimaanishi

kuleta vurugu, fujo, kauli zenye ukakasi na vitisho na zenye kuamsha hisia na kuleta vurugu na uvunjifu wa amani, ni tofauti. Tumeweka vyama vingi, hatukuwa na maana hii, tulikuwa na nia ya kupanua demokrasia na kutoa wigo mpana kwa wananchi kuwa na uchaguzi lakini kupata fikra mbadala kwenye uendeshaji wa Serikali na si vinginevyo.

Fursa ya kuwa na jukwaa la kutoa wazo mbadala lisiwe kibali cha kuendesha siasa za chuki na uhasama, na zinazokwamisha maendeleo ya wananchi. Tukiendesha siasa za namna hiyo tutakuwa tunakwenda kinyume na malengo ya kuanzishwa kwa mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa, kwani hata katika nchi ambazo ndiko mfumo huu wa demokrasia ulikoasisiwa kipaumbele hutolewa kwa ukomavu wa siasa ili kuendana na shughuli za maendeleo ya watu kuliko malumbano ya kisiasa wakiamini kwamba siasa ni nyenzo tu ya kuleta

maendeleo. Kwa hiyo kipaumbele ni maendeleo, siasa itachangia kwenye kuleta maendeleo.

Nitoe ushauri kwenu viongozi wa kisiasa kwamba tutumie fursa ya kuwepo kwa vyama vingi vya siasa kuwaonyesha wananchi ni kitu gani cha tofauti tutafanya ili kuongeza kasi ya kuwaletea maendeleo. Siasa si kulumbana, siasa si matusi, siasa si kusema uongo. Huko nje kuna msemo wanasema ukitaka kusikia uongo nenda kwa wanasiasa. Lakini sio kweli, siasa sio kusema uongo. Siasa si lugha za dhihaka, maneno ya kashfa, kuchochea watu wasishiriki katika shughuli za maendeleo na kutotii sheria. Siasa si uchonganishi baina ya wananchi na Serikali yao. Siasa za aina hii hazina tija yoyote bali ni ukiukwaji wa kanuni za demokrasia ya ushindani.

Tumeweka vyama vingi kuwe na demokrasia ya ushindani, sasa tukifanya haya hayana tija bali ni kukiuka kanuni za demokrasia ya ushindani.

***Waheshimiwa Viongozi na washiriki wa mkutano;***

Katika kukuza na kudumisha demokrasia ya vyama vingi vya siasa, sheria za Bunge zimewezesha vyama 19 kusajiliwa na kufanya kazi, na nimeambiwa vingine zaidi ya 10 vimeomba usajili na msajili anaendelea nah atua za au ndio au sio. Aidha, Sheria mbalimbali za nchi zimeruhusu uwepo wa taasisi za kiraia zenye kutoa elimu ya uraia kisiasa, kijamii na kiuchumi na nadhani nyingi zimealikwa hapa, taasisi hizo za kiraia.

Aidha, Serikali imekuwa ikipokea na kuzifanyia kazi hoja na tathmini zinazotolewa na tathmini zinazofanywa na taasisi hizo na kuzifanyia kazi ipasavyo kwa lengo la kuleta ustawi wa

demokrasia nchini. Nazipongeza asasi hizi za kiraia kwa maoni ambayo kwa kiasi kikubwa yamekuwa chachu ya kuimarisha demokrasia yetu.

Hata hivyo, nitumie fursa hii kuwakumbusha kwamba duniani kuna nchi moja tu inayoitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ni Taifa huru lililojengwa katika misingi ya amani, upendo, mshikamano, na linaoongozwa kwa misingi ya Katiba na Sheria zilizotungwa na Bunge na sio utashi wa mtu au utashi wa mataifa mengine. Na wenye hilo taifa ni sisi tuko hapa. Uendeshaji wa hili taifa utatokana na sisi tuliopo hapa.

Halikadhalika, ni muhimu kutambua kwamba demokrasia ya vyama vingi vya siasa hapa nchini kwetu itakuwa na maana kama tukidumisha amani, utulivu na umoja wa taifa letu. Pamoja

na ukweli kwamba uhuru ni sehemu muhimu ya demokrasia, lakini utii wa sheria una nafasi kubwa katika kuhakikisha uhuru wa kila mtu unaheshimiwa. Mtu kumheshimu mtu mwingine au Serikali kumheshimu mtu. Na hapa nataka nizungumzie kidogo aliloniomba mwanangu Mwenyekiti wa TCD, kwamba yule

mwenzetu msamehe basi aje awe na sisi. Tunasema demokrasia ni kuheshimu Sheria. Unapoheshimu Sheria, ndipo demokrasia inapokuwa, lakini pia ndipo inapoleta heshima. Heshima ya mtu inakuja kwa kuheshimu Sheria za nchi. Unapovunja Sheria za nchi heshima yako haitoheshimiwa, Serikali haitokuheshimu. Lakini lazima ujue kwamba unapotumia uhuru wako, mwisho wa uhuru wako inaanza heshima ya mtu mwingine. Kwa hiyo vyote hivyo lazima tuvipime ili tunapofanya shughuli zetu twende navyo hivyo. Isingekuwa uvunjifu wa Sheria leo isingemlazimu kuomba hapa kuwa yule mwenzetu muachie na hivi na hivi. Lakini unapovunja Sheria, unajivunjia heshima na

Serikali inashindwa kukuheshimu.

Naomba tufanye kazi kwa kuheshimu Sheria. Waswahili wanasema, mtakanyingi nasaba hufanya nini? … ingawa kusameheana napo kupo. Kusameheana napo…

Sasa ili kuifanya demokrasia inawiri lazima twende na matakwa ya Sheria. Na sisi ndio watumizi wa Sheria. Sheria inapotukwaza, vikao vya namna hii tunasema Sheria moja, mbili tatu zinatukwaza. Tunahisi ingekuwa hivi, ingekuwa hivi, ingekuwa hivi. Serikali ipo, itasikia, itachukua nasi tutakuja kupima kwetu. Lakini kama sheria tunazikubali zinapitishwa na Bunge, wananchi wanazikubali lazima tufuate Sheria.

Hivyo, niviase vyama vya siasa na asasi za kiraia kuheshimu Sheria ili Uhuru na mani ya nchi yetu iweze kutamalaki.

***Ndugu viongozi na wanasiasa wenzangu;***

Katika dunia hii hakuna jambo lisilo na kasoro. Hakuna! Popote ulimwenguni, kila kitu kina kasoro zake. Na anaeliendesha jambo haoni kasoro zake, anaemtizama muendeshaji anaona kasoro zake. Hata tunapokuwa kwenye ngoma kama unacheza huendi na mdundo, wan je ndie anakuona

wewe unaedemka humo ndani ya ngoma hujioni kwamba nakosea *steps* au siendi na mdundo, hujioni. Umo tu unahambukwa. Lakini anaekutizama anasema yule.. kwa hiyo vivyo hivyo hakuna jambo lisilo kasoro; katika kuendesha Serikali kuna kasoro, kwenye vyama vyenu vya siasa kuna kasoro tena kubwa tunawasikia mnalumbana huko. Lakini jambo la busara ni kuondoa kasoro kwa kuelimishana,

kuelekezana na kujadiliana. Tukikaa kuelimishana, kuelekezana na kujadiliana tutakuwa tunaondosha kasoro zetu.

Hivyo nitoe rai kwa vyama vya siasa na taasisi za kiraia kwamba kunapokuwa na kasoro zozote katika mifumo yetu, au

kuna mambo fulani hayaendi sawa, jambo la busara ni kuelezana, kujadiliana kama tutakubaliana ama tutatoka bila kukubaliana ni vyema kuwa na msimamo wa kuiwezesha demokrasia yetu kushamiri. Kwasababu si kweli kama tutakaa tuzungumze sote tukubaliane. Mwingine atakuwa ana mambo yake ambayo hayakubaliani. Sasa unapotoka hujakubaliana na wenzio basi tutoke na msimamo kwamba demokrasia iendelee kushamiri. Usitoke kwamba mimi sijaridhika naenda kuvuruga kila kitu cha nchi nzima kwasababu wewe mmoja hujaridhika; yie wawili hamjaridhika. Hatuendi hivyo!

Na ndio mana kuna ule msemo wanasema wengi wape lakini wachache waheshimiwe. Tunapotoka hatujakubaliana, kama wengi wamekubali twende na makubaliano ya wengi. Lakini wachache ambao hawakukubali, tuheshimu mawazo yao, tuyafanyie kazi tuone tunakwendaje ndipo tutakaposhamirisha

au kunawirisha demokrasia ndani ya nchi yetu.

***Ndugu zangu,***

Ndugu zangu nimekuja kwenye mkutano huu nikiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wadhifa ambao unanipa dhima ya jukumu la ulezi wa amani ya nchi hii lakini pia nimekuja nikiwa mkuu wa nchi jukumu ambalo linanitaka kuhakikisha naliunganisha taifa kama Zito alivyosema.

Naliunganisha taifa katika hali ya umoja, mshikamano ili kuwe na utulivu na amani ndani ya nchi yetu. Na hii ndio dhamira yangu kama Mkuu wa nchi, Mkuu wa taifa linaloitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo basi nataka nirudie ombi langu kwa wenzangu wa vyama vya siasa kwamba, kuelekezana, kuelimishana, kujadiliana ndiko kutakakoinusuru nchi yetu na majanga ya kisiasa na vurugu. Linapotokea jambo

hatujakubaliana tukae tuelimishane, tukubaliane, tuelekezane. Hatukukubaliana nimesema tutoke na msimamo ya kwamba nchi yetu ni taifa moja twende tukaimarishe demokrasia.

Lakini kuna haja pia tunapokwenda kuzungumza na hatukukubaliana basi tupingane kwa hoja. Tupingane kwa hoja za kizalendo zenye kuongozwa na uhalisia wetu kiutamaduni, uhalisia wetu kijamii na uhalisia wetu kiuchumi. Tusiende kubishana unang'anga'ana unataka jambo haliendi na tamaduni za kitanzania, uchumi wa kitanzania hauruhusu wala jamii ya Tanzania hairuhusu. Nadhani mnaona huko kwenye mitandao watu wanabishana. Kuna mambo yanalazimishwa yawe na hayaendi na utamaduni wa kitanzania au saa nyingine viongozi wa vyama vya siasa watataka mambo ambayo kwa uchumi wa Tanzania hatuwezi. Sasa tunapokwenda kujadiliana,

kuzungumza, kuelekezana haya mambo ni lazima tuyape umbele wake. Tuzungumze tufikie maridhiano ya kuzizika tofauti zetu, hili ndio lengo langu. Tuzungumze tufikie maridhiano tuzike tofauti zetu. Sisi ni taifa moja. Wala hakuna mwenye cheti akasema mm nina cheti cha kumiliki Tanzania, hakuna. Wote ni watanzania. Wote tuna haki sawa. Hakuna mbora wetu mbele ya Sheria. Mbora wetu ni tule anaefuata Sheria. Kwa hiyo hii inatusukuma kwamba tuna haja ya kukaa kuzungumza kama ndani ya Tanzania. Tuoneshane upendo na mshikamano ili tudumishe amani yetu. Tuenzi utu wetu, uzalendo na utanzania wetu kwa kufuata mila kama nilivyosema, desturi, silka na mambo mengine ya kitanzania. Ninasisitiza tujadili kwa kuongozwa na kuzingatia historia, mila desturi, silka na

tamaduni zetu na muktadha wa hali ya kiuchumi ya nchi yetu.

Kuna mazoea ya kuangalia demokrasia ya vyama vingi kwa kulinganisha nan chi ambazo tunatofautiana kihistoria, kiutamaduni maendeleo ya nchi na hata muktadha wa

kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi. Jambo hili sio sahihi, demokrasia ya wenzetu hata kule mfumo huu ulipoasisiwa na wenyewe wana yao, na demokrasia yao haiwezi kuwa sawa na yetu, na ya kwetu haiwezi kuwa sawa na yao. Ni kwasababu demokrasia haina *formula* kwamba ukichukua moja kwa moja ni mbili na haibadiliki. Haina hivyo. Inaenda na historia ya nchi, uwezo wa kiuchumi wa nchi, mila na desturi za nchi na mambo mengine katika nchi. Mwenendo wa siasa kwenye nchi. Hivyo huwezi kuchukua demokrasia ya taifa lenye miaka 200 na ukalinganisha na ukataka iwe saw anna demokrasia ya taifa la miaka 60. Sisi bado tunaitwa wachanga wa demokrasia. Kwa hiyo tunakwenda kwa uchanga wetu. Na katika uchanga wetu kuna

mambo mengi yanatokea, tutagombana, tutasemana lakini turudi tukae, tuelekezane, tuelimishane, tujadiliane na tukubaliane twende na siasa zetu.

***Ndugu zangu viongozi na wanasiasa wenzangu,***

Kuna msemo wa zamani ulikuwa unasema amani hupatikana kwa ncha ya upanga. Lakini kama nilivyosema huu ni msemo wa zamani. Enzi hizo. Nadhani kwa wale wanaotizama filamu za kituruki zile zinazooneshwa mnaona jinsi walivyopata amani kwa ncha ya upanga. Kwa hiyo huu ni usemi wa wakati huo. Wakati wetu tulio nao amani hupatikana kwa ncha ya ulimi. Ni ndimi ndizo zinazoleta amani, kuliko fimbo au panga na mambo mengineyo. Na hii inaonesha umuhimu wa kukaa na kuzungumza. Tuna mfano mzuri ndani ya nchi yetu Zanzibar mimi ninakotoka. Tuliamini labda amani hupatikana kwa ncha ya upanga, tukajaribu. Tuliipata amani kwa ncha ya upanga miaka

hiyo ilipokuwa ikifanya kazi 64, lakini baadae huku mbele haikuwezekana. Amesema hapa Zitto nadhani au nani 2001 tulijaribu, haikuwezekana. Lakini Zanzibar mnayoiona hii leo

amani imepatikana kwa ncha ya ndimi. Watu walikaa wakazungumza, wakajadiliana, wakaambizana wakaelimishana, wakasema hakuna haja. Tukaeni tujenge Zanzibar yetu. Ndio yanayotokea leo pale. Ni mazungumzo na sio nguvu wala ugomvi, wala matusi wala kutishana. Hapana, ni mazungumzo. Hivyo basi niwaombeni wenzangu wenyeviti wenzangu wa vyama vya siasa tusitazame yaliyopita, tutazame mbele kwa matumaini. Tuweke nguvu yetu pamoja kujenga Tanzania mpya yenye kusameheana, yenya kuheshimiana na kufungua kurasa mpya za kwenda na demokrasia yetu Tanzania. Kama mlezi nilisema hapa kama Mkuu wa Nchi kunanipa jukumu na wajibu wa ulezi. Na kama mlezi natakiwa kuwa mvumilivu, msikivu na

mwenye kusamehe. Na niko tayari kufanya yote hayo. Nitasikiliza, nitavumilia mnayoniambia, mnayonikosoa na niko tayari kusamehe pia ili twende vyema.

Lakini mambo haya ni pande mbili. Mimi nimeshasimama kusema hayo. Na ninasema mbele yenu wengine wako kwenye vyombo vya Habari wananiona na ulimwengu unanitizama. Niko tayari kuvumilia, kustahmili na kusamehe. Lakini nanyi wenzangu kwenye vyama vya siasa muwe tayari kwenye haya;
kufuata sheria, kujadiliana na tufikie pazuri. Tuzike tofauti zetu za nyuma, tufungue kurasa mpya za kuendesha siasa ndani ya nchi. Niko tayari kusikiliza wenzangu. Tushawishiane kusameheana, najua kuna mengi ya kusikiliza pia. Kuna madukuduku, kuna hasira, kuna malalamiko kuna nongwa, yanayotokana na uchanga wetu wa demokrasia. Si mengine, ni uchanga tu wa demokrasia.

Vile vile najua vyama vya siasa vina maoni pamoja na wadau wengine. Vina maoni na mapendekezo yanayopaswa kufanyiwa kazi na Serikali. Tuko tayari kuyapokea na tutayafanyia kazi. Tuzungumze tuone njia bora ya kufanyia kazi hayo yanayotukwaza ili tutoke hapa tulipo. Kama nilivyosema, hakuna mwenye cheti cha kumiliki nchi hii ni nchi yetu sote. Kwa hiyo amani, utulivu na demokrasia itaendeshwa nasisi sote. Ni mfumo tu wa kidunia kwamba huyu anaongoza, huyu anakuwa namba mbili huyu atakuwa mpinzani wake, huyu atakuwa nini. Lakini wote ni watanzania tunaotakiwa kuendesha nchi hii.

Tuna kila sababu ya kujivunia kwa hatua tuliyoifikia katika kuimarisha demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini. Tumeongeza idadi ya vyama vya siasa kama ilivyosemwa hapa kutoka kumi na tatu (13) mwaka 1995 vilivyoshiriki uchaguzi wakati ule hadi sasa tumefikia vyama kumi na tisa (19)

vilivyoshirika uchaguzi mkuu wa Mwaka jana. Na hivi ni vile vyenye usajili wa kudumu. Na kama nilivyotangulia kusema awali, vyama vingine zaidi vinaomba usajili na kazi inaendelea.

Wanachama wa vyama hivyo vya siasa na viongozi wao wana uhuru wa kufanya kazi zao za kichama na kisiasa kisheria, huku wakitumia vyombo vya habari vilivyo huru kujitangaza na kunadi sera zao. Suala la msingi ni kufuata sheria za nchi na kuhakikisha tunafanya siasa ambazo hazicheleweshi au kuvuruga maendeleo ya nchi yetu. Changamoto hazikosekani ndiyo maana kuna mijadala kama hii inayofanyika ili kubadilishana mawazo ya kukabiliana na changamoto zilizopo na kuona namna bora ya kuzitatua. Lengo la mijadala kama hii ni kujenga na sio kubomoa. Hivyo, niwasihi kwamba, katika mijadala itakayoibuliwa kwenye mkutano huu leo naomba pia namna bora ya vyama vya siasa vitakavyoweza kufanya

mikutano ya hadhara bila kuvunjwa kwa sheria za nchi. Bila kuvunjwa kwa sheria za nchi. Najua kuna Sheria ya Msajili wa Vyama vya Siasa, sijui Sura 11 au kifungu 11 nadhani kinatoa insi ya kufanya mikutano ya hadhara. Lakini kuna Sheria au kanuni za Jeshi la Polisi na zenyewe zina mwongozo wa kufanya mikutano ya hadhara. Mnakwenda, mnafuata, mnafanya bila vurugu, bila matusi, bila kutukanana bila kuharibu mali za nchi. Inapotokea mnafanya kinyume, sheria zinachukua mkondo wake. Na sheria zimeeleza; kufungiwa. Isingekuwa kuna matendo haya mikutano isingefungikwa. Lakini ndugu zangu mnaichukulia mikutano kama mmepata uhuru wa ku – *riot,*

kutengeneza *civil strife,* fujo za kijamii. Hatuendi hivyo. Sheria lazima zichukue mkondo wake. Kwahiyo naomba mjadili na mjifunge wenyewe hapa jinsi mtakavyokwenda kufanya

mikutano ya hadhara. Nataka Msajili, Jeshi la polisi kaeni na hawa watu muone kwasababu ni haki yenu ya kikatiba zenu na katiba

ya nchi kufanya mikutano kunadi sera zenu. Lakini mnaivunja nyinyi wenyewe. Mnajinyima nyinyi wenyewe.

Hakunaatakaekubali anaongoza nchi mnapewa kibali kufanya mikutano mnapita kuvunja magari ya watu, kuvuruga. Nani anakubali, hakuna anaekubali, mtafungiwa tu. Lakini onesheni siasa za kistaarabu, onesheni ukomavu wa kisiasa. Onesheni kwamba ninyi ni wanasiasa mnaojua nini mnafanya. Sio Watoto wadogo. Wanaofungiwa ni watoto wadogo wa shule. Ndio wanaoambiwa mkifanya hivi bakora sio watu wazima kama sisi. Kwa hiyo mjadili jinsi mtakavyoweza kufanya, tukiyaona yana mana tutafungua, tukiyaona bado tutaendelea kujadiliana. Lakini la muhimu ni kupata haki yenu ni kufanya mikutano ya hadhara.

***Ndugu zangu;***

Leo mmekutana kujadili hali ya demokrasia ya vyama vingi vya siasa hapa nchini, ukiwa ni mjadala wa kawaida wa wadau

kukutana na kubadilishana mawazo. Natambua kwamba Mkutano huu umewakutanisha vyama vya siasa na wadau wengine wa demokrasia zikiwemo asasi za kiraia.

Sasa niongee na asasi za kiraia na wadau mliopo hapa kuiga utamaduni huu wa vyama vya siasa wa kuandaa mijadala ya kistaarabu ya kisiasa. Ya kistaarabu ya kisiasa yenye kuelimisha wananchi na sio kupotoa wananchi. Ni ukweli kwamba majukwaa haya kwa sasa yamelala. Lakini yamelala kwa sababu. Kwa hiyo mtakapojirekebisa na kufanya vizuri hata sisi tunataka wananchi waelezwe mambo yaliyopo nchini, mazuri yaliyopo nchini kama kuna kasoro zilizopo zisemwe, kwasababu zikisemwa sisi tutapata kuzisikia tutapata kujirekebisa. Zisiposemwa hatuzisikii mtakuwa huko mnafukuta ndani kwa ndani hatujui mliyonayo tunawaona tu mnanenepa kwa presha na *stress,* tunajua mambo mazuri kumbe mapresha na ma-*stress* yamewajaa humo

ndani. Lakini. Kifunguka, mki-*off load* mkisema tutajua kuna nini huko nasi tutakwenda kufanyia kazi.

Nimesema nchi hii ni yetu. Nchi hii ni yetu, hakuna anaemiliki hii nchi. Kwa hiyo mkisema wale ambao tumepata idhini ya wananchi kuongoza, tutayafanyia kazi turekebishe twende vizuri.

Aidha niwasihi Baraza la Vyama vya Siasa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuendelea kutekeleza jukumu lao la kisheria la kuvikutanisha vyama vyote vya siasa vyenye usajili viweze kujadili mambo yao. Hapa kwa maneno ya msajili kikwazo ni bajeti, njoo tuzungumze. Njoo tuzungumze Msajili. Kila kitu ni ncha ya ulimi, si ndio? Njoo tuzungumze, lakini pia tuone mnachokifanya tuone *output* ya vyama vya siasa, tuone mnatuambia nini. Tuiona hakitoki kitu tunasema kwanini nipoteze

pesa wakati huku klorokwini za wananchi hakuna. Napeleka kwenye klorokwini nakata kwenye vyama vya siasa. Lakini tukiona kuna mazuri yanayotoka kwenu, kuna miongozo
kuna mambo yanatoka kwenu ni ya kweli mnatupa tuyarekebishe tuta-*activate* uhai wenu kwa kweli na kwa hakika. Kwahiyo Msajili njoo tuzungumze

Ndugu zangu nimalizie hotuba yangu kwa kuutakia mkutano huu mjadala mwema wenye manufaa. Hasa tukiangalia chaguo la washiriki waliopo ni watu wa marika tofauti wenye elimu na maarifa tofauti, wenye uzoefu wa nyakati tofauti. Ni matumaini yangu kwamba kuwepo kwa upeo mpana wa
washiriki kutafanya mjadala huu uwe huru na wa wazi. Watu wangu wa Serikali wawili watatu watauwepo hapa, hawana ruhusa ya kusema wao ni kupokea labda muulize swali watakiwe kujibu, watajibu. Lakini kunyanyuka wao na kusema, kuchangia

hapana; wasikilize, wapokee tufanyie kazi. Kwahiyo ni matumaini yangu kuwa kuwepo kwa upeo huu mpana kutaleta huo mjadala huru na wa wazi. Tukosoe, tukosoane na tujikosoe pia. Hakuna aliye *perfect.* Kwa hiyo sikiliza mnavyokosoana hapa na jitathmini wewe mwenyewe je mimi nipo kwenye right way

au siko kwenye njia sahihi. Jikosoe mwenyewe. Ndio madhumuni ya mijadala hii.

Katika mijadala hii, kuna uwezekano na tashi binafsi za watu kutaka kutawala mijadala. Tutambue kuwa hakuna

mwenye maarifa yasiyo na mjadala. Hakuna. Ukiwaza wewe lako hili ukiliona liko sahihi mwenzio ana jingine ambalo atakwambia liko sahihi lakini ungeongeza na hiki na hiki ingekuwa sahihi zaidi. Tukubali yote haya. Tuthamini mchango wa kila taasisi na kila mtu atakaepata fursa ya kuzungumza. Tutafakari jinsi tulivyofika hapo tulipo na hatimae tushauriane tunatokaje hapa

tukitizama mbele kwa matumaini makubwa. Mimi naamini hakuna lisilozungumzika hasa kwenye watu wenye maarifa na waungwana kama mliopo hapa. Nilikuwa naangalia sura mbalimbali nilizoziona hapa viongozi wa vyama vya siasa wale ninaowajua natizama mmoja mmoja yupo. Kwahiyo nikajua huu mkutano utakuwa mzuri. Kwahiyo hakuna lisilozungumzika. Tuzungumzeni kwasababu sisi ni wenye maarifa makubwa na waungwana pia na tumebobea kwenye siasa. Wengi wetu hapa tumebobea kwenye siasa.

Ndugu zangu nirudie tena kuwashukuru kwa kunialika mimi na wenzangu Serikalini kuja kushiriki ufunguzi wa mkutano hu una niwatakie kila la kheri katika kujadili mustakabali wetu kisiasa na niimani yangu kwamba mtatuletea

maazimio yanayotekelezeka.

Hasa baada ya kusema hayo, nitamke kwamba ni heshima kwangu na nifuraha yangu kutangaza kwamba mkutano huu

sasa umefunguliwa rasmi.

***Tanzania oyee!***

***Vyama vya Siasa Oyee!***

***Utulivu na amani!***

***Ndio nguvu yetu.***

***NAWASHUKURU SANA, ASANTENI SANA***

Kiambatisho Na. 3

**HOTUBA YA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI, MHESHIMIWA DK. HUSSEIN ALI MWINYI WAKATI WA KUFUNGA MKUTANO MAALUM WA KUJADILI HALI YA MFUMO WA DEMOKRASIA YA VYAMA VINGI VYA SIASA NCHINI TANZANIA.**

**TAREHE 17 DISEMBA, 2021 DODOMA**

**Mheshimiwa Jaji Francis Mutungi;**
**Msajili wa Vyama vya Siasa nchini,**

**Waheshimiwa Mawaziri mliopo,**

**Mheshimiwa Sivangwila Sikalaliwa Mwangesi;**
**Jaji wa Mahakama ya Rufani na Kamishna wa Maadili,**

**Mheshimiwa Pandu Ameir Kificho;**
**Spika Mstaafu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar,**

**Ndugu Joseph Butiku;**
**Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere Foundation,**

**Washiriki wote,**

**Wageni waalikwa,**

**Mabibi na Mabwana**

**Assalamu Aleikum**

Namshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaaliya afya njema na kutuwezesha kufanya mkutano huu maalum wa kujadili hali ya mfumo wa Demokrasia ya vyama vyingi vya siasa nchini Tanzania . Natoa shukrani zangu za dhati kwa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa pamoja na Baraza la Vyama vya Siasa kwa kuja na wazo la kuandaa mkutano huu na kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi katika hafla hii ya kuufunga. Nasema Ahsanteni sana.

Nimeelezwa kwamba, Mkutano huu uliovishirikisha Vyama mbalimbali vya Siasa vilivyopo nchini, uliandaliwa kwa ajili ya kukaa pamoja na kujadili maendeleo, mafanikio na changamoto zitokanazo na mfumo wa Vyama vyingi ulioanzishwa nchini mwaka 1992. Ni dhahiri kuwa kufanyika kwa mkutano huu ni kielelezo cha kukomaa kwa demokrasia na Utawala bora katika pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tangu juzi uliopofunguliwa rasmi mkutano huu na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wafuasi wa siasa za mirengo mbali mbali wamekuwa wakifuatilia mijadala mliyoiendesha kupitia vyombo vya habari ili kuweza kufahamu mambo mengi yaliyojadiliwa na kupangiwa maazimio. Napenda nikupongezeni sana kwa kuonesha ukomavu wa kisiasa.

**Ndugu Viongozi na Washiriki wa Mkutano huu,**

Ni dhahiri kwamba, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mfano wa kuigwa Barani Afrika na duniani kote, kutokana na ukomavu wetu wa kisiasa na juhudi zetu za kuendeleza demokrasia na Utawala bora. Juhudi zetu hizi ni

msingi wa mafanikio tunayoendelea kuyapata katika kuendeleza na kudumisha amani na utulivu pamoja na mshikamano miongoni mwa wananchi. Sio katika nchi nyingi duniani ambapo viongozi na wafuasi wa vyama vya siasa vyenye itikadi tofauti hukaa pamoja kwa lengo la kujadili mambo na maendeleo ya mfumo wa vyama vingi vya siasa nje ya Bunge kama tulivyofanya hapa.

Uwezo wetu huu kutojali na kuendekeza tofauti zetu za kisiasa, dini na kabila ni miongoni mwa mambo yanayoifanya nchi yetu kuwa ni miongoni mwa mataifa saba katika bara la Afrika ambayo yako salama na yenye utulivu mkubwa. Tunawashukuru Viongozi Waasisi wa Taifa letu kwa kutuwekea msingi huo muhimu wa amani nchini mwetu.

Taarifa ya mwaka 2021 iliyotolewa na taasisi ya Economics and Peace (IEP) ya Sydney kuhusu hali ya usalama katika mataifa mbali mbali Duniani imeonesha kuwa Jamhuri ya Muungao wa Tanzania ni moja kati ya Mataifa Saba yenye kiwango kikubwa cha usalama na amani barani Afrika.

**Ndugu Viongozi na Washiriki wa Mkutano huu,**

Itakumbukwa kwamba mwezi Julai mwaka 1992, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliutangazia ulimwengu kuwa imerejesha tena mfumo wa siasa za vyama vingi. Baada ya hapo, Uchaguzi Mkuu wa kwanza uliovishirikisha vyama vya upinzani ulifanyika mwaka 1995. Kwa hivyo, hivi sasa ni miaka 29 imeshatimia tangu nchi yetu iliporuhusu tena siasa za

vyama vingi na miaka 26 tangu wananchi walipopiga kura kwa ajili ya kuwachagua viongozi katika mfumo huo.

Historia hii inatuonyesha kwamba mkutano huu ni muhimu kwa ajili ya kutafakari mafaniko na changamoto zilizojitokeza kwa kipindi hicho cha miaka 29. Bila ya shaka, yako mafanikio mengi ambayo tumeyapata na zipo changamoto kadhaa zilizojitokeza. Naamini kwamba, kupitia mkutano huu mafanikio na changamoto hizo zimejadiliwa vizuri na mmeweza kuja na mapendekezo mbali mbali yatakayotuwezesha kuziondoa changamoto zilizopo.

**Ndugu Viongozi na Washiriki wa Mkutano huu**

Nimefurahi kuona kwamba, miongoni mwa mada zilizowasilishwa katika Mkutano huu ni Historia na hali ya Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa nchini Tanzania. Hilo ni jambo muhimu tukijuwa kwamba, kwa kuifahamu hisitoria ya mfumo wa vyama vingi, tunaweza kujifunza mafanikio tuliyoyapata na changamoto zilizojitokeza hivi sasa na wakati nchi yetu ilipokuwa inafuata mfumo wa Chama kimoja.

**Ndugu Viongozi na Washikiri Wote wa Mkutano huu**,

Nimefurahi kuona kwamba, kupitia Mkutano huu mmejadili na kupitisha maazimio kuhusu Umuhimu wa Kuheshimu Sheria, Kudumisha amani, utulivu, umoja wa kitaifa na kuendelea kukuza uchumi katika Mfumo wa

Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa Tanzania. Hii ni mada muhimu tukijuwa kwamba, amani na utulivu ndio msingi wa maendeleo yetu.

Kwa kipindi hiki cha miaka 29, tumejifunza kwamba, mfumo wa vyama vingi una faida nyingi kwa maendeleo ya Taifa letu, kama ilivyobainika katika mijadala mliyoifanya na maazimio yaliyopitishwa. Ni dhahiri kwamba, mfumo wa vyama vingi umepanua wigo wa majukwaa ya kidemokrasia na uhuru na kutoa maoni na kuchagua kushiriki katika siasa tukiwa na itikadi tofauti. Vile vile, mfumo huu umepanua fursa ya kuikosoa na kuishauri Serikali katika masuala muhimu ya maendeleo yetu pamoja na kuimarisha siasa za ushindani miongoni mwa wananchi, wanasiasa na viongozi.

Watanzania sote tuhakikishe tunaendeleza siasa zenye malengo ya kulinda na kuendeleza maslahi ya Watanzania na kukuza maaendeleo nchini kwetu. Ni vyema tujiepushe na siasa za chuki zenye lengo la kutugawa. Tuendelee kutatua tofauti zetu za kisiasa kwa njia ya majadiliano na maridhiano kama tunavyoendelea kufanya.

**Ndugu Mwenyekiti wa Mkutano,**

Utulivu wa kisiasa mara zote huwa unatokana na majadiliano kama haya, ambapo watu hukaa pamoja na kubadilishana mawazo huku wakiweka mbele masilahi ya nchi kama niliyoyataja awali. Nchi yetu ni mfano mzuri, tunaishi kwa amani na utulivu huku tukichapa kazi kujenga uchumi wetu kwa sababu ya amani na utulivu uliopo hapa Tanzania. Mafanikio haya yametokana na kuzungumza kama mlivyofanya sasa.

Ni dhahiri kwamba mafanikio tuliyopata tangu tulipoanzisha mfumo wa vyama vingi ni ya kupigiwa mfano, kwa nchi zinazoendelea na zilizoendelea. Katiba ya Nchi yetu na za vyama vyetu vya siasa ziko imara hali ambayo inatuwezesha kubadilishana madaraka kwa hali ya amani na utulivu bila ya ubaguzi wa rangi, dini, jinsia au asili ya mtu.

**Ndugu Mwenyekiti wa Mkutano,**

Zanzibar tumekuwa tukizungumza sana baina ya vyama vya siasa, hata tukapata miafaka mitatu kuanzia uchaguzi wa vyama vingi wa mwaka 1995 mpaka sasa. Hata hili Baraza la vyama vya siasa ambalo limeandaa mkutano huu kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ni matokeo ya muafaka wa kisiasa wa Zanzibar wa Mwaka 2001. Baada ya CCM na CUF kuzumngumza na kukubaliana kuondosha tofauti zao na kuahidi kila mmoja kuendesha siasa za kistaarabu zenye kuheshimu sheria za nchi, kulinda amani, utulivu na umoja wa kitaifa, ikaonekana ni vyema kuwa na chombo cha kudumu ambacho kitaendeleza mashauriano baina ya vyama vya siasa na hapo ndipo wazo la kuundwa baraza la vyama vya siasa lilizaliwa na hatimaye baadaye likaundwa na hivi sasa ni chombo ambacho kipo kwa mujibu wa sheria na kinafanya kazi nzuri kama mnayoiona hapa. Hivyo, tuendeleze utamaduni huu wa kuzungumza na kuheshimu sheria kwa maslahi ya nchi yetu na maendeleo tunayohitaji.

**Ndugu Viongozi na Washikiri Wote wa Mkutano huu**,

Namalizia hotuba yangu kwa kutoa shukrani kwa vyama vyote vya siasa vilivyoshiriki katika mkutano huu pamoja na viongozi wao. Aidha, natoa

pongezi na shukrani kwa watoa mada kwa kutuelimisha vizuri na kuendesha mijadala kwa umahiri mkubwa. Hongereni sana.

Kwa mara nyengine tena, natoa shukrani kwa Ofisi ya Msajili wa vyama vya siasa Tanzania pamoja na Baraza la Vyama vya Siasa kwa kuandaa mkutano huu na kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi katika shughuli hii ya kufunga mkutano huu. Ninawaahidi kwamba, Serikali zetu zote mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zitayafanyia kazi mapendekezo na maazimio yaliyopitishwa katika mkutano huu ili kujenga na kuendesha mfumo wa vyama vingi ulio bora zaidi kwa maslahi mapana ya Watanzania wote. Tuone kwamba, sote tuna jukumu la msingi la kuiletea maendeleo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa manufaa yetu sote.

Namuomba Mwenyezi Mungu aizidishie neema na baraka nchi yetu na aidumishe hali ya amani na usalama iliopo pamoja na mshikamano miongoni wa Watanzania. Nakutakieni nyote kila la kheri na utekelezaji mwema wa shughuli zenu za ujenzi wa Taifa.

**Baada ya kusema hayo, sasa natamka kwamba Mkutano huu wa kujadili hali ya Mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa Nchini Tanzania umefungwa rasmi**

**Asanteni kwa kunisikiliza**

Kiambatisho Na. 4

**HOTUBA YA MHESHIMIWA DK. HUSSEIN ALI MWINYI RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KATIKA HAFLA YA UZINDUZI WA KIKOSI KAZI CHA KUCHAKATA HOJA ZILIZOJITOKEZA KATIKA MKUTANO WA WADAU WA DEMOKRASIA YA VYAMA VINGI VYA SIASA - HOTELI YA GOLDEN TULIP AIRPORT - ZANZIBAR**

**TAREHE 10 JANUARI 2022**

**Mheshimiwa Othman Masoud Othman,**
**Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar;**

**Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla,**
**Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar;**

**Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid;**
**Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar;**

**Mheshimiwa Khamis Ramadhan Abdalla,**
**Kaimu Jaji Mkuu wa Zanzibar**

**Waheshimiwa Mawaziri Mliopo hapa;**

**Mheshimiwa Jaji Francis Mutungi,**
**Msajili wa Vyama vya Siasa;**

**Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kikosi kazi Rwekaza Mukandara;**

**Waheshimiwa Wajumbe wa Kikosi Kazi;**

**Waheshimiwa Viongozi wengine wa Serikali na vyama vya Siasa;**
**Waheshimiwa Viongozi wa Dini na Asasi za Kiraia mliopo;**

**Mabibi na Mabwana,**

**Assalam Aleikum**

Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa kwa ajili ya uzinduzi wa Kikosi Kazi kilichoundwa kwa lengo la kuzichambua hoja zote zilizotolewa katika Mkutano wa Wadau wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa uliofanyika tarehe 15 mpaka 17 Disemba 2021 Jijini Dodoma.

Natoa pongezi kwa Mheshimiwa Jaji Francis S.K. Mutungi; Msajili wa Vyama vya Siasa na Mheshimiwa Juma Ali Khatib; Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa kwa kuja na uamuzi wa kuyajadili na kuyatafutia njia ya utekelezaji mambo mbali mbali yaliyojadiliwa katika Mkutano ule. Uamuzi mlioufanya wa kuunda Kikosi Kazi kwa ajili ya kufanya kazi hiyo ni wa busara sana tukizingatia kuwa mara nyingi taasisi zetu huwa zinafanya mikutano na makongamano mengi lakini huwa hatuweki mipango ya utekelezaji wa maazimio yanayofikiwa. **Nakupongezeni sana kwa uamuzi wenu huu wa kuunda Kikosi Kazi.**

Aidha, natoa shukrani kwenu kwa kunialika kuwa Mgeni rasmi katika shughuli hii ya leo ambayo kwa hakika imeandaliwa vizuri. Nathamini sana fursa na heshima mliyonipa. **Ahsanteni sana.**

**Ndugu Viongozi na Wajumbe wa Kikosi Kazi,**

Utamaduni wetu sisi Watanzania wa viongozi na wafuasi wa vyama vya siasa viliopo nchini wa kukaa pamoja kama tulivyofanya leo na mwezi uliopita, kwa ajili ya kujadili masuala muhimu ya maendeleo yetu ni kielelezo cha kukomaa demokrasia nchini na uimara wetu katika kulinda na

kuendeleza umoja wa kitaifa na mshikamano wa Watanzania. Kwa pamoja, tumepata mafanikio mengi katika kipindi cha miaka 29 tangu nchi yetu iliporuhusu mfumo wa vyama vingi vya siasa na miaka 26 tangu Watanzania walipopiga kura kwa ajili ya kuwachagua viongozi katika mfumo huo. Ni wazi kuwa, vile vile, zipo changamoto kadhaa zilizojitokeza katika kipindi hicho ambazo zinapaswa kufanyiwa kazi.

Nimeaarifiwa kwamba viongozi wenye uzoefu mkubwa katika masuala ya siasa kutoka vyama mbali mbali vya siasa viliopo nchini ndio walichanguliwa kuwa viongozi na wajumbe wa Kikosi Kazi hiki ninachokizindua. Kwa hivyo, nachukua fursa hii kumpongeza Profesa Rwekaza Mukandara kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kikosi Kazi, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwa kuteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti na wote walioteuliwa kuwa Wajumbe wa Kikosi kazi hiki muhimu. Nimearifiwa kwamba viongozi na wajumbe walioteuliwa ni wataalamu wabobezi katika masuala ya uongozi, usuluhishi wa migogoro, utawala bora, haki za binadamu pamoja na masuala mbali mbali ya kisheria. Mchanganyiko mzuri wa wataalamu hawa wenye uwezo mkubwa wa kujadili masuala muhimu na mazito ya kisiasa na maendeleo yetu, unanipa matumaini kwamba maamuzi yatakayopitishwa hapa yatakuwa na mchango mkubwa katika kuleta maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii hapa nchini.

Viongozi na wajumbe nyote, muelewe kwamba mmekabidhiwa kutekeleza kazi kubwa yenye maslahi mapana kwa Kitaifa. Naamini kwamba

mtatekeleza majukumu yenu kwa umahiri na umakini mkubwa na hatimae Kikosi kazi hiki kitayafikia malengo yanayotarajiwa kwa ufanisi mkubwa.

**Ndugu Viongozi na Wajumbe wa Kikosi Kazi,**

Kwa mara nyengine, nawaahidi kwamba; Serikali zetu zote mbili zitawapa kila aina ya ushirikiano utakaohitajika katika kutekeleza na kukamilisha majukumu mliyopewa. Tunafanya hivyo sisi viongozi wa Serikali kwa kuzingatia wajibu wa kitatiba uliopo wa kusimamia na kuendeleza misingi ya utawala bora, huku tukijuwa kwamba, maendeleo ya nchi yetu yanategemea sana kuendelea kudumu kwa hali ya amani na utulivu iliyopo nchini. Aidha, tunafahamu kwamba kuendelea kudumu kwa hali ya amani na utulivu, kunatagemea sana kuwepo kwa maelewano na maridhiano ya kweli na endelevu baina ya vyama vya siasa mbali mbali viliopo nchini.

**Ndugu Viongozi na Wajumbe wa Kikosi Kazi,**

Masuala mbali mbali ya siasa yanagusa hisia za wananchi kwa namna mbali mbali. Aidha, wananchi wanapokea na kufahamu matamko na kauli za wanasiasa kwa upeo na uono tofuati. Kutokana na hali hiyo, sisi wanasiasa kila wakati tuna wajibu wa kuwa makini na kauli tunazozitoa pamoja na vitendo vyetu ndani ya jamiii. Aidha, tuhakikishe kwamba sera za vyama vyetu zinazingatia umuhimu wa kuwaunganisha Watanzania na sio kuwafarakanisha.

Kwa hivyo, nyinyi viongozi na wajumbe wa Kikosi Kazi hiki mnapaswa kutumia hekima, busara, uzalendo na uzoefu wenu katika uchambuzi mtakaofanya na muwe tayari kuzibatilisha hoja ambazo baada ya kuzijadili mkahisi zinaweza kuleta migongano au kuwa kikwazo kwa maendeleo yetu. Vile vile, wajumbe nyote lazima muweke pembeni tofauti zenu na mfanye kazi kwa kuzingatia maadili na kanuni zinazoongoza kikosi hiki. Naamini kwamba mtafanyakazi vizuri kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa letu.

**Ndugu Viongozi na Wajumbe wa Kikosi Kazi,**

Siasa ni uwanja mpana uliojengwa kwa nadharia nyingi zenye tafsiri mbali mbali. Nasaha zangu kwenu zitafsirini na zitumieni nadharia za kisiasa mnazozifahamu kwa kuzingatia mazingira halisi ya nchi yetu ya Tanzania. Tuzingatie kwamba yako baadhi ya mataifa yaliyovuraga au kuzorotesha maendeleo yao kwa kujaribu kuiga au kutumia nadharia na falsafa za kisiasa za mataifa mengine bila ya kuzingatia mazingira yao halisi, historia zao na hali za kiuchumi na kijamii za wananchi wao.

Historia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni ya kipekee, Muungano wetu ni wa Kipekee na umoja na mshikamano uliopo ni wa kupigiwa mfano siyo tu barani Afrika bali duniani kote. Kwa hivyo, ni vyema kwamba mtakapokuwa mnachambua hujoa mkazingatia umuhimu wa kuendeleza Muungano wetu pamoja na kuyalinda na kuyadumisha Mapinduzi ya Zanzibar ya 1964. Uchambuzi wa hoja vile vile lazima ulenge katika kuendeleza siasa zenye lengo la kuzidi kuwaunganisha Watanzania na kuimarisha misingi ya usawa, umoja na mshikamano iliyopo.

**Ndugu Viongozi na Wajumbe wa Kikosi Kazi,**

Namalizia hotuba yangu kwa kutoa shukurani kwa mara nyengine kwenu Msajili wa Vyama vya Siasa na Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa kwa kunilika kuja kuzindua kikosi kazi hiki. Aidha, natoa shukurani kwenu wageni waalikwa na waandishi wa habari mlioungana nasi katika uzinduzi huu.

Namuomba Mwenyezi Mungu aizidishie neema na baraka nchi yetu, na audumishe na auzidshe umoja na mshikamano uliopo miongoni mwa Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawatakieni nyote majadiliano mema, na hatimae mje na mapendekezo mazuri zaidi kwa maendeleo ya nchi yetu.

Baada ya kusema hayo, sasa natamka kuwa Kikosi Kazi cha kuchambua Hoja zilizojitokeza katika Mkutano wa Wadau wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa sasa kimezinduliwa rasmi.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA,**

**MUNGU IBARIKI AFRIKA.**

**Asanteni kwa kunisikiliza**

**Kiambatisho Na. 5**

**Mada Zilizowasilishwa Katika Mkutano wa Wadau wa Kujadili Hali ya Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa Nchini, Uliofanyika Tarehe 15 hadi 17 Desemba 2021 Dodoma**

| Na. | Mada | Muwasilishaji/Mchambuzi wa Mada | Jina |
|---|---|---|---|
| 1. | Umuhimu wa uzalendo na maadili ya viongozi wa umma katika demokrasia ya vyama vingi vya siasa | Muwasilisha Mada | Mhe. Jaji wa Rufani Sivangilwa S. Mwangesi, Kamishna wa Maadili, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma |
| | | Mchambua mada | Mhe. Pandu A. Kificho; Spika Mstaafu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar |
| | | Mchambua Mada | Mhe. Joseph W. Butiku, Mkurugenzi Mtendaji, Mwalimu Nyerere Foundation |
| 2. | Historia na hali ya Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa nchini Tanzania | Muwasilisha Mada | Pofesa Bernadeta M. Killian, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar-es salaam (Utafiti). |
| | | Mchambua mada | Mhe. Anne S. Makinda, Spika Mstaafu wa Bunge |

| Na. | Mada | Muwasilishaji/Mchambuzi wa Mada | Jina |
|---|---|---|---|
| | | | la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| | | Mchambua Mada | Mhe. Hamad B. Mshindo, Katibu Mkuu Mstaafu, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar |
| 3. | Umuhimu wa Kuheshimu Sheria, Kudumisha Amani, Utulivu, Umoja wa Kitaifa na kuendelea kukuza uchumi Katika Mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa Tanzania | Muwasilisha Mada | Profesa Alexander B. Makulilo<br>Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (Taaluma, Utafiti na Ushauri kwa Umma) |
| | | Mchambua mada | Mheshimiwa Hamad R. Mohamed Mwenyekiti wa Taifa chama cha siasa Alliance for Democratic Change (ADC) na Waziri Mstaafu katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| | | Mchambua mada | Mhe. Balozi Amina S. Ali Waziri Mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi |

| Na. | Mada | Muwasilishaji/Mchambuzi wa Mada | Jina |
|---|---|---|---|
| | | | ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar |

**Kiambatisho Na. 6**

**Maoni na Mapendekezo ya Wadau Yaliyotolewa Katika Mkutano wa Wadau wa Kujadili Hali ya Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa Nchini, Uliofanyika Tarehe 15 hadi 17 Desemba 2021 Dodoma**

1) Mkutano huu ni muhimu na tudumishe utaratibu wa kukutana mara kwa mara ili kutatua changamoto zetu kwa njia ya mazungumzo;
2) Kiundwe kikosi kazi (TaskForce) cha kuchambua maoni ya wadau yatakayopelekwa kwa Mhe. Rais kutoka katika mkutano huu;
3) Kwa kuwa baraza la vyama vya siasa lipo hakuna haja ya kuwa na chombo kingine cha kuchambua maoni ya wadau na kuyawasilisha sehemu husika.
4) Baada ya mazungumzo kuwepo na utekelezaji wa masuala yanayojitokeza, kwani usipo kuwepo itaonekana kwamba Baraza la Vyama vya Siasa halifanyi kazi vizuri;
5) Serikali irudishe Imani kwa wananchi walioathirika na vurugu za kisiasa za mwaka 2001 Zanzibar, kwa kutimiza ahadi yake ya kuwapatia kifuta machozi;
6) Kuna umuhimu wa wadau wa siasa kufuata Sheria, kanuni na miongozo ya Serikali katika kutekeleza majukumu yao;
7) Vyombo vyenye maamuzi vina wajibu wa kutenda haki, hivyo amani msingi wake ni haki;
8) Wanasiasa tujenge tabia ya kusema ukweli, kwani tabia ya kusema uongo na kujipendekeza madhara yake ni makubwa;

9) Viongozi wa siasa waepuke vitendo vya rushwa na pia taasisi zinazopewa taarifa za rushwa wawe wasiri na kuzingatia maadili ya kazi zao;
10) Vyama vya siasa vitoe nafasi maalum kwa makundi maalum hususan wanawake na watu wenye ulemavu, kwani michango yao ni muhimu kwa Taifa;
11) Demokrasia inategemea na mazingira ya nchi husika, uchumi, utamaduni, mila na desturi, hivyo tusiwe watu wa kuiga demokrasia ya nchi zingine;
12) Elimu ya uraia iwe endelevu na ianzie ngazi ya shule za chekechea, vilevile isisubiri wakati wa uchaguzi;
13) Tunapokaribia kumaliza dira ya taifa ya miaka mitano, tufikirie dira inayokuja ili iwe kama Dira ya Afrika inayoishia 2063 na wadau washirikishwe kikamilifu katika kutengeneza dira mpya ili waweze kuitekeleza;
14) Viongozi wa dini wanaposhawishi watu kujiunga na madhehebu yao huwa hawachokonoi madhehebu mengine, hivyo vyama vya siasa viige utaratibu huo katika kueneza sera zao na kujenga vyama vyao;
15) Wajumbe wa Baraza la Vyama vya Siasa siyo lazima wawe ni Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa chama, hivyo waongezwe wajumbe wengine watatu na kusisitiza viongozi wakuu wa chama Mwenyekiti na Katibu Mkuu lazima wahudhurie vikao ili maamuzi yanayotolewa yawe na nguvu. Idadi hiyo ya wajumbe itawezesha kuweka usawa kuhusu suala la jinsia na pande mbili za Muungano katika ujumbe wa Baraza la Vyama vya Siasa kwa kila chama.

16) Baraza la vyama vya siasa litengeneze Kanuni ambazo zitawawezesha wanasiasa kuadhibiana wao kwa wao bila kuhusisha vyombo vingine vya dola;
17) Serikali na vyombo vya dola viepuke upendeleo vinapohudumia vyama vya siasa;
18) Wakati wa utekelezaji wa majukumu kusameheana ni muhimu, lakini tusisahau ya nyuma ili yasije kujirudia;
19) Maadili ya viongozi wa umma yawahusu pia viongozi wa Vyama vya Siasa;
20) Sheria ya vyama vya siasa ya mwaka 2019 ifanyiwe mapitio upya na mchakato uwe shirikishi;
21) Sheria ya Jeshi la Polisi ifanyiwe mapitio yatakayofanya liwe na weledi na kuondoa uonevu unaofanywa kwa kisingizio cha kutekeleza sheria;
22) Viongozi wa vyama vya siasa wawe wavumilivu na wajenge desturi ya kuacha tabia ya kususia vikao muhimu vya maamuzi au kususia mijadala ya bajeti ya nchi;
23) Viongozi wa kisiasa wawe na hofu ya Mungu katika utendaji wa kazi zao na wawe waadilifu, na watii Sheria, wazalendo na wawe na uchungu na nchi yao. Kila mmoja anawajibu wa kulinda amani na utulivu wa nchi yetu, na kwamba wote tunatembea katika jahazi moja likitobolewa tunazama wote.
24) Viongozi wa dini hawapaswi kuwa na chama chochote cha siasa lakini waumini wao ni wanachama wa vyama mbalimbali vya siasa;
25) Malalamiko juu ya ukiukwaji wa demokrasia yanapojitokeza yashughulikiwe mapema kabla madhara hayajajitokeza;

26) Mapendekezo ya asasi za kiraia toka uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi vya siasa yafuatiliwe ili yatekelezwe;
27) Iundwe Kamati ya wazee kwa ajili ya kulishauri Baraza la Vyama vya Siasa;
28) Baraza la Vyama Vya Siasa lipewe jukumu la kushughulikia migogoro ndani ya vyama vya siasa;
29) Kuwepo na mikutano inayoangalia hali ya kisiasa ya nchi na iwe na kalenda maalum;
30) Vyama vya siasa viwaelimishe wanachama wao nini wananchi wanataka na viandae viongozi wa Taifa wa baadaye;
31) Tuwe na sera endelevu ya kitaifa ambayo kila chama kikiingia madarakani kiwe na wajibu wa kuifuata;
32) Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa iwezeshwe kifedha, ili iweze kuandaa makongamano ya kisiasa yenye kujumuisha viongozi wenye uzoefu;
33) Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa awe na bajeti yake;
34) Serikali ya umoja wa kitaifa Zanzibar inaundwa na vyama viwili pekee jambo ambalo linanyima vyama vingine fursa ya kuwepo kwenye Serikali hiyo;
35) Kwa mujibu wa kifungu cha 11 cha Sheria ya Vyama Vya Siasa, ni haki ya vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara, hivyo tujadili namna vyama vitakavyoadhibiana pale watapokiuka taratibu za mikutano hiyo;
36) Suala la kura ya mapema Zanzibar linaleta uhasama;

37) Kuwepo na usawa wakati wa uchaguzi ili kuleta ushindani huru, vyama vyote vipewe kiwango sawa cha fedha walau Milioni 50, ili viweze kuendesha kampeni za uchaguzi;

38) Badala ya kuendelea na mchakato wa Katiba mpya tunaweza kuchagua mambo machache yanayolalamikiwa sana, mfano tume huru ya uchaguzi na tukaanza nayo;

39) Katika chaguzi zetu kuna uvamizi wa watu kugombea bila ngazi ya taifa ya chama husika kuwatambua kama ni wanachama halali wa chama hicho;

40) Fursa ya kutoa maoni kuhusu marekebisho ya sheria inapotokea vyama vya siasa na wadau wengine watoe maoni badala ya kulalamika tu.

41) Mchakato wa kuandaa katiba mpya ni gharama kubwa pia wakati wa mchakato wa kutunga katiba mpya watu walitofautiana sana mpaka wengine wakasusa, hivyo ni vyema kujipa muda na kujitafakari kabla ya kuendelea na mchakato huo.

42) Rushwa katika uchaguzi ni tatizo ambalo linapaswa kufanyiwa kazi kwa umakini,

43) Ni vyema kuwa na Baraza la Vyama vya Siasa lenye nguvu;

44) Kuna watu wanakaa nje ya nchi kwa ufadhili wa watu wanaowajua wao, lakini kazi yao ni kutukana nchi yetu, hawa ni adui wa nchi ambao wanapaswa kukataliwa kushiriki uchaguzi wowote wa nchi hii.

45) Mkutano huu unatoa nafasi kwenda hatua ya pili ya mazungumzo;

46) Nchi ina matatizo ya kisiasa yayofanya tusishirikiane, yanatokana na mgongano wa vyama,

47) Mheshimiwa Rais kasema tuzingatie Katiba, Sheria na Kanuni za nchi;

48) Hiki siyo kipindi cha malalamiko bali ni kipindi cha kutafuta ufumbuzi wa malalamiko;

49) Kuna mtindo siku hizi wa kujadili watu badala ya hoja;

50) Kuwa na vyama vingi peke yake siyo kuwa na demokrasia kamili, demokrasia ni kuhakikisha watu wanapata fursa ya kuchangia mawazo ya kuendesha nchi yao;

51) Katika mchakato wa kukusanya maoni ya kutunga Katiba mpya, Swananchi walisema kuwa viongozi wako mbali na wananchi;

52) Msingi wa demokrasi ni watu, vyama viwe na utaratibu wa kutekeleza demokrasia, hivyo vyama vinapaswa kuwa karibu na wananchi;

53) Ukabila, udini, na ukanda umeanza kurudi katika shughuli za kisiasa na inavunja misingi ya amani, hata ikitokea uteuzi tu utaona katika mitandao ya kijamii watu wanaongelea ukabila na ukanda;

54) Vyama vimeanza kugawa wananchi kwa kubaguana kwa misingi ya uanachama wa vyama vya siasa, Viongozi wa dini ndiyo wanaohangaika kuwaweka watu pamoja.

55) Bila amani hakuna vyama vingi;

56) Maadili yanaanzia kwa viongozi, viongozi wasipokuwa na maadili jamii haiwezi kuwa na maadili; Katika mchakato wa marekebisho ya Katiba wananchi walizungumza sana kuhusu maadili.

57) Katika rasimu ya Katiba kuna tunu za taifa na uzalendo. Lakini bahati mbaya rasimu ikasambaratishwa na Bunge la Katiba; Katika rasimu ya katiba kuna misingi na miiko ya uongozi;

58) Wakati wa uchaguzi, taratibu za vyama vya siasa hazijali wananchi, hivyo itafika wakati wananchi hawatosikiliza vyama; katika uchaguzi mkuu wa 2020 ni asilimia 50 tu walipiga kura.

59) Suala la mikutano ya hadhara lishulikiwe, pili suala la Katiba, hakuna haja ya kurudi mwanzo, turekebishe sheria ya katiba, turekebishe katiba pendekezwa na kuipitisha;

60) Kila baada ya uchaguzi tumekuwa na tabia ya kufanya marekebisho ya sheria za uchaguzi.

61) Tangu mwaka 1995 katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ndio wagombea wengi walienguliwa katika uchaguzi.

62) Kutofautina ni kawaida;

63) Binadamu tumeumbwa na mapungufu; Serikali na Vyama vya Siasa vinaongozwa na watu wenye mapungufu. Serikali inaongoza vizuri hivyo tuikosoe tu mahali inapokosea. Kuikosoa Serikali siyo kutokuwa mzalendo. Uzalendo ni kusema mazuri na mabaya ya Serikali ndani ya nchi kwa staha, lakini siyo kwenda kusema nje ya nchi.

64) Mahakama inaandaa semina wakati wagombea wanataka kugongewa muhuri na mahakimu, hii siyo sawa.

65) Uenguaji wa wagombea kwa kushindwa kujaza fomu na matatizo mengine ya kiutendaji yashughulikiwe kwani siyo sawa masuala haya kuwepo katika jamii;

66) Viongozi wa vyama vya siasa wawajibike, kwani mtu huwezi kutangaza maandamano yasiyo na mwisho wakati watu wanataka kufanya kazi;

67) Katiba kwa nini isirekebishwa badala ya kuwa na katiba mpya; kero za kikatiba zipunguzwe kama zilivyopunguzwa za Muungano;
68) Kanisa lipo tayari kusaidia kufanikisha mazungumzo ya kisiasa.
69) Wasiokuwepo iundwe njia bora ya kuwashawishi washiriki, wakishindikana tuachane nao.
70) Baraza la Vyama vya Siasa liimarishwe ili litekeleze vyema majukumu yake;
71) Masuala yanayohusu Tume ya Taifa ya uchaguzi yamepokelewa na yanayohitaji kufanyiwa kazi yatafanyiwa kazi;
72) Ni muhimu kuzingatia Sheria na Kanuni za nchi tunapojadili na kutenda mambo yetu.
73) Hotuba ya Rais ilijikita katika Ibara ya 26 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
74) Ni vyema kujiuliza kuwa, je mambo yanayoongelewa katika mkutano huu yameshindwa kujibiwa na Sheria zilizopo na mamlaka zilizowekwa kusimamia Sheria hizo? Kama kuna upungufu katika Sheria basi ipendekezwe Bunge lifanye marekebisho, kwani tume za uchaguzi hazina mamlaka ya kufanya marekebisho ya Sheria.
75) Ni kweli kuwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 wagombea walienguliwa, kwa kuwa Sheria inaruhusu wagombea kuwekeana mapingamizi na hili haliwezi kuwekewa ukomo kwamba mapingamizi yawe idadi fulani;
76) Mfumo wa haki katika mchakato wa uchaguzi upo, kwa mtu kukata rufaa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, hata kwenda mahakamani kwa mujibu wa kifungu cha 151 cha Sheria ya Uchaguzi. Kifungu hicho kinaruhusu mgombea na mpiga kura asiyeridhika kupeleka shauri

Mahakamani. Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kesi za uchaguzi za ubunge zilikuwa ni 4 tu na udiwani ni 11 tu;

77) Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 Tume ya uchaguzi ilipokea rufaa 165 za ubunge kati ya hizo 98 zilikuwa ni za wagombea ubunge walioenguliwa, tume iliwarudisha wagombea 67 na watia nia 31 tu ndiyo hawakurejeshwa.

78) Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kulikuwa na rufaa za wagombea udiwani 451 kati ya hizo 389 zilikuwa ni wa wagombea walioenguliwa ambapo 235 walirejeshwa katika uchaguzi. Rufaa 162 zilikuwa ni maombi ya kuwaengua wagombea udiwani lakini tume haikuengua hata mmoja;

79) Je kuna haja ya kulalamika kwa suluhu inayopatikana katika sheria. Sheria za uchaguzi zimejitosheleza katika utatuzi wa migogoro, tatizo ni watu kutopenda kufuata utaratibu wa kisheria katika kushughulikia migogoro.

80) Kama mtu anasema tume zetu za uchaguzi siyo huru, ni vyema aseme nini ni kinafanya zisiwe huru, pia aseme tume huru inakuwaje? Je tunataka tume itakayochaguliwa vingine, tume nyingine au watu wengine katika tume tulizonazo?

81) Tatizo ni kutoaminiana, hivyo hata wakichaguliwa watu wengine watu ndiyo sisi watanzania na wanachama wa vyama ndiyo nyie. Hivyo, tusipoaminiana maneno yataendelea; Nchini Ufaransa wagombea ndiyo wanatengeneza karatasi zao za kura kwa pesa za Serikali na kumpa msimamizi wa uchaguzi. Hakuna mwangalizi wa uchaguzi wa chama au mgombea.

82) Uzalendo ni kuifia nchi yako kwa namna yoyote. Hivyo, kila kiongozi ajitathimini je yeye ni mzalendo.

83) Kila kiongozi ajitathimini kuwa ni mwadilifu. Kwani watoto hufuata anayotenda mzazi. Tuachane na rushwa na ubaguzi.

84) Uwepo wa vyama vingi vya siasa siyo kuwa na uhasama na utengano, bali ni kuwa na mawazo mbadala, matumizi ya nguvu ndani na nje ya vyama vya siasa yana madhara. Hivyo, tufuate utaratibu na kuwa waadilifu.

85) Kuna Sheria za Mwenyezi Mungu na za Dunia, vyote vimewekwa ili binadamu tusiishi kama wanyama na tusigongane, kwani binadamu tuna mapungufu. Sheria hizi zinaturatibu tuishi vizuri na hakuna aliye juu ya Sheria, hivyo kiongozi asiyezingatia Sheria hana nia njema na nchi yetu;

86) Kila kiongozi katika nchi yetu wakiwemo viongozi wa vyama vya siasa aheshimu tunu za taifa ikiwamo uhuru na mapinduzi ya Zanzibar.

87) Washiriki wote wa mkutano waondoke na dhamira safi ya mazungumzo;

88) Suala la Kikosi Kazi liachwe kwa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ili ifanyiwe kazi vizuri, ili taarifa ya Kikosi Kazi ipitiwe vyema katika Baraza la Vyama vya Siasa na hatimaye iwasilishwe kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

89) Tume ya Taifa ya Uchaguzi ishirikiane na Kikosi Kazi kupata maelezo ya kutosha kuhusu kero za uchaguzi.

90) Katika usimamizi wa uchaguzi tatizo siyo tume bali ni watendaji kule chini.

91) Mkutano wa wadau ukitoa maazimio bila kujumuisha uchambuzi utakaofanywa na Kikosi Kazi hicho, ni kitendo sawa na kurusha jiwe gizani. Kikosi Kazi ni jambo muhimu, kwani litaeleza nini kifanyike, vipi kifanyike, na kwa wakati gani;

92) Kikosi Kazi kiundwe na Msajili wa Vyama vya Siasa;

93) Kuna shida ya uadilifu na kuheshimu sheria, wasimamizi wa uchaguzi hawaheshimu Sheria, hali ipo siyo tu ndani ya Serikali na chama tawala, bali hata katika vyama vya upinzani. Kuna vyama vingi vimezaliwa kutokana na vyama vya upinzani kutoheshimu sheria, kuna vyama vimeanzishwa kwa kuneemesha familia.

94) Ruzuku inavigawa vyama.

95) Sheria ya Vyama vya Siasa imebagua vyama kwa kutoa fedha za ruzuku kwa baadhi ya Vyama vya Siasa na kutowapa wengine, hivyo ni vyema Sheria irekebishwe ili asilimia 30 ya fedha hizo itolewe kwa vyama vyenye wabunge na 70 itolewe kwa vyama vyote.

96) Kutakuwa na hadidu rejea kwa Kikosi Kazi;

97) Kikosi Kazi kitajumuisha wawakilishi wa wadau wote walioshiriki mkutano wa wadau;

98) Kikosi Kazi kitaundwa ndani ya mwezi mmoja na kitapitia hoja zote zilizotolewa na washiriki wa mkutano wa wadau na kutoa mapendekezo yake.

**Kiambatisho Na. 7**

## Orodha ya Vyama vya Siasa Vyenye Usajili Kamili

1. Chama cha Mapinduzi (CCM)
2. The Civic United Front (CUF-Chama cha Wananchi)
3. Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA)
4. Union for Multiparty Democracy (UMD)
5. National Convention for Construction and Reform (NCCRMageuzi)
6. National League for Democracy (NLD)
7. United Peoples' Democratic Party (UPDP)
8. National Reconstruction Alliance (NRA)
9. African Democratic Alliance Party (ADA-TADEA)
10. Tanzania Labour Party (TLP)
11. United Democratic Party (UDP)
12. Chama cha Demokrasia Makini (MAKINI)
13. Democratic Party (DP)
14. Sauti ya Umma (SAU)
15. Alliance for African Farmers Party (AAFP)
16. Chama cha Kijamii (CCK)
17. Alliance for Democratic Change (ADC)
18. Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA)
19. Alliance for Change and Transparency (ACT-Wazalendo)

**Kiambatisho Na. 8**

**Vyama vya Siasa Vinavyopata Ruzuku Kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**1. Vyama vya Siasa vinavyopata ruzuku kwa kuwa na Wabunge**

| Na. | Chama |
|---|---|
| 1. | Chama cha Mapinduzi (CCM) |
| 2. | Alliance for Change and Transparency (ACT-Wazalendo) |
| 3. | The Civic United Front (CUF-Chama cha Wananchi), |
| 4. | Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) |

**2. Vyama vya Siasa vinavyopata ruzuku kwa kuwa na Madiwani**

| Na. | Chama |
|---|---|
| 1. | Chama cha Mapinduzi (CCM) |
| 2. | Alliance for Change and Transparency (ACT-Wazalendo) |
| 3. | The Civic United Front (CUF-Chama cha Wananchi), |
| 4. | Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) |
| 5. | National Convention for Construction and Reform (NCCRMageuzi) |
| 6. | Democratic Party (DP) |

**Kiambatisho Na. 9**

## Orodha ya Wadau Waliowasilisha Maoni Kwenye Kikosi Kazi

### A. Orodha ya Wadau Waliowasilisha Maoni kwa Kufanya Mazungumzo na Kikosi Kazi

**Taasisi za Dini**

1. Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA);
2. Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC);
3. Kanisa la SABATO Tanzania;
4. Baraza Kuu la Jumuiya na Taasisi za Kiislam Tanzania; 5. Baraza la Makanisa ya Kipentekoste Tanzania (CPCT); na
6. Jumuiya ya Wahindu Tanzania (HCT).

**Taasisi za Kiraia**

1. Legal and Human Rights Center (LHRC);
2. Media Council of Tanzania (MCT);
3. Tanganyika law Society (TLS);
4. The Right Way;
5. Centre for Good Governance and Development in Tanzania (CEGODETA);
6. Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA);
7. Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA);
8. Shirikisho la Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu Zanzibar (SHIJUWAZA);
9. Jumuiya ya Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO) ;
10. Ushiriki Tanzania;
11. Mtandao wa Wanawake wa Katiba, Uchaguzi na Uongozi Tanzania;
12. Mtandao wa Wanawake Watetezi wa Haki za Wanawake (Coalition for Women Human Rights Defenders Tanzania);

13. Academic Staff Association of Public Universities and Colleges of Tanzania (ASAPUCT);
14. Umoja wa Makatibu Wakuu Wastaafu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
15. Chama cha Muziki Tanzania;
16. Shirikisho la Filamu Tanzania;
17. Umoja wa Mabalozi Wastaafu; na 18. Tanzania Diaspora Council (TDC).

**Watu Mashuhuri**

1. Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania'
2. Mhe. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais Mstaafu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
3. Mhe. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
4. Mhe. Salmin Amour Juma, Rais Mstaafu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
5. Mhe. Amani Abeid Karume, Rais Mstaafu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
6. Mhe. Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar**;**
7. Mhe**.** Cleopa David Msuya, Waziri Mkuu Mstaafu;
8. Mhe. Joseph Sinde Warioba, Waziri Mkuu Mstaafu;
9. Mhe. Frederick Tluway Sumaye, Waziri Mkuu Mstaafu;
10. Mhe. Pandu Ameir Kificho, Spika Mstaafu wa Baraza la Wawakilishi;
11. Mhe. Damian Zefrin Lubuva, Mwanasheria Mkuu Mstaafu na Mwenyekiti Mstaafu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi;
12. Mhe. Andrew John Chenge, Mwanasheria Mkuu Mstaafu na Waziri Mstaafu;
13. Mhe. Frederick Mwita Werema, Mwanasheria Mkuu Mstaafu;
14. Dkt. Abdulhamid Yahya Mzee, Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
15. Prof. Mussa Assad, CAG mstaafu;

16. Bwana Ludovick Utouh, CAG mstaafu;
17. Mhe. Jaji Mstaafu Juxton Isaac Mlay;
18. Mhe. Augustino Lyatonga Mrema;
19. Mhe. Joseph Butiku;
20. Mhe. Philip Mangula;
21. Mhe. Anna Margareth Abdallah;
22. Mhe. Getrude Mongella;
23. Mhe. Vuai Ali Vuai;
24. Mhe. Stephene Masatu Wasira;
25. Balozi Ali Abeid Karume;
26. Bwana Yahya Khamis Hamad'
27. John B. Tendwa;
28. Askofu Dkt. Benson Bagonza;
29. Bwana Hamdani Omari Makame;
30. Sheikh Ponda Issa Ponda;
31. Profesa Issa Shivji;
32. Bi. Fatma Karume;
33. Bwana Jenerali Twaha Ulimwengu;
34. Mhe. Ismail Jusa Ladhu;
35. Dkt. Hellen Kijo Bisimba; 36. Bwana Rajab Kiravu; na
37. Bwana George Mlawa.

**Taasisi za Serikali**

1. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Tanzania;
2. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar;
3. Tume ya Taifa ya Uchaguzi;
4. Wizara ya Fedha na Mipango ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
5. Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
6. Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar;
7. Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU);
8. Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA);
9. Umoja wa Wabunge Wanawake;
10. Ofisi ya Rais, TAMISEMI; na

11. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Vyama vya Siasa**

1. Chama cha Mapinduzi (CCM)
2. The Civic United Front (CUF-Chama cha Wananchi)
3. Union for Multiparty Democracy (UMD)
4. National League for Democracy (NLD)
5. United Peoples' Democratic Party (UPDP)
6. National Reconstruction Alliance (NRA)
7. African Democratic Alliance Party (ADA-TADEA)
8. Tanzania Labour Party (TLP)
9. United Democratic Party (UDP)
10. Chama cha Demokrasia Makini (MAKINI)
11. Democratic Party (DP)
12. Sauti ya Umma (SAU)
13. Alliance for African Farmers Party (AAFP)
14. Chama cha Kijamii (CCK)
15. Alliance for Democratic Change (ADC)
16. Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA)
17. Alliance for Change and Transparency (ACT-Wazalendo)

**B. Orodha ya Wadau Waliowasilisha Maoni kwa Maandishi**

1. TWAWEZA;
2. Shirika la Msaada wa Kisheria Mingoyo (SHIMKIMI)- Kutoka Lindi;
3. Tanzania Peace, Legal Aid & Justice Centre;
4. Ndugu Sia Ulomi Furia;
5. Maj. (mst) John. L. Liyanakile;
6. Bwana Eugs Furia;
7. Waasilia Asilia;
8. Vijana Pambana Pata Maendeleo Rukwa (VIPAMARU);
9. The Popular Inspiring & Relief Organization (PIRO);
10. Bwana Abdul Kawinga Abdulrahman;
11. Bwana Alloyce D. H. Mbunda-Kutoka Songea;
12. Umoja Wa Kudai Katiba Mpya Tanzania (UKUKAMTA)- Kutoka DSM;

13. Bwana Jeremiah- Kutoka DSM;
14. Bwana Michael A. Mburuma;
15. Mwanza Youth And Children Network;
16. Bwana Nobert Jason Dotto- Kutoka DSM;
17. Bwana Severine Niwemugizi; na
18. Bwana Neema Kabale.